**23 MEI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 23 Mei, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Maswali, Waheshimiwa Wabunge tunaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Sasa namuita Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, aulize swali lake.

Na. 401

### Ujenzi wa Barabara ya Mombo – Mzeri – Korogwe

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza: -

Je, lini barabara ya Mombo Mzeri itajengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mombo - Mzeri ina urefu wa jumla ya kilometa 30 inayounganisha barabara kuu ya Segera – Same na Makao Makuu ya Kata ya Magambakwalukonge, Mkalamo na Wilaya ya Handeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaanza kufanya Upembuzi yakinifu na Usanifu wa kina katika barabara hii na kazi hii inatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 ili kupata gharama halisi za ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* imeendelea kuimarisha barabara hii kwa kiwango cha changarawe pamoja na kujenga vivuko na makalavati ili kuhakikisha inapitika majira yote ya mwaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paul Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu ya Serikali nina mswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, barabara hii ni mihimu sana, ndiyo barabara fupi na rahisi kuunganisha Kijiji cha Msomela Kijiji cha mfano, na barabara kubwa ya Segera - Arusha. Sasa kwa sababu ya umuhimu huo;

Je, ni lini Serikali itakubali kuipandisha hadhi barabara hii iwe barabara ya Mkoa ihudumiwe na *TANROADS*, barabara hii pamoja na zile barabara nyingine kama ile ya Msambiazi - Lewa - Lutindi na barabara ya Kwetonge – Tonge – Kizara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mvua zinazonyesha sasa hivi Korogwe zimeathiri sana barabara zetu za changarawe;

Je, Serikali iko tayari kuwapa *TARURA* fedha za dharura ili wakatusaidie kurekebisha hali ya barabara zetu kwenye maeneo ambayo yameathiriwa na mvua?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, 0FISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane na Mheshimiwa Mnzava kwamba barabara hii ni muhimu sana na barabara hii pia imetajwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025 Ibara ya 55(c)(4) katika ukurasa wa 77. Hivyo ni kipaumbele cha Serikali kuhakikuisha barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupandisha hadhi taratibu ziko wazi za kisheria, inatakiwa wao kule waaanze katika vikao vyao vile vya *DCC* itoke pale ipite katika kikao cha Bodi ya

Barabara ya Mkoa, na ikitoka kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa waende wapitishe kwenye *RCC* na iwasilishwe kwa Waiziri mwenye dhamana na *TANROADS* ambaye ni Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili; fedha za dharura kwa *TARURA*, tayari Serikali inaliangalia hilo na tayri ilikuwa bajeti yao *TARURA* wao kwa mwaka ya dharura ilikuwa ni bilioni 11. Hivi sasa tunaangalia namna ya kuweza kuwaongezea fedha Kwenda mpaka bilioni 43 ili kuhakikisha kwamba wana fedha ya kutosha ya dharura kwa ajili ya ujenzi wa barabara wakati wote; ije mvua lije jua barabara ziwe zinapitika na ndiyo maana Serikali pia imeiongezea *TARURA* bajeti kubwa sana kutoka bilini 226 mpaka bilioni 776.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Reuben Kwagilwa swali la nyongeza.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Barabara hii iliyotajwa na Mheshimiwa Mnzava lini Serikali wataanza kuiwekea changarawe ili angalau ianze kupitika wakati wote maana kwa sasa kuna maeneo mengi hayapitiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, 0FISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi ni barabara ambayo ipo kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, na inaunganisha pia wilaya mbili. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 barabara hii ilitengewa shilingi milioni 230 kwa ajili ya ukarabati wa kiwango cha changarawe, na Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara hii kuhakikisha makalavati yanapitika lakini pia na ule upembuzi yakunifu kwa ajili ya kuwa barabara ya lami.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea. Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela, sasa aulize swali lake.

Na. 402

**Kituo cha Afya Msanda Muungano – Tarafa ya Mpui**

**MHE. DEUS C. SANGU** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Kituo cha Afya cha Msanda Muungano katika Tarafa ya Mpui?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, 0FISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Jimbo la Kwela, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kukarabati vituo vya afya vikongwe nchini kikiwemo Kituo cha Afya Msanda Muungano kwa kutenga bajeti kwa ajili ya kuongezea miundombinu ili kuviwezesha kutoa huduma muhimu ikiwemo upasuaji wa dharura kwa mama wajawazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya Afya ikiwemo kituo cha Msanda Muungano katika Tarafa ya Mpui

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sangu swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa ya maswali madogo ya nyongeza. Nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maneno yenye matumaini kwa wananchi wa Kata ya Msanda Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Serikali imetumia fedha takribani shilingi 500,000,000 kujenga kituo cha afya katika Kata ya Kipeta, Tarafa ya Kipeta lakini mpaka sasa haijapeleka vifaa tiba;

Je, ni lini Serikali itapeleka vifaa tiba kwenye kituo hiki ambacho kilisubiriwa kwa muda mrefu na wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Serikali ilipeleka fedha takribani shilingi milioni 100 kwa ajili ya kujenga zahanati katika Vijiji vya Nderema, Mpembano, Mpona na Lyapona, lakini mpaka sasa zahanati hizo zimekamilika na hazina vifaa tiba;

Je, ni lini sasa Serikali mtapeleka vifaa tiba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, 0FISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii mbele ya Bunge lako Tukufu kumpongeza Mheshimiwa Sangu, kwa sababu ni majuzi tu alikuja ofisini kwa ajili ya kuangalia zahanati hizi katika Jimbo lake la Kwela. Tayari kuna milioni 150 ambayo imetengwa. Kwenye swali lake la kwanza imetengwa shilingi milioni 150 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwenye bajeti hii ya 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile nikienda kwenye swali lake la pili; kwenye zahanati zilizokamilka vilevile imetengwa shilingi milioni 50 kwa jili ya ununuzi wa vifaa tiba. Na fedha hizi mtakaponunua vifaa tiba pale Sumbawanga *DC* ninyi ndio mtaamua viende kwenye vituo vipi; lakini *priority* iwe katika hivi ambavyo vimekamilika na vinasubiri kutoa huduma kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tarafa ya Nkwenda ina kituo cha afya kimoja na kituo hiki kimezidiwa na wagonjwa wengi;

Je, ni lini Serikali itajenga kituo ha afya kwenye kata ya Songambele ambako tayari tulishaleta maombi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, 0FISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la Mheshimiwa Bilakwate linalohusiana na Tarafa ya Nkwenda kuzidiwa; ni adhma ya Serikali kuhakikisha inajenga vituo vya afya katika kata za kimkakati kote nchini ikiwemo Jimbo lake lile la Kyerwa. Tutaangalia katika bajeti ya 2023/2024 kama imetengwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya. Kama haikutengwa tutatenga fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025 kadri ambavyo fedha itapatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wananchi wa kata ya Kenyamanyoli waliamua kujenga kituo cha afya kwa nguvu zao wenyewe, kwa maana Kituo cha Afya cha Kenyamanyoli, lakini Serikali iliahidi kupeleka fedha kuanzia mwaka 2019 kwa ajili ya umaliziaji wa maboma yale, mpaka leo hawajapeleka. Ningetaka kujua ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa yale maboma ili wananchi wa Kenyamanyole waweze kupata huduma ya afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, 0FISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kipaumbele cha Serikali kuhakikisha inaunga mkono jitihada za wananchi popote pale nchini ambapo wamejitoa kujenga huduma mbalimbali wao wenyewe kwenye jamii yao; na Serikali itatafuta fedha kadri ya upatikanaji wake ili iweze Kwenda kuunga mkono hujudi hizo katika Kituo hiki cha Afya cha Kenyamanyoli. Vilevile nichukue nafasi hii kumuelekeza Mkuruhenzi wa kule Tarime Mjini, kuhakikisha anatenga fedha kwenye mapato yake ya ndani kuunga mkono jitihada hizi za wananchi wa Kenyamanyoli.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini sasa aulize swali lake, kwa niaba yake Mheshimiwa Boniventura Kiswaga.

Na. 403

**Changamoto zinazokabili Taasisi za Afya za Kidini - Muleba**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI K.n.y. MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE** aliuliza: -

Je, kwa nini Serikali isikae na taasisi za afya za kidini Wilayani Muleba ili kupunguza changamoto zilizopo katika kutoa huduma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, 0FISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mbunge wa Jimbo la Muleba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Muleba ina vituo sita vya kutolea huduma za afya vinavyomilikiwa na mashirika ya kidini. Hospitali tatu za Lubya, Ndolage na Kagondo, Kituo cha Afya kimoja na zahanati mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inao utaratibu wa kukaa na hospitali teule za wilaya kupitia bodi ambazo zimejumuisha wataalam wa kutoka ngazi ya mkoa na halmashauri husika. Bodi hizo hukutana kila robo mwaka kwa ajili ya kupitia taarifa za utendaji pamoja na kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza wakati wakutoa huduma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Mkundi swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa taratibu kama hizo kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri zipo, lakini utekelezaji wake wakati mwingine unaleta changamoto;

Je, ni kwa nini Serikali sasa isifuatilie kujua hatma ya yale mazungumzo yanakuwaje ili mwisho wa siku wananchi wapate huduma wanazozitarajia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili. Kituo cha Afya cha Nakatunguru Jimboni Ukerewe ni muhimu sana, kinahudumia watu zaidi ya 10,000 kwenye Mji wa Nansio pale lakini kina upungufu mkubwa wa miundombinu;

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa miundombinu kwenye kituo kile cha afya cha Nakatunguru ili kiweze kutoa huduma zinazostahili kwa wananchi wa ukerewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, mjibu.

**NAIBU WAZIRI, 0FISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi katika majibu yangu ya msingi kwamba utaratibu upo wa kamati hizi za kitaalamu za kushauri katika ngazi ya mkoa. Kuna timu ya mkoa, kuna timu ya halmashauri na mashirika ya kidini ambayo yanamiliki hospitali hizi. Kwa hiyo nipende kuchukua nafasi hii mbele ya Bunge lako Tukufu kuwataka waganga wote wakuu wa mikoa hapa Tanzania kuhakikisha wanakaa vikao hivi ambavyo vipo kisheria na wenzetu wamiliki wa hospitali hizi ambao ni taasisi za kidini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kweenye swali lake la pili la kituo cha Nakatunguru kule Nansio Ukerewe, kwamba ni lini

Serikali itapeleka fedha kumalizia. Serikali itapeleka fedha kumalizia kituo hiki kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi. Kwa kuwa changamoto za hospitali za kidini inaikumba pia hospitali ya Mbagala *Mission* kwa jina jingine kwa Buluda, ni hospitali ya muda mrefu, na wananchi wote wa Mbagala na maeneo mengine ya Dar es Salaam wanaitegemea sana hospitali hiyo;

Je, Serikali haioni haja kuwaongezea nguvu kituo kile cha *Consolata Sisters* Mbagala *Mission* ili waweze kusaidia vizuri zaidi wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, 0FISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee tena majibu yangu ya msingi, kwamba Serikali inao utaratibu wa kukaa na hospitali hizi teule katika maeneo mbalimbali hapa nchini na kama nilivyokwisha toa maelekezo kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa waganga wakuu wote wa mikoa kuhakikisha wanakaa kuangalia uendeshaji wa hospitali hizi teule na kuona ni namna gani ambavyo zinaweza zikaboreshewa huduma zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongezee tu kwa faida ya Bunge lako Tukufu, kwamba Serikali hupeleka watumishi katika hospitali hizi teule lakini vile vile inapeleka mgao wa fedha katika hospitali hizi teule kuweza kusaidia ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata huduma ambayo wanastahili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Hospitali ya Mji wa Mafinga inahudumia watu wengi sana kwa sababu jiko barabarani pale, watu wa kutoka

Mufindi wanahudumiwa pale lakini miundombinu yake ni chakavu;

Je, ni lini Serikali itakarabati miundombinu hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, 0FISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itakarabati miundombinu hii chakavu pale katika Hospitali ya Mji Mafinga kadri ya upatikanaji wa fedha. Lakini nirudie tena kwamba Wakurugenzi wa Halmashauri wana wajibu wa kuhakikisha wanatenga fedha kwa ajili ya kuanza kutengeneza miundombinu mbalimbali kwenye halmashauri zao. Tayari Serikali kuu mmeona imefanya mengi chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupeleka fedha nyingi kwenye halmashauri hizi. Ni wakati umefika kwa wakurugenzi, mabaraza ya madiwani nao kuweka kipaumbele cha kusaidia wananchi pale na kuujnga mkono juhudi ambazo Serikali hii ya awamu ya sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya kwa kupeleka fedha nyingi kwenye sekta hizi za elimu na afya.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Afya, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa sasa aulize swali lake.

Na. 404

### Tatizo la wizi wa dawa na vifaa vya afya nchini

**MHE. LUHAGA J. MPINA** aliuliza: -

Je, upi mkakati wa kutokomeza wizi wa dawa na vifa vya afya, hatua zilizochukuliwa kwa wahusika na fedha zinazopotea kwa mwaka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Afya, Mheshimiwa Godwin Mollel majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Suala la kupambana na wizi na ubadhirifu wa bidhaa za afya si la Serikali pekee bali ni suala letu sisi wote, hasa wawakilishi wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali katika kutatua tatizo la wizi wa dawa na vifaa tiba kama ifuatavyo: -

a) Kufanya agenda ya ulinzi wa bidhaa za afya kuwa agenda ya kudumu katika vikao vya kamati za ulinzi na usalama za mikoa na wilaya.

b) Kujenga uwazi wakati wa kupeleka bidhaa za afya na kuwapa wakuu wa wilaya na Wabunge nyaraka za makabidhiano ya dawa na vifaa tiba kwa ajili ya rejea.

c) Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa bidhaa za afya ikiwemo kufunga mifumo ya kielektroniki pamoja na kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara.

d) Kuimarisha kamati za usimamizi za vituo kwa kuzijengea uwezo kuhusu majukumu yao katika usimamizi wa bidhaa za dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilifanya uchunguzi wa ubadhilifu wa bidhaa za afya na taarifa kuwasilishwa kwenye semina ya wabunge, na kupelekwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ili kufanya thamani halisi ya bidhaa zilizopotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, swali la nyongeza.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu hayo mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kwa kuwa tathimini iliyofanywa na Wizara Novemba 2021 ilibaini kwamba jumla ya bilioni 83 za bidhaa za dawa pamoja na bidhaa za afya zilikuwa zimeibiwa.

Je, Serikali ilichukua hatua gani na imechukua hatua gani kwa hao watumishi ambao wamefanya ubadhilifu wa dawa hizo kwa ajili ya wananchi kwa ajili ya kutolea huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa, uwezo wa Bohari ya Dawa *(MSD)* kusambaza dawa pamoja na bidhaa nyingine za afya ni asilimia 59 tu. Hii inatokana na malimbikizo ya madeni ambayo ni zaidi ya bilioni 259, lakini pia mtaji wa bilioni 593. Je, Serikali inatoa tamko gani kumaliza matatizo haya, ili kuiwezesha taasisi yetu ya *MSD* kuwa na uwezo mkubwa wa kusambaza dawa pamoja na bidhaa nyingine za afya kwa maslahi ya wananchi wetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru Mbunge mwenzangu kwa swali lake zuri, lakini swali la kwanza ni kwamba, wamechukuliwa hatua gani wale walioonekana kufanya ubadhiriru wa bilioni 83. Moja, sisi kama wataalam wa Wizara ya Afya tulifanya kazi yetu na kuona kwamba, kuna dalili za upotevu wa bilioni 83.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi yetu iliyofuata ni kukabidhi kwenye taasisi yetu ya TAKUKURU ambayo ina wataalam wa kujua sasa ili kufuata sheria na taratibu na haki za watumishi wa umma, tumepeleka kule wanafanya uchunguzi. Miezi miwili iliyopita walituambia kwamba, wako kwenye hatua za mwisho sasa kuweza kubaini *specifically* ni nani kafanya nini na ni nini kimefanyika ili wahusika waweze kuchukuliwa hatua. Hilo ni swali lake la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, ni kweli kwamba, Waheshimiwa Wabunge fedha wanazopitisha hapa bilioni 200 kwa ajili ya vifaa tiba na dawa ni fedha za vituo vyetu kwenye majimbo yetu. Maana yake tukipitisha hapa kwenye bajeti tunapitisha pesa kwa ajili ya vituo vyetu. Vituo vyetu vikipata pesa zinapelekwa *MSD,* maana yake ni nini? *MSD* tulitegemea i-*operate* kama bohari ya dawa, lakini ina-*operate* kama *procurement entity.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hilo la kwamba, wapewe mtaji, nafikiri liliibuka wakati wa bajeti yetu na Wizara ya Fedha wamelichukua na wiki iliyopita tulikutana kujadili kuona namna gani *MSD* wanaweza wakapatiwa mtaji, ili sasa tukiwapitishia fedha hapa Bungeni, basi vituo vyetu vikiomba dawa *MSD* wakutwe tayari walishanunua dawa hizo. Hilo ni suala la kulichukua tu ili kuondoa ucheleweshaji uliopo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amsabi, swali la nyongeza.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya mwaka jana tulipata bahati ya kupita naye katika baadhi ya zahanati zetu Wilayani Serengeti alishuhudia upungufu mkubwa wa dawa na vifaa tiba. Sasa je, ni lini na kuna mpango gani wa kuhakikisha uwepo wa dawa na vifaa tiba vya kutosha katika zahanati ya Kemgesi, Maburi, Busawe, Nyansulula, Mbalibari, Koleli, Rubanda, Kituo cha Afya Nata na Zahanati ya Rigita? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulikuwa naye pamoja Serengeti, tuliona hilo tatizo. Sasa namwagiza *DMO* wa Serengeti leo aandike mahitaji ya hiyo hospitali na wiki hii watapata dawa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, sasa aulize swali lake.

Na. 405

**Kumaliza tatizo la umeme - Mtwara**

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza tatizo la umeme Mkoani Mtwara hususani Wilaya ya Masasi na Jimbo la Lulindi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Nishati. Mheshimiwa Byabato, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Masasi inapata umeme kutoka katika Kituo cha Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi cha Mtwara chenye uwezo wa megawati 30.4 na pia umeme wa Gridi ya Taifa kupitia njia ya msongo wa kilovoti 33 kutokea Songea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya umeme Mkoani Mtwara, Wilayani Masasi ikiwemo Jimbo la Lulindi inatokana na Umeme mdogo usiotosheleza *(low voltage)* kwenye baadhi ya maeneo ya Wilaya hiyo kwa sababu ya umeme kusafiri umbali mrefu, uchakavu wa miundombinu hasa nguzo na vikombe pamoja na uharibifu kwenye miundombinu ya njia ya msongo wa kilovoti 132 unaotokana na watoto kupiga manati vikombe katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa tatizo hili Serikali kupitia *TANESCO* imetenga shilingi bilioni mbili ili kujenga njia ya kutoka Nanganga hadi Masasi. Aidha, ufungaji wa *Auto Voltage Regulator (AVR)* mpya yenye ukubwa wa *MVA* 20 kati ya Tunduru na Namtumbo unaendelea ili kuwezesha umeme wa kutosha kutoka Ruvuma kufika Masasi na maeneo ya jirani. Pia, kwa

kutumia Shilingi Milioni 600 Serikali inaendelea kubadili vikombe vilivyopasuka na kuweka vya plastiki na nguzo za miti zilizooza zinabadilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la umeme katika Mkoa wa Mtwara, Serikali imepanga kuunganisha Mkoa wote na Gridi ya Taifa kupitia miradi miwili ya Gridi Imara ambayo ipo katika hatua za utekelezaji. Miradi hii ni ujenzi wa njia kuu ya umeme ya msongo wa kilovoti 220 kutoka Songea hadi Tunduru na kutoka Tunduru hadi Masasi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nisikitike sana kutokana na majibu ya Naibu Waziri, haya majibu sidhani kama wanafanya *research*. Manati, watoto wanapiga vikombe kweli? Ni kitu cha kushangaza sana, lakini sasa kinachonishangaza zaidi kwenye chanzo cha umeme ndiko kwenye shida kubwa ya umeme. Je, ni lini Serikali itatuhakikishia kwamba huku tunapata umeme wa uhakika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikilalamika hapa kila siku kuhusiana na Jimboni kwangu Lulindi. Mkandarasi alipewa vijiji takribani 30 kushughulika na umeme kwa maana ya viunganishi, hakushughulikia hata kijiji kimoja, nimekuwa nikiimba kama wimbo. Je, ni lini nitaacha kuja hapa kulalamika kuhusiana na suala la umeme jimboni kwangu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyomalizia *paragraph* ya mwisho; upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa Mkoa wa Mtwara utatokana na kukamilisha hizi njia mbili ambazo zinaleta umeme wa gridi ya Taifa kutoka katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna tatizo kwenye njia ya umeme, hata kama ni kwenye eneo la chanzo umeme utakatika.

Kwa hiyo, azma ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuhakikisha kwamba, miundombinu yote hii inarekebishwa na kuimarishwa, ili iweze kusafirisha umeme kwa wakati wote na kuwafikia wale walengwa ambao wanatakiwa kuutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la pili; mkandarasi anayetekeleza miradi ya *REA* katika eneo la Lulindi ambalo ni Masasi, ana Wilaya ya Masasi na Nanyumbu, anaitwa Namis, alikuwa katika wale wakandarasi wenye *lot* zile saba ambazo zilikuwa zinasuasua, lakini tumesukumana naye na kuwekeana masharti na tunaamini kufikia Disemba na yeye atakuwa amekamilisha kazi yake. Kwa Lulindi alishawasha vijiji kama sita au saba kutoka kwenye vile alivyokuwanavyo na tunaamini kabla mkataba haujaisha atakamilisha kazi kwa sababu, tunasimamiana naye kwa karibu sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza swali la nyongeza. Kupitia Bunge hili tuliahidiwa kwamba, umeme wa Makete watabadilisha *line* kutoka Mbeya kuja Makete ni *line* ambayo inasumbua na imechoka kwa muda mrefu na inasababisha umeme Makete kukatika mara kwa mara. Wakatuahidi kwamba, watajenga *substation* Wanging'ombe ili wananchi wa Makete tuchukue umeme kutoka Njombe. Je, hatua hiyo imefikia wapi ili wananchi wa Makete wanaosikiliza sasa hivi wapate uhakika wa majibu ya Serikali? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya changamoto ambayo tumekuwa nayo ni umeme kusafirishwa umbali mrefu kutoka kwenye chanzo. Tulifanya tathmini kupitia *TANESCO* na tukabaini makundi matatu, kuna wale ambao wana shida zaidi, kuna wenye shida za kati na kuna wale ambao maisha yanaweza yakaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye maeneo yenye shida zaidi tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita imetupatia pesa bilioni 500 kwa ajili ya kutekeleza Mradi unaitwa Gridi Imara na utajenga vituo vya kupoza umeme 14 katika awamu hii ya kwanza. Sasa nimhakikishie Mheshimiwa Festo kwamba, eneo lake nitaenda kuliangalia limewekwa kwenye *category* ipi katika yale maeneo matatu yenye matatizo makubwa, matatizo ya kati na matatizo ya juu na nitamfahamisha endapo kitajengwa kituo cha kupoza umeme kipindi hiki au kitajengwa katika awamu inayofuata, lakini kabla ya miaka sita ijayo kwisha tunatarajia kuwa na kituo cha kupooza umeme kwa kila wilaya ili kuondoa matatizo ya umeme kusafirishwa kwa muda mrefu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wilaya ya Ngorongoro tangu iunganishwe na Gridi ya Taifa mwaka jana tatizo la umeme limezidi kuongezeka. Gridi ile iliunganishwa kutoka Wilaya ya Longido, ikitokea hitilafu ya umeme katika Wilaya ya Longido, Ngorongoro wanakosa umeme, ikitokea hitilafu Ngaramtoni, Ngorongoro wanakosa umeme na ikitokea hitilafu wilayani kwao wanakosa umeme. Imekuwa changamoto kubwa sana kwa wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro. Je, ni lini wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro watapata umeme wa uhakika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kujibu swali la Mheshimiwa Festo, maeneo yote ambayo yana changamoto ya umeme kufika katika maeneo yale kwa sababu ya kusafirishwa kwa umbali mrefu yamechukuliwa katika Mradi wetu wa Gridi Imara. Nimhakikishie Mheshimiwa Catherine Magige nitawasiliana naye kumwonesha *plan* ya Serikali ya kuhakikisha Wilaya yetu ya Ngorongoro inapata umeme wa uhakika na unaotoka katika maeneo yake kwa sababu, kuna wananchi ambao wanatakiwa pia wapate huduma hiyo kwa usahihi kabisa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Subira Mgalu.

Na. 406

**Ukarabati wa Gereza la Dimani, Kibiti**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE K.n.y. MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukarabati na kuongeza uwezo wa Gereza la Dimani Wilayani Kibiti?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali itatenga fedha shilingi milioni 350 kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa baadhi ya Magereza nchini. Gereza la Dimani Wilaya ya Kibiti ni moja ya magereza yatakayokarabatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali, kupitia mpango na bajeti wa kila mwaka itaendelea kutenga fedha za ukarabati na upanuzi wa Magereza yenye uhitaji huo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu yenye kuleta matumaini ya Serikali nina

maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, Serikali imesema imetenga fedha milioni 350; na kwa kuwa, Gereza la Dimani ni miongoni mwa magereza ambayo yatafanyiwa ukarabati. Je, Serikali inasema nini juu ya nyumba chakavu zilizopo kwenye Gereza hili la Dimani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa, changamoto ya uchakavu wa miundombinu inafanana na Gereza la Kigongoni, Bagamoyo na binafsi niliwahi kulitembelea na nikaona jitihada zao wenyewe askari magereza kwa kujenga nyumba na nikawachangia mifuko 50 ya simenti, lakini bado nyumba nyingine ni chakavu. Je, Serikali ina mpango gani wa muda mrefu wa kuwajengea nyumba askari magereza kwenye magereza mbalimbali kama inavyofanya kwenye majeshi mengine likiwemo Jeshi la JKT na Jeshi la Wananchi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchakavu wa nyumba kama pia zitahusika katika ukarabati huu, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, fedha za ukarabati zinapelekwa kwenye gereza. Mkuu wa gereza pamoja na menejimenti yake wataangalia wapi pana tatizo kubwa zaidi na wanalipa kipaumbele katika ukarabati. Hatuta-*prescribe,* hatutaagiza kwamba, karabati gereza acha nyumba kwa hiyo, kama nyumba zina hali mbaya zaidi wataanza kukarabati nyumba, kama gereza lina hli mbaya zaidi wataanza na gereza. Kwa hiyo, uhuru tunawaachia wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukarabati wa Gereza la Bagamoyo ambalo pia, Mheshimiwa Mbunge amesema limechakaa sana. Nimhakikishie tu mpango wetu wa ukarabati na ujenzi wa magereza unaenda sambamba kama tulivyokwishasema. Tumeanza mwaka jana, mwaka huu tunaendelea na mwaka ujao pia tutaendelea. Kwa hiyo, gereza la Bagamoyo kulingana na hali ya upatikanaji wa fedha litakuwa moja ya magereza yatakayoingizwa kwenye mpango wa ukarabati. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pondeza, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nilikuwa na swali dogo la kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, sasa Serikali haioni umefika wakati wa kuboresha magereza haya ambayo yapo Tanzania nzima ambayo Serikali imerithi na kujenga ya kisasa ambayo yataendana na mfumo wa sasa hivi wa teknolojia ambayo hata Mahakama sasa hivi wanaendesha kesi kwa mfumo wa mtandao ambao iepushe Serikali kutumia gharama ya kuwatoa mahabusu hapa na kuwapeleka mahakamani. Je, kwa nini Serikali isijenge magereza mapya ambayo yatakuwa yana mfumo wa kiteknolojia? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, yapo mabadiliko makubwa ya teknolojia na uendeshaji wa mashauri, hasa Mahakama imeshapiga hatua kubwa. Kwa msingi huo pia, Wizara ya Mambo ya Ndani, kupitia Jeshi la Magereza pia tumeanza. Magereza yanayojengwa sasa yanazingatia mahitaji hayo ya teknolojia na mengine yaliyo bora zaidi ikiwemo pamoja na ukaguzi, vitawekwa vifaa vya elektroniki, ili kuepusha watu kuguswaguswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa magereza ambayo tunayo haiwezekani yote tuyabadilishe siku moja. Tutaendelea kuyakarabati, yatakayofaa kuingiziwa vitendea kazi vya kisasa, vifaa vya kisasa zaidi, tutafanya hivyo, lakini mengine tutaendelea kuyakarabati ili yatoshe kulingana na uwezekano wa bajeti tutaimarisha kwenda kama anavyoshauri Mheshimiwa Mbunge katika siku zijazo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 407

**Utaratibu wa kurudisha Mlima Nkongore kwa wananchi**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Je, lini Mlima Nkongore utarudishwa kwa Wananchi wa Kata ya Katare baada ya kuchukuliwa na Jeshi la Magereza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya hifadhi na milima kama ilivyo kwa Mlima Nkongore, kisheria huwa yapo chini ya Halmashauri ya uendelezaji miji husika. Aidha, mwanzoni mwa mwaka 2016 baadhi ya wananchi walianzisha shughuli za kilimo cha mazao mbalimbali ikiwemo mazao haramu ya bangi katika eneo la kuzunguka Mlima Nkongore uliopo chini ya Halmashauri ya Mji wa Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kilimo kilichokuwa kinafanyika katika maeneo ya Mlima Nkongore, pia kutokana na Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004, kifungu cha 58(1) na (2) kinachozuia kufanya shughuli zozote zinazoweza kupelekea hifadhi ya mlima kuharibiwa kwa kuwa maeneo hayo yanatakiwa yahifadhiwe kisheria. Kikao cha Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya cha tarehe 11 Novemba, 2017 kiliazimia kuwa eneo la Mlima Nkongore likabidhiwe kwa Jeshi la Magereza ili kuimarisha shughuli za ulinzi na usalama. Kupitia barua Kumb. Na. AB.284/311/01C/59 ya tarehe 17 Novemba, 2017 ni idhini rasmi ya kukabidhi eneo la mlima Nkongore kwa Jeshi la Magereza kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama pamoja na uhifadhi wa mazingira, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Baada ya wananchi kunyang'anywa ile ardhi, wananchi wa Nkongore mwaka 2020 kabla ya uchaguzi walikuja hapa Dodoma kumwona Waziri Mkuu na Waziri Mkuu aliahidi kwamba, wataenda kurudishiwa lile eneo. Sasa mpaka leo bado hawajarudishiwa na mbaya zaidi hao magereza ambao wamekabidhiwa kwa ajili ya ulinzi kuna shughuli tena wanafanya. Nataka kujua ni kwa nini sasa pale ambapo Serikali imeamua kutwaa ardhi kwa ajili ya matumizi mbadala isiwalipe fidia wananchi? Ni nini taarifa ya fidia ya wananchi wa Nkongore ili waweze kupata kifuta jasho waendelee na shughuli zao ambazo walikuwa wakifanya Serikali inachukua ile ardhi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali pili. Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa kwamba, imesababisha kwa sababu ya taratibu za kimazingira wakakabidhi Jeshi la Magereza, ulinzi na usalama, lakini wananchi wale wakati ardhi inachukuliwa walikuwa wamepanda miti ya kudumu pamoja na mazao mbalimbali. Sasa mbaya zaidi askari magereza hawa wanavuna ile miti ya kudumu ya wananchi, wanaenda kufanyia shughuli nyingine. Ni kwa nini sasa kama ile miti inaruhusiwa kuvunwa nje ya hizo taratibu ambazo amezitaja hapa, wasiruhusu wananchi wale wavune miti yao ambayo walikuwa wameipanda kwa ajili ya biashara ili waweze kupata fedha zao stahiki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili la wananchi kuwalipa fiidia ya maeneo yanayotwaliwa kwa mujibu wa sheria, nimeeleza kwenye jibu la msingi kama Mheshimiwa Mbunge amenisikiliza kwa makini kwamba, maeneo ya milima ni maeneo yanayohifadhiwa. Hakuna mtu anayeweza akadai kwamba, anamiliki mlima, kwa hivyo, kama walikuwa wanafanya shughuli za kibinadamu kando mwa milima ambazo sio sehemu ya mlima tutawasiliana na mamlaka husika, kwa maana ya Mji wa Tarime. Namwomba Mheshimiwa Esther Matiko tukutane baada ya kipindi cha

maswali na majibu ili anipe ufafanuzi mzuri, niweze kutoa maelekezo stahiki kwa wenzetu w akule Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwepo wa miti iliyokuwa imepandwa na wananchi. Kama kuna uthibitisho huo tutawasiliana na mamlaka husika, kwa maana ya Magereza Mara na Tarime, Rorya, ili waweze kuwaruhusu wananchi wakate miti yao, lakini tunachoshukuru ni kwamba, hata Jeshi la Magereza katika hali ya kutunza ile hifadhi ya mlima wameshaanza kupanda miti na sasa wamepanda karibu miti 1,000 kuzunguka ule mlima kama sehemu ya kuhifadhi mazingira yale, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ghati Chomete, swali la nyongeza.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa maeneo haya wananchi walikuwa wanalima na wanayatumia kwa ajili ya kujipatia chakula. Je, Serikali haioni haja sasa ya kuwarudishia maeneo haya na ikawasimamia ili waendelee kulima na kuendelea kujipatia chakula?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Ghati, anayetetea wananchi wake wa Tarime, lakini nimweleze kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu langu la msingi ni kwamba, eneo lile limechukuliwa ili kutunza mazingira, lakini pia na kutunza shughuli za usalama ambazo wengine walikuwa wanatumia maeneo yale kulima kilimo cha mazao haramu ya bangi, kwa hiyo, uwepo wa magereza umesaidia kudhibiti hali ile ili isitokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, mlima ule uko karibu sana na mjini. Nadhani shughuli za kilimo mijini zinaruhusiwa, lakini huwezi ukasema pale kwa namna mji unavyoendelea kukua

patakuwa na maeneo mengi ya kulima zaidi ya kutunza usalama uliopo. Hata hivyo, tutaongea na Mamlaka ya Mji wa Tarime ili kuona kama kweli yako maeneo pembeni ya mlima yanaweza kutumika na wananchi basi wananchi waruhusiwe kuendelea na shughuli zao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba, sasa aulize swali lake.

Na. 408

**Ujenzi wa Daraja la Kijiji cha Kalema Maziwani – Chemba**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga Daraja la Kijiji cha Kalema Maziwani linalounganisha Wilaya za Kiteto, Chemba na Kondoa.?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS),* tayari imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kujenga upya Daraja la Kalema Maziwani katika barabara ya Kondoa – Bicha – Dalai ambalo liliititia kutokana na mvua kubwa za mwaka 2019. Ili kujenga daraja hilo mnamo tarehe 19 Mei, 2023 Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imetangaza zabuni kwa ajili ya

ujenzi na zabuni hizo zimepangwa kufunguliwa Tarehe 05 Juni, 2023, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Lujuo, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri sana, kwamba tayari kandarasi imeshatangazwa, pamoja na majibu hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, tangu 2019 daraja lilipokatika walitengeneza *diversion* ambayo magari yote yalikuwa yanapita pale lakini kwa bahati mbaya sasa ile *diversion* imeharibika kabisa.

Nini mkakati wa Serikali wa kuimarisha hiyo barabara ya mchepuo?

Swali la pili, katika barabara hiyo kutoka Kijiji cha Kalema Maziwani mpaka Mondo, mkandarasi aliyepewa kazi ya kuweka mifereji aliweka chini ya kiwango na hivyo kipindi cha masika maji yale yanaharibu kabisa barabara. Nini kauli ya Serikali juu ya mkandarasi huyu? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *diversion* naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa tayari tumeshatangaza tenda na Mkandarasi atakwenda *site* ni wazi pia kwamba wakati anajenga lazima hiyo *diversion* aiimarishe. Kwa hiyo, pia nitoe maagizo na maelekezo kwa Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Dodoma kuhakikisha kwamba anakwenda kuimarisha hiyo *diversion* ili wananchi na wasafiri wanaopita pale

waweze kupita sehemu salama ambapo sasa ni kiangazi, naamini ataitengeneza hiyo *diversion.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mifereji. Ni kweli barabara hii tunatengeneza mifereji kwa awamu, tumeendelea kutenga bajeti na hata mwaka huu wa fedha tunakokwenda mifereji itaendelea kutengenezwa. Kwa hiyo, pia nimuagize Meneja wa Mkoa wa Dodoma, kwamba kipindi hiki cha kiangazi ndicho kipindi sahihi cha kutengeneza mifereji, pia niwaombe wananchi wa Chemba kutokufanya shughuli za kijamii karibu na barabara na kuweza kusababisha baadhi ya mifereji kuziba na kuleta changamoto kwenye miundombinu ya barabara. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa hii nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Manyoni Mashariki kuna Daraja la Sanza ambalo upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na ulipaji wa fidia wananchi ulishakamilika. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja la Sanza? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli daraja la Sanza ni kati ya madaraja makubwa ambayo yanaunganisha Mkoa wa Singida na Mkoa wa Dodoma na Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba tulitangaza tenda lakini bahati mbaya sana, Mkandarasi aliyepata hiyo tenda alijitoa na sasa tunaendelea na *negotiations* na Mkandarasi wa pili kwa maana ya kulijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo daraja lilikuwa limepangwa *actually* liwe limeanza kujengwa katika mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira hiyo ipo, tunaendelea na *negotiations* na yule mshindi wa pili ili aweze kuanza kulijenga hilo daraja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara hiyohiyo, Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Malum, sasa aulize swali lake.

Na. 409

**Ujenzi wa kiwango cha lami Barabara ya Mlowo – Kamsamba**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Mlowo – Kamsamba kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza ujenzi wa barabara ya Mlowo – Kamsamba yenye urefu wa kilometa 130.1 kwa awamu kwa kuanza na ujenzi wa Daraja la Momba lenye urefu wa mita 80 pamoja na barabara zake unganishi zenye urefu wa mita 950 na kazi ya ujenzi imekamilika. Aidha, Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii. Katika mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imepanga kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Naibu Waziri, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, ninataka nijue barabara hizo unganishi ambazo zimejengwa kwa kiwango cha lami ni zipi.

Swali langu la pili, barabara hii ya Mlowo – Kamsamba imekuwa na changamoto kubwa sana kwa wananchi wetu, lakini changamoto hizi zinatukosesha fursa muhimu za kiuchumi. Nataka kujua Serikali ina mkakati gani wa maksudi kuhakikisha inajenga barabara hizi kwa wakati na muda muafaka ili kuondoa changamoto ambazo wanakutana nazo wananchi wa Mkoa wa Songwe, Momba na maeneo mengine kwa ujumla. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande cha kwanza cha swali lake sikukipata vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, rudia sehemu ya kwanza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kujua, barabara hizo unganishi ambazo zimejengwa kwa kiwango cha lami ni zipi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nimemuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nasema tumeanza kuijenga, tuna Daraja la Mto Momba ambalo liko katika hiyo barabara, katika hilo daraja tumejenga *approach roads* ambazo zinaunganisha lile daraja ukitokea Mkoa wa Songwe na Mkoa wa Rukwa. Kwa hiyo, kwa pande zile mbili tayari kuna lami upande huu na huu, zile ndiyo barabara unganishi na lile daraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maksudi, kwamba je, tuna mkakati gani kuhakikisha kwamba tunajenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami. Bajeti inaendelea, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imetenga fedha, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, kwamba tutaanza kuijenga hiyo barabara ili kukuza uchumi pia kurahisisha usafiri kwa wananchi wa Mkoa wa Songwe wa Mlowo, Igamba, Utambalila, Kamsamba lakini pia Utambalila kwenda Makao Makuu ya Mji wa Momba ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edwin Swalle, swali la nyongeza.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Hii barabara ya Kibena – Lupembe – Madeke mpaka Morogoro ni barabara ya Kimkoa na ni kero ya muda mrefu ya wananchi wangu. Tarehe 19 Bungeni hapa Serikali iliahidi kuanza ujenzi wa kilometa 25 na sasa tuko kwenye bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Naomba kauli ya Serikali barabara hii inaanza ujenzi lini? Ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ni kweli ni barabara inayounganisha Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Morogoro, pia yalitolewa maelekezo maalum na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwamba barabara hiyo ni lazima ianze kujengwa. Nami nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Lupembe kwamba katika bajeti hii tayari tumeshaanza taratibu za kuanza kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami, na tutaanza na kilometa 25 kwa kuanzia upande wa Mkoa wa Njombe, upande wa Morogoro tayari tuna kilometa 100 ambazo zinaendelea kujengwa na ziko kwenye taratibu za manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande kilichobaki *African Development Bank* watakifanyia usanifu ili barabara yote iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mchafu, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimwia Mwenyekiti, *Great Nyerere Road* ni barabara muhimu sana kwa utalii wa Selous. Nimeona kwenye mapendekezo ya bajeti zimetengwa shilingi bilioni mbili ambayo ni sawa na kilometa mbili. Ni lini sasa Serikali itaanza kutenga fedha za kutosha ili tupate kilometa za kutosha kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii? ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba aitaje barabara aliyoisema.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, taja barabara kabisa washa *microphone*.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Great Nyerere Road* au Kisarawe – Maneromango mpaka Mloka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa mpango wa bajeti kiasi tulichotenga aangalie kilometa ambazo tuna mpango wa kuzijenga. Ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba barabara hii ya Kisarawe – Maneromango kwenda Hifadhi ya Taifa ya Nyerere yote inakamilika kwa kiwango cha lami. Ndiyo maana katika

bajeti hii tumeshaweka fedha kuendelea na ujenzi wa hiyo barabara kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 410

**Ukarabati wa meli katika Ziwa Tanganyika**

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA** aliuliza: -

Je, kwa nini Serikali haijazikarabati Meli za MV Liemba, MV Mwongozo na MV Sangara ambazo zimesimama kufanyakazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kukarabati meli za MV. Liemba, MV Mwongozo na MV Sangara ili kuboresha huduma za usafiri kwa njia ya maji katika Ziwa Tanganyika. Ili kufikia azima hiyo, Serikali kupitia Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL)* inaendelea na ukarabati wa Meli ya MV Sangara ambapo kwa sasa kazi hiyo imefikia asilimia 90.7 na inatarajiwa kukamilika Septemba, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *MSCL* ilikamilisha taratibu za zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ukarabati wa meli ya MV Liemba tarehe 5 Machi, 2023 na kwa sasa *MSCL* inaendelea kufanya majadiliano na mkandarasi kabla ya kusaini

mkataba. Mkataba wa ukarabati wa meli hiyo unatarajiwa kusainiwa Juni, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kuhusu Meli ya MV Mwongozo ambayo ilisimamishwa kutokana na changamoto ya msawazo *(stability), MSCL* inakamilisha taratibu za kumwajiri Mhandisi Mshauri kwa ajili kufanya tathmini ya kina na kuishauri Serikali ipasavyo. Mhandisi Mshauri anatarajiwa kuanza kazi hii mwezi Juni na kukamilisha mwezi Novemba, 2023. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilumbe, swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwanza nilitaka ifahamike kwamba meli ya *MT* Sangara ambayo imefikia asilimia 90.7 ni meli ya mafuta siyo ya abiria wala mizigo, inabeba mafuta tu na kwa maana hiyo haina msaada mkubwa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa imekuwa kawaida kwa Serikali kila mwaka kutenga bajeti na kuleta hapa kwenye Bunge lakini hakuna utekelezaji, na kwa kuwa, katika Ziwa Tanganyika kwa sasa hakuna meli hata moja ya Serikali inayofanya kazi. Nataka *commitment* ya Serikali kwamba bajeti itapungua kwenye eneo lingine lolote la Wizara na siyo kwenye meli hii, kwamba lazima meli hizi zitatengenezwa na kurudi majini, nataka *commitment* ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Waziri wetu wa Ujenzi na Uchukuzi amesoma bajeti ya Wizara yetu na ameonesha *commitment* ya kiwango cha juu kabisa kuhusiana na namna ambavyo Ziwa Tanganyika tunakwenda kujenga meli mbili mpya pamoja na chelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi, *commitment* nyingine ya Serikali ni hizi meli ambazo hazifanyi kazi kwa sasa na tayari kwa mfano, hii MV Mwongozo ambayo tayari Mkandarasi ameshapatikana, ni Chuo cha Bahari Dar es Salaam *(DMI)* pamoja na hii meli ya MT Sangara ambayo amesema kweli ni ya mafuta lakini inafanya kazi katika Ziwa Tanganyika na iko asilimia 90. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wa Mikoa ya Kigoma, Rukwa pamoja na Katavi, kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika mwaka wa fedha ujao inakwenda kufanya haya ambayo imeahidi hapa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Mheshimiwa Mbunge. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 411

**Ukosefu wa Maji kwenye Vijiji Newala Vijijini**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka maji katika Vijiji 62 Jimbo la Newala Vijijini ambavyo havina huduma ya maji.?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Newala ina jumla ya vijiji 155 na kati yake vijiji 77 vinapata huduma ya maji. Serikali inaendelea na jitihada za kupeleka huduma ya maji kwenye vijiji visivyo na huduma na katika mwaka wa fedha 2022/2023 miradi

12 inaendelea kutekelezwa ukiwemo mradi mkubwa wa Makonde. Kukamilika kwa miradi hiyo kutanufaisha vijiji 61. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali itafanya usanifu wa miradi ya maji katika vijiji 17 vilivyobaki ikifuatiwa na utekelezaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini pia naishukuru Serikali kwamba kuna mradi mkubwa wa Makonde ambao wametupatia fedha unatekelezwa kwenye Wilaya yetu ya Newala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la msingi lilihusu Jimbo la Newala Vijijini. Kumbuka kwamba Newala ina Majimbo mawili ambayo ni Newala Mjini na Newala Vijijini, kwa hiyo swali lilikuwa *specific* kwa Newala Vijijini. Sasa kwa kujumlisha hivi tutashindwa kupata uhalisia wake wa tatizo hasa ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi sasa, pamoja na yote yaliyojitokeza, kwenye Jimbo la Newala Vijijini kuna Mradi wa Maji wa Mnima – Miyuyu ambao umeanza kutekelezwa tangu mwaka 2018, na mradi ule ulikuwa ni wa miezi tisa. Mpaka sasa utekelezaji wake ni asilimia 65 tu. Pia changamoto ambayo inasababisha mradi huu kutokamilika ni kukosekana kwa fedha. Fedha zilizokuwa zimetengwa ni bilioni 1.3, zimelipwa milioni 614 tu. Je, ni lini Serikali itamaliza fedha zilizobakia ili wananchi wa Newala Vijijini waweze kupata maji?

Swali la pili, kwenye Vijiji vya Mkudumba, Mnyengachi, Mnyambe, Mnima, Bahati, Mikumbi, Mkongi, Namangudu, Nangujane, Chilende, Mkoma, ‘two’ pamoja na Lihanga kuna miradi ya maji ambayo inatekelezwa. Lakini miradi ile ina changamoto ya upatikanaji wa fedha.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha ili miradi hii ikamilike? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Miyuyu tatizo ni fedha na swali lake la pili tatizo pia ni fedha. Naomba niwe nimepokea masuala haya ya Newala Vijijini na nitafanyia kazi mimi mwenyewe kwa ukaribu kuhakikisha fedha zinakwenda na kazi inakamilika kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tecla Ungele, swali la nyongeza.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa maeneo mengi katika Mkoa wa Lindi yana maji ya chumvi. Je, ni lini Serikali itawapatia maji safi na salama wananchi wa Kata za Ngunichile, Tarafa ya Kilimarondo na Namapwia kwenye Wilaya ya Nachingwea, Lihimalyao, Kibata na Kandawale kule Wilaya ya Kilwa? ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tecla kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yote aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge ni kweli yana shida ya maji ya chumvi, Mheshimiwa Mbunge unafahamu mradi wetu mkubwa ambao tayari tumeongea, hata juzi tulikuwa pamoja na tayari tunautengea fedha ule mradi ili sasa tuweze kupata maji ya uhakika yakiwa safi na salama na kuondokana na visima hivi vinavyotuletea maji ya chumvi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Furaha Matondo, swali la nyongeza kwa ufupi.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la

nyongeza. Katika kupunguza adha ya maji hususan Manispaa ya Ilemela, Serikali iliahidi kufufua visima vyote ambavyo havifanyi kazi. Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kufufua visima hivyo ili kuondokana na changamoto ya maji katika Manispaa ya Ilemela? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Furaha Matondo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu visima kufufuliwa Ilemela, tayari tumeshaagiza na katika mwaka ujao wa fedha tutahakikisha visima hivi vyote ambavyo vimechimbwa na bado vina maji mazuri tutavitumia kuhakikisha vinaongeza huduma ya maji katika maeneo yote ya Ilemela. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara swali la nyongeza kwa ufupi.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kupeleka fedha, kiasi cha shilingi bilioni 138 kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Rorya na Tarime. Nini kauli ya Serikali juu ya maji hayo kwenda katika Kata ya Komaswa, Manga, Nyamongo, Sirari, Pemba, Mbugi na Nyamwaga? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Marwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Ziwa Victoria wa kupeleka maji Rorya na Tarime, tayari usanifu unaendelea na Mheshimiwa Mbunge tumezungumza hapa juzi na nimekupa Katibu wangu amefanya kazi nzuri na wewe. Tutahakikisha mradi huu tunakuja kuutekeleza kwa wakati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Zaytun Swai.

Na. 412

**Mkakati wa kufikia usawa wa kijinsia 50/50 ifikapo 2025**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI K.n.y. MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza:-

Je Serikali inachukua hatua gani za kimkakati kufikia usawa wa kijinsia 50/50 ifikapo_2025?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwanaidi Khamisi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuundwa kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kama chombo maalum cha kuratibu ajenda ya kufikia usawa wa kijinsia. Aidha, hatua nyingine ni Serikali kuendelea kutoa fursa na nafasi za uongozi na maamuzi kwa wanawake mathalani, kipengele cha 12(4) cha Kanuni za Utumishi wa Umma mwaka 2013, kinasema, "Inapotokea mwanamke na mwanaume wametimiza vigezo sawa kwa kulingana, basi kipaumbele atapewa mwanamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Miji na Wilaya ya Mwaka 1982, inasema kuwe na asilimia 25 ya ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi na

maamuzi. Aidha, katika uchaguzi wa mwaka 2000 na 2005 asilimia hizo zilipandishwa hadi kufikia asilimia 31 ambayo ni moja ya tatu ya ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi na maamuzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na mikakati hiyo mizuri ya Serikali, wanawake wa Tanzania wanataka kusikia: Je, ifikapo mwaka 2025 asilimia hii 50 kwa 50 itakuwa imefikiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Hivi sasa tumeshuhudia jinsi wanawake waliopo kwenye nafasi mbalimbali wanavyofanya kazi kwa weledi na ufanisi mkubwa. Kwa mfano tu, Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Spika wetu, Mheshimiwa Dkt. Tulia: Je, Serikali ina mikakati gani sasa ya kuwainua kiuongozi wanawake hasa kwenye ngazi ya chini ili basi wainuke kiongozi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Husna. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ni mtekelezaji mzuri wa ilani. Katika kipindi chake cha miaka miwili ameshafikia asilimia 31 ya uteuzi wa wanawake viongozi. Kwa vile mamlaka ya uteuzi ni yake, tuendelee kumwamini katika majukumu yake na kufikia 50 kwa 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, Serikali imeridhia na inatekeleza mikataba ya Kimataifa na kikanda kuhusu usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake, lengo ni kukuza ushiriki wa wanawake katika nyanja zote za maendeleo ikiwemo kuhakikisha usawa katika ngazi nyeti na nafasi nyeti za uongozi na maamuzi nchini, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Ng'wasi Damasi Kamani, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 413

**Saa za kufundishwa wanafunzi**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI** aliuliza:-

Je, kwa nini ukomo wa saa za kufundisha Wanafunzi haujawekwa kisheria kama ilivyowekwa kwa saa za kazi kwa Waajiriwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Mkenda, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ng'wasi Damasi Kamani, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Elimu haijaweka ukomo wa saa za kufundisha wanafunzi ili kutoa fursa ya mtaala kuwa nyumbufu kulingana na mahitaji maalumu ya ujifunzaji wa wanafunzi wote pamoja na mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mitaala ya Elimu ya Msingi na Sekondari imeweka bayana Muda *(duration)* unaopaswa wanafunzi kusoma. Mtaala wa Elimu ya Msingi unaeleza kuwa muda wa kusoma Elimu ya Awali na Darasa la I - II ni masaa matatu tu kwa siku na kipindi kimoja ni dakika 30. Aidha, Muda wa kusoma kwa darasa III - VII ni masaa sita kwa siku na kila kipindi ni dakika 40. Aidha, kwa upande wa Elimu ya Sekondari muda wa

kusoma ni masaa matano na dakika 20 na kipindi kimoja ni dakika 40. Aidha, kwa mwaka wanafunzi hutakiwa kusoma kwa siku 194.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ng'wasi, swali la nyongeza.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Tunatambua kwamba lengo la Serikali kuweka utaratibu huu ni pamoja na kutambua uwezo wa kiakili wa watoto wetu pamoja na uwezo wao wa kusoma kwa muda fulani. Tunavyozungumza, kuna shule za *primary* hasa za watu binafsi ambazo mwanafunzi wa kutwa anaenda shuleni kuanzia saa mbili asubuhi mpaka saa kumi na moja na wa bweni anasoma tena kuanzia saa moja mpaka saa tatu au saa nne usiku, zaidi ya muda ambao umepangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Je, Serikali inatambua kwamba kuna shule ambazo zinafanya utaratibu huu ambao ni kinyume kabisa na utaratibu na inahatarisha afya za akili za watoto wetu? Kama inatambua, inachukua hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa ajili ya umuhimu wa afya za akili za watoto wetu: Je, Serikali haioni haja kwenye marekebisho haya yanayofanyika ya utaratibu wa elimu na mfumo wake kuliingiza suala hili katika mfumo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli kwamba ziko shule ambazo wanafunzi wanakaa muda mrefu zaidi shuleni na vile vile wanatumia muda mrefu sana kwenda shuleni na kuna aina mbili ya changamoto katika jambo hili. Kwanza, sio wanafunzi wote wanatumia mitaala ile ile. Ziko shule ambazo zinatumia mitaala tofauti na ile ambayo imetolewa na Serikali. Kwa mfano, kuna wale wanaotumia mitaala ya *Cambridge* na muda wao wa kusoma siyo lazima uwe sawa na muda wetu. Pili, kwa kuchagua

shule, hasa hizi binafsi na umbali wa shule na nyumbani, baadhi ya wanafunzi wanajikuta wanaondoka mapema sana nyumbani na wanarudi kwa kuchelewa sana, kwa sababu tu ya *choice* ya wazazi kwamba pengine wanaishi *Mbezi Beach* lakini mtoto wako anaenda kusoma Kimara tofauti na kusoma eneo lile lile la *Mbezi Beach*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili suala ni changamoto kweli kwa sababu tungependa watoto wapate fursa vile vile ya kucheza na kuwa watoto na kuwa na makuzi mazuri na wasitumie muda wote tu kwa ajili ya shughuli za darasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutajitahidi kuendelea kukaa na wadau wa shule binafsi kuangalia namna bora zaidi ya kutatua changamoto hii. Vile vile tunaendelea kuhimiza ujenzi wa shule mbalimbali za watu binafsi ziwe karibu zaidi na makazi ya watu na kuhimiza wazazi wachague shule ambazo ziko karibu zaidi na nyumbani ili watoto wasitumie muda mrefu sana barabarani wakati wanaenda shuleni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shigongo, swali la nyongeza.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Shule ya Msingi Bupandwa, Kasisa, Ruhama, Mwabasabi zina uhaba mkubwa sana wa walimu na hivyo kuwafanya walimu kufundisha kwa masaa mengi kuliko kawaida na watoto kushindwa kuelewa: Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuwasiliana na Waziri wa TAMISEMI ili aweze kututafutia walimu wa kutosha watoto wetu waweze kujifunza kwa urahisi na kuelewa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shigongo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna maeneo yana uhaba mkubwa wa walimu, mtawanyiko wa walimu siyo sawia kama

ambavyo tungependa. Bahati nzuri kuna nyongeza, walimu wataajiriwa hivi karibuni na tunazungumza na wenzetu wa TAMISEMI ili kuhakikisha kwamba walimu wale wanatawanywa maeneo yale ambayo yana uhitaji mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, sasa hivi tuna utaratibu wa kuweza kutumia walimu wa kujitolea kwa ajili ya kuendelea kupunguza uhaba wa walimu na tutaendelea na jitihada hizi ili kuhakikisha kwamba kweli wanafunzi wote popote pale Tanzania wanapata huduma ya kufundishwa kama inavyotakiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salma Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tunatambua na tunajua kwamba elimu ni haki ya msingi kwa mtoto na kwa mwanadamu; na amesema kwamba kuna ile ratiba ambayo imepangwa elimu ya awali, elimu ya msingi mpaka elimu ya Sekondari; sambamba na hilo, kuna suala zima la watoto wenye mahitaji maalum hasa *autism*: Je, ratiba hii inaenda sambamba na hayo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyasema?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tuna wanafunzi wenye mahitaji maalum na ambao wanahitaji muda mrefu zaidi kusoma kwa ajili ya kuweza kulingana na wenzao darasani. Njia mojawapo ambayo inatumika sasa hivi wakati wa kufanya mitihani kulingana na changamoto ambayo inafahamika, wanafunzi wanapewa muda tofauti wa kufanya mitihani. Vile vile katika mitaala mipya hii, hili suala limeangaliwa kutokana na maoni ya wadau ili kuhakikisha kwamba kweli tunatoa unyumbufu wa kutosha kuweza kuwa-*commodate* wale wanafunzi wenye mahitaji maalum hasa wakati wa kufundisha darasani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, sasa aulize swali lake.

Na. 414

**Kuongeza eneo la Skimu ya Umwagiliaji Mto Ruvu - Bagamoyo**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaongeza eneo na kuboresha Skimu ya Umwagiliaji ya Mto Ruvu – Bagamoyo?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Skimu ya Kisere ambayo ni miongoni mwa skimu katika bonde la mto Ruvu. Aidha, Serikali inaendelea na hatua mbalimbali za kubaini maeneo yanayofaa kwa ujenzi wa mabwawa ili kuhudumia skimu zilizopo katika bonde hili, kwani hii itaepusha changamoto ya ukosefu wa maji kwa wakulima kwa kuwa Mto Ruvu unategemewa kwa matumizi mbalimbali ikiwemo matumizi ya majumbani kwa wakazi wa ukanda wa Pwani na Dar es Salaam.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Muharami, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza. Bonde la Mto Ruvu katika sehemu ya Bagamoyo lina wakulima wengi sana ambao wanatokea Kata za Yombo, Magomeni na Makurunge: Je, ni lini sasa Serikali itawaombea wananchi hawa kupata eneo la Magereza ambalo ni kubwa na halina kazi yoyote inayoendelea ili waweze kufanya kilimo na kupata mahitaji yao?

Swali la pili. Mheshimiwa Waziri ni lini atakuja Bagamoyo kutembelea skimu ya umwagiliaji Ruvu inayojulikana maarufu kama *JICA* ili kuweza kuja kuzungumza na wakulima pale na kutupa matumaini kwa ajili ya kutengeneza skimu ile? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli pale kwenye eneo la Gereza la Kigongoni tunazo hekta zaidi ya 1,350 na kumekuwa na changamoto juu ya matumizi ya wananchi katika ardhi ya eneo hilo. Nachukua fursa hii kumwagiza Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji waende kukaa na uongozi wa gereza ili waone namna ambavyo wananchi wa kata ulizozitaja wataweza kushiriki kilimo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili la kuhusu kutembelea Bagamoyo baada tu ya vikao vya Bunge la Bajeti, mimi na wewe tutakwenda kuzungumza na wakulima ili tuweze kusikiliza changamoto zao na tuweze kuwatatulia ili wafanye kilimo cha umwagiliaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Je, ni lini skimu ya umwagiliaji ya Kwamtonga iliyopo

kwenye Kata ya Sungaji Wilayani Mvomero itafanyiwa uboreshaji kusudi wananchi wengi waweze kulima kwa mwaka mzima kwani maji ya kutosha yapo? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kiambatanisho Na. 8 katika bajeti ya Wizara ya Kilimo aliyosoma Mheshimiwa Waziri, tumeorodhesha skimu zote ambazo tutazifanyia ukarabati na ikiwemo skimu ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja. Nimwondoe hofu, hii kazi itafanyika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Skimu ya Umwagiliaji ya Ndungu, Jimboni Same Mashariki, imepoteza ubora wake kabisa. Ni skimu ambayo wananchi wanaitegemea sana katika Tarafa ya Ndungu: Je, Mheshimiwa Waziri ni lini utakuja kuiona ili uone pamoja na Mto Saseni? Vipo karibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ahadi ya Serikali kupitia Bunge lako Tukufu ambayo tuliitoa humu ndani kwamba tutakwenda kuzitembelea skimu hizo, lakini kabla sijafanya hivyo, nitamwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Umwagiliaji pamoja na wataalam wake wapite kwanza kuangalia, nami na Mheshimiwa Mbunge tutaongozana pamoja kwenda kuzungumza na wananchi na kutatua kero ambazo wananchi wanazo katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wananchi wa Ushetu wametenga hekta zaidi ya 5,000 ambazo ni nzuri na zina mtiririko wa maji kwa ajili ya umwagilijaji: Serikali inakuja lini kuwajengea skimu ya umwagiliaji wananchi wa Jimbo la Ushetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze Halmashauri kwa kutenga eneo kubwa hilo kwa ajili ya umwagiliaji. Maelekezo yangu ni kumwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kupeleka wataalam kwenda kuliangalia eneo hilo kama linafaa kwa ajili ya kuweka miundombinu basi, Serikali itahakikisha kwamba inaweka miundombinu katika eneo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Kata ya Litumbandyosi tulipata skimu katika bajeti hii. Ni lini sasa skimu hii inaenda kuanza ujenzi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu**.**

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bonde la Litumbandyosi ni kati ya mabonde 22 ambayo tarehe 20 mwezi wa tatu mwaka huu tulisaini mkataba na wakandarasi kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kazi hii inaendelea. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi hii inakamilika mwaka wa fedha huu ambao unaishia. Kuanzia Julai kazi itaanza ili

kuwafanya wananchi wako waweze kufanya Kilimo cha Umwagiliaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Halmashauri ya Mji wa Bunda inazungukwa na Ziwa Victoria na hatuna uhaba kabisa wa maeneo. Je, Mheshimiwa Waziri, ni lini mtatujengea skimu ya umwagiliaji ikiwa ni moja ya mkakati wa kuhamasisha vijana kujihusisha na kilimo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti yetu tumeeleza vizuri kabisa, maeneo yote ambayo yana vyanzo vya uhakika vya maji hasa ikiwemo mito na maziwa tutahakikisha tunawawezesha wakulima wa maeneo hayo kufanya kilimo kupitia umwagiliaji. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge juu ya eneo lake la Bunda, pia tutafanya kazi hiyo kuhakikisha kwamba wakulima wa Bunda wanafanya kilimo cha umwagiliaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu ya maswali kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Ninayo matangazo machache kwa asubuhi hii.

Wapo wageni waliopo Bungeni, kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Makame Mbarawa, Mbunge na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni 13 wa Mheshimiwa Jumanne Sagini, Mbunge na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ambayo ni Makatibu wa Wabunge wa Mkoa wa Mara, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni 35 wa Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, Mbunge na Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Waislam kutoka Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Joseph Tadayo, kutoka Mwanga Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wapo wageni 65 wa Mheshimiwa Miraji Mtaturu ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni saba wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni watumishi wa Mungu kutoka *Tumaini University* Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Muharami Mkenge kutoka Ujerumani na Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Maimuna Mtanda kutoka Newala Vijijini Mkoa wa Mtwara. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa ambaye ni Chifu wa Biharamulo kutoka Mkoa wa Kagera, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Edwin Swalle, Mbunge ambao ni Wachungaji, Padri na Makatibu wa Mbunge kutoka Lupembe, Mkoa wa Njombe, karibuni sana. *(Makofi)*

Yuko mgeni wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambaye ni Meneja Mahusiano wa *Maendeleo Bank* kutoka Jijini Dar es salaam, ahsante na karibu. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Santiel Kirumba ambao ni wafanyakazi wa Taasisi ya *Internal Perspective Foundation* kutoka Kahama, Mkoa wa Shinyanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Yuko pia mgeni wa Mheshimiwa Ali Mohamed ambaye Katibu wa CCM Tawi kutoka Shaurimoyo – Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Yuko mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi ambaye Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa kutoka Muhambwe, Mkoa wa Kigoma, karibu sana. *(Makofi)*

Yuko mgeni wa Mheshimiwa Bonnah Kamoli kutoka jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima kutoka Jijini Dar es Salaam, ahsante na karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni 35 wa Mheshimiwa Sylvia Sigula ambao ni wajasiriamali kutoka Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Jafari Chege kutoka Rorya Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Venant Protas kutoka Jijini Mwanza, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wapo wanafunzi 60 kutoka Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Mkoani Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wanachama 50 cha *Omega Champion* kikundi cha wazalishajimali kutoka Kata ya Mnadani Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wanawake tisa kutoka Jukwaa la Wanawake *Dodoma Gala,* karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wa hoja iliyoko mbele yetu ambayo ni bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Hapa ninayo orodha ya wachangiaji tutaanza na Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mheshimiwa Oran Manase Njeza atafuata na Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula ajiandae.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Mwneyekiti, kwanza nichukue fursa hii kuipongeza sana Wizara hii ya Ujenzi inafanya kazi kubwa sana. Sisi tumefanya ziara na Kamati, iko miradi mikubwa inayosimamiwa na *TANROADS*. Daraja la Kigongo – Busisi shilingi bilioni 716 fedha za ndani, kazi inaendelea vizuri sana. Iko barabara kubwa ya Kabingo – Kasulu – Manyovu kilometa 260.6 wakandarasi wako *site* na itafungua sana Mkoa wa Kigoma. Pongezi nyingi Wizara, Dkt. Samia Suluhu Hassan na wenzetu wa *TANROADS. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kule Jimbo la Ukonga na Dar es Salaam, barabara ya *BRT* Awamu ya Tatu, kuanzia Gongo la Mboto mpaka Kariakoo, mkandarasi yuko *site* na kazi kubwa ya mradi huu inafanyika, ni kazi ya kupongezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia maeneo matatu; eneo la kwanza ni reli katika ukurasa wa 74.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali, wakati Dkt. Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani kulikuwa na vipande

viwili vya reli ya *SGR* vinajengwa; Dar es salaam - Morogoro na Morogoro – Makutupora, lakini bajeti hii inavyowasilishwa hivi sasa tayari vipande vyote vitano vya kuanzia Dar es Salaam mpaka Mwanza kilometa 1219 vina wakandarasi, kilometa 506 Tabora – Kigoma ina mkandarasi yuko *site. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niseme jambo moja, Tanzania ndio nchi inayojenga reli ya *SGR* kwa gharama nafuu zaidi kuliko nchi zote Afrika. Wakati Tanzania iko kwenye dola milioni 4.3 kwa kilometa anayefuatia ana dola milioni 5.9 kwa kilometa, ni kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba hii haina eneo la ongezeko la bei, *whether* kuna *inflation* hakuna *variation,* bei iliyosainiwa kwenye mkataba ndio bei atalipwa mkandarasi mpaka mwisho. Hili linatufundisha nini? Linatufundisha kwamba suala kubwa kwenye miradi mikubwa ya ujenzi ni uadilifu na sio njia ya kumpata mkandarasi. Hizi nchi ambazo zinajenga kwa milioni sita, saba zilifanya *competitive bidding,* lakini Serikali ya Awamu ya Sita kwa njia yao ya *single source* bado ndio nchi ya Afrika ambayo inajenga reli kwa gharama ya chini zaidi. *(Makofi)*

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jerry, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kingu.

**TAARIFA**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mchangiaji kwamba anachokisema hata ukiangalia *BOQ* zilizotumika katika kujenga *standard gauge* bado mkandarasi ameshinda *tender* chini ya kiwango cha *BOQ* zilizopitishwa. Kwa hiyo, ninaungana naye kwamba gharama tulizozitumia Tanzania kujenga *SGR* ni gharama za chini ukilinganisha na mataifa mengi duniani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jerry, unaipokea taarifa?

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea, Mheshimiwa Kingu una akili nyingi, utafika mbali, una kitu ndani yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niseme tu amesema vizuri *engineers estimate* ziko juu kuliko gharama ya reli inayojengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ni eneo la bandari. Nchi yetu imepata kudra ya Mwenyezi Mungu ya kuwa *strategically geographically located,* kuwa nchi ambayo inahudumia nchi zaidi ya saba ambazo ziko *land locked.* Bandari yetu imekuwa na miradi mingi ya uboreshaji, Serikali imefanya lazi kubwa, lakini bado kuna suala la *efficiency.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo bandari yetu wale wageni wa Dar es Salaam wakifika pale *Coco beach* usiku wanaona taa kule baharini wanadhani ni majengo, kumbe ni meli zinazosubiri kutia nanga kutokana na masuala madogo tu kiutendaji ya *efficiency. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niishauri Serikali, yako mambo ambayo kuna watu wamebobea kuliko sisi. Tunapo *invest* kwenye miradi mikubwa masuala ya *operations* ni vema tukawaacha watu wenye tija kubwa ya *operation*, tija kubwa ya *investment* ili bandari iwe *efficient. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeisemea reli ya *SGR;* reli ya *SGR* ikikamilika itahitaji mzigo mkubwa sana wa kupeleka Mwanza, Kigoma na nchi za Jirani na itahitaji mzigo mkubwa sana wa kuja bandarini na bila kuwa na *efficient port* tutatkuwa tumefanya kazi bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo matatu; jambo la kwanza ambalo linatutatiza sana Watanzania ni ujuaji, yaani tunakuwa wataalamu kuliko wataalamu wenyewe kwenye baadhi ya mambo ya maamuzi ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni hofu; yaani mtu anakuwa na hofu ya jambo ambalo hajawahi kuliona na jambo la tatu ni imani. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuwe na imani na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, itupeleke kwenye uendeshaji wa bandari ambayo tija yake ndiyo itakuja kujenga shule, barabara, elimu na afya kwenye majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kudra ya biashara Mwenyezi Mungu hajaijalia. Tufanye yale ambayo tunaweza kuyafanya kwa ubora zaidi lakini yale mengine ambayo yanafanywa na *private sector,* tuwaachie *private sector*.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Jerry, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Catherine Magige.

**TAARIFA**

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mchangiaji anechangia kuwa bandari kubwa duniani ya Singapore inaendeshwa na sekta binafsi pamoja na Serikali na ndio tegemeo la nchi hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jerry, taarifa unapokea?

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea mwanangu Catherine, hii ndio inaitwa *beauty of brains,* mwanangu uko vizuri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ni *ATCL;* Shirika la Ndege la *ATCL* lilipotoka na lilipo sasa ni kazi kubwa sana ambayo Serikali imefanya. Shirika limetoka kwenye ndege moja leo tuna ndege 11. Shirika limetoka kwenye mapato ya bilioni 23 leo tuna mapato ya bilioni 254; Shirika hili linafaida nyingi. Leo Babu Tale enzi hizo yuko *Tiptop Connection* tunakuja na ndege hapa Dodoma nauli shilingi milioni moja. Leo kuna *flight* tatu zinakuja

Dodoma, leo kuna *flight* inakwenda Mpanda, watalii waliokuwa wanakwenda Mbunga ya Katavi walikuwa wanalazimika kukodi ndge leo wanakwenda kwa *commercial flight*. Shirika hili lina faida ya biashara, faida ya utalii, limeifungua nchi, linaitangaza nchi. Leo wapo Watanzania na wageni wanaokwenda kupata matibabu India, watu wanakwenda China wanapata *direct flight* kutoka nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukisoma vitabu vyake vya hesabu, sasa hapa ni eneo la kuwa makini, utasoma vitabu vya hesabu utaambiwa kuna hasara. Ni kweli? Ndio kuna hasara, hasara ni nini? Hasara ni *revenue* ukiondoa *expenditure* ndio unapata hasara. Kwa nini kuna hasara? Kuna hasara kwa sababu shirika hili linazo changamoto nyingi. Moja kati ya changamoto ni kukodisha ndege kutoka *TGFA* ambalo Serikali imeliona, Rais amelitolea maelekezo, Kamati yetu sisi tumekwishatoa mapendekezo hapa Bungeni na tukaazimia na Serikali inalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua zile *lease expenses* za *ATCL* ukaweka na zile *maintenance reserve* na *interest* za yale madeni, yuko Mbunge mmoja hapa jana ameomba Serikali iendelee kulipa yale madeni. Kwa gharama ya mwaka wa fedha 2021/2022 zaidi ya bilioni 89 zimetumika kwenye maeneo haya. Ukisema uondoshe zile gharama maana yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022 unaona hasara ya bilioni 35 kuna faida ya bilioni 54 kwenye Shirika hilo, tuwatie moyo. Mwenyekiti, wa Bodi Profesa Neema Mori anafanya kazi kubwa mwanamama huyu na wamesema hapa kwenye swali leo asubuhi wakina mama wakipewa nafasi hizi wanafanya kazi nzuri. *Engineer* Matindi na wenzake jana wametuletea hapa marubani. Shirika hili ni moja kati ya mashirika Afrika yenye watumishi ambao ni wazawa wa nchi zao. Tunao marubani wanawake, wako ma-*cabin crew* wazuri walikuja hapa ningewataja majina, lakini nitapata tabu nyumbani, lakini wanafanya kazi nzuri, tuwapongeze na tuwatie moyo shirika hili linakwenda kuifungua nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya ya kibiashara ni vema tunavyoyafanyia *analysis,* tuyafanyie *analysis* kwenye

uwanda mpana zaidi kuliko kuangalia *items* chache kwenye *financial statements* ambazo zinaweza zikakatisha tamaa watu wanaolitumikia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini Serikali kwenye bajeti hii imesema inanunua ndege nne mpya. Ndege hizi zikija na hizi zilizopo na matatizo haya yakitatuliwa, matatizo ya *Covid* yamekwisha, shirika hili linakwenda kuingiza faida na kuwa shirika kubwa sana hapa nchini. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jerry, ahsante sana.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nusu dakika niseme tu kwamba hata hiyo mikataba ya kukodisha ndege ni mikataba ile ambayo inakwenda kwa *style* ile ya Mandonga. Ndege ikiruka inalipa, ndege isiporuka inalipa. Kwa hiyo, kipindi cha *Covid* wakati ndege ziko chini, zilikuwa zinaingiza hasara kwa matumizi makubwa ya *lease* wakati mapato ya tiketi na usafiri yalikuwa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana naunga mkono hoja, naipongeza Wizara hii, niwatie moyo waende wakatekeleze majukumu yao. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jerry, ahsante sana tunashukuru sana. Mheshimiwa Oran Manase Njeza, atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, ajiandae.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Wizara hii muhimu ambayo inafanya kazi nzuri. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kweli kwa kazi nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri nakupongeza ulipokuja Mbeya uliweza kutusainia mkataba wa barabara muhimu ya njia nne kuanzia Uyole mpaka Songwe licha ya wewe unasema kutoka Uyole

mpaka Ifisi. Mheshimiwa Waziri hiyo ni hatua nzuri sana. Kwa sababu uchumi wa Tanzania kwa kiasi kikubwa unategemea zaidi barabara hizi za *TANZAM*. Vilevile jana umeongelea kuhusu kujenga barabara hiyo ya *TANZAM,* kipande cha Igawa mpaka Tunduma kwa *EPC + Finance*. Hiyo ni hatua muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri, alipokuwa anasaini mkataba pale Mbeya aliwaahidi wananchi wa Mbeya Vijijini kuwa bajeti hii atahakikisha kuwa barabara ya Mbalizi – Shigamba inakuwemo kwenye bajeti hii ili ijengwe kwa kiwango cha lami. Mheshimiwa Waziri ninakuamini sana na ninaimani kabisa kuwa ile ahadi yako kwa wananchi sio wa Mbeya tu, lakini Tanzania nzima ni ahadi muhimu utaitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri kuna bartabara ambazo ni kiunganishi kikubwa kwa nchi zetu zinazotuzunguka Malawi pamoja na Zambia, lakini na kulisha uwanja wa ndege. Kuna barabara Isyonje – Kikondo – Makete ni barabara muhimu sana. Mheshimiwa Waziri hebu chukulia hiyo umuhimu wa kipekee na kuipa kipaumbele ili iweze kujengwa haraka. Kwa sababu uchumi wa mikoa yetu Mbeya, Njombe, Ruvuma na Iringa inategemea zaidi usafirishaji wa mizigo ili iweze kubebwa na kupelekwa nje na Tanzania iweze kupata pesa za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini barabara nyingine ambayo ni muhimu ni barabara ya Mbalizi – Chang'ombe – Mkwajuni kwenda mpaka Makongorosi. Kwa umuhimu wake namuona Mheshimiwa Mulugo amekuja kukaa hapa karibu ili nisije nikasahau kuizungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri hii barabara ni ahadi ya muda mrefu sana, lakini imekuwa haipewi umuhimu. Nakuomba sana katika bajeti hii, barabara hii ipewe kipaumbele cha pekee iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumzia umuhimu wa nchi yetu kijiografia. Kiushindani Tanzania Mwenyezi Mungu ametupa neema ya sisi kiushindani akatupa jiografia nzuri, tuna bandari, tuna maziwa, lakini bado hatujazitumia vizuri hizi kwa upendeleo ambao Mwenyezi Mungu ametupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari yetu ya Dar es Salaam ufanisi wake ukilinganisha na bandari nyingine inawezekana sisi ni wa pili kutoka mwisho na wa mwisho nafikiri ni Mogadishu – Somalia. Sasa hatuwezi kuanza kujilinganisha namna hiyo. Tuchukue hatua za haraka ili tuboreshe ufanisi wa bandari yetu. Pia sio kuboresha bandari tu lakini tuboreshe na reli zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali na Mheshimiwa Rais kwa pesa nyingi alizozipeleka kwenye *SGR*, lakini tunakuomba Mheshimiwa Waziri, kwa umuhimu huo huo hebu iboreshe Reli ya *TAZARA*. Reli ya *TAZARA* ni muhimu sana kwa ushindani wa Bandari yetu ya Dar es Salaam, lakini vilevile Bandari ya Katanga kwa ajili ya soko la *DRC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunapoteza biashara zetu kwa kiasi kikubwa kwa nchi jirani kwa bandari jirani kutokana na ufanisi tulio nao kwenye bandari yetu ya Dar es Salaam. Mfano mdogo tu, kwa kupitisha mizigo yetu Zambia, Tanzania inapoteza karibu shilingi bilioni 60 kwa kipande hicho tu cha Tunduma mpaka Zambia ili mzigo ufike Congo, hii sio pesa ndogo. Pesa hii ukiijumlisha kwa miaka mitano inatosha kabisa kuboresha Bandari ya Katanga na hata kujenga barabara kwenda Lubumbashi. Hiyo itaongeza ufanisi na vilevile itanongeza ushindani.

Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, toa umuhimu kwenye Bandari yetu ya Dar es Salaam ipate wawekezaji wazuri na biashara sio ifanye Serikali, biashara tuwaachie watu binafsi. Mfano ni *TAZARA* watu binafsi wafanya vizuri na *TAZARA* imepata pesa nyingi kwa sababu ya wale watu mliokodisha wafanye biashara ndogo ya *TAZARA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna changamoto nyingine ambazo ziko bandarini kutokana na ufinyu wa bandari yetu. Mimi

binafsi naona Bandari ya Bagamoyo itatuweka Tanzania mahali pazuri zaidi na tusifikirie kujenga wenyewe, tufikirie uwekezaji wa wenzetu kwa *PPP*. Ninaimani bandari ya Bagamoyo ambayo ina kina cha asili cha mita 18 ina uwezo wa meli kubwa kuja Tanzania zenye ukubwa wa mpaka mita 400. Hiyo itatufanya sisi tuweze kufanya biashara vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile nilikuwa naangalia Shirika letu la Ndege la Tanzania; wenzangu wameongelea ni namna gani tuliweke katika *position* ambayo inaweza kufanya vizuri zaidi. Mimi ningejikita zaidi kuhakikisha kwamba tuna nunua ndege za mizigo, lakini tunajenga viwanja vya ndege vingi zaidi na hivyo vilivyopo tuviboreshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nakuomba Serikali inunue ndege za ziada za mizigo ili mizigo yetu iweze kufanya vizuri kwenye soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Njeza. Mheshimiwa Stanslaus Mabula, atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilonga Malecela, Mheshimiwa Munde, ajiandae

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi angalau kwa dakika chache niweze kusema mambo yafuatayo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mungu kwa kunipa nafasi lakini la pili na mimi nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ya kipekee ambavyo amekuwa mtu mwema sana katika kuhakikisha kwamba fedha nyingi zinazokwenda kwenye miradi zinasimamiwa na zinatekeleza miradi ambayo imekusudiwa. Na hakika, kama mwenyewe anavyosema, hakuna mradi uliosimama kila mradi uliokusudiwa unaendelea na tumekuwa na miradi bora sana. Nimshukuru kwa kuhakikisha ya kwamba tunavyozungumza kama wenzangu waliokwisha kupita

wamesema; ukitazama Daraja la Busisi ambalo linaunganisha Mkoa wa Mwanza na mikoa mingine ya Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale kwenye bandari utakuta kuna meli kubwa ambayo itakuwa ni meli ya kipekee katika ukanda wa maziwa makuu; *MV.* Mwanza, ambayo kwa hakika iko hatua za mwisho kabisa kukamilika. Ukitazama *standard gauge* ambayo inaanzia Mwanza kwenda isaka nataka nikuhakikishie kwamba miradi hii yote inatekelezeka na iko, wakandarasi wako kazini, na hakika wanafanya kazi nzuri sana. Ba hii peke yake imefanya Mji wa Mwanza kuwa *busy*, Mji wa Mwanza kuwa mji ambao unampishano wa watu kila mara na kwa wingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? tafsiri yake ni kwamba uchumi unaojitokeza kwenye uendelezaji wa miradi unaotoa ajira nyingi kwa vijana tafsiri yake ni kwamba kukamilika kwa miradi hii kunaifungua mkoa wa Mwanza kunaifungua Kanda ya Ziwa na kufanya sasa mji huu uendelee kuwa mji wa pili mashuhuri na kwa ukubwa katika nchi hii katika kuhakikisha kwamba miradi hii inakuja kuleta tija kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusudi hilo nataka nimuombe Mheshimiwa Waziri mambo mawili peke yake. Kama tunazungumzia miradi yote hii na haina muda mrefu inakwenda kukamilika tunao Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Mheshimiwa Waziri nikuombe sana, unapozungumza ujenzi wa Daraja la Busisi, unapozungumza ujenzi wa *SGR* kutoka Mwanza kwenda Isaka unapozungumza uboreshaji wa bandari na ujenzi wa meli kubwa tafsiri yake ni kwamba Mji wa Mwanza unakwenda kuwa mji wa kitalii lakini unakwenda kuwa mji wa biashara asilimia 100. Hivyo nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, ninafahamu, ujenzi wa uwanja wa ndege, njia ya kukimbila ndege imeshakamilika lakini hivi tunavyozungumza ni aibu sana kuendelea kusema tuna jiji la pili kwa ukubwa lakini bado tuna uwanja wa ndege unaoweza kupokea ndege za kwetu za ndani peke yake na si ndege za mashirika mengine makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu Halmashauri za Jiji la Mwanza na Manispaa ya Ilemela zilianza mchakato wa ujenzi wa jengo la abiria lakini ukweli, ni kwamba Mheshimiwa Waziri na wewe utakubaliana na mimi haiwezekani imefika sehemu zimegota na sio jukumu lake kimsingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukuombe Mheshimiwa Waziri kama ambavyo tumekwisha kuzungumza uwanja huu wa ndege urudi *TAA* usimamiwe na wataalamu wenyewe na hazi halmashauri mbili kwa sababu mpaka sasa zimeshagharamia takribani shilingi bilioni nne fedha hii baada ya kuwa uwanja huu umerudi na jengo hili limechukuliwa zitatazamwa kwenye namna nyingine ili ziweze kupata *share* na zenyewe ziweze kufaidika na mapato haya ya ndani kwa sababu ni kodi za wananchi zimepelekwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunasema uwanja wa ndege wa Mwanza? Leo ukitazama unapokea abiria zaidi ya milioni moja kwa mwaka lakini majengo yanayosubiri abiria, maeneo ya kupumzika, maeneo ya kusubiri kuondoka na kuingia hakika hayafanani kabisa na ule uwanja ulivyo hivyo nikuombe sana Mheshimiwa Waziri halmashauri hizi zimesharidhia ziko tayari ni kazi kwako kuhakikisha ya kwamba uwanja huu unauchukua na unauboresha kwenye mazingira ambayo yatafanya uwe uwanja wa kimataifa ndege kubwa zije ili na sisi tuweze kuona faida ya kuruka kutoka Mwanza moja kwa moja kwenda Dubai na maeneo mengine duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu barabara, Mheshimiwa Waziri unafahamu tunayo barabara moja kubwa ya Kenyatta na ya Nyerere. Barabara ya Nyerere na ya Kenyatta ni barabara ambazo zinapitisha abiria wengi sana ukiitaja kwa mfano barabara ya kenyatta peke yake abiria wote wanaoingia Mwanza kutokea Mikoa ya Dar es salaam na mikoa mingine yote ikiwemo mikoa inayounganishwa na Daraja la Busisi wanatumia barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni nini? Barabara hii imekuwa finyu na haina tena uwezo wa kuwahudumia wakazi

wanaokuja Mwanza. Kwa hiyo ninachokuomba Mheshimiwa Mbarawa barabara hii ilishafanyiwa upembuzi yakinifu kwa njia nne na ulishakamilika siku nyingi, basi tuitazame kwa jicho la pekee na tuanze kuijenga angalau hata kwa kilometa kumi kwa mwaka wa fedha ujao, itakuwa imesaidia sana kuondoa changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakazi peke yake wa Mwanza wanaokadiriwa laki sita na sehemu nusu ya wakazi wa Mwanza wanatumia barabara hii, hapo hujawataja wageni. Barabara ina uwezo wa kuchukua magari zaidi ya 3,000 mpaka 6,000 kwa siku hii siyo jambo dogo, ni jambo kubwa, hivyo ni lazima tulitazame kimahesabu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hiyo tu, Mheshimiwa Waziri tumezungumzia namna ya kuipandisha hadhi barabara inayotoka Mkuyuni inapita Kanyenyere inakwenda Tambuka Reli inakwenda mpaka Nyanguruguru inakwenda kutokea Mandu na Mahina. Barabara hii ni muhimu sana kwa wakazi wa Jiji la Mwanza na ni muhimu sana kwa Mkoa wa Mwanza kwa sababu itasaidia kwenye maeneo mengi ambayo tunayategemea mno kwa ajili ya kuwavusha wananchi kwenda kwenye shughuli zao za kiuchumi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja, na ninaipongeza Wizara ya Ujenzi na taasisi zake zote kwa kazi nzuri wanayoifanya, na Mungu aendelee kuwasaidia kulitumikia Taifa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe, Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, ajiandae.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata muda, naomba leo niongee kwa kifupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kusema ukweli; hakuna awamu ambayo imejenga barabara katika nchi yetu kuzidi awamu ya sita. Hakuna mahali ambapo sasa hivi hapajengwi barabara. Ukienda mijini barabara zinajengwa, ukienda vijjijini *TARURA* wanafanya kazi ya kujenga barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nichukue nafasi ni kwa mara nyingine niishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Sita, na niipongeze kwa kujenga barabara nchi nzima. Nimalizie kwa kusema kwamba Tanzania iko *busy* sana sasa hivi kwa miradi ya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, nirudi kwa Mheshimiwa Waziri Mbarawa. Hii Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, hii ni Wizara pana sana, ni Wizara ambayo ina shughuli nyingi sana. Amesema Mheshimiwa Mbunge jana pale, hii Wizara ina taasisi 22. Tuchukue taasisi moja tu ambayo nashukuru Waheshimiwa Wabunge mmiongea sana; taasisi ya *TPA* (bandari).

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari ni lango kuu la uchumi, na kweli kabisa; mimi niwapongeze Waheshimiwa Wabunge, mko *very positive* na kupata wawekezaji wa kusaidiana na Serikali upande wa bandari. Iwapo ile bandari tutaitumia vizuri, Serikali itaangalia vizuri na sisi Wabunge tukaridhia tunakwenda kukomboka, kukombolewa nchi yetu na Bandari ya Dar es salaam pamoja na bandari zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi huwa na-*google* sana na kuangalia, ukienda India tukubali Waheshimiwa Wabunge kwamba Wahindi ni wachumi wazuri; wenzetu India wametengeneza Wizara maalum ya bandari ambayo inaitwa *Ministry of Ports Shipping and Water Ways.* Wametengeneza Wizara maalum kwa ajili ya bandari kwa sababu wanajua uchumi uko kwenye bandari. Mimi nimesema tu sijasema zaidi ya hapo Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi jimboni kwangu sasa. Mheshimiwa Waziri nakupongeza tena, nimesikiliza hotuba yako vizuri mno niende kwenye kifungu chako cha namba 106 ulipoongelea barabara yangu ya Mkomazi – Kisiwani – Same. Naomba nikushukuru, si mimi wananchi wa Jimbo la Same Mashariki wamenituma, Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana, Waziri Mbarawa tunakushukuru sana. Tunakupongeza kwa sababu hii Serikali ya awamu ya sita imesikiliza kilio cha wananchi wa Jimbo la Same Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Same Mashariki silisemei kwa ukubwa, kwa ukorofi, tarafa mbili zote ziko milimani, narudia zinalima Tangawizi asilimia 72 ya tangawizi ya nchi nzima. Tarafa ya chini, Tarafa ya Ndungu inalima Mpunga, inalima inalisha Kilimanjaro inalisha Tanga. Lakini tulikuwa tunaponzwa na barabara ya Mkomazi – Kisiwani – Same Mheshimiwa Waziri tunakushukuru wananchi wamenituma nikushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu la 116 limeniambai kwamba barabara ya Mkomazi - Kisiwani - Same sasa imepata wakandarasi wawili na inajengwa kwa kiwango cha lami kilometa zote 97. Mkandarasi wa kwanza anaanza Same – Kisiwani – Mroyo kilometa 56.83 Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana, mkandarasi wa pili anaanzia Ndungu – Mkomazi kilometa 36. Mikataba hii itasainiwa mwezi wa sita, ambao ni mwezi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie kabisa Mheshimiwa Waziri kwamba wananchi wameshona nguo, wanaume wameshona suti, wanawake wameshona vitenge; tutakuwepo kwa wingi sana mwezi wa sita utakapo kuja kwa ajili ya kusaini mikataba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi wananchi wa Same mashariki huu ni ukombozi mkubwa. Jimbo hili lilizaliwa mwaka 1995, Mbunge wa kwanza alikuwa ni Daniel Yona, alizungumza akiwa Waziri, huku akiwa Waziri alifanya kazi kuhusu barabara hii. Nikaingia mimi kwa kipindi cha miaka kumi kila wakati nazungumzia barabara hii. Akaingia mdada pale alipoingia naye akazungumza, na mimi nikaingia saa hiyohiyo nikawa Mbunge wa

kuteuliwa nikasimama imara nikizungumzia barabara hii, nimerudi sasa nazungumzia barabara hii; lakini awamu ya sita tunaishukuru imetusikia imetupa barabara hii, ahsante sana, ninaishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nazungumza kwa uchungu sana kuhusu Dar es salaam. Nazungumza kwa uchungu kuhusu Dar es salaam na ninaomba Serikali mnisikilize vizuri. Dar es salaam yalikuwa ndiyo makao makuu ya nchi yetu tangu tumeitwa nchi. Awamu ya tano ndiyo imekuwenda kufanya kimatendo kuhamisha makao makuu kutoka Dar es salaam kuja Dodoma tunashukuru sana. Lakini, Dar es salaam inajengwa barabara nzuri, lakini Dar es salaam inatatizo kubwa mvua zinaponyesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali inisikilize, siitumi, inisikilize. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aandike historia, aandike historia ya kuitoa Dar es salaam kwenye matatizo ya maji wakati wa mvua. Kwa nini nasema hivyo? Sisi tuna ma-*engineer* wengi sana. Ukienda *TANROADS* yenyewe ina ma-*engineer* 306 walioko kwenye ajira za kudumu. *TANROADS* hiyo ina Ma-*engineer* 238 walioko kwenye ajira za mikataba. Hivi wananshindwaje hawa Ma-*engineer* kukaa chini wakatumia Elimu yao wakaondoa lile tatizo lililopo Mkoa wa Dar es salaam?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Dodoma ni makao makuu, lakini hata kama Dodoma ni makao makuu, Dar es salaam itaendelea kuwa mji mkuu wa kibiashara na Tanzania tukubaliane kwamba Dar es salaam bado itaendelea kuwa ni jiji ambalo linavuta watu na linapendeza mpaka mwisho wa maisha ya kuishi huku duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naiomba Serikali kipindi hiki cha Mama Samia Suluhu Hassan asimalize kipindi chake hiki cha kwanza kabla hajatatua tatizo la maji yanayotuama, yanayojaa na kukosa njia kiasi kwamba wananchi wanashindwa kuendesha magari mimi juzi alipokuja Makamu wa Rais nilishtuka nikasema atashindwa kupita akitoka *airport*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona nimegongewa kengele lakini naiomba Serikali itumie Ma-*engineer* wote tulionao kipindi hiki hiki cha Mama Samia cha kwanza iondoe matatizo ya Mkoa wa Dar es Salaam. Ma-*engineer* tumieni elimu yenu Mheshimiwa Mbarawa una ma-*engineer* wengi kaeni muangalie hili tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Paramagamba Kabud, Mheshimiwa Hassan Mtenga, ajiandae.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambazo anaendelea kuzifanya kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kwa kweli ataacha alama kubwa kwenye nchi yetu kwa kipindi chake cha miaka kumi. Kama tu sasa anamiaka miwili amefanya mambo makubwa sana kama vile amekaa miaka mitano au sita na-*imagine* akikaa miaka kumi atafanya mambo mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameweza kupigana na miradi mikubwa ya mikakati, ameweza kwenda nayo sambamba kiasi kwamba tumeona juzi amekamilisha Ikulu lakini anaendelea na Bwawa la Mwalimu Nyerere anaendelea na *SGR* anaendelea na meli ameenda kwenye ununuzi wa ndege, ananunua ndege nne, lakini analipa madeni ya ndege zilizokamatwa na Daraja la Busisi, Daraja la Tanzanite *(Salender Bridge)* yote hayo ni mambo makubwa na mengine mengi aliyoyafanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona madarasa lukuki yamejengwa bila mchango wowote kwa Watanzania kaya kwa kaya wala nini kwa nini, amefanya yeye kama Rais amesimama wima. Amepeleka pesa nyingi za kutosha kwenye halmashauri zetu. Wakati huu mgumu wa *Corona*, wa vita ya Urusi na Ukraine majirani zetu wanashindwa kulipa mishahara, Mheshimiwa Samia analipa malimbikizo ya watumishi, Mheshimiwa Samia ameahidi kuongeza mishahara ya watumishi; hakika ana haki ya kupongezwa. Na ndio maana kuna siku nilichangia hapa nikasema Mheshimiwa Rais Samia wale wenzetu wa upande wa pili wana haki sasa ya kumpa heshima ya kumwachia apite bila kupingwa kwa kazi kubwa ambayo anaifanya Mheshimiwa Rais anastahili kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi zangu za dhati kwa Wizara ya Ujenzi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Wakurugenzi wake wote wa taasisi akiwepo Katibu Mkuu na Menejimenti nzima. Tunawapongeza sana kwa kazi zote zinazoendelea nchi nzima kila mtu ukizunguruka kazi zinaendelea kufanyika tunaziona na tunawapongezeni sana sana. Kaka yangu Mbarawa hana maneno mengi lakini vitendo vyake ni vikubwa tunakupongeza sana kwa kazi nzuri unazozifanya

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri, akiomba ridhaa ya kuingia ubia kwenye bandari yetu. Nikwambie Mheshimiwa Mbarawa kanyaga twende tumechelewa sana, huu ni usemi alikuwa anapenda kuutumia marehemu kaka yangu Le Mutuz anakwambia kanyaga twende tumechelewa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbarawa tumechelewa. Kwa nini nasema tumechelewa? Wenzangu waliotangulia kusema wamesema kontena lina toka *China* mpaka Dubai kwa dola 500 lakini Kontena hilo linatoka Dubai mpaka Tanzania kwa dola 4500. Hiyo ni gharama ambazo wafanyabiashara wataendelea kuilaumu Serikali kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie, Serikali haiwezi kufanya biashara. Hivi, *crane* moja tu likiaharibika linatengenezwa

kwa dola elfu 18 utaambiwa kaa pale dokezo linaandikwa kwa Waziri dokezo linapelekwa kwa Katibu Mkuu, dokezo linaenda kwa Mhasibu, mtandao leo umekwama haufanyi kazi, yaani ni mambo ambayo hatutaweza kama Serikali, tutaendelea kulaumiwa; lakini tutaendelea kupata kodi ndogo ambayo itakuja kuwaumiza wafanyabiashara ili Serikali itimize malengo yake. Lazima kama Serikali ibuni vitu vya kuweza kupata kodi nyingi ili kupunguza kodi kwa wafanyabiashara wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni wajibu wa Serikali na siyo mtu mwingine yoyote kuhakikisha kodi inapatikana lakini walipakodi hawaumii. Leo walipakodi wanaumia tumeona mkutano wa Kariakoo wamelalamika mambo mengi na yote hii ni kwa sababu hatuna vyanzo vingi vya kukusanya kodi leo hii Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Rais ame-*organize* tukaenda kwenye *Expo Dubai*, wameenda kusaini mikataba chungu mzima ili tupate wawekezaji watusaidie. Leo Mheshimiwa Mbarawa amethubutu kupata mtu wa kuingia ubia na sisi tunaomba jambo hili liende kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Mawaziri wote, tulikuwa wote Dubai mimi nilienda. Wameingia mikataba waendelee kufuatilia wapate wawekezaji ili nchi yetu izidi kupiga hatua. Jambo hili sio geni linafanyika dunia nzima, sio kwetu sisi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie kitu, nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Kilimo lilikuja suala kwamba mazao ya *horticulture,* mbogamboga na matunda yanasafirishwa kupitia Mombasa. Yanatoka Arusha, parachichi zinatoka Njombe, zinawekwa kwenye magari zinakwenda Mombasa, tukagombana na Waziri na Mkurugenzi wa *TAHA* tukawaambia kwa nini msisafirishe na Bandari ya Dar es Salaam? Dar es Salaam wakatuambia hakuna *facilities* za kusafirisha mbogamboga, ni aibu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashindwa kutafuta wabia au kitu gani? Nashindwa kuelewa, lakini tunaona kwamba Mheshimiwa Rais ameifungua nchi ni sisi tu wenyewe. Leo hii parachichi zinatoka Njombe zinapelekwa Mombasa, Mombasa

ndio wanapakia kutupelekea nje ya nchi, ndio maana wananchukua vitu wanavi-*label* Kenya, tunaonekana sisi hatuna kitu chochote, vitu vyote vinatoka Kenya. Niwaambie hivi, katika hili linalofanyika la kwenda kuingia ubia, tutakwenda kuweka heshima kubwa ya nchi yetu ambayo Mheshimiwa Rais ameitengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii dunia nzima wanamuongelea Samia Suluhu Hassan, dunia nzima anaongelewa, anaonekana Rais mahiri, Rais mwanamke wa mfano, lakini leo tunachukua mazao tunapeleka Mombasa, hiki ni kitu gani? Tunaomba sana ikiwezekana huyo Mbia aingie na Tanga, Mtwara na Bandari ya Bagamoyo ijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa nchi hii utapanda lini ikiwa malighafi inasafirishwa kwenye vitu vya bei kubwa. Mtu akifikisha hapa malighafi ya kiwanda amefikisha kwa bei kubwa, akitengeneza kitu lazima akiuze kwa bei kubwa ili na yeye apate fidia na aweze kulipa kodi, lakini leo hii tukiingia ubia malighafi zetu zitafika kwa bei nzuri, wafanyabiashara wetu wakulima watasafirisha mazao yao kwa bei nzuri, watapafa faida kubwa lakini nchi itapata kodi, ikipata kodi mambo yatazidi kwenda vizuri zaidi. Nilikuwa napitia wanasema tukiweza kuingia ubia na hiyo kampuni ya DP tunaweza tukaingiza trilioni moja kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuombe sana na baadaye sisi tulimbana Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe angekuwa hapa angesema. Tukamwambia je tukipata hizo *facility* wanaweza wakapita Tanzania badala ya Mombasa? Akasema haiwezekani. Tumefanya *research* wakipita Tanzania hata kama tungekuwa na hizo *facility* wangelipa asilimia ya faida yao ingeenda asilimia 25 zaidi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tambwe muda wako umeisha.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniongeze dakika moja nimalizie jambo moja.

**MWENYEKITI:** Malizia sekunde 30, tafadhali.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongee kuhusu Tabora Manispaa. tunaomba barabara ya *ringroad* inayozunguka Tabora kuchepusha magari. Sasa hivi Tabora imefunguka magari yote yanayokwenda Kigoma, Rwanda, Congo, Sikonge, Mpanda, Mbeya yakipita katika ya mji utakuwa msongamano mkubwa. Tumekaa kama *Board Road,* tumekubaliana tuweke *ringroad,* magari haya yatachepushwa nje ya Mji wa Tabora Manispaa kuepusha ajali, lakini kuepusha msongamano mkubwa utakaojitokeza. Tunaishukuru sana Serikali kwa kutufungulia mkoa wetu, lakini tunaomba bado watusaidie hili ili kupunguza ajali na kupunguza misongamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi atafuatiwa na Mheshimiwa Mtenga na Mheshimiwa Aeshi Khalfan Hilaly ajiandae.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Rahim* kwa ruzuku ya uhai na afya. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi; Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya, Naibu Waziri Ujenzi; Mheshimiwa Atupele Mwakibete Naibu Waziri Uchukuzi; Balozi Mhandisi Aisha Amour, Katibu Mkuu Sekta ya Uchukuzi; Bwana Gabriel Migire, Katibu Mkuu Sekta ya Uchukuzi; Bwana Ludovick Nduhiye, Naibu Katibu Mkuu Ujenzi na Dkt. Ally Possi, Naibu Katibu Mkuu Uchukuzi. Nawapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya katika Sekta hii muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu na kwa ustawi wa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba yangu na ya wananchi wote wa Jimbo la Kilosa, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa fedha nyingi za kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika Jimbo la Kilosa. Tunamshukuru sana kwa mabilioni ya fedha ambayo ameyaleta Kilosa kujenga barabara na madaraja kupitia *TARURA* na *TANROADS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TARURA* tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutupa shilingi bilioni nane na milioni 300 kwa ajili ya kujenga Daraja la Berega ambalo litaunganisha Wilaya ya Kilosa na Wilaya ya Kilindi ya Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kupitia *TARURA* kutupa shilingi milioni 500 kujenga Daraja la Masombawe kule Mamboya, lakini shilingi milioni 800 kujenga Barabara ya Mvumi – Ngege ambaye baadaye itatuunganisha na Wilaya ya Gairo, lakini Barabara ya Parakuyo shilingi bilioni 150 na pia kutoa shilingi milioni 800 kwa ajili ya ukarabati wa barabara na mifereji katika Mji wa Kilosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TANROADS,* namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutupa shilingi 4,714,000,000 kwa ajili ya kumalizia Madaraja ya Kobe, Kwa Ilonga na Mazinyungu na madaraja haya yatakapokamilika sasa Barabara ya Dumila – Ludewa – Kilosa itakuwa imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika sana kuona katika ukurasa wa 287 wa bajeti ya sasa kwamba Wizara imetenga fedha kwa ajili ya *feasibility study* na *detailed design* ya Daraja la Mto Mkondoa. Daraja hili ambalo liliondolewa na mafuriko ni daraja muhimu sana na hasa ukizingatia kwamba kwamba sasa tutaanza kujenga Barabara ya Kilosa – Ulaya – Mikumi na daraja hili ni muhimu na kwa muda wote huu tulikuwa tunatumia daraja la reli kuvuka Mto Mkondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi yangu kwa Serikali kwamba *feasibility study* hii na *detailed design* isihushishe Daraja tu la Mto Mkondoa, lakini lihusishe Kingo yote ya Mto wa Mkondoa kuanzia Mkadage kwenye Daraja la *SGR* mpaka Magomeni ili kuimarisha kingo za Mto Mkondoa unaohamahama lakini pia kuzuia mafuriko kwa ajili ya Mji wa Kilosa. Ifahamike Wajerumani walipojenga reli ya kati walijenga mabwawa matano ya punguza ikiwa ni pia pamoja na Bwawa la Kidete. Naomba pia bwawa hili Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Wizara ya Kilimo washirikiane ili Bwawa hili likikamilika litakuwa kinga nzuri kabisa ya mafuriko kwa Mji wa Kilosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuomba ujenzi wa Reli ya Kilosa – Kidatu kama ilivyoainishwa katika bajeti ufanyike. Reli hii ni muhimu sana kuunganisha Kilosa, Mikumi na Kidatu. Itaunganisha reli ya kati na reli ya *SGR* kutoka Kilosa kwenda mpaka Mlimba ambako itaunganisha na reli ya *TAZARA*. Maombi yangu huko mbele ya safari ikiwezekana reli yote hiyo ya Kilosa – Mikumi mpaka Mlimba ama iwe ya *cape gauge* au iwe ya *SGR* ili kurahisisha usafiri wa mizigo kati ya Reli ya *TAZARA* na Reli ya *NGR* na Reli ya *SGR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii sasa kuzungumzia maombi mengine ambayo nayaomba na hii ni ya ujenzi wa lami wa Barabara ya Chanzuru kupitia Kimamba kupitia Parakuyo kupitia Mkata *station* kwenda Melela. Barabara hii itakamilisha mzunguko wa Barabara ya Melela kuja Kilosa, Kilosa kwenda Mikumi na hivyo kuongeza ufanisi wa usafiri katika eneo hilo na kuufanya Mji wa Kilosa sasa kuwa ni Mji wa Kimkakati katika usafarishaji na uchukuzi nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha *G7* kilichofanyika Hiroshima Japan, Serikali ya Marekani imetangaza kupitia *Parternship for Global Infrastructure and Investment,* kwamba itatoa fedha sasa kufufua Reli ya Benguela *the* Lobito *Corridor* maana yake kutoka Ndola kwenda Lubumbashi kwenda mpaka Lobito. Huu ndio wakati sasa na wao wamesema wanaweza pia kuiunganisha Tanzania. Sasa tunapata fursa ambayo ni vizuri tukaitumia vizuri ya kuunganisha Bahari ya Hindi na Bahari ya

Atlantic na ukiiangalia Afrika ni nchi mbili ambazo zinaunganisha bahari hizi mbili yaani DRC na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa reli hii itakapoanza maana yake tunaweza tukaitumia fursa hiyo vizuri kutoa mizigo Dar es Salaam mpaka Lobito ikaenda Marekani na Nchi za Carribean na kutoa mizigo kutoka Nchi za Carribean zikaingia Lobito zikaja Dar es Salaam kwenda Nchi za Asia na Nchi za Mashariki ya Mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake nini? Ni lazima sasa tuimarishe Reli ya *TAZARA* ili iwe na ufanisi mkubwa sana bila kufanya hivyo ina maana mizigo mingi ya *DRC* na mizigo mingi ya Zambia sasa itakwenda Bandari ya Lobito badala ya kuja katika Bandari zetu za Tanzania. Kwa hiyo, tuna umuhimu wa kuongeza ufanisi wa bandari zetu, tuna umuhimu wa kuongeza ufanisi wa Reli ya *TAZARA* ili badala ya kupoteza mizigo, sasa tuweze kuunganisha Bahari ya Antlantic na Bahari ya Hindi kupitia bandari zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bandari hizi tusiimarishe Dar es Salaam tu. Tuimarishe Tanga, Mtwara na tuanze kujipanga kujenga bandari nyingine zaidi na katika bandari hizi ambazo tuzifikirie kuzijenga iko bandari moja tusiiache kuifikiria ni Bandari ya Kilwa. Tumeamua sasa Kilwa iwe Bandari ya Uvuvi, lakini tuangalie uwezekano wa baadaye Kilwa kuwa bandari ya mizigo mingi. Bandari ya Kilwa ina historia ndefu toka wakati wa Ibni Batuta na ndio bandari pekee katika upande huu wa magharibi wa Bahari ya Hindi yenye kina kirefu cha asili na ina milango miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo miaka ijayo *Insha Allah* Bandari ya Kilwa ndio inaweza kuwa Bandari ya *trust shipment* ya meli kubwa kuingia kushusha mizigo na baadaye kwenda bandari ndogo. Sisi tuna bahati kubwa sana, tuna uwezo pia wa kuifanya Pangani kuwa bandari. Kwa hiyo, katika *master plan* ya bandari pamoja na hizo zilizotajwa ya Tanga, Bagamoyo, Dar es Salaam na Mtwara lakini tuanze kufikiria pia kuimarisha Bandari ya Kilwa ili

isiwe ya uvuvi tu. Bandari ya Kilwa ndio bandari ambayo miaka ijayo itakuwa bandari kubwa kuliko zote katika Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuifanyie bandari hiyo sasa maandalizi makubwa ili Kilwa ichukue nafasi yake na tuanze kufikiria kutoa Reli ya *SGR* kutoka Kilwa kuja kuunga ama Pugu au maeneo ya Pwani, ili baadaye mizigo ikitoka Kilwa iweze kwenda moja kwa moja katika Reli ya *SGR* na kwenda moja kwa moja mpaka sehemu nyingine. Kwa hiyo, tunaweza kuona utajiri mkubwa ambao Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* ameijalia Tanzania katika haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia, ni sasa Tanzania lazima tuanze kujiweka sawa kuanza kutumia magari na mabasi ya umeme. Dunia inahama kutoka kwenye magari ya mafuta, dunia inahama kutoka kwenye magari ya gesi, dunia sasa inakwenda kwenye magari ya umeme. Tuanze kufikiria mwendokasi Dar es Salaam badala ya kutumia gesi na *petrol* itumie umeme. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu ametujalia vyote, naona muda wangu umekwisha, naunga mkono hoja asilimia 100 kwa Wizara hii, lakini Mheshimiwa Mbarawa asiisahau Kilosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa Kabudi. Mheshimiwa Hassan Mtenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Aeshi Khalfan Hilaly na Mheshimiwa *Doctor* Florence Saminzi ajiandae.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kukushukuru kwa kupata nafasi hii adhimu ya kuchangia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Nami niungane na mwenzangu kumshukuru Rais wetu mpendwa wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan na ni wajibu wetu kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu kwenye jimbo langu ni mabilioni ya shilingi ambayo yameingia kwa kipindi kifupi na kazi zinaendelea. Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe pongezi kwa Waziri wetu Mheshimiwa Mbarawa, lakini na Naibu Mawaziri kwa kazi kubwa wanazozifanya kwenye Wizara hii. Kule kwangu siwezi kumuacha *Engineer* wa *TANROADS*, Ndugu yangu Dotto, kwa kweli anaiwakilisha Mtwara vizuri na utendaji kazi wake ni mzuri kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maeneo kama kama matatu ya kuchangia, lakini eneo la kwanza ili kupunguza urasimu wa mambo yote ambayo tunayajadili ndani ya Bunge hili. Tunazungumza mambo mengi sana ya msingi, lakini kila tutakalozungumza kwenye Bunge hili linagusa sheria kwenye eneo husika. Sasa kwa nini nimezungumza sheria. Tunaizungumzia sheria leo tunazungumza masuala ya uwekezaji ndani ya nchi yetu lakini kwenye suala la uwekezaji bado kuna sheria ambayo zinatufungwa, tunashindwa kuondoka pale tulipokuwa kuelekea kwenye eneo lingine. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri katika Wizara yake watuletee sheria hapa, hata kesho tuweze kufanya mabadiliko ili tusonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi wagonjwa wa malaria nyumba moja hawawezi wakaamshana kwenda hospitali. Sasa kwa nini nazungumza hivi? Ziko hoja ambazo tunazungumza kuhusu uwekezaji wa bandari. Uwekezaji huu wa bandari kila mtu ana mawazo yake ndani ya Bunge hili, lakini kuna wengine wanasema tuendelee kujifunza, lakini *TICTS* wana miaka mingi wako pale bandarini na kama ni shule kwenye Serikali wamepata kupitia *TICTS*. Ni vyema sasa shule ile tulioipata kutokea *TICTS* twende tutafute wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ambayo inazungumza kwamba bandari yetu ni ndogo, bandari ile imeingia kwenye upanuzi zaidi ya mara tatu, wakati tunaanza Bandari ya Dar es Salaam haikuwa vile. Kama tunampata mwekezaji na tunasema

bandari ile itakuwa ni *busy* zaidi kwenye mikataba tuingize suala la yeye kupanua bandari, ni kitu ambacho kinawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari yetu ya Dar es Salaam inatumika na nchi zaidi ya nne na ndio maana tunaiona ipo *busy* sana. Sasa niishauri Serikali katika Bandari ya Dar es Salaam pamoja na uwekezaji mkubwa tunaotaka kuufanya, ziko bandari zingine ambazo inawezekana vile vile tukazisaidia. Mfano, leo tunaichukua Zambia na Malawi tukasema wafanyabiashara wote wa Zambia na Malawi watumie Bandari ya Mtwara. Tukaichukua Burundi na nchi zingine na Congo waje watumie Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili inawezekana likatupatia kipato kikubwa sana na hili nimekuwa napiga kelele sana Bungeni. Yawezekana naeleweka au inawezekana nisieleweke, lakini kwa hali nyingine nimshukuru Rais, nilikuwa napiga kelele sana kuhusu Daraja la Mto Ruvuma kule Kilambo. Naishukuru Serikali imeridhia kujenga daraja lile. Daraja lile ukubwa wake inawezekana ukawa zaidi ya kilometa mbili na *point* au tatu. Katika Afrika inawezekana likawa ni daraja la kwanza kuwa na ukubwa mrefu namna ile ambalo litatumia mabilioni ya shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu amefanya maamuzi magumu ya kuwasaidia Wananchi wa Mtwara, lakini ujenzi wa daraja lile sio la wasaidie Wananchi wa Mtwara, daraja lile ni ujenzi wa Kitaifa kwenye rasilimali ya Kitaifa kwenye mapato ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la reli. Tulikuwa na *package* ya Mtwara *Corridor,* tunazunazungumza bandari, tunazungumza *airport*, tunazungumza na reli. Reli ya Mtwara Mbamba *Bay* imekuwa ipo kwenye makabrasha miaka yote toka mimi nazaliwa na Wabunge wote waliopita kutoka Mtwara wanaizungumzia reli hata kama ilikuwepo na ikaondolewa. Sasa leo Mchuchuma na Liganga tayari tuna madini ghafi na madini haya yanatakiwa lazima tuwe na reli ya

ufanisi ili yaweze kusafiri kwa wakati na mzigo ifike ikiwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, suala la Reli ya Mtwara Mbamba *Bay* ipewe kipaumbele sasa…

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kingu.

**TAARIFA**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nimpe taarifa mchangiaji kwamba, kwa mujibu wa *feasibility study* iliyofanywa mwaka 2016, jumla ya tani 500,038 za makaa ya mawe zilipita kwenye barabara na kwa *feasibility study* ya mwaka 2022 tani milioni 1,233,000 zimepita kwenye barabara na *feasibility study* ya mwaka huu tani milioni 2.3 zimepita kwenye barabara. Kwa *trend* hii naomba nimpe taarifa mchangiaji kwamba anachokizungumza kina *make sense* kujenga reli ya kusini ili kuokoa barabara zetu kwa maslahi ya Taifa. Natoa wito kwa Mheshimiwa Waziri *feasibility study* ya ujenzi wa reli hii uanze haraka kwa maslahi ya Taifa na kuwasaidia watu wa Kusini, wamelia muda mrefu, inatosha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtenga taarifa unaipokea?

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *microphone* zimegoma.

**MWENYEKITI:** Hamia kwa jirani yako hapo Mheshimiwa.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko sawa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan taarifa unaipokea?

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii naipokea kwa mikono yote na miguu na ninampenda sana, mtoaji taarifa huyu ana akili kubwa sana,Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *International Airport Mtwara*. Uwanja huu naishukuru sana Serikali namshukuru Rais, tumejenga uwanja zaidi ya shilingi bilioni 14 na *something* lakini uwanja huu tunazungumza leo katika fedha zote zilizopangwa kwenye bajeti tulikuwa tupate na gari ya zimamoto *(fire),* lakini kila ukiuliza watu wa manunuzi leo ni mwaka wa tatu tunazungumza kwenye manunuzi ya kuleta gari la zimamoto Uwanja wa Ndege Mtwara, ni mwaka wa tatu tunazungumzia manunuzi. Ni vitu vya hatari sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni Sheria ya *Procurement* inakuwa hivi, tunatokaje hapa tulipo? Uwanja wa ndege kulikuwa kuna *package* ya kujenga majengo ya kukaa abiria mpaka leo kwenye bajeti hii nimechungulia sijaona na wala sijasikia. Sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri unapokuja hapa utupe majibu mazuri kuhusu uwanja ule, gari la zimamoto, tunahitaji na jengo la abiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza utanuzi ndani ya nchi haswa wa barabara na mimi naipongeza sana Serikali yangu, imefanya kazi kubwa kwenye miundombinu. Watu ambao wanatoka Mtwara na Lindi wanakwenda zao Dodoma au wanakwenda Morogoro, iko *shortcut* ambayo inawezekana Wizara ikakaa ikajipanga tutengeneze barabara ambayo ni *shortcut.* Tunafika mpaka Kibiti, unaingia mpaka Mloka, Bwawa la Mwalimu Nyerere tunakwenda hadi Morogoro. Barabara ile inakuwa ni fupi kuliko gari za mizigo zinazunguka mpaka zinaenda Dar es Salaam, zikitoka Dar es Salaam zitafute Kibaha, zitafute Morogoro, mambo mengine ya msingi yapo kwenye uwezo wetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtenga, muda wako umeisha.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aeshi Hilaly atafuatiwa na Mheshimiwa Dokta Florence Samizi, Mheshimiwa Esther Matiko ajiandae.

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuongea. Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya na Watanzania wote wanajua na wanaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu Ndugu yangu, Kaka yangu Mheshimiwa Prof. Mbarawa kwa kazi kubwa anayoifanya, ama kweli Wizara hii ni ngumu lakini amekuwa akifanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kwamba maendeleo yanapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii tena kwa niaba ya Wanarukwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Nimekuwa Bungeni nikapambana sana kuhusiana na Uwanja wa Ndege wa Sumbawanga Mjini. Mwaka jana nilisimama hapa nikasema endapo hatutaweza kufanikiwa kujenga uwanja wa ndege kwa mwaka huu nilitaka niiombe Serikali na niliombe Bunge lako litoe hiyo bajeti kwa sababu tumekuwa tukiipigania mwaka wa saba leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tu Mheshimiwa Waziri alinipigia simu na hatimaye ombi letu limekubaliwa tukaenda kusaini mkataba na wananchi wakaona na wakafurahi sana na mwezi ujao Mkandarasi atakuwa *site* anaanza kazi. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nikupongeze sana Kaka yangu kwa kazi kubwa uliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili naomba niongelee maeneo matatu au manne hivi. Barabara zetu za Mkoa wa Rukwa, tumetembelea barabara mbili ya kutoka Matai kwenda

Kasesha na ya kutoka Ntendo kwenda Muzi. Mheshimiwa Waziri nikuombe, Rukwa tunajivunia sana kilimo lakini Rukwa tuko pembezoni mwa *Lake* Tanganyika, tunapakana na Congo, Burundi na Zambia. Tumejenga bandari nzuri sana, tumejenga bandari ya Kipili, tumejenga bandari ya Kasanga, tumejenga bandari ya Karema na maeneo mengine kwenye Mikoa mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya barabara tukuombe sana, kuna barabara ya kutoka Namanyere kwenda Kirando inaelekea Kipili. Mheshimiwa Waziri tumewekeza vya kutosha lakini tusipojenga barabara zile bandari zitakuwa tumewekeza kama kwa kazi bure. Sasa nikuombe sana kwenye bajeti ya mwaka huu barabara ya kutoka Namanyere kwenda Kipili kwa kweli tuweze kuijenga kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Lyazumbi kwenda Kabwe ambako na kwenyewe tumejenga bandari kubwa sana na yenyewe tujenge barabara kwa kiwango cha lami ili kuwe na tija ya zile bandari tulizozijenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana lengo la kujenga zile bandari ni kusafirisha mizigo kwenda Congo, Burundi na kwenda Zambia, tusipojenga barabara za lami, bandari zile zitakuwa ni kazi bure. Kwa hiyo, tukuombe sana barabara zipitike na bahati nzuri Kamati tulikwenda kutembelea tukaona kwa kweli kuna kila haja ya kujenga barabara zile. Mheshimiwa Waziri nikuombe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwenye barabara naomba niishauri Wizara kwamba tumekuwa na barabara nyingi, tumekuwa na Wakandarasi wengi lakini wazawa hawa ambao tunao hawanufaiki mara nyingi na hii miradi ya barabara za kiwango cha lami kutokana na masharti magumu ambayo Mkandarasi wa kawaida kuweza kujenga hizi barabara kwa kweli wameshindwa. Nikuombe Mheshimiwa Waziri rekebisheni masharti ni makubwa mno na mazito. Unapomwambia mkandarasi wa kawaida au mzawa awe na *turnover* ya shilingi bilioni tano anaitoa wapi? Kwa mradi upi

alioupata? Kwa hiyo, nikuombe barabara hizi tukipata wazawa wetu wakijenga, maendeleo yatabaki ndani ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakandarasi wa nje wengi wakipata barabara hizi mara nyingi sana wanakwenda kuwekeza huko kwao. Kwa hiyo tuangalie sana na uzawa, tupunguze masharti kidogo angalu hata wa kilometa 10, 15 basi wakandarasi wa hapa nchini wapewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta Mheshimiwa Waziri barabara ya kilometa 15 ama 20 masharti yanayowekwa hakuna mzawa ambaye ameweza kupata kujenga barabara. Kwa hiyo, nikuombe sana katika hili unapokuja utusaidie na wazawa wakandarasi waweze kupata kazi ili waweze kunufaika na wakinufaika maendeleo yanabaki nchini kwetu, wakinufaika watajenga kama ni hoteli zitabaki kwetu, wakinufaika kama watajenga maeneo mengine ya maendeleo lakini yote yatabaki kwetu. Kwa hiyo, kwenye hizi kazi ndogo ndogo, kilometa 10, 15 basi *at least* Watanzania waweze kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza unakuta kuna kampuni inajenga barabara zaidi ya kilometa 100, kilometa 200 bado ukitangaza *tender* ya kilometa tano unamuona na huyu bwana naye anakuja kuiomba hiyo tano. Kwa hiyo, ni vigumu sana kwa Mkandarasi wa Kitanzania kupata kazi. Kwa hiyo nikuombe sana katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kumekuwa na kilio *Lake* Tanganyika tumejenga kweli bandari lakini cha kushangaza hatuna hata meli moja inayotembea, hakuna! Ukienda kwenye Shirika la *Meli* wakakutembeza kule Kigoma utakuta kuna meli moja wanaisifia sana tumeikarabati, meli yenyewe ya *MV* Sangara*,* meli ya mafuta! Leo hii tumeona bora mafuta kuliko wananchi waweze kupata huduma ya usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanakufa sana, maboti yanazama sana, mizigo inazama. Kwa hiyo nikuombe, meli ile ya *MV Liemba* nimekuwa nikipambana sana ndani ya Bunge

kuhakikisha kwamba ile meli inafufuliwa lakini mpaka leo. Mwaka jana tumepitisha bajeti, mwaka juzi tumepitisha bajeti na mwaka huu tunaipitisha tena bajeti. Sasa Mheshimiwa Waziri mimi nakuamini sana, tuangalie sana wananchi tunaoishi pembezoni mwa *Lake* Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na hoja ya kujenga meli ya tani 2,000, hoja ni nzuri lakini inawezekana tunaifikiria hii tani 2,000 labda kwa miaka mingine 50 ijayo. Kwa miaka hii ya sasa hivi tuhakikishe kwamba meli hii ya tani 2,000 tuigawe iwe meli ya tani elfu moja moja ziwe zinapishana. Ukijenga meli moja ukawa unasubiria mzigo wa kwenda Congo, kuna watu hapa wanafikiria Kalemi ni Mji mkubwa kama Dar es Salaam siyo kweli! Kwa hiyo tunajikuta meli ya tani 2,000 itakaa inasubiria watu wapate mzigo, wajichange, wajichangae waende kuusafirisha. Hiyo inakuwa ni ngumu zaidi. Kwa hiyo, ninakuomba sana tani 2,000 mimi siungi mkono lakini nimekuwa nikikushauri mara nyingi na umekuwa ukikubali ushauri wangu naomba katika hili tujenge meli za tani elfu moja moja ili ziwe zinaenda kwa wakati na kwa muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho naomba nikupongezeni sana Wizara ya Ujenzi.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hilaly kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa.

**TAARIFA**

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa mzungumzaji anayezungumza kwamba, ni kweli hii meli ya tani 2,000 ni nia njema ya Serikali kweli lakini tani elfu moja moja ni nzuri hasa kwa wafanyabiashara ambao utaratibu wakati mwingine kukodi meli ni ngumu kukodi meli ya tani 2,000 lakini tani 1,000 ni rahisi. Kwa hiyo nampa taarifa mzungumzaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aeshi taarifa unaipokea?

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa na kwa kuongezea tu tuna mfano Congo wamejenga meli ya tani 2,000 inaitwa MV Amani, ile meli haisafiri! Kwa hiyo tuige tuone kule Congo ile meli waliyoiunda inatembea? Leo hii ina mwaka wa pili au wa tatu nafikiri imeenda *trip* tatu au nne. Sasa kama wenzetu wamejenga meli ya tani 2,000 sisi tujenge meli za tani elfu moja moja ambazo zitakuwa zinabeba mzigo kirahisi na zinaweza kufikisha mzigo na wafanyabiashara wakafanye biashara zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze sana Wizara ya Ujenzi lakini niipongeze *TRC* kwa kazi kubwa wanayoifanya. Tumeenda kutembelea miradi, tumetembelea *SGR* kwa kweli inajengwa kwa kiwango kinachotakiwa. Naomba niwe mkweli nisiwe mnafiki katika hili. Tumetembelea *lot* namba moja na namba mbili, kwa kweli kuna watu ambao hawajawahi kufika kwenda kuangalia. Tunaweza kuwa tunafikiria kuna jambo linajengwa siyo la uhalisia lakini kimsingi kwa kweli Serikali imefanya kazi kubwa. Nikuombe sasa Mheshimiwa Waziri mabehewa ambayo tumeambiwa yapo njiani basi yafike ili na wananchi waweze kuona sasa kile ambacho tulikuwa tumekusudia.

Ninaamini wananchi watajenga imani na mimi niseme nisiwe mchoyo wa fadhila, nawapongezeni wote Wizara ya Ujenzi na taasisi zote. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa sana anayoifanya, lakini nimuombee kila la kheri awe na afya njema aweze kutuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kuna wageni walioko Bungeni muda huu. Tunao wageni wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, ahsante na karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 40 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni Kwaya ya Bethania Kanisa la *Anglican* Mlowa kutoka Jijini Dodoma, ahsante na karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mfunzo; tunao wanafunzi 150 kutoka Chuo cha Mipango na Maendeleo ya Vijijini cha Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanakwaya 30 kutoka Kanisa la *Anglican* Nzuguni C ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo ajiandae.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuiongoza nchi yetu lakini kipekee kwa nia yake ya dhati kabisa ya kuifungua nchi yetu kwa miradi mikubwa ya barabara, reli, ndege wote tunaona jinsi gani nchi yetu inakwenda kufunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri Profesa Mbarawa na Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa mashirika yote, Bandari, *TASAC,* Shirika la Ndege wote vijana wanachapa kazi, wanafanya vizuri tunaona jinsi gani wanaweza kuyaendesha hayo mashirika na tunaona jinsi gani Tanzania inakwenda kubadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwe mchoyo wa fadhila, nimshukuru Kaka yetu *Engineer* Choma, *Engineer* wa *TANROADS* Mkoa wa Kigoma anachapa kazi vizuri katika Mkoa wetu wa Kigoma, anatupatia ushirikiano wa kutosha, tunaona jinsi miradi ya Mkoa wa Kigoma inavyofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Muhambwe nasimama hapa leo kutoa shukurani nyingi kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo miradi ya barabara inaendelea katika Jimbo la Muhambwe. Tunao mradi wa Barabara wa Mvugwe – *Nduta Junction* kilometa 59 ambao mwaka huu umefikia asilimia 66, mwaka jana ulikuwa asilimia 25, tunaipongeza Serikali inafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunayo barabara ya Nduta *Junction* - Kibondo Mjini kilometa 25.9 mwaka jana ilikuwa asilimia 44 na mwaka huu sasa hivi wako asilimia 58. Tumesaini mkataba wa ujenzi wa barabara kutoka Kibondo Mjini kwenda Mabamba kilometa 47.9 kwa gharama ya takribani shilingi bilioni 69. Hizi ni jitihada za dhati kabisa za Serikali za kuendelea kuwaunganisha wananchi wake kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee tunaenda kufaidika kabisa maana barabara hii inakwenda kuboresha soko la ujirani mwema pale katika Kijiji cha Mkarazi ambacho tunafanya biashara na ujirani mwema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo ya miradi hii inayoendelea katika Jimbo la Muhambwe, bado ziko changamoto ndogondogo. Kwanza kabisa barabara hizi zitategemewa kuisha mwaka huu Desemba na kama tuko kwenye asilimia 66 ni ukweli usiopingika kwamba tunatakiwa kuongeza kasi. Wananchi wa Muhambwe wamenituma wanaomba kasi ya ujenzi wa hizi barabara ili tuweze ku-*meet target*. Ziishe kwa wakati kwa sababu hili ni Jimbo ambalo lilikuwa halijaunganishwa kwa lami bado. Kwa hiyo, nawaomba watendaji kwa nia ya dhati kabisa Mheshimiwa Rais ya kutuunganisha na lami basi kazi ifanyike kweli kweli ili barabara hizi ziweze kuisha kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi pia zina miradi ya *CSR* ambayo miradi hii ilitegemewa kujengwa Kibondo, Kasulu na Buhigwe. Barabara zimefikia asilimia 66 lakini miradi hii bado haijaanza. Ninajua michakato inaendelea, niiombe Serikali miradi hii ya *CSR* ambayo inategemewa kujengwa katika Majimbo haya

matatu Kibondo, Kasulu na Buhigwe basi nayo iende kwa kasi ili barabara zitatakapoisha na miradi hii pia iwe imekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipo kipande cha barabara ambacho Wabunge wa Mkoa wa Kigoma tumekuwa tukikisemea sana, Uvinza – Malagarasi kilometa 51. Ukipita kwenye ile barabara ni changamoto yaani ukimaliza pale lazima upeleke gari yako *service*. Kipande kile ni kibaya sana na kwa taarifa ya Mheshimiwa Waziri kipo asilimia 26 kwa hiyo ni ukweli usiopingika kwamba bado kiko nyuma sana. Tunaomba Serikali itusaidie sisi Wabunge wa Mkoa wa Kigoma barabara hiyo inatupa changamoto siyo nzuri, haipitiki tunaomba kasi iongezeke. Kama kuna changamoto kwenye kile kipande basi zifanyiwe kazi ili kipande kile nacho kiweze kuisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi hii ya lami bado ziko barabara za *TANROADS* ambazo tunahitaji ziwe kwenye kiwango cha lami ambapo kwa sababu ya mvua hizi zinazonyesha barabara hizi hazipitiki. Hii ni barabara ya Kitaha na Nyange ni mbaya sana haipitiki, iko chini ya *TANROADS,* hii ni Barabara ya Kifura – Nyange haipitiki, Barabara ya Bunyambwe – Nyange haipitiki. Nimuombe *Engineer* Kaka yangu *Engineer* Choma ninamuamini sana anaweza. Tunamuomba kule Kibondo atusaidie kutengeneza hizi barabara kwa kiwango cha changarawe na kipekee niombe kusisitiza kwamba barabara hizi zinavyotengenezwa basi ziwekwe mifereji kwa sababu mvua imekuwa chanzo kubwa cha kufanya ziharibike sana. Naamini zitatekelezeka kwa sababu *TANROADS* wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wote wamesema Wabunge wa Mkoa wa Kigoma, Rukwa na Katavi kwa kweli tunaipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo wamejenga *MT* Sangara na tumeona ipo asilimia 90 meli ambayo itaenda kubeba mafuta. Hii Serikali imelenga kufanya biashara lakini Serikali kama Serikali mbali na biashara lengo kuu la Serikali kwanza ni kuwahudumia wananchi, ustawi wa wananchi wake. Jamani wananchi wa Mkoa wa Kigoma, Wananchi wa Rukwa na Katavi tunaomba meli ya abiria na mizigo midogo midogo ili wananchi wetu waweze kusafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona imepita bajeti hapa ya kutengeneza MV Liemba, MV Mwongozo, tunaomba kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ameweka *commitment* kwamba itaanza mwezi wa sita na mwezi wa nane itakuwa imeisha. Tunaomba mchakato huu uende haraka sana. Kwa nini? Mwenzangu amesema tumejenga bandari, Kigoma tumejenga, tumejenga Karema, tumejenga Kabwe, Kipili, Kasanga. Kama hatuna meli tulitaka ku-*achieve* nini kwa ajili ya hizi bandari? Tunajenga *SGR* inakwenda kupeleka watu kule, bila kuwa na meli tunaenda ku-*achieve* nini? Tunaiomba Serikali ituangalie Wananchi wa Mkoa wa Kigoma, Katavi na Rukwa ili tuweze kufunguka kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamesema sana kuhusu Shirika la Ndege. Ni ukweli usiopingika kwamba shirika hili linafanya kazi sana. Tumeona lilikotoka na lilipo sasa, ninampongeza sana Mkurugenzi na watumishi wote. *CAG* amesema pamoja na jinsi ambavyo shirika linafanya, bado hili shirika ukisema mashirika ambayo yanajiendesha kwa hasara kwa miaka mitano mfululizo basi unataja shirika hili. Ukisema shirika ambalo lina mitaji hasi unataja shirika hili na tumeona kinachochangia kikubwa ni uendeshaji wa hili shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Kamati imeshauri, *CAG* ameshauri. Nafikiri ni muda muafaka sasa Serikali kurudi nyuma na kuangalia jinsi gani ya uendeshaji na kipekee kuwapunguzia hii gharama ya kukodi ndege, kwa sababu tumeona *CAG* amesema mikataba mibovu katika kukodi ndege imesababishia shilingi bilioni 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya ndege ya Tanzania, wakala wa ndege wa Tanzania mikataba inakuwaje mibovu kiasi kwamba shirika linapata hasara? Basi tuwape nafasi tuwapatie hizi ndege ili waweze kuendesha wenyewe. *CAG* anasema, Serikali ilitoa ruzuku, shilingi bilioni 30, lakini shirika likapata hasara ya shilingi bilioni 35. Ina maana bila ruzuku, shirika lingepata hasara ya shilingi bilioni 65. Sasa kama tunapeleka ruzuku na tunataka wafanye vizuri, tuwasaidie kwa sababu wanafanya vizuri

ili waweze kujiendesha. Wapewe ndege na pia walipiwe madeni yao ili waweze kuendelea kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo inaendelea kutuangalia Mkoa wa Kigoma na inaendelea kutaka kutufungua kwa uhakika. Bajeti ya Uwanja wa Ndege wa Kigoma ilitengwa mwaka 2021, hakikufanyika kitu; 2022 imetengwa, hakikufanyika kitu; 2023 imetengwa tena shilingi bilioni tisa. Wananchi wa Kigoma wamechoka kuambiwa kwamba bajeti imetengwa, wanataka kuona utekelezaji. *Running way* tumesaini mkataba pale, tunaamini mkandarasi atafika *site* kwa wakati.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Florence, muda wako umeisha.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, na Mheshimiwa Silyvestry Koka, ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi. Kwanza niseme, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu ambao tumekuwa tukiipigia kelele sana, ingawa bado ni asilimia 47 tu kwenye ukarabati wa ujenzi wa Kiwanja cha Musoma. Tunaomba sana ukamilike kwa haraka kwa sababu pale ndipo anapotoka Baba wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchangia kuhusiana na ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Serengeti. Tulizungumza hapa na tukaonesha jinsi gani uwanja ule ukijengwa utaenda kufungua fursa za kiuchumi kwa sababu una *multiplier effect* na Serikali hapa ikatuhakikishia, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara yenu ya Ujenzi na Wizara ya Fedha, mlikaa mkasema kabisa kwamba ule

Uwanja wa Serengeti unaenda kujengwa na umetengewa shilingi bilioni 147. Nimepitia hotuba yako yote, sijaona sehemu yoyote ambapo umeainisha. Baada ya kusema vile, wananchi na wawekezaji mbalimbali walikuja Serengeti wakanunua maeneo mbalimbali ya ujenzi wa hoteli na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi ilivyo, watalii wakitoka huko kwenye mataifa mengine, wanaopita *route* ya huku, wanashukia Nairobi *then* wana-*drive* na magari kuja Serengeti. Sasa kuna wengine wanakuwa *disgusted,* tunapoteza mapato. Tunaiomba sana Serikali, ili kuweza kukuza utalii wa nchi yetu, ili kuweza kukuza uchumi wa Tanzania, mtujengee uwanja wa Serengeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tokea iende *re-allocation,* basi Wizara iweze kuchukua hatua kuhakikisha kwamba wanaanza angalau kwa mwaka huu wa fedha wanatenga fungu kidogo kuelekeza hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kipekee kabisa niwapongeze madada ma-*pilot* ambao wapo kwenye *Air Tanzania,* walikuja hapa jana, walikuwa 10 kati ya 106, bado idadi ni ndogo sana, tunatamani wafike 50/50, lakini ni hatua nzuri kuelekea hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mchango wangu zaidi nitajielekeza *ATCL* na muda ukitosha nitaenda na kwenye *TPA*. Ni dhahiri kabisa kwamba mashirika ya ndege ili yaweze kuwa endelevu na yajiendeshe kwa tija zaidi, kuna *some components* ambazo zinahitajika. Kwanza inahitaji uwekezaji mkubwa sana, mtaji mkubwa kwenye uwekezaji *(capital intensive)*. Pili, lazima tuwe na udhibiti wa gharama za uendeshaji. Usipokuwa na udhibiti na gharama za uendeshaji hata ununue ndege ngapi sijui, lazima utakuwa unaona hasara zikijitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa viwango vya Kimataifa vya gharama za uendeshaji ambazo ni *standard* zinajulikana, tunajua kwa upande labda wa mafuta ni asilimia 30. Utakuta kwenye *maintenance cost* inakuwa labda asilimia 20, kuna rasilimaliwatu

kati ya asilimia 10 mpaka 15 na kuna vikosi vingine vidogo, hivyo ni kwa mashirika yote hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili shirika letu la *ATCL* liweze kuwa shindani, ukitoa hizo *component* za gharama ambazo nimesema, tumeipa *burden* tena kwa hizi fedha za kukodi ndege kutoka *TGFA*. Mkataba huu wa kukodisha ndege, na huu nitauongea *very bitterly,* tumezungumza mara nyingi hapa, mpaka hata Katibu Mkuu Kiongozi wa Ikulu aliongea kuhusu kuhakikisha kwamba ndege zinarudi *ATCL.* Ni mzigo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi Serikali ikasema imeweka huo mkataba kama *caveat* ya ndege zisikamatwe. Ndege zinakamatwa sana, zinashindwa hata kuruka kwenda kwenye vituo vya nje ambavyo ni vya kimkakati. Mathalani, ndege zetu zinashindwa kwenda *Johannesburg* ambapo zilikuwa zinatengeneza fedha nyingi sana. Kuanzia 2018 *August* kila mwaka tunapoteza takribani *37 billion* kwa sababu haturushi ndege kwenda *Johannesburg*. Kwa nini? Tunaogopa zitakamatwa? Sasa huu mkataba ambao tumeweka ambao ni mzigo unasaidia nini? Ukiangalia pia tunakataa kupeleka ndege *Landon* au Ulaya, tunaogopa zitakamatwa. *We are losing a lot of money, 13 billion* zinapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndege za kukodi, kwa mfano hii tu ya kwenda *South Africa* Machi, 2022 mpaka Machi, 2023 tumepoteza *17.3 billion*, halafu tunaendelea kukumbatia huu mkataba ambao *it is a burden.* Sasa ukiangalia ripoti ya *CAG* ikitoka, wanasema shirika linajiendesha kihasara. Kwa mfano, huu mwaka 2021/2022 imerekodi kwamba imejiendesha kihasara kwa *35 billion*, lakini ukiangalia kiuhalisia, *direct cost* ambazo zinatokana na ukodishaji wa ndege ni *85 billion,* ukitoa hiyo hasara, unajikuta shirika *in fact* lingeweza kuwa na faida *over all most 50 billion,* kama ingekuwa hatujaweka huu mkataba wa kukodisha ambao hauna tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mlikuwa mnataka mweke mkataba kuzilinda ndege, mngeweka tu hata shilingi milioni 100 au shilingi milioni 200, si mnataka mwoneshe kama *TGFA*

inakodisha kwa *ATCL?* Kwa nini mweke *burden* kubwa hivyo? Hela nyingi za kukodi, bado sijui una-*reserve maintenance, process* zenyewe za *procurement* ni ndefu, unakuta wanachukua hela zao nyingine wanakarabati, kunakuwa kuna *double count.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni *direct cost*. Ukichukua tu *direct cost* uka-*oversight* na hiyo hasara uliyosema, una *profit* ya *50 billion*. Sasa ukiongeza kwa mfano huo mwaka wa 2022 ambao nimesema, fedha ambazo tumepoteza, *37 billion* ndege ya abiria kwenda *South Africa,* uongeze *17.3 billion* uje uongeze na hii ya kwenda Landon *13 billion* unapata *all most 37 billion. 37 billion* ukijumlisha *50 billion* hili shirika lingekuwa linajiendesha kwa faida kubwa, *all most 117 billion*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haihitaji kukodi wataalaam sijui uunde tume kutoka nje kuja kutushauri juu ya uendeshaji wa shirika letu na umiliki. *It is just a mere wastage* wa fedha za walipakodi masikini. *It is just a common sense,* yaani ukifikiria tu, *is just a mere common sense,* hauhitaji kuunda timu ya wataalam eti kushauri ni jinsi gani uweze kuwa na muundo *ATCL,* ni jinsi gani uweze kumiliki ndege. *Are we serious real* kama Taifa, *and yet* tunatumia hela za walipakodi masikini kulipa hao *the so called* wataalam kuja kutushauri sisi. Serikali tunaomba, huu mkataba ufe, *ATCL* ikabidhiwe hizi ndege, *after all* ndege hazitakamatika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwenye hotuba yako Mheshimiwa Waziri umeandika Ibara ya 260 kwamba unaboresha Shirika *of which I agree,* unanunua ndege unaleta, unasema unaboresha uendeshaji kupunguza gharama. *Component* namba moja kupunguza gharama ya uendeshaji, ondoa huo mkataba feki kati ya *TGFA* na *ATCL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu ningependa sana katika kupitisha hii bajeti tuazimie Serikali ivunje huu mkataba ambao ni *burden* kwa Taifa. Tunapoteza fedha kwa mfano kutokurusha ndege, hizo fedha, shilingi bilioni 67, zingeweza kuja Serikalini na zikajenga madarasa ya kutosha, vituo vya afya vya kutosha, *but we are wasting them.* Hizo ni *forgone revenue* kwa

uzembe tu wa kuona kama umekodisha ndege. Haikubaliki kabisa. Lazima huo mkataba ufe. Haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, Mheshimiwa Waziri ukitaka kweli shirika letu likue, tukishaondoa huo mzigo sasa, kwa sababu huo mzigo upo, lakini unaandika kwamba unataka iwe *competitive* labda na mashirika mengine…

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mchango ambao anatoa dada yangu, Mheshimiwa Esther, tayari Mheshimiwa Rais alishaunda tume ambayo inashughulikia kuondoa ndege kutoka *TGFA* kwenda kwenye Shirika la *ATCL* ili kuondoa hizo *burdens* ambazo anazizungumza. Kwa hiyo, tume tayari ilishaundwa na Serikali ilishachukua hatua. Kwa hiyo, hili Mheshimiwa Rais aliliona kwa jicho la karibu sana, ndiyo maana ameshaunda tume tayari kwa ajili ya kuondoa hicho anachokizungumza, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther, taarifa unaipokea?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei, kwa sababu hata wanaomshauri Mheshimiwa Rais, hawaitendei haki nchi hii. Kwa sababu hii tume imeundwa kitambo, halafu kwanza hata walifikiaje kumshauri Mheshimiwa Rais waunde tume wakati *this thing was obvious?* Sidhani hata wakati wanaunda hiyo tume kuleta mkataba huu waliunda hizo tume ambazo zinatumia fedha. Ndiyo maana nasema, tusipoteze *at a time* fedha, unaunda tume, unaleta watu sijui kutoka nje, *they are using money* ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ATCL* ukilinganisha na *Ethiopian Airlines* kutoka Afrika tu hapa hapa, wenzetu wale kwanza *Ethiopian Airline* wenyewe ni kampuni ambazo zinajiendesha zikiwa sanjari na kampuni nyingine hodhi, ambapo kwa mfano kwenye uendeshaji wa viwanja, sijui mambo ya *inflight catering* na mambo mengine mengi…

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Deo Sanga.

**TAARIFA**

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema wanaomshauri Rais wanamshauri vibaya, Rais huyo huyo ndio wamemshauri, amefanya maridhiano na ndiyo maana mambo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Esther, taarifa unaipokea?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana mzee pale, lakini kuna ushauri wenye tija na ushauri mwingine hauna tija. Hatujakataa ushauri wote wanaoushauri kwa Rais yanaenda vibaya, lakini *in particular this one* wamemshauri Rais vibaya na kweli hao wataalam wanapoteza fedha za Watanzania…

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa hili narudia kusema *it is a mere common sense*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilindie muda wangu kwa hizi taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mchangiaji anasema kuna ushauri wenye tija na usiokuwa tija. Ningetamani atuambie wenye tija ni upi na usiokuwa na tija ni upi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther, malizia mchango wako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanawasikia, kwa sababu wanaweza tu wakatumia *their common sense.* Katibu Mkuu Ikulu mwaka 2022, *a year now,* alisema kabisa kwamba hili la mikataba limeshaisha. *ATCL* wanarudishiwa ndege na mkataba una…, mwaka jana 2022 Katibu Mkuu Ikulu *said that, and then… (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wabunge, tumetumwa humu ndani kuishauri na kuisimamia Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatakiwa kuhakikisha kwamba rasilimali za nchi yetu zinatumika vizuri. Tunashauri kwa nia njema kabisa, *soberly.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaheshimu sana mchango wa Mheshimiwa Mbunge. Wabunge kadhaa na mimi naomba kuungana nao, tunachokisema ni kwamba ni mapema sana. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani, kati ya mambo ambayo aliyaona ni mambo ya

kuyafanyia kazi kwa haraka ni pamoja na mkataba huo wa *ATCL* na akaagiza ni lazima tupate ushauri wa kitaalam, kwa sababu, tunaposema ushauri wa kitaalam, maamuzi tutakayoyafikia yatutoe moja kwa moja na yasitupeleke tena kwenye hasara ambayo imejitokeza huko nyuma. Kwa hiyo, sioni kama ni sahihi kuendelea kutumia maneno ambayo yanadhalilisha kazi hiyo nzuri, mawazo na maamuzi mazuri aliyoyafanya Mheshimiwa Rais kupitia watendaji wake kuhakikisha jambo hili tunalimaliza salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimpe taarifa Mheshimiwa Esther, Serikali jambo hili imelipa kipaumbele na baada ya muda siyo mrefu, tutakuwa tumefikia *conclusion* na shirika hili kila mmoja anatamani liweze kufanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Esther, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anajaribu kupita pale pale tu, anarembaremba mambo. Mimi nakubali, nasema hivi, na Kamati yako ya Bunge ya Miundombinu ilishasema hili jambo hapa, *TGFA* warudishe hizi ndege kwa *ATCL*. Mheshimiwa Rais ana dhamira hiyo nzuri kwa sababu hizi *forgone revenue* zinazopotea zingeweza hata kusaidia, mama anazunguka kutafuta fedha *while* mnapoteza fedha hizi hapa, *why are you doing that, guys?* hamlioni hili? *It is just a simple logic.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana. Mheshimiwa Waziri na timu yako na watendaji, tuone hili ni la muhimu sana. Hapa naongea tu, kama unaweza ukaleta ndege kwa mfano hiyo unayoleta ya mizigo, itaruka kwenda wapi? Ulaya si tumefungiwa, hatuwezi kupeleka ndege zinakamatwa. Hiyo ndege ya mizigo inayokuja, tunaipeleka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, tunahitaji kupata mapato. Ndege mmeileta sawa, baada ya wiki mbili inakuja. Mmeirusha wapi? Hata wa *East Africa*

mkienda Nigeria nasikia mtakamatwa. Mtairusha wapi? *South Africa* hampeleki, mnapeleka wapi?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *let us be sincere. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha, nashukuru sana. Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, atafuatiwa na Mheshimiwa Silyvestry Koka na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, ajiandae.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Ujenzi. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na uzima ambao nipo nao sasa hivi, nimepata nguvu ya kusimama, kuongea kwenye Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mbarawa pamoja na Naibu Waziri, kaka yangu Kasekenya; Mheshimiwa Naibu Waziri, kaka yangu Fredy Mwakibete; nawapongeza kwa kazi nzuri mnazozifanya na namna ambavyo mnazipitiapitia hizi barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiomba kitu ukapewa unapaswa kushukuru. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwa namna alivyoguswa na barabara yetu ya Inyala. Ajali zilikuwa nyingi sana, akatutumia fedha kiasi cha shilingi 6,998,000,000 tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuokoa uhai wa watu wengi pale Inyara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ahadi ya awamu ya nne, ahadi ile ni ya barabara ya kutoka Katumba kupita Suma kwenda Mwakaleli, Ruangwa, Mbwambo mpaka Tukuyu Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile barabara ni muhimu sana, kwa sababu inapita barabara inatokea Rungwe inatokea Busekelo kule halafu inarudi tena Tukuyu Mjini. Naiomba sana Serikali, sijasikia hapa kwamba kuna fedha yoyote ambayo imetengwa kwa ajili ya barabara hiyo ya kutoka Katumba Suma - Mwakaleli kutokea Tukuyu Mjini. Hivyo, naomba kwenye mipango yenu ya bajeti msiisahau barabara hiyo kwa sababu tumeiomba kwa muda mrefu. Naishukuru sana Serikali kwa kipande kwa sehemu kuanzia Tukuyu Mjini kule imeanza kufanya kazi nzuri ya kuweka lami, ninaishukuru Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ambayo ilikuwa ni korofi sana Barabara ya Ibanda kwenda Itungi *Port*. Barabara hiyo ni muhimu sana ambayo inapitia Kyela Mjini. Naishukuru Serikali ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ni Sikivu, hiyo barabara mkandarasi yuko *site* inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya kutoka Igawa kwenda Tunduma Mkoa wa Songwe. Ile barabara ni barabara muhimu sana. Zinapita gari ambazo zinakwenda kwenye *border* mbili; *border* ya kwenda Malawi na *border* ya kwenda Zambia. Ile barabara ni barabara ambayo ninaiongelea kila wakati hapa Bungeni. Ile barabara ni nyembamba ambayo inapitisha makontena ya 40ft, 20ft, pamoja na *petrol-tank,* lakini na mabasi yote yanapita hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile barabara ni nyembamba halafu ina *corrugation* ajali kila siku. Wananchi wa Mkoa wa Mbeya kwa tatizo la barabara ile, wengi wamekuwa walemavu, lakini wengi wamepoteza familia zao kwa ajali zinazotokea kutokana na barabara ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali ilipokuwa inawasilisha hapa sijasikia hizo kilometa 181 kwamba ni lini itaanzwa kujengwa hiyo barabara. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hiyo barabara ni barabara ambayo ina misiba, kila siku tunalia wananchi wa Mkoa wa Mbeya. Tumechoka kulia misiba. Pia walemavu wengi wanapatikana kupitia barabara ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, sijajua kwamba Mheshimiwa Waziri ile misiba ungekuwa unaona namna tunavyolia, ni kwa sababu huoni. Ungekuwa unaona, nakwambia ungepata uchungu kwamba ile barabara uipe kipaumbele. Naongea kwa uchungu kiasi kwamba natamani hata misiba wakati fulani tukiihamishia humu Bungeni kupiga yowe labda ndiyo Serikali itasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa namna ambavyo imetenga fedha, ile barabara ya kilometa 29 ya Mbeya Mjini barabara nne. Pia namshukuru Mheshimiwa Rais, katuongezea kilometa nne zingine za kuanzia pale Uyole kwenda mpaka Mlima Nyoka. Mheshimiwa Waziri akiwasilisha hapa ameongea kwamba mkandarasi yupo ameishafika na andaa utaratibu. Wananchi wa Mkoa wa Mbeya hatuona kwamba ameshaanza huyo mkandarasi, kwa sababu hatuoni mitambo yoyote, tungeanza kuona mitambo imefika, hekaheka zimeishaanza za kuandaa juu ya barabara ile basi tungejua barabara ile imeshaanza rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa namna ambavyo umenipa hii nafasi, Kkuna barabara ya kutoka Makongorosi – Lupa mpaka Rungwa ile barabara ni kilometa 356 ni barabara muhimu ambayo inakwenda kuunganisha Mkoa wa Singida na Tabora. Ningeiomba sana Serikali angalau kwa kilometa 100 ingewekea bajeti ya kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya Rujewa – Madibila; barabara ya Rujewa – Madibila ni kilometa 92, ni barabara muhimu sana kule kuna mazao mengi, mazao ya kutosha ile barabara ni mbaya. Ninaomba sana Serikali kwa matamko mliyotamka hapa kwamba mnaitambua, naomba muiwekee bajeti ya fedha ile barabara ikikamilika kilometa hiyo 92 inakwenda kuunganisha na barabara kilometa 60 kutoka Madibila mpaka Mafinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa namna ambavyo unavyoendesha Bunge letu hapa mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wastaafu ambao walistaafishwa *Air Tanzania*, wana kilio kikubwa sana, mwaka jana kuna fedha za waastafu ambazo tulipitisha hapa Bungeni, wastaafu wale wana kilio kikubwa sana, wafanyakazi ambao walikuwa wakifanyakazi *ATC*. Ninaomba usikie kilio cha wale watumishi wa *Air Tanzania* tangu walivyostaafishwa wengine miaka kumi mbili imepita hawajapewa mafao yao, wengine miaka sita na wengine wamekufa bila kupata fedha zao, ninaomba hili ulichukulie kipaumbele. Hawa watu mkiwafuta machozi yao, mkawapatia fedha zao za kustaafu basi watawashukuru sana, lakini sijajua ni nini kina zuia kama mwaka jana tulipitisha bajeti hapa mlisema ni za wastaafu ni kwa nini hamjawafikishia fedha zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimshukuru na kumpongeza sana *Engineer* wa *TANROADS* wa Mkoa wa Mbeya *Engineer* Masige, amekuwa akisimamia vizuri sana hizi barabara za mkoani kwetu Mbeya, pongezi nyingi sana zimuendee Mheshimiwa *Engineer* Masige chini ya kiongozi mkuu ambaye ni Mkuu wa Mkoa wetu Homera.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma ahsante sana. Muda wako umeisha.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. SILYVETRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Wizara yetu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kipekee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na watendaji wake wote kuanzia Wizara hadi Mikoa, hakika ni kazi kubwa inafanyika kwa miradi mikubwa mbalimbali inayofanyika kuanzia viwanja vya ndege, reli, barabara na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada za kutaka kujenga barabara ya *express way* inayoanzia Kibaha kuja Morogoro na hatimaye Dodoma ambayo itajengwa kwa ubia, hakika hii inakwenda kuwa ni mkombozi wa usafiri kutoka Dar es salaam – Kibaha hadi Dodoma ambayo leo hii unachukua muda mrefu sana na kupoteza muda wa kufanya kazi zenye tija kwa ajili ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, lakini tunazo changamoto mbalimbali katika maeneo yetu na hususani katika Jimbo la Kibaha. Mimi niseme kwamba kazi inayofanywa na *TARURA* ni kazi inayoleta siasa lakini ni kazi ambayo ina mhudumia mwananchi mpaka eneo lake ikiwa ni pamoja na mitaa katika maeneo mbalimbali na hususani Kibaha Mjini. Pamoja na ujenzi mkubwa wa hizi barabara kubwa, lakini bado wananchi wetu wanapata adha kubwa sana kwa kukosa barabara zinazoingia katika mitaa yao na wakati mvua zikinyesha wanakuwa na changamoto kubwa sana ya kufanya shughuli za kiuchumi na ukizingatia Kibaha ni Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo barabara inayotoka Sheli - Maili Moja - Shule hadi Muheza; barabara hii mvua zikinyesha haipitiki ingawa iko katikati ya Mji wa Kibaha ambao ni Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani; lakini tunayo barabara ya Tumbi – Boko Timiza, tunayo barabara ya Kwa Mathias hadi Mikongeni ambako kuna Makao Makuu ya Chuo Kikuu Huria, lakini vilevile tunayo barabara ya Kongowe – *Forestry* mpaka Yombo ambayo inaunganisha Kibaha na Bagamoyo, lakini Kongowe - Soga na Visiga - Madafu hadi Mbwawa; hizi ni barabara ambazo ziko ndani ya Mji wa Kibaha na ni barabara muhimu ambazo ningeomba ziko katika *network* ya *TARURA*. Sasa *TARURA* wapewe fedha waweze kuhudumia barabara hizi ili ziweze kutengeneza

uchumi katika miji wetu wa Kibaha na ili ziweze kuleta tija kwa wananchi ambao wanataabika sana hasa mvua zinaponyesha, wanashindwa kufanya kazi zao za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TANROADS* kazi zinaendelea kuwa nzuri, lakini bado kuna maeneo mbalimbali ambayo tunaendelea kusuasua. Barabara ya *TAMCO* - Mapinga kweli ujenzi unaendelea lakini unakwenda kwa kasi ndogo sana, lakini tunayo barabara ya Makofia – Mlandizi kupitia Mbwawa hiyo barabara iko katika Ilani toka mwaka 2015 na kila mwaka inasemekana fedha zinatengwa, lakini utekelezaji haufanyiki. Mwaka huu tunaona kwamba zimetengwa fedha kidogo sana takribani shilingi milioni 600; sasa fedha hii itafanya nini? Italipa fidia, itaanza ujenzi au itafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe kwamba sasa tunapokwenda katika miradi mikubwa na ya kimsingi kama hii ya kuunganisha mikoa basi fedha itoke ya kutosha ili ifanye jambo ambalo litaleta tija na kuonekana machoni mwa watumiaji ikiwa ni pamoja na wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunayo *Kisarawe road*, barabara ambayo inatakiwa itoke pale Kibaha Mkoani ambayo itatuunganisha na Kisarawe na yenyewe hii imekuwa katika upembuzi yakinifu, bado haijaweza kuanza ujenzi. Naomba barabara hii ijengwe ili iweze kuunganisha Wilaya ya Kisarawe pamoja na Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani ambayo ni Kibaha Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo tunayo barabara ya zamani kwa jina maarufu barabara ya Zamani. Barabara hii inaanzia pale Picha ya Ndege hadi Mlandizi; hii ni barabara ambayo naweza nikasema ni barabara muhimu na ambayo inasaidia sana hasa tunapokuwa na matatizo katika hiyo barabara kuu ya Morogoro. Ninyi ni mashahidi kunapokuwa na ajali katika barabara hii magari hayawezi kupita na ucheleweshwaji unakuwa ni mkubwa sana, hata kama kuna majeruhi kuwakimbiza hospitalini Tumbi inakuwa ni changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiyo barabara ni mkombozi katika katika jambo hilo kwamba ni barabara iliyokuwepo toka zamani na inahitaji tu ukarabati wa kawaida, sasa ukarabati umeanza kidogo, kidogo na kwa mafungu. Mimi nilikuwa naomba kwamba basi *TANROADS* ikarabati barabara hii ambayo itakuwa ni mbadala na kupunguza vilevile msongamano katika hiyo barabara kubwa ya Morogoro. Mtu anayetoka Kibaha kwa mfano anatoka pale Picha ya Ndege anataka kwenda Kongowe hana sababu ya kuja kwenye barabara kubwa na kuongeza foleni, anaweza tu akapita kwenye barabara hii na ikawa inaleta tija kusaidia kupunguza foleni katika barabara kubwa ambayo kwa sasa hivi ndiyo barabara kubwa ya kiuchumi inayopitisha zaidi ya asilimia 85 ya magari yote yanayoingia na kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka nitoe ushauri wa Wizara, kwamba *TARURA* ambayo inakwenda kutoa huduma kwa wananchi na ndiyo inayotengeneza siasa ya miundombinu kwa wananchi wetu, hakika bado hawajapata fedha za kutosha. Barabara nyingi ziko katika *network* yao, lakini fedha ya kuhudumia barabara hizi hata katika kiwango cha changarawe zipitike muda wote bado hawanazo jambo ambalo linaifanya azma hii njema ya kumpelekea mwananchi maendeleo kwa karibu ishindwe kufanyika.

Mimi ombi langu kwa Wizara, waangalie ni namna gani *TARURA* itapewa fedha zaidi ili barabara hizi zote ambazo ziko katika *network* angalau zifike katika kiwango cha changarawe kama hazitaweza kwenda katika kiwango cha lami ili azma ya kumuhudumia mwananchi kwa karibu iweze kuwepo na waweze kunufaika sasa na hizi barabara kubwa za *highway. (Makofi)*

Mheshiwa Mwenyekiti, ya kwangu ni hayo machache na ninaunga mkono hoja, tuko pamoja na Wizara yetu ya Miundombinu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Koka, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma atafutiwa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile na Mheshimiwa Robert Maboto ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Geita Vijijini kwa kazi kubwa aliyotufanyia na nasimama kwa kujiamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaiona hii siti niliyokaa, hata mwaka 2026 niko hapa hapa, kwa sababu ya hii Wizara. Mimi nakaa kilometa 54 tu kutoka ninakotoka jimboni kwangu kwenda Geita Mjini, lakini kilometa kama 105 kutoka jimboni kwangu kwenda Mwanza ambayo ndiyo Geneva yetu kwa Kanda ya Ziwa. Tulikuwa tunatumia saa saba hadi kumi kwenda Mwanza; saa tatu kwenda Geita. Pamoja na kwamba sina lami, lakini nikupongeze sana kaka yangu Mbarawa, Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa na Wizara yako unayoendelea kunifanyia kwenye jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli pamoja na kwamba umenipiga kidogo kanzu kwenye kusaini, sijaona kwangu lakini Meneja wangu yuko hapa tusije tukakabana baadae naamini kabla ya mwezi wa saba na mimi nitafanya sherehe kubwa ya kusaini mkataba wa lami kwa mara kwanza toka miaka 60 ya uhuru na tunapata hizo kilometa 20 na nikuombe Mheshimiwa Mbarawa tutakutana kwenye *corridor* pale, ongeza tano ziwe hata 25 *at least* sijaona humu, lakini mimi naamini Serikali inafanya kazi kubwa, imetutambua hata sisi watu wa kijijini, wananchi wangu wananiona hapa, nina kila sababu ya kukupongeza na kuipongeza Wizara yako kwa sababu kwa kweli pamoja na kuwa hatuna lami, kwetu kunapitika Mheshimiwa Waziri kunapitika, unatereza hata mimi mwenyewe naenda vizuri tu nalala kijijini kwangu wala sina shida, Mungu akubariki sana wewe pamoja na Wizara yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri wananchi wangu wananisikiliza. Tumehaidi mwaka jana na mzee wa sarakasi tulikuwa *batch* moja. Umeishasaini kule kwa mzee wa

sarakasi, sasa mimi bahati nzuri sana ni bondia ambaye nilitarajiwa kupambana na January akanimbia, sitaki kupambana mimi na wewe maana mimi nakula ugali Mheshimiwa Waziri kisije kikakutokea kitu cha ajabu.

Naomba ukamilishe mchakato uje usaini mkataba kwa wananchi wangu nakuomba na mkataba huo utasainiwa Nkome watu wanasuburi kuona lami. Unajua kwetu ukiona lami Gwajima yuko hapa, ndiyo itakuwa sehemu ya kwenda kuogea hata mizimu Mheshimiwa Mchungaji hata mizimu unaogea maana tunaogea kwenye mawe sasa tukipata ka-lami utakuwa unaogea hata *roundabout*. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, wananchi wa jimbo langu wanatamani kuona lami na nikuombe nisikilize na njoo uweke mimi na wewe hatuna tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nilindie dakika zangu mimi ni mmoja wa Wabunge nilioenda Dubai kuona uwekezaji ulioko Dubai wala sijifichi nilienda kwenye ziara ya Kamati ya Mheshimiwa Mbarawa na mimi kidogo sijui unaweza ukanunua akili yangu bei gani, maana na mimi ni la saba mwaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tunachelewa kwenda kwenye maendeleo kwa sababu ya *degree*. Mimi na twende taratibu *degree risk assessment,* mchakato; haya mambo yatatuchelesha, upembuzi yakinifu jamani..., tulikuwa humu Bungeni Bunge lililopita. Mimi nilikuwa Mbunge wa kwanza kwenye Wabunge tulioenda kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, *risk assessment* humu, sijui nini walichelewesha haya mambo na kuna wengine wanapinga humu ndani walikuwa Mawaziri kwenye hizo. Mazingira tutakata miti, kuna vyura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi unajengaje reli ya kisasa ya matrilioni kwenda Congo, kwenda Mwanza halafu una bandari inayotoa mabehewa 120 kwa siku. Tunachelewa sana ni lazima ninyi wasomi sasa ikifika mahala tutagawana, unajua gita lina kitu cha kukoleza, Nape ni mtaalam, mimi nitaondoka na kale kakukolezea spika hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachelewa kwa sababu ya watu wachache wajinga ambao kila kitu unataka ushirikishwe, sawa. Tunataka tuletewe mkataba humu kila mtu atachangia dakika kumi lipi ambalo unaweza kupinga kwenye dakika kumi? Twende taratibu ni lipi? Niulize humu lipi? hivi tumefika mahala sasa na watalamu wotee ni wajinga? Mpaka *CAG* naye anayetugombanisha humu nae ni mjinga? Maana sisi tuna jicho lakini hatuamini, haya mtu anakuja anazungumza miaka kumi, miaka 20 ya *TICTS* ilitufikisha, ikatupeleka; sawa miaka 20 si tulikuwa darasani au wenzangu hamsomi? Tumefika mahala sasa tunang'amua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dubai *DP World* ukifika pale mimi nilienda na Wabunge wenzangu tukawa kama 30; kule bandarini mimi sikuona watu, niliona mashine tu zinapishana hivi "*kakakaka*" kadada kadogo hivi nikakaomba na namba ninayo hapa kakibonyeza hivi kontena linaenda. Tutoke huko tulikobaki hatuwezi kwenda kwenye hiyo mifumo...

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti)*.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Nasikia sauti Mheshimiwa naongea na kiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma, endelea na mchango wako.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Naendelea.

Mheshimiwa Mwambe nakuheshimu sana, usiingie kwenye kumi na nane, mimi hunipigi *swagga brother*. Tulikupa nafasi na uli-*fail,* ndiyo maana uko-*backbencher,* tena nyuma yangu nipige taarifa uone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwasikilize watu wa hovyo, hii nchi ni yetu wote, tunajenga meli Mwanza ya mabehewa kwenda Uganda, tunatengeneza reli kwenda Congo halafu unakuwa na watu kama Mwambe huyu, simama huyu. Wewe

mchakato, tulikupa nafasi kutoka *EPZ* mimi mwenyewe umenifelisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Taifa ni letu wote, mliosoma na sisi, niwaombe tena tumechelewa, tumechelewa kila mtu ana uwezo wake humu ndani, kuna mtu ana uwezo wa akili na mtu mwingine anauwezo kama wa kwangu mimi najivuna kwa sababu gani? Sina shule, lakini mimi ni msukuma, najisimamia mwenyewe, hatuwezi kutembeza *imprest* Bungeni humu. Tusitembezee mawazo ya watu wachache kuja kununua Bunge, pinga haya tusimamishe anayepinga hapa atueleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanajua tunatoka sasa reli ya ngongongo au labda mwenzangu hajapanda treni, ngongongo tunaenda mshale, halafu una watu 900/1200 bandarini hayo si mawazo potofu kama ya kina Mwambe hawa. Nikuombe sana huyu ni Mbunge mwenzangu, usijichanganye kunipiga *swagga*, kwa sababu nimemsikia amesema wewe; na yeye ni mpingaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma endelea na mchango wako…

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nikuombe hii nchi ni ya kwetu wote na nazungumza kwa sababu mimi ninafaida na reli ya mwendokasi, tusisubiri haya mawazo ya kujaribisha, twende mbele, hawa watu wanao tuletea mawazo ya kujaribisha kutegana tegana humu mimi nina miaka 61 leo ya uhai wangu tusije kuchambuliana ma–*file* humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe na niwashawishi Wabunge wenzangu kwamba kiukweli huwezi kuwa na *train* ya mwendokasi, unatoka kwenye makontena ya kusahihisha, basi inawezekana wenzangu hawajawahi kupita bandarini. Ukipita pale bandarini usumbufu uliopo unaweza ukalipa *TPA,* ukaambiwa leo sijui *portal,* sijui Harris hayupo, mnakaa hata wiki mnasubiria makontena na *storage* inasoma. Jamani hatuwezi, tunasomesha watoto wenye *degree* zao watu wa *IT* halafu

tunang'an'gana kukaa *analogue*. Mimi mwenyewe natoka kwenye *analogue* sasa hivi ni *doctor. (Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niangalieni vizuri natoka kwa sababu naendana na wakati ningepewa hii *doctor* ya heshima miaka kumi iliyopita nisingeelewa lakini leo tu–*complete* na mimi na mtu anayepinga hapa tukakae kwenye *tv* watu watusikilize tumwage *material*, hatuwezi kuwa na *degree* ambazo hazija..., kizungu mnasemaje?

**MBUNGE FULANI:** Hazija-*qualify.*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Hazi–*qualify,* yaani kwenye maisha halisi, nashukuru kukaa na yaani lazima tutoke huku, unaweza ukajaza Taifa la *degree* za watu wa hovyo na mkabaki kuwa wa hovyo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Sekunde 30.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja. Ukienda Dubai nakupa mfano mzuri. Mimi nimebahatika kumuona Mfalme wa Dubai, huyu hapa nilikuwa na mtafsiri wangu. Ziara yangu kutoka jimboni na wananchi wangu wananisilkiliza. Nikamuuliza umeijengaje Dubai? akaniambia wakati naanza kutoka kwenye maisha ya Dubai kuwatengeneza watu waione Dubai tunayoiona leo, wakaniambia nilivyoanza kuwaruhusu watu wajenge kutoka mataifa mbalimbali wale wazee maarufu wa Dubai wakaandamana. Walivyoandamana akawaambia njooni tuzungumze Ikulu. Wakaenda kuzungumza akawaambia mna shida gani? Unauza Dubai kila mtu unampa hati; kuna Wanaigeria kuna Watanzania, kuna Wahindi kuna Wazungu; mwisho wa siku sisi tunaondoka Dubai, akasema, sasa

mna tatizo na nilichokifanya? ndio. Tufanyeje? akawaambia sasa nyie mmekuja wangapi? 150. Nawagawanya mara mbili 75 mtakaa *airport,* 75 mtakaa bandarini. Ndio njia ya kutoka Dubai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona mtu amekuja na nyumba anaipakia kwenye meli nakutumia na jeshi mnisaidie kunipigia simu tu. Leo Dubai ukienda pale sijui vizuri kizungu utaona majumba. Nyinyi mnang'ang'ana na vitu vya kijinga. Mtu akitaka kujenga unawaambia huyu ni mzungu, ukimpa ardhi tuta, ndiyo tutabaki na tunalima mazabibu. Haiwezekani. Tuachane na wapingaji tutengeneze Tanzania ya kisasa, tupambane na bandari zinazotuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, atafuiatiwa na Mheshimiwa Robert Maboto, Mheshimiwa Ally Mlangila Jumbe, ajiandae.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata na fursa ya kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi. Wizara hii kwangu kama Mbunge wa Jimbo la Kigamboni ni Wizara ambayo inagusa maisha ya kila siku ya wananchi wa Kigamboni. Kwa sababu hiyo nitajielekeza katika hoja tatu ambazo zinagusa Jimbo langu la Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni suala la Daraja la Nyerere. Daraja hili limejengwa kwa ubia kati ya Serikali na Shirika la *NSSF*. Daraja hili ni la kulipia; hoja ya wananchi wa Kigamboni bado iko palepale. Wananchi wa Kigamboni ni walipa kodi wa nchi hii. Wananchi wa Kigamboni michango yao na kodi zao zinachangia katika ujenzi wa madaraja mengine nchini lakini wananchi wa Kigamboni ni wananchi pekee katika nchi yetu ambao wao pekee wanachangia katika kuingia na kutoka Kigamboni. Kwa hiyo wananchi wa Kigamboni wamenituma kuja kusisitiza hoja yao ya kutaka daraja lile liondolewe ile tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri, tulifanya mapunguzo ya tozo lakini bado wananchi wa

Kigamboni wanasisitiza kwamba tozo ile iondolewe ili wapate ahueni ya maisha. Gharama za maisha kwa wananchi wa Kigamboni kwa kweli ni kubwa sana, hususan katika bidhaa zote zinazoingia Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nilikuwa nataka kuchangia ni suala la vivuko. Kivuko cha Kigamboni kinapitisha takribani watu 50,000 mpaka 60,000 kila siku na magari takribani 2,000 kila siku. Ni watu wengi sana. Lakini kumekuwa na changamoto nyingi sana katika kivuko kile. Kwanza, sehemu ya kusubiria abiria ni ndogo sana, hususan katika kipindi cha asubuhi na jioni. Lakini mifumo ya ulipaji fedha, kwa maana ya *N-card* nayo imekuwa na changamoto ya mifumo kuwa *down,* jambo ambalo linapelekea wananchi kupata usumbufu muda mrefu. Vile vile njia za kuingilia na kutokea katika kivuko hususani kwa upande wa Kigamboni na upande wa Magogoni nazo zimekuwa ni finyu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katia taarifa ya bajeti hii kwamba mmetenga milioni 300 kwa ajili ya kulipa fidia, fedha hizi ni ndogo sana. Mwende mkaangalie jinsi gani ya kuweza kufanya. Lengo letu na kusudio letu mfanye kama ilivyofanyika pale kwenye Daraja la Nyerere, kuwe na njia saba za kuingilia na njia saba za kuweza kutokea na hii itasaidia sana. Muangalie vile vile jinsi gani ya kuweza kufanya kuhakikisha kwamba tunakuwa nae neo la ku–*park.* Si kila mtu anataka kuvuka na gari. Nilikuwa natamani kuona kwamba kuna sehemu ya *parking* ambayo mtu anaweza aka–*park* gari yake akavuka akaenda mjini kwa sababu kuna watu wengine wanaofanya kazi pale maeneo ya Kivukoni haitaji kuvuka na gari Kwenda mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ukishatoka kwenye kivuko upande wa kushoto ni eneo la bandari, hii ni Taasisi mama na sisi dada na *TEMESA*. Mimi nadhani suala hili liko ndani ya Wizara yenu, naomba mkae muangalie jinsi gani ya kufanya mawasiliano ili eneo ambalo halitumiki kwa upande wa bandari baada ya kuvuka upande wa kigamboni basi liweze kutumika katika sehemu ya *park and go.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nitoe ushauri kwa Mheshimiwa Waziri, *TEMESA* ni Taasisi ambayo inasimamia masuala ya ufundi umeme na masuala ya vivuko. Mimi ushauri wangu, tuwekeze katika Nyanja ambazo tunaona zinakwenda kuwa na tija. Sasa hivi TEMESA Imejitawanya sana katika masuala ya *mechanical*, masuala ya *electrical* pamoja na masuala ya vivuko. Tukiweza kuijengea uwezo vizuri *TEMESA* katika masuala ya ufundi wakaweza kufanya matengenezo ya magari yote nchini, kwa maana ya magari ya Serikali, jukumu hilo peke yake linawatosha sana. Lakini vilevile wakatoa ushauri katika masuala ya umeme tukawanunulia vifaa, tukawapatia nyenzo za kuweza kufanya kazi. Majukumu haya yanatosha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mimi kama Mbunge nitaendelea kusimama na kusema kwamba suala la vivuko liondolewe *TEMESA*. Wapeni watu wenye uwezo waende wakaifanye hiyo kazi. Wananchi wa Kigamboni wanahitaji usafiri wa uhakika ili wasafiri salama. Sasa hivi kutoka Kigamboni sehemu ambayo *straight* haifiki hata kilomita moja watu wanasubiria Zaidi ya saa moja. Tunataka ifike mahali ambapo mwananchi akifika pale dakika tano yuko upande wa pili wa mjini. Kwa hiyo nitaendelea kusisitiza kwamba huduma za vivuko zibinafsishwe. *TEMESA* ibaki na majukumu ya msingi ya huduma za umeme na ufundi na hao mkiwawezesha vizuri wataweza kufanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ambalo nilikuwa nataka nilisemee ni suala la miundombinu ya barabara. Katika wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam Wilaya ya Kiagamboni ndiyo wilaya pekee katika Mkoa wa Dare es Salaam ambayo iko nyuma sana katika miundombinu ya barabara. Katika miundombinu ya barabara za *TANROADS* tuna asilimia 37 tu; na zaidi ya asilimia 50 ya barabara zote za *TANROADS* katika Mkoa wa Dar es Salaam ambazo hazijawekwa lami ziko katika Wilaya yetu ya Kigamboni. Tumechelewa sana na tuko nyuma sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigamboni ni Wilaya ambayo inakuwa kwa kasi kubwa mno. Sasa hivi uwekezaji wa viwanda ni mkubwa, kasi ya ujenzi ni kubwa, na Kigamboni ndilo eneo pekee ambalo sasa hivi vinapatikana viwanja vingi sana, na hata

nikiangalia hapa ndani ya Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nina Wabunge nadhani theluthi moja kama si zaidi ni wakazi wa Kigamboni. Wamejenga au wana nyumba kule Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niombe sana Wizara ya Ujenzi iweke msukumo katika miundombinu ya barabara. Sasa hivi barabara ya kutoka Gomvu Kwenda Pembamnazi tulikuwa tumeijenga kwa kilomita moja moja ni ndogo sana. Kumekuwa na ujenzi mkubwa wa viwanda katika maeneo ya Kimbinji na tumetenga eneo la uwekezaji kule Pembamnazi, na hata Wizara ya ardhi imepima viwanja kule lakini watu wanashindwa kujenga kwa sababu hakuna miundombinu ya kuweza kufika kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Barabara ya Kibada – Mwasonga kueleke Kimbiji na Tundusongani, hili nisipolisema kwa kweli wananchi wa Kigamboni hawatanielewa. Barabara hii tuliipitisha katika bajeti ya mwaka jana, katika barabara chache ambazo Serikali iliridhia na tukaipitisha kwenye bajeti. Lakini nitoe malalamiko yangu makubwa sana, kwamba mchakato wa barabara hii umekwenda taratibu sana. Ni jana tu Mheshimiwa Waziri ndipo amekuja kunithibitishia, jana, kwamba tenda imefunguliwa juzi, Mkandarsi amepatikana. Na mimi nimemwambia Mheshimiwa Waziri jana, kwamba mchakato utakapokamilika aje yeye mwenyewe Kigamboni kutia saini ule mkataba na kuwaambia wananchi wa Kigamboni ujenzi unaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka umeniambia kwamba mkandarasi amepatikana, na tunategemea ndani ya mwezi mmoja ujenzi wa barabara mkandarasi wa barabara ya Kibada Kwenda Mwasonga atakuwa amepatikana. Nikutake Mheshimiwa Waziri uje wewe mwenyewe Kigamboni katika sherehe ya utiaji saini ya ile barabara ili na wewe useme na wananchi wa Kigamboni. Nimechoka kuwasemea kwa niaba yako, mchakato umekuwa ni mrefu sana, barabara hii tulipitisha kwenye bajeti ya mwaka jana, na sasa hivi imebakia mwezi mmoja kabla ya mwaka wa fedha kuisha. Kwa hiyo nikuombe sana, kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha uje Kigamboni utie

saini hii barabara. Umenithibitishia wewe mwenyewe kwamba mkandarasi ameshapatikana kwa hiyo ndani ya mwezi mmoja kamilisha hizo taratibu za mikataba ili uweze kuja kuwatangazia wananchi wa Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimuombe vilevile Mheshimiwa Waziri kuhakikisha kwamba hizi barabara nyingine *especially* ya Gomvu, Kimbiji mpaka Kwenda Pembamnazi nayo tunaiongezea wigo kuhakikisha kwamba nayo inafika Pembamnazi kwa sababu hili ni eneo la kimkakati na ni eneo la uwekezaji. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri wakati unapokuja kuhitimisha mimi nitaomba nipate *commitment* yako katika maeneo haya yote ambayo nimeweza kuyataja ili wananchi wa Kigamboni waweze kusikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndugulile. Mheshimiwa Robert Maboto atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, Mheshimiwa Kingu ajiandae.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii mchana huu wa leo ili na mimi niweze kuchangia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya kwa ajili ya kupeleka fedha za maendeleo katika majimbo yetu ili kukamilisha miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niishukuru Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inayoongozwa na Mheshimiwa Makame Mbarawa na Naibu wake kwa kazi kubwa ambayo wameendelea kuifanya, lakini pia kwa namna ambavyo wametekeleza mradi mkubwa wa barabara ya kiwango cha lami kutokea Jimbo la Mwibara, Jimbo la Bunda Mjini, na Jimbo la Bunda Vijijini. Barabara hii ilisumbua kwa muda mrefu lakini kwa sasa imeendelea kukamilishwa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Wizara ni kuhakikisha kwamba barabara hii wakati inajengwa tuta lile lililowekwa kwenye barabara ile limekuwa juu sana kuliko makazi ya wananchi wetu. Niwaombe sana Wizara ikumbuke kuwawekea wananchi wetu barabara zile zinazoingia katika makazi yao ili ziweze kuendana na hali halisi ya barabara yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine katika barabara hii. Wizara ituwekee taa za barabarani ambazo zitakuwa zinatokea kwenye maungano ya barabara pale kuelekea barabara ya Kibara na hii barabara inyokwenda Nyamuswa, watuwekee taa za barabarani. Lakini pia katika barabara hii tuna taa za upande mmoja kutokea Balili Kwenda Nyasura, ambako taa hizi zimewekwa upande mmoja na upande mwingine hakuna taa. Kuhusiana na jambo hili mimi nilishajaribu kuzungumza na Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa, nikamuomba, kwamba, katika meneo mengine mengi ambayo mimi nayaona taa zote za barabarani zimewekwa kwa pande zote mbili, ni kwa nini, Bunda tu peke yake kuwe upande mmoja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri atusaidie kwenye jambo hili ili liweze kuendana na hali halisi; ambapo taa zinawekwa katika maeneo yetu. Lakini jambo jingine, Mheshimiwa Waziri nikushukuru katika Jimbo letu la Bunda Mjini katika Bajeti tumepata taa za kuongozea magari kwenye makutano yale ya barabara ya Kisorya, Nyamuswa, Mwanza na Musoma; tumepata taa za kuongozea magari. Na jambo hili mimi nililisema nikasema kwenye eneo lile tukisema tuweke ule mzunguko eneo lile ni dogo kwa sababu litatulazimisha kwenda kubomoa makazi ya wananchi wetu. Naishukuru Wizara, na kwa sababu imekubaliana na hili jambo lile likifanyika naamini kwamba litaufanya Mji wetu wa Bunda uweze kukaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia jambo jingine tunaishukuru Wizara kwa sababu wanatekeleza miradi mikubwa pale ya kujenga mizani katika Halmashauri yetu ya Mji wa Bunda Kata ya Balili na kata ya Buta. Sasa mizani hii ina muda mrefu. Niwaombe sana Wizara muhakikishe kwamba viongiozi wetu wa

Mkoa wa *TANROADS* wanasimamia miradi hii ili iweze kukamilika vizuri, lakini mizani hii ikikamilika kwa wakati itatusaidia kulinda zile barabara zetu, hasa hii barabara mpya inayokwenda Kisorya na inayokwenda Nyamuswa, ya lami, mzani ule utatusaidia kulinda sana ule ulioko kule Buta; na hii barabara kuu ambayo inakwenda Mwanza na Musoma. Mizani hii ikamilika kwa wakati ili iweze kulinda barabara hizi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Mheshimiwa Waziri jambo jingine ni kuhusiana na Mfuko wa *TARURA*. Tuiombe Wizara iendelee kuwaongezea fedha watu hawa wa *TARURA* ili waendelee kutusaidia katika barabara zetu zile za mitaa ili zikamilike. Kazi imefanyika Mheshimiwa Waziri lazima tukuthibitishie hilo lakini bado tatizo lipo, kwa sababu barabara zile kwa muda mrefu zimekuwa hazifanyiwi matengenezo. Kwa kipindi hiki tumeona matenegenezo yanafanyika na wananchi wanaona hatua zinachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana tuendelee kuwapa *TARURA* nguvu kwa kuwapitishia bajeti ya kutosha ili kwamba weze kutusaidia kuhakikisha kwamba barabara hizi zinapitika kwa muda wote, na hasa kwa sababu mji wa Bunda ndio sura halisi ya Mkoa wa Mara. Utakapokaa vizuri mji wa Bunda ndiyo picha halisi ya Mkoa wa Mara, na kwa sababu pia tuko pembezoni mwa Mbuga ya Serengeti. Mtu yoyote mtalii anayekwenda Mbuga ya Serengeti lazima apite Bunda. Mtu yoyote anyetoka Mwanza nakwenda Silali Kenya lazima apite Bunda. Anaweza asipite mahali pengine popote lakini Bunda Mjini lazima apapite. Kwa hiyo ni vizuri Mheshimiwa Waziri jambo hili la taa za barabarani, taa za kuongoza magari zikawekwa katika Halmashauri ya Mji wa Bunda ili iweze kuleta mvuto mzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri jambo jingine ni suala la Barabara ile ya Manyamanyama, Kabulabula, Muhoji, Masinono Kwenda Bugwema ambayo inakwenda kwenye shamba la kilimo la Bugwema. Barabara ile ni pamoja na barabara ile ambayo inatoka Musoma Mjini kwenda Majita ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo Barabara hii nayo ya Manyamanyama, Kabulabula, Muhoji, Masinono

ikijengwa kwa kiwango cha lami itawasaidia wale watu wenye magari makubwa ambao wanalazimika kwenda kupita kuzunguka kule mbali, wakapita hapa ikawa ni rahisi kwenda kwenye shamba letu la Bugwema na kwenda kuchukua mazao ya wananchi huko. Kwa hiyo niwaombe sana Wizara jambo hili na lenyewe waliangalie ili waliweke kwenye mpango wao ili liweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii itakapokamilika vizuri itaufanya Mji wetu wa Bunda ukae vizuri. Na sasa hivi tatizo kubwa ambalo tunalo pale lililobakia ni hizo barabara za mitaa. Niwaombe sana Wizara, na kwa sababu bahati nzuri tumepata Meneja mzuri pale wa *TARURA* wa Wilaya ndugu yangu Baraka na Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa, tunashirikiana nao vizuri kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo hili la uchakavu wa barabara katika maeneo yetu. Niwaombe sana Wizara watu hawa twende nao vizuri ili waweze kutusaidia kuhakikisha kwamba changamoto zetu hizi za wananchi tunazitatua vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninakushukuru na ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Robert. Mheshimiwa Ally Mlangila Jumbe, atafuatiwa na Mheshimiwa Kingu na Mheshimiwa Lusinde, ajiandae.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilipokuwa najiandaa kuchangia nilikuwa na mlolongo mrefu sana wa pongezi na shukrani. Nilitaka nianze na Waziri nikimlinganisha na msemo usemao wembamba wa reli unapitisha gari moshi, lakini nikarudi kwamba yupo Kasekenya yupo Atupele Mwakibete, wao wana uwezo pia wa kuongeza kidogo huku kwa Mheshimiwa Waziri. Nikataka niende kwa ma–*DG* ndugu zetu akina Kadogosa, akina Mbosa, akina Matibila mpaka kwa Meneja wangu wa *TANROADS, Engineer* Masige.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho wa siku nimejikuta pongezi hizi nazijumuisha sehemu moja tu kwa yule ambaye alipewa jicho na Mwenyezi Mungu la kuwatambua vipaji vya

hawa watu na kuwapa kuendesha Serikali hii, naye siyo mwingine anaitwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pongezi nyingi sana na shukrani kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani hizi zinakuja pia kutoka kwa Wanakyela. Ni hapa juzi tu tulipata janga la kukatika daraja pale Nsesi. Nilipopiga simu moja tu kwa Mheshimiwa Waziri daraja pale tayari. Mheshimiwa Waziri nataka nikwambie daraja liko tayari *Engineer* Masige ameshafanya mambo, daraja lile mpaka wiki ijayo litakuwa limeanza kupitika, ahsante sana. Wananchi wa Ngonga, Katumba Songwe, na Ikolo wanakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya ni lazima nitoe shukrani kwa mambo makubwa yaliyofanyika Kyela. Barabara ya Ibanda - Itungi *Port* kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania, imekuwa kuwekewa saini pale Kyela, na ndipo tulipoanzia. Hii ni historia kubwa Kyela kuanzisha na haya ni mapenzi ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu kumtuma Waziri kuja hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi yanayoenda kufanyika. Tunaanza kujenga barabara ya Katumba – Songwe – Ileje ambayo tayari imeshaanzia upande wa Ileje inarudi huku; hii ni heshima kubwa. Vilevile kuna madaraja makubwa kama Daraja la Ipyana, Daraja la Bujonde pamoja na Daraja la Irondo; haya ni mambo makubwa ambayo tunafanyiwa shukrani nyingi sana. Pamoja na hayo nimeona leo nitoe pongezi kwa Waziri na Wizara yake kwamba kwa mara ya kwanza sasa nchi yetu inaanzisha mfumo mzuri sana wa ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nimeona leo nitoe pongezi kwa Waziri na Wizara yake kwamba, kwa mara ya kwanza sasa nchi yetu inaanzisha mfumo mzuri sana wa ujenzi wa barabara pamoja na sehemu nyingine za bandarini. Haya yote yanatokea kwenye mfumo wa *PPP*. Ningeomba hata hii *EPC + Finance* bado tuiache nyuma tukimbilie kwenye *PPP,* kwa sababu moja tu kwamba, huu ndio mfumo ambao uko duniani kote, yaani habari ya mjini, habari ya dunia ni *PPP*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe Mheshimiwa Waziri mfano mmoja, Bandari ya Hamburg, Wajerumani wanaita Hamburg Hafen, ni bandari ambayo wao wenyewe kwa heshima wanaiita *Das Tor zur Zukunft*, maana yake ni lango la kwenda *to the future, a door to the future*. Pale yupo mtu mmoja anayeitwa CSCO *(Chinese Shipping Company),* wanaendesha *terminal* ya *container* pale, lakini ukienda Rotterdam pale *CSCO* wapo. Wajerumani walikuwa wanajiuliza hivi tumeuza bandari hii kwa Wachina?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujerumani wamesema hapana. Mfumo wa sasa ni wa kuendesha kwa pamoja Serikali na wawekezaji. Nataka nimwambie Waziri tunampigia makofi kwa kuingia kwenye mfumo huu, ataitoa Tanzania ilipo kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunataka tutoke kwenye bandari twende kwenye barabara. Mfumo wa sasa wa ujenzi wa barabara kwa pesa tulizonazo hatutaweza kusonga mbele kwa kutumia pesa za nchi hii, ni lazima tuweke uwekezaji na tunashukuru tayari umeshaanza. pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri. Pamoja na pongezi hizi naomba sana baadhi ya mambo yafanyike kwa ufanisi na tuendelee kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mbeya ni Mkoa mkubwa sana, lakini ni Mkoa ambao mazingira yake ni tofauti kabisa na mikoa mingine. Ninachokiomba ni kwamba, tunapojadili na Mheshimiwa Waziri anapofikiria juu ya kutoa bajeti kwa Mkoa wa Mbeya, kwa barabara za Mkoa wa Mbeya, asiwaze jinsi ya kugawa, hebu afikirie mambo mawili tu makubwa, aangalie jiografia, lakini angalia *terrain* ya Mkoa wa Mbeya. Ukishuka kule Kyela, Kyela iko chini ya maji, ili ujenge barabara unahitaji ujaze mita mbili ndipo barabara ipitike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka Kyela kilometa 50 tu, ukipandisha Rungwe, ukifika Mbeya, barabara inahitaji ukate milima mita sita, haya hayatokei mahali pengine, yanatokea Mbeya na ndio maana nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri, leo hii barabara imeshindwa kutoka Matema kwenda Ikombe na

niliwahi kusema hapa, watu walishangaa kwamba, hii ni Tanzania au uongo na kuna watu walinifuata wakaniuliza unachokisema ni kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwaambia Kijiji cha Ikombe tangu kuumbwa kwa dunia hawajawahi kuona gari, watu wakashangaa. Nataka niseme ni kweli hakuna gari, lakini kibaya zaidi tangu tumeanzisha dunia hii kila Mbunge anayeenda kule analiliwa kilio akifika, mimi naanza kuogopa kwenda; nimeenda mwezi juzi, wananchi badala ya kunipokea wakaanzisha misiba, hiyo misiba ni ya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni misiba ya akinamama ambao walishindwa kujifungua kwa sababu Ziwa lilichafuka wakashindwa kuja Matema, akinamama wamefariki na mimba. Hii ni nchi ya Tanzania ambayo inaendeshwa na mwanamke mwenye uchungu. Nataka niombe, Barabara ya kutoka Matema kwenda Ikombe, tafadhali sana wananchi wamelia wamechoka, hatutaki tuendelee na misiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ninayoyasema wananchi wanayasikia na Tanzania sasa iangalie. Kuna sehemu ambazo ni lazima ziwe za kipaumbele pamoja na kwamba, bajeti ni finyu, lakini wapo wananchi ambao wanahitaji huduma hii kwa umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jumbe. Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, tutamalizia na Mheshimiwa Livingstone.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu kabisa naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa heshima kubwa uliyonipa ya kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara hii nyeti kabisa ambayo inahusiana kabisa na kuchochea maendeleo ya Taifa letu. Nakwenda kuzungumza maeneo mawili matatu kwa kifupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nitumie nafasi hii kama wengine walivyofanya kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Mbarawa na wasaidizi wake wawili Manaibu Waziri pamoja na Makatibu Wakuu wanaoongoza Wizara hii kwa ufanisi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Singida, nimuombe Mheshimiwa Profesa Mbarawa, tunatambua kazi kubwa sana wanayoifanya Mheshimiwa Profesa na Wizara yake katika ujenzi wa kufungua barabara za kiuchumi. Barabara ya Tanga inayotokea Kiteto kuja kutokea Kondoa kwenda mpaka Singida, tunampongeza sana Mheshimiwa Profesa Mbarawa na Wizara yake. Sasa nimwombe, ili tuwasaidie wananchi wa Mkoa wa Tabora na Singida, wananchi wanapotoka Tabora wanazunguka Nzega, Igunga, Arusha, wanakwenda Same, wanakwenda Tanga, hiyo barabara ni ndefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nampa Mheshimiwa Profesa *alternative* ya barabara. Hii ambayo ameifungua kutoka Tanga kuja mpaka Singida, aje jimboni kwangu kuna barabara inatoka kwangu inakwenda Mtunduru, inakwenda Igombwe, inakwenda Iyumbu, inakwenda mpaka Tabora, hapa atakuwa amekata zaidi ya kilometa 200 za watu kuzunguka kufika Tanga. Sasa namwomba kaka yangu Waziri na Wizara yake, afanye *feasibility study,* afungue barabara hii na kuna shughuli nyingi za kiuchumi zinakwenda kufanyika pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naomba niwasemee watu wa Kusini. Inawezekana kabisa watu wa Kusini wametumia muda mwingi sana kujisemea wakaonekana huenda wanazungumza sababu wao wanatoka Kusini. Sasa huenda leo mimi Mbunge wa Singida Magharibi nikizungumza kwa maslahi ya Taifa na nchi, huenda naweza ninaweza nikaeleweka na kuleta tija kwa maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma *statistics* hapa, *feasibility study* inaonesha sasa hivi ndani ya miezi 14 zimesafirishwa tani za makaa ya mawe milioni 2.3. Ukienda kwenye *statistics* unahitaji kama lori moja litakuwa linafanya kazi ya kusafirisha haya makaa

ya mawe, unahitaji malori 2,000 kuweza kuya-*tap* makaa ya mawe kule yanakozalishwa kuyafikisha kwenye bandari tayari kwa kusafirishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nchi, kupanga ni kuchagua. Hivi kweli barabara zetu zinaweza zika-*afford* malori 2,000 kupita barabarani na kuangalia gharama kubwa ambayo Serikali inaingia katika kujenga barabara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa niaba ya watu wa Kusini. Leo nazungumza kama Mbunge wa Singida Magharibi, mimi sitoki Kusini, lakini nazungumza jambo hili kwa sababu limebeba maslahi mapana ya Taifa hili, limebeba maslahi ya kiuchumi ya Taifa hili. Mheshimiwa Profesa Mbarawa *feasibility study* iliyofanywa mwaka 2016 chini ya *RAHCO* inaonesha namna gani *potential* ya kiuchumi ya ile *corridor* ya Mtwara tunayoizungumza jamani. Kuna *potential* za kiuchumi kule, kuna *potential* za utalii, kuna *potential* za kilimo, kuna *potential* za *investment* nyingi zimewekwa kule. Naomba nitoe ushauri, wamwache Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aandike kitabu chake mwenyewe, wamwache mama Samia atengeneze *legacy* yake mwenyewe kwenye uongozi, wamwache mama yetu aruhusu mifumo ya uwekezaji. Tukajenge reli ya *corridor* ya Mtwara tuweze ku-*tap coal* inayozalishwa kule na kuileta katika Bandari ya Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie, tukiwa kama Wabunge, tukiacha kuangalia ukanda tukaweka maslahi ya nchi mbele, Taifa hili litapiga hatua. Nataka nikwambie wapo wawekezaji wako tayari kufanya *investment* za *build, operate* na ku-*transfer,* wamejaa Mheshimiwa Profesa Mbarawa, lakini *PPP* pia zinafanya kazi. Kama Serikali hawana *finance,* watafute *private sector* wakawekeze, hawa watu wa Mtwara wakiwekeza haitakuwa kwa faida yao, itakuwa ni kwa faida pana ya maslahi ya hili Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Profesa Mbarawa chondechonde, kama kuna vitu atakuwa amemsaidia Rais wetu kuacha *legacy* ni kumruhusu Rais wetu wa Awamu ya

Sita ajenge reli ya *corridor* ya watu wa Mtwara kwa lengo la ku-*tap resources* zilizoko kule kwa maslahi mapana ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, hili la bandari sikuwa na nia hata ya kulichangia sana kwa sababu, jamani kwa dunia ya sasa hivi Waheshimiwa Wabunge, hivi kweli kwa dunia ya sasa hivi tunaweza tukawa na hofu ya kubinafsisha mwendeshaji wa Bandari hii ya Dar-es-Salaam, kweli? *(Makofi)*

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kingu kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Maimuna Pathan.

**TAARIFA**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. naomba kumpa Taarifa Mbunge anayeongea sasa hivi, Rais wetu wa kwanza, Mwalimu Nyerere, alikuwa hataki mambo ya ukabila, ukanda, wala udini. Kwa hiyo, nampa pongezi kubwa sana bado anamuenzi Rais wetu wa kwanza kwa kuondoa ukabila, udini na ukanda. *Big up* na huo ndio Ubunge tunaoutaka wa kitaifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kingu, Taarifa unaipokea?

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hii kwa sababu imeni-*recognize* kwamba, ni Mbunge wa Kitaifa, nimeipokea kwa mikono miwili. Namshukuru sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la bandari, jamani kwa wale tunaotembea duniani hebu tuwe na *trust* nak il ambacho mamlaka inafikiria kwa lengo la kuongeza *revenue* kwenye hii nchi. Hili la bandari, hivi kweli kuna mashaka kwamba, tukibinafsisha bandari yetu ile katika *operation,* si walikuwa wanafanya *TICTS* jamani, si walikuwa wanafanya *TICTS* juzi tu

hapa, sasa kuna ubaya gani kampuni nyingine ikaja kuleta ufanisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa, mimi natoa mfano, juzi kati niliingiza vitanda vya kusaidia akinamama jimboni kwangu, miaka miwili iliyopita. Ukiangalia gharama ya kukodi *container* moja mpaka hapa dola 4,000, lakini wenzetu wanalipa dola 1,600 au 1,800 jamani kuna shida gani kubinafsisha bandari, tija ipatikane, maendeleo ya nchi yapatikane? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine jamani tuangalie maslahi ya nchi. Huyu Rais aliyeko madarakani hawezi kufanya jambo kwa maslahi ya familia yake na watoto wake. Chochote atakachokifanya mama yetu atafanya kwa ajili ya maslahi ya nchi na sisi Wabunge huwa tuko wazi hapa, mambo yakija ndivyo sivyo, hatuogopi kusema, tunasema wazi, lakini hili lina maslahi ya nchi. Rais wetu aungwe mkono, Bandari ya Dar-es-Salaam, tena nawaambia, nashangaa sana kwa sababu, Serikali sisi Wabunge kazi yetu ni kuwashauri, lakini nashangaa sana, hili jambo wanataka kulifanya kama vile mpaka sijui fulani aamue, hapana. Jambo linalohusiana na maslahi ya nchi na ndio maana tuna Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wafanye kazi wasiogope.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi matarajio yetu ni kuona bandari ile inapata ufanisi na mambo yanakuwa mazuri kwa maslahi ya Taifa hili. Wala wasisubiri eti kumuuliza na kuhoji mtu fulani aone nini kinafanyika. Ndio maana tuna Amiri Jeshi, yuko Kikatiba, yuko kisheria, hakuna mtu wa kuweza kuuliza kinachofanyika, zaidi tutahoji tunapoona kuna *violation* ya maslahi makubwa ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo naomba nichangie, wengi wamezungumza kuhusiana na mambo mazima ya ujenzi wa *SGR* na mambo mengine. Nataka niseme kitu kimoja, lazima kwenye hili tuelewane, wakati mwingine tunaweza tukawa na hisia za kuhisiana tu ambazo zinaweza zisilisaidie hili Taifa. Niwaombe sana, Mheshimiwa Jerry Silaa leo amezungumza mchana na nimempa Taarifa, takwimu zinaonesha na kuna muda

nilikosea nikatamka kwamba, *engineering estimates* nikazitaja kama *BOQ.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zinaonesha Tanzania ndio nchi ambayo kwa kutumia rasilimali zetu na mikopo tunayokopa tumeweza kujenga reli kwa bei nafuu sana ndugu zangu. Hii habari tunazungumza sijui ya mabehewa, sijui ya nini, hivi kweli leo kama nchi, tumepata mkandarasi anaambiwa na Serikali tunaomba utupe *guarantee* ya ubora wa mabehewa yako, anasema hapana najitoa, Serikali gani itakuwa tayari kumpa mtu huyo kazi? Haipo duniani *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kingu, muda wako umekwisha.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nikushukuru sana kaka yangu Mungu akubariki sana. Japokuwa Mheshimiwa Shigongo alikuwa anaomba niongezewe muda, lakini naomba kwa heshima yako nikae. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mchangiaji wetu wa mwisho mchana huu ni Mheshimiwa…

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mchangiaji wetu wa mwisho mchana huu ni Mheshimiwa Livingstone Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, kwa hiyo, kwa kuwa, ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, la kwanza kabisa niunge mkono hoja ya Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipita nje hapo unaona limeandikwa Bunge la Tanzania, kwa hiyo, Wabunge kutoka majimbo mbalimbali tukiingia humu tunakuwa Wabunge wa Taifa. Serikali inaposhauriwa na Waheshimiwa Wabunge ichukulie kwamba, Bunge linaishauri Serikali ili kuweza kuleta maendeleo ya wananchi wa Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango mingi imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge hapa, wamezungumza kwa kishindo sana kuhusu barabara, lakini kwa kuwa na mimi ni mmoja wa Wabunge wa Taifa, nataka nianze na wastaafu wa *ATCL*. Kuna watu wameshafariki hawajalipwa pesa zao, kuna watu wako kitandani hawajalipwa pesa zao, kuna watu wana mazingira magumu, Mheshimiwa Waziri atakaposimama hapa atupatie majibu hawa wastaafu watalipwa lini? Maana deni lao lilishafanyiwa uhakiki, upembuzi yakinifu ulishafanyika kwa hiyo, tupate majibu kwamba, lini watalipwa pesa zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili, nataka nizungumzie Barabara ya Ntyuka *Junction* - Mvumi Makulu - Mvumi *Mission* - Handali kwenda Kikombo. Barabara hii ina wakandarasi wawili, kuna mkandarasi ameanzia mjini na mwingine ameanzia Kikombo. Nataka Mheshimiwa Waziri anihakikishie kwamba, hawa wakandarasi wanakwenda kutuacha sisi kama kisiwa au wanaenda kumaliza kazi ya kutuunganisha Makao Makuu ya Jimbo la Mvumi pamoja na Mji wa Dodoma na Mji wa Chamwino wa Kiserikali? Majibu hayo yatakuwa majibu mujarabu sana kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Mvumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulizungumzia hapa, kwa suala la kipande maana hatuzungumzi kubinafsisha bandari yote, tunazungumza kipande ambacho walikuwa wanafanya kazi *TICTS*. Mimi huwa nafananisha na mtu amenunua lori lake, amenunua semi, matairi yameisha, *propeller* imekatika, huna uwezo umeli-*park* nje, sasa kazi yako ni kuonesha wajukuu gari la kwangu hili, lakini wajukuu hawana chakula, wamefukuzwa ada, wewe kazi yako kuonesha lile gari bovu, gari hili langu bwana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunachofanya hapa, tunaiomba Serikali itafute mwekezaji wa kuja kutia matairi mapya, kununua *propeller* jipya, ili mtoto wetu sisi awe tingo, wakusanye pesa, maisha yaendelee. Kwa hiyo, eneo hilo tunaomba Serikali ikatafute mwekezaji mwenye uwezo mkubwa, lakini wakati wakitafuta mwekezaji mwenye uwezo wahakikishe jambo la kwanza wanalinda ajira za Watanzania walioko katika eneo lile. Tusije tukaanza tena kuathirika, watoto wetu wakafukuzwa kazi, hapana, tunataka mwendo mkubwa zaidi kutoka pale walipoishia *TICTS* kwenda mbele, ili tuweze kujiletea maendeleo ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishabinafsisha bandari katika kipande hicho kidogo tutapata tija kutoka makusanyo tunayokusanya sasa yataongezeka zaidi, lakini na uharaka. Juzi tumeona wafanyabiashara namna ambavyo wamelalamikia suala la uharaka, tunaambiwa meli moja kila siku moja tunayoichelewesha tunalazimika kuilipa Dola 25,000. Sasa hebu niambie na pale kuna meli kibao zinasubiri ziko foleni, tuweke mwekezaji ambaye atatuondoa kwenye deni lile, tuweke mwekezaji ambaye *speed* yake ya kutoa ma-*container* itakuwa kubwa ili kuondosha ile gharama ambayo tunaipata pale.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Lusinde, Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Songe.

**TAARIFA**

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe Taarifa Mchangiaji kwamba, zile gharama ambazo anazisema za ucheleweshaji kwa siku dola 25,000, mwisho wa siku analipa mlaji wa mwisho. Kwa hiyo, tunaongeza gharama kwa vitu vyetu bila sababu ya msingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde, Taarifa unaipokea?

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea maana inatoka kwa Mbunge kijana kabisa, mtu *smart,* nawezaje kuikataa Taarifa ya kijana wangu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yake ni njema, yote hayo ndio tunayoyazungumza sisi kama Wabunge, kuishauri Serikali kwamba, itupunguzie hizo gharama kwa sababu, gharama mwisho wa siku zinakuja kwa anayetumia. Unaweza kuona hata bidhaa hizo ambazo zilitakiwa ziuzwe hapa kwa bei ya chini zaidi zinauzwa bei ya chini Zambia, zinauzwa bei ya chini Kongo, halafu zinaturudia tena sisi hapa. Kwa hiyo, soko letu linakuwa gumu, lakini tukiweza kuboresha hiyo, bidhaa zetu zitakuwa za bei ya chini na hapo wageni wengi watakuja kununua hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nilizungumze. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais ametupatia pesa milioni 500 kujenga Daraja la Mloa Barabarani kuunganisha na Makang'wa na ile ni barabara ya lami ambayo baadaye inakuja kujengwa kuja tena kuunganisha Mvumi. Vilevile *connection* ya watalii tunapata uwanja mkubwa wa ndege hapa Dodoma Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu uwanja utakuwa na faida kama tutafungua barabara mpya kutoka hapa Dodoma Mjini, kupitia Nagwelo, kwenda Huzi, kwenda Manda, kwenda Ilangali, iingie ndani ya hifadhi kwa njia ya mkato. Badala ya watalii kuzunguka kupita Iringa watakuwa wanakatiza hapa tu taratibu wameshaingia kwenye *Ruaha Game Reserve* na baadaye wanaingia kwenye *National Park* ya Ruaha kwa ajili ya kuona wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ya barabara yamezungumzwa kwa umakini. Kuna barabara ambazo zinajengwa Dodoma za mzunguko, lakini barabara nyingine za mzunguko ambazo Wizara izifikirie ni Barabara ya Mpwapwa inayotokea Kibakwe kwa Mheshimiwa Simbachawene. Hii barabara ni ya muhimu sana, badala ya mtu akitoka Iringa kuja moja kwa moja anaweza kuingilia pale Kibakwe akaja kuunganisha Kongwa kwa Mheshimiwa Mzee Ndugai, tayari

tumepata barabara nyingine ya lami inayotokea Kiteto, moja kwa moja anakwenda Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana ujenzi wa Dodoma ukatuondolea adha ambazo wanapata sasa hivi Dar-es-Salaam. Tunapozungumza jiji tusiseme tu Dar-es-Salaam maji yakijaa kuna shida, hata Dodoma mvua ikinyesha kuna shida. Nje ya Bunge hapa kunakuwa na foleni kubwa kabisa. Kwa hiyo, tuangalie majiji yote, *modal* ya Dar-es-Salaam ya kuondoa matatizo ya mvua hiyo hiyo itumike kwa Dar-es-Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Dodoma, tusiseme leo tunazungumzia Dar-es-Salaam halafu kesho Dodoma inapata shida, tunaanza kusema, aah, na Dodoma, hapana. Wasomi wetu lazima waiangalie sasa nchi namna inavyokuwa na namna ya kuondoa misongamano ya magari pamoja na maji mvua ikinyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kama nilivyosema. Sina shida na Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake. Sina shida na watendaji wote wa taasisi zake wamejipanga vizuri, ni matarajio yetu kwamba, watakwenda kwa kasi zaidi kuweza kuondoa matatizo yanayolikabili Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Livingstone. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa mchango wetu wa mchana huu.

Wakati anachangia Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila kuna daraja lilitajwa kwamba lilikatika na kujengwa. Sasa naomba isomeke ni Daraja la Nsesi na sio Mbasi kwa hiyo watu wetu wa Kumbukumbu Rasmi zikae salama hizo.

Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na mjadala mchana na tutaanza na Mheshimiwa Jafari Chege, atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Komanya, Mheshimiwa Tauhida Gallos pamoja na Mheshimiwa Antipasi Mgungusi na *list* itaendelea.

Baada ya kusema haya, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge Lilirudia)*

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Jafari Chege, atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Komanya, Mheshimiwa Tauhida Gallos Nyimbo ajiandae.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa kwanza jioni ya leo.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba leo nimesimama, sitakuwa na mambo mengi zaidi ya kutoa shukrani zangu za dhatii kwa niaba ya wananchi wa Rorya, kwanza kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, pili, kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na Manaibu wake wawili, hasa Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya. Pia nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa Watendaji kwa maana ya Makatibu Wakuu wa Wizara hii hasa Dada yangu Ndugu Aisha, pia nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Spika, nimeanza kutoa pongezi hizo kwa kipekee kabisa kwa niaba ya wananchi wa Rorya kwa Serikali hii ya Mama Samia kuridhia maombi zaidi ya miaka 40 ya barabara ambayo tumekuwa tukiiomba muda mrefu hapa ya lami kutoka Mika – Utegi – Shirati mpaka Mpakani mwa Kenya Kirongwe kuingizwa kwenye mpango wa bajeti kwa ajili ya ujenzi wa lami.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru wananchi wangu na kwa kuwa wananisikia na waliniambia nifikishe salamu na pongezi hizi na shukrani za dhati kabisa kwa sababu barabara hii siyo tu kwamba ni barabara ambayo inatuimarisha usalama kati ya nchi na nchi, lakini ni barabara ambayo ikijengwa kwa kiwango cha lami inakwenda kuinua uchumi wa Halmashauri yenyewe, uchumi wa Mkoa wa Mara, lakini uchumi wa Serikali kwa ujumla kwa sababu inakwenda kugusa nchi mbili.

Mheshimiwa Spika, mbali ya hivyo, hii ni barabara ambayo kimsingi tumeiomba kwa muda mrefu sana. Ilani ya Chama cha Mapinduzi toka mwaka 2010 ilikuwa inasemwa barabara hii itaingizwa kwenye mpango wa utekelezaji lakini ilikuwa haifanyiki, toka 2005, 2010 mpaka leo kwa Awamu hii ya Sita angalau imeweza kuingia kwenye mapendekezo ya ujenzi wa lami.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwa maana ya Wizara hii, niombe sasa kwa kuwa tayari imekwishaingia kwenye mpango wa utekelezaji wa lami, iweze kutengewa fedha, kwanza itangazwe lakini itengewe fedha ambazo itaweza kujengwa kwa kilometa zote 56. Ninaamini wananchi wamefarijika sana na ndiyo furaha yao kubwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili nataka tu nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, kama nilivyosema leo mimi sina mambo mengi kwenye Wizara hii, kwa furaha tulizonazo sisi tunaamini kabisa kwamba wananchi wote katika Wizara hii wamefarijika sana. Natamani nimkumbushe Mheshimiwa Waziri juu ya Kivuko cha *MV* Musoma. Kwa kuwa kivuko hiki kilikwenda kwenye matengenezo, mara nyingi Mheshimiwa Waziri nimekuwa nikikuuliza ndani hapa, kwenye majibu ya nyongeza umekuwa

ukitoa ahadi kwamba angalau kile kivuko, mwanzoni ulisema tarehe 30 Aprili kitarejea na kitaanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, Kiongozi kwa maana ya Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama, Mwenyekiti wa Umoja wa Wazazi Taifa, naye alipokuwa katika eneo lile alikupigia simu ukaahidi kile kivuko kitarudi kabla ya tarehe 05 Aprili. Leo ni tarehe 23 Mei, Mheshimiwa Waziri ninatamani wakati unafanya majumuisho, wale wananchi wanaotumia kivuko kile wangetamani wapate kauli yako, ni lini kile kivuko kinarudi kwa ajili ya kutoa huduma kwa kuwa kile kivuko kilichopo ni kidogo na siyo salama kwa maisha yao.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo ninatamani pia nikukumbushe ni juu ya bandari ya Musoma. Nimeona kwenye hotuba yako Mheshimiwa Waziri, zipo bandari kadhaa ambazo zinakwenda kufanyiwa matengenezo, bandari za Mwanza na maeneo mengine, lakini sijaiona bandari ya Musoma ikitajwa.

Mheshimiwa Spika, nilichangia mwaka jana kwenye hotuba ya bajeti ya Wizara yako na nikakuomba sana kwa unyenyekevu mkubwa, bandari ile sisi kwetu ndiyo kiungo muhimu cha kuinua uchumi wa Mkoa wa Mara. Nasi Mheshimiwa Waziri wewe ni shahidi, ile bandari imesahaulika kabisa. Kwa sasa ilivyo imechakaa na haifai. Ninaomba sana kwenye bajeti hii, pamoja na kwamba tayari mmetaja bajeti zingine, muone namna ya kuifufua ile bandari.

Mheshimiwa Spika, kwetu ile bandari ndiyo kiungo muhimu cha kuinua uchumi wa Mkoa ule wa Mara. Lakini sisi tunaitegemea ile bandari iweze kufanya kazi, kwa sababu tunayo bandari ya Sota eneo la Rorya ndiyo muunganiko wa bandari zote mbili. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti na utekelezaji kwenye hotuba yako umesema hapa tunajenga Reli ya *SGR,* matarajio yetu ni kwamba reli ya *SGR* baada ya kuwa inafika Mwanza, tunatamani kutokea Mwanza kwenda maeneo mengine kwa maana ya Nchi za Kenya na Uganda, waweze kutumia bandari ya Musoma, waweze kutumia bandari ya Sota kufika maeneo ya Kenya na Uganda. Sasa isipokuwa inawekwa

kwenye bajeti kila mwaka inakuja haitengewi fedha na ilivyochakaa pale Mheshimiwa Waziri, haipendezi. Ninatamani sana na yenyewe muiweke kwenye vipaumbele Bandari ya Musoma Mjini na Bandari ya Sota. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kama nilivyosema, ni juu ya jengo la abiria kwenye eneo la kivuko cha Musoma na upande wa Kinesi. Wananchi wale wakati wa mvua na wakati wa jua kali Mheshimiwa Waziri, hawana mahali pa kujikinga jua wala mvua wakiwa wanasubiri kivuko. Ninaomba pia, nimeona kwenye bajeti umelisemea, kivuko hiki kiharakishwe kwenye pande zote mbili, upande wa Kinesi na upande wa Musoma ili angalau kuweza kurudisha matumaini na kuweza kuwasaidia hawa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, nimeona hapa Barabara ya Kuruya – Makutano kwa maana ya Makutano – Komuge mpaka Kinesi mmeiweka kwenye utekelezaji kwa ajili ya kuandaa mpango kwa maana ya ufanisi. Ninaomba barabara hii pia kwa bajeti ya mwakani tuiwekee lami kwa sababu ni muhimu sana kiunganisho kati ya maeneo ya kivuko, maeneo ya Kinesi na upande wa Kuruya kuja maeneo ya Musoma mpaka Mwanza. Kwa kuwa mmetenga fedha za upembuzi yakinifu, ninaomba sana mwakani Mheshimiwa Waziri barabara hii pia uikumbuke.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mimi kwenye Wizara hii sikuwa na neno kubwa zaidi ya kutoa shukrani kwa furaha kubwa ambazo wananchi wangu wamefarijika. Nitumie nafasi hii kukuomba sasa Mheshimiwa Waziri usiishie tu kuiweka kwenye bajeti, barabara hii ni muhimu sana kwa kiungo cha Mkoa mzima wa Mara iwekee fedha itangazwe ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami kwa maana ya kutoka Utegi – Shirati kwenda mpaka kule Sota na maeneo ya Kirongwe. Ninaamini kabisa itafungua uchumi wa hizi Nchi mbili kwa maana ya Kenya na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante sana. naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Tauhida Gallos, Mheshimiwa Antipas Mgungusi ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi jioni ya leo nami nitoe mchango wangu katika hoja iliyopo mbele yangu. Lakini leo nitajikita kushukuru kwa yale tuliyofanyiwa katika Jimbo la Meatu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa namna anavyofanya kazi na kwa namna alivyoiendeleza miradi iliyoanzishwa Awamu ya Tano na sasa mingi amekwenda kuikamilisha, likiwepo Daraja la Tanzanite, anaendeleza ujenzi wa Daraja la Magufuli la Kigongo – Busisi ambapo kazi inaendelea na mwaka huu tunaokwenda kuuanza ametenga bilioni 15 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri na Watendaji wote kwa kazi nzuri wanazofanya. Mheshimiwa Waziri hana maneno mengi lakini ana utekelezaji mkubwa nae nimshukuru. Miradi ambayo mimi binafsi niliongea na Mawaziri watangulizi wake ilikuwa haijaanzishwa lakini yeye ameianzisha na inaendelea, nakushukuru sana Mheshimiwa Profesa na Naibu Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia Meneja wetu wa *TANROADS* Mkoa wa Simiyu kwa kazi nzuri anazofanya za kiwango kwa barabara nzuri zinazojengwa, zinanyanyuliwa juu kiasi kwamba hakuna sasa kukatikakatika kwa barabara wakati wa mvua, lakini pia kwa usimamizi wa fedha mpaka unaona thamani ya pesa inakuwepo.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru katika mpango huu ahadi ya kujenga barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Mto Sibiti – Lalago – Maswa ni ahadi ya muda mrefu, ilikuwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, na sasa Serikali imekwenda kufunga mkataba unaotarajiwa kusainiwa kabla ya mwisho wa mwezi wa Juni kwa mfumo wa *EPC+F,* lakini imetengwa bilioni 5.5 kwa ajili ya

kuanzisha ujenzi huu. Mimi nashukuru kwa sababu hata hiyo bilioni tano itafanya kazi za awali ikiwemo kulipa malipo ya awali.

Mheshimiwa Spika, niendelee kushukuru, tarehe 14 mwezi huu wa Mei, Mheshimiwa Waziri akiwa Itigi wamefunga mkataba wa kilometa 25 katika maingilio ya Daraja la Sibiti kwa shilingi bilioni 21.77. Mimi nashukuru sana, ilikuwa ni kilio cha muda mrefu cha watu wa Jimbo la Meatu, Wilaya ya Meatu na Mkoa wa Simiyu kwa ujumla kwa sababu ni watumiaji wakubwa wa barabara hii wanapokuja Dodoma. Nikuombe tu utakapofunga mikataba ijayo katika hii barabara niliyoitaja mwanzo basi uje ufungie katika maeneo husika ya urefu ule ikiwemo Meatu na wananchi wafurahi kuona, lakini sisi tunafurahi kwa sababu mkataba umeshafungwa na ujenzi utaanza wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa ajili ya daraja la Itembe tumetengewa bilioni 8.4 na Mkandarasi ameshalipwa *advance payment* ya bilioni 1.2, lakini sasa hivi tayari ana *certificate* ya kwanza, ninaombe tu malipo ya awali yalichelewa na mkataba huu ni wa mwaka mmoja leo tumebakiza miaka mitano tu lakini bado iko chini. Niombe Serikali iongeze kasi ya ulipaji. Pia madaraja yaliyobaki ya Lyusa, Chobe na Nkoma, naomba na yenyewe pia yawekwe kwenye mpango wa kuyajenga.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru tuliomba lami kilometa mbili pale Mjini Mwanuzi, mmetupatia bilioni moja kwa ajili ya kujenga kilometa 1.25. Barabara hii inakwenda kuwasaidia akina mama kufanya biashara zao usiku na mchana kwa sababu pia inaweza kuwekewa mataa, lakini inakwenda kupunguza mavumbi yaliyokuwa yanachafua maduka ya watu, yalikuwa yanasababisha ajali wakati wa misafara.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru daraja la Paji ambalo lilikuwa ni kilio cha muda mrefu, milioni 389 lilishatekelezwa. Watu wa Meatu hatukutarajia kama daraja la chini litaweza kujengwa, lakini Serikali imetoa milioni 90 kwa ajili ya kufanya usanifu, mimi nashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ninakuomba tuna barabara yetu ya *TARURA* ya kilometa 45 inayotoka Mwanuzi kwenda Mwabuzo, tunaomba ipandishwe hadhi imekidhi vigezo, barabara hii ni muhimu kwa uchumi wa Meatu, Wilaya ya Maswa na Mkoa wa Simiyu kwa ujumla. Wataalam kutoka ofisi yako walikuja kuiangalia iweze kuunganishwa na Wilaya ya Igunga, basi naomba uridhie upandishe zile kilometa 45. Nikuombe Meneja wa *TANROADS* Shinyanga na *TANROADS* Tabora na wenyewe basi tuungane pale, kwa sababu wafanyabiashara wengi wa Meatu wanaelekea kule Igunga na kusisimua biashara na uchumi wa pale Igunga.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru Serikali kwa jitihada inazofanya daraja la Mwamanongu ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Samia ya 2015 akiomba kura akiwa mgombea mwenza aliahidi kujenga daraja. Daraja lile lina mita 120 ni daraja la *TARURA,* uhakiki umeshafanyika litagharimu bilioni saba. Naomba sasa upande wa *TARURA* na wenyewe walitekeleze kwa sababu sikupata muda wa kuongea kwenye Wizara ya TAMISEMI. Naomba sasa na lenyewe litekelezwe, liko katika hii barabara kilometa 45.

Mheshimiwa Spika, nimalizie sasa kwa kuwaambia wananchi na kuwashukuru Serikali kwa kupewa fedha za *bottleneck* kutoka katika Mfuko wa Fedha wa Dunia, shilingi milioni 400, ambapo tunakwenda kujenga Daraja la Mang'wina kwenda London na Mwajidalala.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tauhida Gallos, atafuatiwa na Mheshimiwa Antipas Mgungusi, Mheshimiwa Amandus Chinguile ajiandae.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wake kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kujenga Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mambo mawili ambayo naweza kuyachangia kwa siku ya leo. Ninampongeza Waziri pamoja na wafanyakazi wote kwa kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la bandari ni suala ambalo kila ninaposimama huwa nawasemea wanawake wa Tanzania. Kwangu kumekuwa na kero kubwa na bado haijapatiwa ufumbuzi. Baada ya kuwa kila nikisimama nikiwa miongoni mwa wanaolalamika na suala la bandari na mimi nikiwa miongoni mwao, sasa nimetoka kwenye kulalamika nimeamua kwa maksudi kwenda kuangalia hasa tatizo lililoko huko bandarini ni nini.

Mheshimiwa Spika, kwa kufahamu kwa undani kabisa bandari kila siku tumekuwa tukitupia lawama kwa Waziri, lakini kuna matatizo ambayo yanasababishwa pia kutoka kwenye Wizara nyingine. Kero kubwa iliyopo ndani ya bandari inasababishwa na *TRA*. Pia wanaosababisha kero wapo Askari Polisi na Bandari wenyewe.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeamua kwa maksudi kwenda kujua haya matatizo tunayolalamikia kila siku bandari yanasababishwa na nini? Tulikuwa mwanzoni hatufahamu tunayemlalamikia hasa ni nani, lakini nimuombe Waziri mzigo mkubwa bandari unaubeba wewe na unaubeba wewe kwa sababu wewe ndiyo kioo cha bandari, wewe ndiyo mhusika wa bandari, lakini una watu kiungo ambao wanafanya kazi na wewe.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nitumie fursa hii sasa kukushauri upate fursa ya kukutana na Mawaziri wenzio wanaohusika na masuala ya kodi, Mheshimiwa Waziri wa Fedha lazima ukae naye upate muafaka wa kwenye suala la bandari kodi zinazotozwa kwa wanawake wajasiriamali wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, haiingii akilini kila tunaposimama hapa tunapigia kelele wanawake wafanyabiashara ndogo ndogo. Kwa nini tunazungumza wakati huu wa bandari, kwa sababu shida anayoipata mwanamke wa Kitanzania awe anatoka Zanzibar au Bara anaipatia bandarini anapopita na mzigo wake mdogo. Tukuombe ukae na Waziri mwenzio muone mnatatuaje matatizo yaliyopo katika maeneo ya bandari.

Mheshimiwa Spika, pale kuna Askari pia, lakini anapofika pale anakuwepo ndani ya bandari, ninadhani lazima mpate muda wa kufanya kazi kwa pamoja, Mawaziri wapo ambao mnaweza mkakaa mkazungumza na mkatatua changamoto zinazokuwepo pale.

Mheshimiwa Spika, pale ndani ya bandari napazungumza kuna mambo mengi na kuna watu wengi. Tumekuwa muda mwingi tukishauri lakini tunalalamika. Niseme kwamba kuna mazuri yanayofanyika pale ndani ya bandari. Kuna watu wanatoa huduma vizuri, Waziri tunachukua fursa za kukushauri yale mazuri yaendelee, lakini maeneo ambayo yanahitaji maboresho tukuombe Mheshimiwa Waziri utusaidie kuweza kufanya maboresho ili wanawake na vijana wa Tanzania waweze kufanya mahitaji yao kwa wepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazungumzia bandari kwa sababu kuna mambo mengi yanayoendelea pale, siamini kama yote yanaweza kumfikia, lakini kwa sisi ambao tunaitumia bandari, Mheshimiwa Waziri kilio hiki kwangu kimekuwa cha muda mrefu. Ninaelewa kama siyo la kwako, lakini usipokaa na wahusika matatizo haya hayawezi kuondoka. Tunaomba utusaidie ili matatizo yanayosonga pale bandarini yaondoke.

Mheshimiwa Spika, kuna wanawake wajawazito wanapita bandarini, kuna akina mama wanaougua wanapita bandarini, bado kwenye mifumo ya maeneo hayo Mheshimiwa Waziri hapajakaa vizuri, ninadhani hapajakaa vizuri wewe umeshikilia bandari lakini kuna wengine wanakuja kutoa huduma ndani ya bandari. Hawa watu kila mmoja anafikiria huduma ya mwenzie wakati hajulikani mhusika hasa nani. Tunakuomba Mheshimiwa

Waziri ikiwezekana tutengenezee utaratibu kuona tunapata njia ya kupita akina mama wajawazito, watu wenye mahitaji maalum vilevile wale ambao wanakuwepo pale wagonjwa.

Kuna muda tunawashukuru wafanyakazi wanaotoa huduma kwa *VIP,* huwa wanalazimika kuisaidia jamii japo najua hii kazi wanayoifanya siyo yao. Kwa hiyo, huwa wanasaidia kwenye maeneo ya wagonjwa wajawazito. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, pamoja na kazi nyingi na kubwa unazozifanya na sisi tukizishuhudia kwa macho yetu, bado kilio cha bandari na kero za bandari hazijaondoka moja kwa moja. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri, fanya ziara maeneo yale na kuweka mikakati ya makusudi kuweza kulisaidia Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye hoja yangu ya pili ambayo ni suala la uwekezaji ndani ya bandari. Mwenyezi Mungu alivyotujalia, kila mmoja amemuumba na karama yake, kila mmoja amemuumba na majaliwa yake. Namwomba Mheshimiwa Waziri, hili jambo analotaka kwenda kulifanya la uwekezaji ndani ya bandari, niseme kweli, kwa namna nilivyojiridhisha, naomba niseme kwamba tunamridhia aende akaendelee nalo kwa utekelezaji. Huwa mgumu sana wa kukubali kitu haraka haraka, lakini kwenye eneo hili nimejiridhisha vya kutosha, uzalendo na utu uliokuwanao, hao wawekezaji wanakuja kuifungua Tanzania, usiache kuweka mbele uzalendo na ubinadamu na utu.

Mheshimiwa Spika, nimejiridhisha kwa kuuliza maswali, nimejiridhisha kwa hoja ambazo zimekuwa zikinisumbua. Nilikuwa najiuliza, tukienda kuwekeza: Je, wazawa wetu wataondolewa? Waziri ameniridhisha kwa majibu kwa kuniambia hapana, wataendelea na kama kuna watu watakuja kufanya kazi wageni ni kwa muda. Kwa suala hili Mheshimiwa Waziri sina namna, lazima niungane nawe kusema bandari sasa ifunguke. Mheshimiwa Waziri, anayesifia mvua maana yake imemnyeshea, tunaelewa na kufahamu matatizo makubwa yaliyokuweko ndani ya bandari yetu. Hatuwezi kung'ang'ania vitu ambavyo hatuna uwezo wa kuvifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba bandari itakapoenda kufunguka, Tanzania itafungua milango yake zaidi. Bandari itakapofunguka, itaenda kufungua njia na itaongeza ajira. Nimemwuliza Mheshimiwa Waziri kuhusu mapato yetu kama Watanzania, kodi itakuwaje? Jibu lake ni kwamba kodi itaongezeka.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TAUHIDA C. GALLOS:** …Niwe na ugumu gani wa kusema Waziri endelea na suala zima la uwekezaji wa bandari? Mheshimiwa Waziri…

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ilishagonga, nilikuwa nataka umalizie hoja yako. Sekunde thelathini malizia sentensi.

**MHE. TAUHIDA C. GALLOS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaunga mkono hoja, lakini niungane na Mheshimiwa Waziri kwenye suala la uwekezaji wa bandari, ni jambo jema. Mheshimiwa Waziri tanguliza uzalendo mbele, tanguliza ubinadamu mbele.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Antipas Mgungusi, atafuatiwa na Mheshimiwa Amandus Chinguile na Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, ajiandae.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi kuwa mtu wa nne kuchangia jioni ya leo kwenye Wizara hii ambayo nina *interest* nayo kubwa sana kama mtu wa Malinyi na bonde la Kilombero hasa kutokana na changamoto ya Barabara. Nina masuala kadhaa hapa ya kuchangia yale ya jimboni kwa maana ya barabara yetu ya kwenda Songea kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Ruvuma na pia kuna kipande cha kuunganisha Wilaya ya Malinyi na Kilombero kwa maana ya Mlimba kupitia kivuko. Vile vile kwa masuala ya kitaifa, kuna hili sakata la bandari ambalo linasemwa semwa, nami nitasema kidogo. Pia kuna suala la uchumi wa masaa 24, kwa

maana ya kutamani kuona usafiri wa mabasi yanakesha hapa nchini na mwisho, kuhusu mabasi madogo *(Costa Mini Buses)* kutoa huduma kubwa kabisa kama mabasi makubwa.

Mheshimiwa Spika, nitoe shukrani zangu kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maana ametuheshimisha watu wa Malinyi na watu wa bonde la Kilombero wote. Imekuwa historia tangu dunia imeumbwa, sisi hatukuwahi kuwa na lami. Leo hii ukijadili Wilaya ya Malinyi, ni mara tano, yaani uchukue Mkoa wa Dar es Salaam wote uuzidishe mara tano au mara sita ndiyo unakutana na Malinyi moja na hatuna lami hata kilometa mbili. Kwa hiyo, hata watoto wanaozaliwa kule, lami ni mpaka uende Morogoro Mjini.

Mheshimiwa Spika, kwenye Kampeni tumesema sana tutakwenda kufanya jambo la lami kuunganisha Morogoro na Ruvuma kwa maana ya kupita Ifakara, Malinyi na kutokea Namtumbo kule, watu wanasema hii siasa ni uongo uongo, miaka yote mbona inasemwa? Litawezekanaje jambo hili? Hata mimi nilikuwa nazungumza, kwenye kampeni tumeahidi na nimeendelea kuwaambia Wana-Malinyi tutafanya, huku kimoyomoyo kidogo moyo unadunda, unaogopa, unasema hawa jamaa (Serikali) watasaidia kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais amekwenda kunitoa hofu, amekwenda akuwafurahisha Wana-Malinyi, tunakwenda kusaini mkataba mwezi ujao kwa huu mtindo wa *EPC+ F* kwa maana ya kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Ruvuma, Malinyi inakwenda kuwa na lami. Pia kipande cha kutoka Ifakara kwenda Ulanga - Mahenge inakwenda kuwa na lami, ni sehemu ya mradi huu mmoja. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Rais na zaidi wasaidizi wake.

Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa nani?

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Kunambi, Kunambi, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa unajua ukikaa kwenye kiti siyo chako inakuwa mtihani kweli. Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nampa taarifa mzungumzaji, katika Mkoa wa Morogoro, kwa muda mrefu ilikuwa kilio cha Mkoa mzima wa Morogoro. Mkoa huu tangu tupate uhuru haukuunganishwa na Mkoa wa Ruvuma kama anavyosema mzungumzaji, siyo tu Mkoa tu wa Ruvuma, bali sasa historia inakwenda kuandikwa. Mlimba inakwenda pia kuunganishwa na Njombe. Kwa hiyo, Mkoa huu kwa mwaka huu wa fedha unakwenda kuunganishwa na Mikoa yote miwili, Ruvuma na Njombe kwa upande wa Mlimba na Malinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa niwakumbushe tu kwamba muda wa taarifa ni muda wa anayekuwa anazungumza. Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi unaipokea taarifa hiyo?

**MHE.** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa, lakini naomba unisaidie hata dakika moja ya nyongeza muda wangu ukiisha. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Hapana. Muda huu ninaotumia sasa hivi ni wa kwangu, kwa hiyo huu unalindwa. Kwa sababu nikiwakumbusha kila wakati, mnaona kama kiti kinawabana. Kwa hiyo, taarifa muwe mnaambiana wenyewe huko. Mkishakubaliana ninyi, mimi sina hiana hapa mbele. Kanuni zinawaruhusu kabisa. Mheshimiwa Mgungusi.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwenye jambo hilo hilo, tunafahamu, nadhani mmekuwa mkiona hata kwenye taarifa ya Habari kila masika watu wa Malinyi tumekuwa tukilia mabasi yanakwama, Malinyi hapaingiliki wala hapatokeki. Hata juzi imetokea hivyo, lakini kwa mara ya kwanza kabisa hili jambo naamini linakwenda kuisha.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kipindi hiki wakati tunasubiri hili jambo litokee barabara ianze kujengwa mwaka huu, basi ukarabati ambao unaenda kufanyika na watu wa *TANROAD* ufanyike kwa ubora ambao unapaswa. Sehemu kubwa ya maeneo ya barabara ambapo tunakwama ni matope ambayo wakandarasi huwa wanaleta wakati wa kiangazi, wanakarabati barabara inaonekana safi, ikija mvua tunapata shida kubwa. Kwa hiyo, niseme tu Mheshimiwa Waziri wasiliana na watu wako wa T*ANROAD,* ingawaje wananipa ushirikiano mkubwa sana, wakandarasi awamu hii wasilete tope, wakati wa kiangazi kukarabati vije vifusi vya changarawe au mawe.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, ilikuwa ahadi yetu ya Chama cha Mapinduzi, naimi kama Mgombea wao wa Ubunge kuunganisha Wilaya ya Ulanga na Wilaya ya Malinyi kupitia kivuko pale Kikove kwa maana ya Kijiji cha Lupunga na Ngalimila kule Mlimba. Kwa mara ya kwanza mwaka huu inapaswa twende kuunganika, tutakuwa na kivuko. Ile pantoni itakuwa pale inaunganisha watu wa Malinyi, maana yake hata watu wa Njombe watakuwa wanapita pale kwa mwaka huu. Jambo hili linaonekana kama ni ndoto, lakini linaenda kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ila changamoto ni kwamba Mkandarasi ambaye yuko *site* hebu saidia kumkimbiza kimbiza. Mimi sitaki kugombana na wewe, ni mtu mzuri, umenipa ushirikiano mkubwa, nachoka kufuatilia mkandarasi mmoja mmoja. Kwa hiyo, naomba hili jambo ulichukue waweze kuharakisha kuhakikisha kwamba lile gati linakamilika kwa wakati tuweze kupitisha watu wa Malinyi na Mlimba kuungana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye masuala ya Kitaifa, kuna suala hili la bandari ambalo linazungumzwa; maboresho au kubinafsisha ile shughuli ya *operation*, menejimenti. Mimi binafsi kama mpenda maendeleo, naunga mkono jambo lifanyike kwa sababu kadhaa kubwa. Naamini ni vema mtumishi wa Umma ukawa mbunifu, ukabuni vitu vya kufanya kuhakikisha kwamba huduma zinakwenda vizuri na mapato yanaongezeka kuliko kutofanya lolote kabisa. Kwa hiyo, kubaki kama tulivyo kama bandari siyo jambo ninalotamani kuliona au kurudi nyuma tulikotoka, siyo

jambo ninalotamani kuliona. Natamani tusogee, lakini ninaamini kwenye majaribio ya nia njema inaweza kutokea tukakosea mbeleni, bora likazungumzika tukifanya makosa mbeleni kuliko kutofanya mabadiliko kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kimsingi nawatia moyo wale wanaofanya, watu wa Wizara endeleeni kusaidia. Matamanio yangu ni kwamba, hata *TANESCO* na taasisi nyingine za maji, sijui *RUWASA* na kadhalika ikibidi kupata *private sector* siku za mbeleni ikitufikirisha tufanye. Tunafahamu utendaji wa Serikali kidogo sehemu kubwa watumishi hawako *serious* sana, lakini *private sector* naamini inaweza ikafanya vizuri. Kwa hiyo, jambo hili naliunga mkono ila tu zile hofu za watu zijibiwe. Wengine wanasema kuna masuala ya usalama, wengine mapato yatakuwaje? Ajira za ndugu zetu zitakuwaje? Wale wanaohusika na Wizara wazijibu kuwatoa watu hofu, lakini ni jambo jema, mimi naunga mkono liendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchumi wa masaa 24, mnafahamu dunia nzima tunazunguka, watu wanakesha, mabasi yanakesha, sisi kwa nini tulale? Mnaona yale magari madogo ya *IT* yanaenda nje ya nchi, mnaona magari ya magazeti yanagombaniwa Dar es Salaam kila mahali kusafirisha watu usiku, kwa nini? Uhitaji ni mkubwa sana kusafiri usiku. Kwa nini sisi tulale? Wenzetu wa *LATRA* tunagombana nao, lakini najua wao wanasimamia sheria au maelekezo ya wakubwa kwa maana ya Wizara. Wizara ikiwaambia vinginevyo, watatekeleza kama wanavyoambiwa, hawawezi kujiamulia wenyewe. Naomba niishawaishi Wizara turidhie.

Mheshimiwa Spika, umekuwa ukilisemea sana hili. Hili jambo ni la kwako, umelisema muda mrefu, na sasa mabasi nafikiri yanaanza kuanzia saa tisa usiku. Kama unakubali saa tisa mabasi yaanze, kwa nini yasianze saa saba? Kwa nini yasianze saa mbili usiku? Kuna shida gani? Madereva ni wale wale. Kwa hiyo, naomba sana hili jambo Waziri wakati ana-*wind up* alisemee, atoe maelekezo, kwa sababu hata zuio la kusafiri usiku halikuwa kisheria. Tumefanya tu mazoea. Sisi tangu tukiwa wadogo kuna mabasi yalishatekwa, wakasema tusisafiri usiku. Sasa kama

tunaogopa kusafiri usiku kuogopa majambazi, maana yake tunawapa umaarufu majambazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna Polisi, majeshi na kila kitu, tunaogopa majambazi kusafiri usiku, kwa nini? Kwa hiyo, hatutakiwi kuwapa wahalifu umaarufu mwepesi. Serikali inaweza kufanya, tutoe tamko, watu wasafiri masaa 24. Hamna suala la kusikilizia kusema tuanze kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, kuhusu mabasi madogo, kwa maana ya *minibuses* na *Costa* haziruhusiwi kupewa *route* rasmi kupeleka watu mikoani, lakini mabasi makubwa yanafanya. Mabasi makubwa hayana uwezo wa kumaliza watu wote. Nadhani mnafahamu barabarani, wote tunapenda kudandia magari ya kuunga. Kwa nini *Costa* hazipewi vibali au kufunguliwa zipate *route* kama mabasi makubwa? Wanafanya kama *special hire;* ukiwa na msiba unakodisha; ukiwa na shughuli za Kwaya, watu wanaenda wanakodisha. Kwa nini wasipewe *route* rasmi?

Mheshimiwa Spika, watu wakifariki, familiwa wanaruhusiwa kusafirisha msiba na kutumia *Costa* usiku, lakini mfanyabiashara akitumia *Costa* kupeleka hizo dawa ili watu wasife anaambiwa sheria hairuhusu, lakini wakifariki watu wake, anaruhusiwa kusafirisha. Haileti maana katika hali ya kawaida. Kwa hiyo, naomba kushawishi, naomba Bunge lako liridhie, kama Waziri akihitimisha lazima tusafiri masaa 24 na *Costa* ziweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, watu wa *LATRA* wanasema, sheria inataka basi angalau liwe na watu 40 ndiyo linaweza kusajiliwa kupewa *route*. Sasa mbona *taxi* ina watu wanne, lakini inasafirisha mtu Dar es Salaam mpaka Mwanza? Idadi ya watu inahusianaje? Hai-*make sense*. Kwa hiyo, naomba kuwafikirisha ndugu zangu, tusiwe na mawazo mgando, tubadilike. Basi linabeba watu 65 linapeleka Mwanza, taxi watu wanne inapeleka Mwanza, kwa nini *coster* yenye watu 29 au 39 haitakiwi kubeba mtu mpaka itimie 40? Mantiki ni nini kuhusu idadi ya watu? Suala *security* nafahamu tuna vyombo vyetu, vifanye kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la barabara kama siyo salama, *TANROADS* na mamlaka nyingine zifanye kazi zao. Sasa muda mwingine watu wa Serikali huwa wanaamua tu kuwaza kidogo halafu jambo tunalimeza wote, Mawaziri nao wanalichukua linakuwa jambo la kitaifa, lakini hai-*make sense*. Kwa hiyo, naomba nishawishi Bunge lako liridhie kama watu wa Serikali wataleta kama ni sheria, tuko ladhi kuunga mkono ibadilishwe lakini watu wakeshe barabarani. Tunalala ili itokee nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa leo, lakini nasisitiza kwamba namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa barabara yetu ya Malinyi kutokea Songea.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Amandus Chinguile, atafuatiwa na Mheshimiwa Nashon Bidyanguze na Mheshimiwa George Kakunda, ajiandae.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami niungane na wenzangu kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nachangia Bajeti Kuu ya Serikali mwaka 2022 niligusa barabara ya Masasi - Nachingwea na Liwale. Wakati naendelea na mchango, alisimama Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri bingwa kabisa na Mcha Mungu akanipa taarifa ya kwamba haijaondolewa barabara hiyo, bado itajengwa kwa kiwango cha lami. Kadri miezi ilivyokuwa inaenda sasa kwenye ukomo wa mwaka wa Serikali, nilikuwa naendelea kupata shida, lakini leo ninayo furaha, wakati wa bajeti ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 11 nimeona ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami unakwenda kufanyika na mkataba utafanyika kabla ya mwezi Juni 30.

Mheshimiwa Spika, habari hii ni njema kwa wananchi wa Jimbo la Nachingwea. Barabara hii wanufaika siyo tu Jimbo la

Nachingwea, ni majimbo manne; Jimbo la Nachingwea, Jimbo la Liwale, Jimbo la Masasi na Jimbo la Ndanda. Kwa niaba ya Wabunge ambao hawatapa nafasi ya kuchangia kwenye bajeti hii wanayotokea kwenye maeneo hayo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jambo hili jema. Barabara hii tulilia kwa miaka mingi, tulisema kwa muda mrefu, tulipiga magoti, lakini leo Mheshimiwa Rais anakwenda kujenga historia kujenga barabara hii. Tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi pamoja na Manaibu wake, pia na Katibu Mkuu anayeshughulikia ujenzi, Mhandisi Aisha na Katibu Mkuu mwingine na Naibu Katibu Wakuu na watumishi wote wa Wizara hii. Tunawashukuru na tunawapongeza sana kwa kazi hii ya kihistoria. Leo wananchi wa Nachingwea wameniambia niseme kwa unyenyekevu mkubwa, tunamshukuru Mheshimiwa Rais na kazi yetu ni kuendelea kumwombea. Sisi mwaka 2025, mguu kwa mguu na Mheshimiwa Rais. Kazi hii ni ya kihistoria na haijawahi kutokea na hatukuwahi kulala usingizini. Jambo hili ni kubwa. Waliniambia nisiseme sana, nisije nikapoteze madhari ya kushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeagizwa pia nikumbushe jambo moja ambalo nimekwenda mara kadhaa kwenye ofisi yake. Tunao wananchi ambao walipisha upanuzi wa uwanja wa ndege wa Nachingwea. Namwomba sana Waziri, jambo hili tumezungumza mara kadhaa alifuatilie kwa karibu ili wananchi wale ambao walipisha kwa nia njema upanuzi wa uwanja wa ndege wa Nachingwea, kwa sababu tathmini imeshafanyika waweze kulipwa ili waweze kuendelea na shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, baada ya kusema maneno hayo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nachingwea, nashukuru sana na ninaunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana. Mheshimiwa Nashoni Bidyanguze, atafuatiwa na Mheshimiwa George Kakunda na Mheshimiwa Agnes Methew Marwa ajiandae.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami naomba niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza Rais wetu, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoendelea kufanya katika Taifa letu. Pia naomba nimpongeze Waziri, amesoma bajeti yake vizuri, pia wanaomsaidia kwa maana ya Naibu Mawaziri, wanachapa kazi vizuri. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye eneo moja la Bandari ya Lagosa na Sibwesa. Mheshimiwa Waziri, hizi bandari zilitengewa fedha na zilishajengwa kwa kiasi kikubwa tu, bado kidogo kumalizia. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, peleka fedha katika eneo la Lagosa na Sibwesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi, pamoja na kwamba tunahitaji bandari hizi zianze kufanya kazi pamoja na kwamba meli hazijakamilika, lakini wananchi wa maeneo yale, wanawadai wakandarasi fedha nyingi sana. Yaani watu wamefilisika, watu waliamini kwamba watalipwa lakini baada ya Serikali kusitisha kupeleka fedha pale kwenye zile bandari, wananchi wanapata shida sana. Nakumbuka juzi kwenye semina niliwahi kuongea jambo hili na majibu niliyopata ni kwamba fedha tayari Mkandarasi wa Lagosa ameshapata na kwa hilo naomba nikushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naomba nilete shukurani ni kwenye daraja la Malagarasi Chini. Ni kweli fedha ilikwenda kwa ajili ya upembuzi yakinifu na kwa sasa hivi taarifa ya Serikali ni kwamba mwezi Novemba Mkandarasi yule atamaliza kazi. Naomba sana amalize kazi mapema iwezekanavyo ili tuanze kuweka mchakato wa kuona namna ya kwenda kujenga hilo daraja kwa sababu ni kiunganishi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, sisi Mkoa wa Kigoma tuko pembezoni na ile barabara ni kubwa ambayo inaweza kututoa kwenye Mkoa

mwingine wa Katavi na Mkoa wa Sumbawanga pia. Sasa unaweza kuona kabisa kwamba barabara ile ni muhimu sana na hasa hilo daraja. Viel vile, kwenye barabara hiyo hiyo ambayo ni barabara ya Nsimbo – Kalya, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, inaendelea kutengewa fedha mara kwa mara, na inasimamiwa vizuri sana na Meneja wa *TANROAD* ambaye anaendelea kuisimamia na kwa kweli inapitika. Nashukuru sana kwa jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwenye barabara ya Kalya - Sibwesa, Mheshimiwa Waziri barabara ya Kalya - Sibwesa ni barabara ambayo inakwenda bandarini kwenye hiyo bandari ambayo nimesema ya Sibwesa. Naomba sana, uliweka fedha kwa ajili ya kuifungua na mimi kwenye Mfuko wa Jimbo ile milioni 500 aliyotupatia Mheshimiwa Rais, nikaweka pale, *TARURA* wakaenda pale kujenga madaraja pamoja na fedha za *TANROADS,* barabara ile imekwishafunguka, lakini bahati mbaya bado haijakamilika. Naomba sana unapoendelea kujenga na kukamilisha bandari hiyo ya Sibwesa na hii barabara ni vizuri uiwekee fedha ili iweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia iko barabara hii kubwa ambayo inotoka Tabora. Sisi kipande cha Mpeta – Uvinza ni kilometa 51. Naishukuru Serikali, Mheshimiwa Waziri uliweka fedha na mkandarasi yuko kazini lakini anasuasua, tatizo ni nini? Mheshimiwa Waziri hebu nenda uone inawezekana vifaa ni vichache, lakini inawezekana fedha pia hapati vizuri. Naomba sana kwenye jambo hili kwa sababu kwenye kipindi hiki cha mvua wananchi wamepata shida sana. Kwa sababu *diversion* anazotengeneza haziko imara, magari yalikuwa yanakwama sana, nakuomba sana na bado wana umbali mrefu sana, kwa kweli jambo hili naomba nipongeze, lakini naomba nisistize kipande kile kiweze kutengenezwa kwa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa barabara ya Katavi – Uvinza – Kasulu, barabara hii sijasikia imezungumziwa kabisa. Hii yote ni kufungua Mkoa wa Kigoma. Naomba utakapokuja ku–*wind up* hili jambo kwa kweli ulizungumze kabisa. Hakuna haja ya mtu wa

Kigoma kupita Tabora wakati anakwenda kwa Mheshimiwa Tulia pale Mbeya, njia yetu ndiyo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwenye habari ya meli; nakushukuru umetoa habari nzuri hapa Bungeni kwamba kuanzia mwezi wa sita ambayo ni kesho kutwa tu, mkandarasi anaanza kukarabati Meli ya Mv Liemba. Huo ndio ukombozi wa sisi watu wa Kigoma, yaani Kigoma, Katavi na Sumbawanga ukweli ni kwamba ziwa lile limetufanya tuwe karibu na nchi tatu kwa maana ya Congo, Zambia na Burundi. Sasa nchi zile tunabaki tunaziangalia tu kwa sababu hatuna usafiri wa kwenda kule. Pia ninataka nikwambie Mheshimiwa Waziri, meli zile ndizo zimekuwa zinasababisha kupata uchumi kwenye Mkoa wa Kigoma na uchumi wa mtu mmoja mmoja kwa wananchi wetu wa Kigoma, kwa hiyo ni jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwenye eneo lile la utengenezaji wa meli mpya na mimi niungane na wenzangu, meli kubwa sana nadhani itakuwa haiwezi kusaidia, kwa sababu mizigo sio mingi ni mizigo kidogo kidogo. Kwa hiyo, kwa meli ile ambayo inaweza kuwa na tani 2000 tukipata hata meli mbili za tani 1000 kila meli ni jambo jema sana. Itakuwa inakwenda-inarudi haraka haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nizungumzie kwenye uwanja wa ndege wa Kigoma; Mheshimiwa Mbarawa wewe ulikuja Kigoma, sisi Wabunge tulikuwepo, ulisaini mkataba mbele yetu tuliona, tulitaka tuone kazi inafanyika tusiishie kuona mkataba peke yake, wananchi wasije wakafika mahali wakachoka. Kwa kweli nataka nikwambie, Mheshimiwa Rais wetu wananchi wa Kigoma wanampenda sana na wanamwamini sana kama sisi Wabunge tunavyompenda na kama tunavyomwamini. Kwa kweli kwenye majimbo yetu hali ni nzuri na haijapata kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi ya maji, barabara za *TARURA* yaani huwezi kuamini mimi kule kwenye jimbo langu hata huko bondeni kwenye ziwa barabara zimefika, kitu ambacho kilikuwa hakijawahi kutokea wananchi wanashangaa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba nikupongeze na niseme hayo machache lakini pia nikutie moyo, pambana na fanya kazi vikwazo ni vingi lakini mimi ninaamini Mheshimiwa Mbarawa utashinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nashon wakati unataja zile barabara, ile ya kutoka Uvinza inayounganisha Katavi ndiyo hiyo umeitaja au hiyo haipo?

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, hiyo ni nyingine. Hiyo ya Katavi ni nyingine, hii nyingine inaitwa Simbo-Kalya.

**SPIKA:** Sawa, Waziri mwenyewe atakuwa ameelewa lakini nilikuwa naisema hii moja barabara hii kama haipo kwenye bajeti hebu itazameni, maana nilishapita kwenye hiyo barabara ilikuwa mtihani kidogo. Kutokea Uvinza kwenda kuikuta Katavi yaani ilikuwa hatari sana. *(Makofi)*

Sawa, naona Waheshimiwa Wabunge waliopita hiyo barabara wanaunga mkono. Hata kama sio kwa safari hii lakini huko mbele ile barabara ni ya muhimu, lakini pia ni barabara ambayo ina hatari kama haikutengenezwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa George Kakunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi niungane na Wabunge wenzangu kutoa pongezi nyingi sana kwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na Mawaziri wote kwenye sekta hii na wataalam wote kwa namna ambavyo wamejipanga katika kuhudumia uchumi wa nchi hii. Niwape hongera sana wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Jimbo langu la Sikonge, nitoe shukrani za dhati kabisa. Mwaka 2022 Waziri alimleta Mheshimiwa Rais, kuzindua barabara ya Tabora hadi Mpanda. Wananchi wa Sikonge wanatoa shukrani kubwa sana kwa barabara ile, lakini kuna barabara nyingine ambayo mmetujengea kutoka Sikonge – Mibono hadi Kipili na barabara nyingine mmeendelea kuimarisha kutoka Tutuo hadi Usoke. Kwa hiyo, kwa kweli kwa Wizara hii tunatoa pongezi nyingi na shukrani nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi niseme kwamba wawekezaji, wafanyabiashara, wenye viwanda, wakulima wanaendelea kuitegemea sana Wizara hii kwa ajili ya kushusha gharama za usafiri na usafirishaji. Kwa hiyo, juhudi zote ambazo mnazifanya zina *impact* kubwa sana kwa Watanzania. *(Makoifi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani hiyo ndio maana Serikali imekuwa ikiboresha miundombinu yake kwa mfano Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Mtwara, Bandari ya Tanga na Bandari za kwenye maziwa kama Mwanza na Kigoma. Hizi juhudi ambazo mnaendelea nazo mimi nawaungeni mkono na wananchi wangu wa Sikonge wanawaungeni mkono kwa ajili ya mafanikio ya uchumi wa nchi yetu. Tunategemea sana hizi bandari ziwe na ufanisi. Hatuwezi kuwa na ufanisi kwa kutegemea sekta ya umma peke yake. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuchanganya sekta ya umma na sekta binafsi ili kupata matokeo bora zaidi. Hawa jamaa wa *Dubai Port* naamini watasaidia sana kuboresha utendaji kwa sababu wana uzoefu mkubwa sana duniani na nadhani kule ambako wamefanya kazi wameweka rekodi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nipongeze uboreshaji wa viwanja vya ndege katika nchi hii unaonendelea, lakini vilevile ujenzi wa reli ya viwango vya Kimataifa hasa reli ya *SGR* ambayo itaongeza mzigo unaosafirishwa kutoka takribani tani 400,000 za sasa hivi mpaka tani zaidi ya milioni 10. Hiyo itakuwa ni faida kubwa sana kwa uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile ujenzi wa barabara za lami na madaraja makubwa. Hii ni mchango mkubwa sana kwenye

uchumi wa nchi yetu. Maendeleo kwenye sekta hizo ukichanganya na maendeleo kwenye sekta nyingine, kwa mfano sekta ya umeme limekamilika Bwawa la Mwalimu Nyerere na *LNG* kwenye gesi. Vile vile, Mradi kama wa ujenzi wa *VETA* kwenye halmashauri zetu za wilaya ambao utachangia sana upatikanaji wa nguvu kazi yenye ujuzi kwenye viwanda ambayo itazidi kuvutia wawekezaji katika nchi hii. Kwa hiyo, nawapeni moyo endeleeni kuchapa kazi, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa na maoni kwenye maeneo machache hasa kwenye eno la barabara. Kwa mujibu wa mpangilio wa barabara nchini ambao unatambulika kimataifa, barabara zetu za kiwango cha lami hizi ndefu zimepangwa katika herufi "T" zamani kulikuwa na herufi A, B, C lakini sasa hivi wamebadilisha ziko kwenye herufi "T" kwa maana ya *trunk road*.

Mheshimiwa Spika, barabara ambazo zimepangwa kwenye herufi "T" ziko zaidi ya 23 na mimi napenda kuzungumzia barabara ambazo zina matatizo makubwa na zimejengwa kwa muda mrefu na mpango wa kuzikamilisha hivi karibuni bado haujaonekana kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, hapa nazungumzia barabara mbili; barabara ya kwanza ni barabara ambayo inajulikana kama (T – 8) kwa maana ya *trunk road number* 8 ambayo inaanzia Ziwa Victoria pale Mwanza, inapita Nzega inakwenda Tabora, Ipole, Rungwa, Makongorosi, Chunya, Mbeya inakwenda mpaka Tunduma kwenye mpaka wa Zambia. Barabara hii urefu wake ni kilometa zaidi ya 1000. Pia kwa miaka 40 iliyopita maana ilianza kujengwa kule Mwanza mwaka 1992, kwa miaka kama 40 iliyopita zimejengwa kilometa 549 tu kwenye barabara hii, ina maana kilometa 430 hazina mkandarasi yoyote mpaka sasa hivi. Sasa tunapanga kujenga barabara hii kwa miaka mingapi? Je, miaka 100? Miaka mia ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa naomba barabara hii ipewe kipaumbele. Kumekuwa na vipaumbele vinawekwa kwenye barabara hii kwa mfano, tawi la kutoka Ipole – Mpanda limekwishajengwa, hongera sana Serikali, tawi la kutoka Mkiwa –

Itigi mpaka Rungwa nalo tayari limeanzwa kwa kilometa 50... *(Makofi)*

Naomba barabara hii ipewe kipaumbele inaunganisha mikoa zaidi ya mitatu. Mimi naomba Serikali muipe kipaumbele barabara hii na kwa kweli kama hakutakuwa na maelezo ya kutosha kwa kweli mwishoni huko itabidi nishike mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ambayo ningependa kuizungumzia ni barabara bamba T9; hii barabara inaanzia Biharamulo – Lusahunga – Nyakanazi – Kibondo – Kasulu - Kanyani ifika pale inakata kona inakwenda Uvinza - Mpanda, Sumbawanga - Tunduma mpakani mwa Tanzania na Zambia. Barabara hii nayo ni zaidi ya kilometa 1000, barabara hii vipande ambavyo havina mkandarasi kabisa ni viwili, kutoka Kanyani mpaka Uvinza kilometa 57 na kutoka Ruhafu mpaka Uvinza kilometa 134 jumla kilometa 191. Hii nayo ni barabara muhimu sana katika nchi hii. Wekeni vipaumbele kwenye hizi barabara ndefu ambazo zinashikilia uchumi wa, nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama barabara ya (T8) ingekuwa imejengwa, kiwanda cha nguo cha *Mbeya Textile* kisingekufa. Kwa sababu kingepata *supply* ya pamba kutoka Mwanza, kutoka Shinyanga. Kilikufa kiwanda kile kwa sababu namba T8 ilikuwa haijajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kutokuwa na wakandarasi mpaka leo barabara hiyo, mimi nilikuwa naomba sana Serikali kwa ujumla wake iweke kipamubele kwenye hizo barabara ili kusudi wananhi wa nchi hii waweze kuhudumiwa vizuri kiuchumi. Kwa sababu sehemu zote hizo kuna shughuli za kiuchumi. Sio kwamba kule ambako kunajengwa tu ndiko kuna uchumi huku hakuna. Kote kuna shughuli za kiuchumi. Kwa hiyo, naomba sana na hayo ndiyo ya muhimu zaidi mimi mengine sina.

Mheshimiwa Spika, juzi nilikuwa Sikonge, wananchi wa Sikonge wakanituma nenda kapiganie barabara hii vinginevyo hatutakuelewa. Sio kwamba hawatanielewa mimi tu, hata Serikali

hawataielewa. Mimi naomba sana ili tuelewane vizuri wekeni kipaumbele na naomba *commitment* kubwa. Mheshimiwa Waziri, anaposimama hapo naomba *commitment* kubwa kuhusiana na barabara hizi mbili T8 na T9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mheshimiwa Charles Kajege ajiandae.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuongea katika Wizara hii. Kwanza nimpongeze sana Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazozifanya. Mama alituambia hakuna kitakacholala na kweli tunaona hakuna kinacholala kila kitu kinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, na Wizara nzima kwa ujumla kwa kazi nzuri wnayoifanya. Sisi wananchama au watu wako tunasema piga kazi, chapa kazi, mama amekuamini na Watanzania tunakuamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niende moja kwa moja kwa kusema namshukuru Mheshimiwa Rais kwa miradi mingi mizuri aliyoileta Mkoa wa Mara, lakini pesa nyingi tulizozipata Mkoa wa Mara kwa ajili ya maendeleo ya Mkoa wetu. Kipekee zaidi niombe kiwanja cha ndege cha Musoma kinachoendelea kujengwa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais ametoa pesa nyingi, lakini hadi sasa kinachoendelea ni kwamba mpaka dakika hii kuna watu ambao bado wanadai fidia zao. Basi nikuombe Mheshimiwa Waziri ujitahidi watu hawa wapate fidia zao ili na wao wafanye mambo yao mengine kwa sababu mpaka sasa mambo yao mengi yamesimama. Kwa hiyo, uchumi kidogo unakuwa unasuasua.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi niombe pia kutokana na hali halisi ya Mkoa wa Mara ndio Mkoa uliomtoa Mwasisi wa Taifa hili

Mwalimu Julius Kambarage Nyerere basi ni mkoa ambao pia unapaswa kupata upendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara hii inayotoka Majita - Musoma – Busekela ambayo imekwishajengwa kilometa tano tu na bado kilometa 87. Kilometa hizi zilizobaki ni nyingi sana na ukizingatia tangu Uhuru wa Taifa hili Wilaya ya Musoma Vijijini walikuwa hawajawahi kuiona lami. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, mimi nikuombe sana utuangalie kipekee Mkoa wa Mara na barabara hii ya Majita. Pia ukizingatia mimi mtoto wa Chifu Hangaya naishi huko Majita, kwa hiyo, inakuwa ni ngumu kidogo kwenda mpaka kule kwa sababu inakuwa ni ngumu kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kipkee nimpongeze Meneja Waheshimiwa Wabunge, *TANROADS* Mkoa wa Mara kwa kazi nzuri anayoifanya. Kwa kweli ni mchapakazi, anafanya kazi vizuri na mimi mwenyewe ni shahidi. Kuna daraja ambalo lilikuwa limeharibika muda si mrefu sana ambalo linaunganisha Musoma mpaka Mwanza, Daraja la Nyamika A pale Sabasaba. Mimi nilipita pale usiku nikamshuhudia Meneja amesimama wakati kazi zikiwa zinaendelea. Basi tukiwapata viongozi wa hivi basi naamini Taifa letu litaendelea mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kipekee mimi pia niongelee kuhusu uwekezaji; uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam ni muhimu sana kwa Taifa la Tanzania, lakini pia utaongeza ajira kwa Watanzania na kuongeza kipato katika Taifa hili. Ninamuamini sana Mheshimiwa Rais kwa kazi anazozifanya na ndio maana anakwenda kutafuta mahusiano nchi za nje kila kukicha. Mama halali asubuhi, mchana na usiku, anafanya kazi *twenty-four-seven,* yeye halali wala hapumziki kwa ajili yetu, anakwenda kututafutia wawekezaji. Naamini kabisa mama hawezi kwenda kututupa shimoni, mama ni mlezi, kwa hiyo, uwekezaji huu wa bandari mimi nina amini kabisa ni uwekezaji salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi niwaombe tu hata wale waliokuwa Mawaziri kipindi hicho wanapobeza inakuwa sio jambo zuri, hata wao wakati huo walipokuwa Mawaziri na wao

walikuwa wanafanya kazi kwa kipindi hicho. Kwa hiyo, kwa kipindi hiki wawaache Mawaziri walioko madarakani wafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili suala linatukera sana, unamkuta mtu alikuwa Waziri kipindi chake na yeye mwenyewe wakati akiwa Waziri hakufanya vizuri, lakini sasa hivi kwa sababu sio Waziri anaona wenzake wanafanya kazi anawazongazonga. Hawa ni wateule wa Mheshimiwa Rais, wawaache wafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi kama Mbunge kilichoniuma sana, kuna Mbunge mwenzetu huku ndani ambaye kipindi hicjho alikuwa Waziri, muda wote kazi kusema sema wenzake. Mara Mwigulu ajiuzulu, Mwigulu ana makosa gani amemfanyia nini; lakini Wizara hii sio ya Mwigulu. Kwa hiyo, ni kitendo ambacho kinatuudhi sana mtu kwenda kwenye mitandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi niseme tu tunamtia moyo Mheshimiwa Waziri Mbarawa, afanye kazi uwekezaji huu ni mzuri sana. Hata sisi tulikwenda kujifunza katika Bandari hii ya Jebel Ali ambayo ni katika hii Kampuni ya *DP World.* Hii kampuni sisi kama Wabunge tuliangalia vitu vingi, tuliona kwa kweli ufanyaji kazi wao ni mzuri, wana vifaa vya kisasa na wako vizuri kabisa, lakini kama Wabunge tumejiridhisha. Mimi nilimuuliza Mheshimiwa Waziri, inakuwaje katika uwekezaji huu mbona Watanzania wanalalamika? Mheshimiwa Waziri, akatuelewesha kwamba Watanzania wataendelea kufanya kazi kama kawaida na wawekezaji wataendelea kuwkeza, lakini wameweka mikataba mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, hawezi kututupa shimoni. Mimi niwaombe ndugu zangu tumwamini Mheshimiwa Rais, kwa manufaa ya bandari yetu imesuasua kwa muda mrefu. Tukipata wawekezaji wazuri, lakini tukaweka mikataba mizuri inayotusaidia sisi ama kutu-*support* sisi kama Watanzania, mimi ninaamini kabisa ndio mikataba tunayoihitaji na ndizo kazi ambazo tunazihitaji sisi zifanywe na Mawaziri za kutafuta wawekezaji wazuri. Kwa hiyo, ndugu zangu Watanzania kuweni na imani na Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa

sababu yeye ni mama, yeye ni mzazi, tena mkae mkijua na mnajua mimi naamini kwamba mwanamke ni mwaminifu kuliko mtu yeyote duniani kwa sababu yeye ni mzazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Tecla Ungele ajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuchangia Wizara hii muhimu. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya na nguvu kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kupongeza, Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yako, mnafanya kazi nzuri mimi nimekuwa Mwanakamati wa Wizara yako, hivyo ninajua kazi nyingi na kubwa unazozifanya. Wewe pamoja na timu yako tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nianze kuongelea barabara zangu, Barabara ya Mlushaka kwenda mpaka Murongo; Mheshimiwa Waziri umeandika mwenyewe na hayo umeyasoma mbele ya Bunge, Barabara ya Mlushaka kwenda mpaka Mrongo itasainiwa kabla ya Mwezi wa Saba. Barabara ya Mgakorongo kwenda mpaka Murongo umeahidi itasainiwa kabla ya Mwezi wa Saba. Mheshimiwa Waziri ninakuheshimu sana na nisingependa niongee maneno magumu. Maneno haya umeyasema ndani ya Bunge hili na umeyasema mbele ya Mungu na Mungu amesikia. Niombe sana, hakuna cha kusainia Dodoma, barabara hii ikasainiwe Kyerwa ili Wanakerwa waone kazi kubwa ambayo anaifanya Mama Samia lakini pia waone kazi kubwa anayoifanya Mbunge wao ambaye amekusumbua mara kwa mara. Kwa hiyo ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri uzingatie, tunapomaliza bajeti twende Kyerwa tukasaini barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine kwa upande wa barabara, mimi nipongeze sana Meneja wetu wa Mkoa anafanya

kazi nzuri sana. Kijana huyu ni mtulivu na ni msikivu sana. Lakini bajeti ambayo inatengwa kwa Mkoa wa Kagera ni ndogo. Mkoa wa Kagera una vipindi virefu vya mvua, takriban miezi saba yote tuna vipindi vya mvua. Kwa hiyo unakuta barabara za Mkoa wa Kagera hazipitiki kwa sababu bajeti inayotengwa ni kidogo sana. Kwa hiyo niombe sana Mheshimiwa Waziri mnapokuwa mnatenga bajeti angalieni hii mikoa ambayo ina changamoto ya vipindi virefu vya mvua ili iweze kupewa bajeti na barabara ziweze kupitika hasa hasa zile barabara za udogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la uwekezaji kwenye bandari. Bandari yetu mimi niseme ndio moyo wa Taifa, lakini bandari hii ni lango kwa nchi zinazotuzunguka kwa sababu ya umuhimu wake. Hakuna nchi ambayo inatuzunguka haihitaji Bandari ya Dar es Salaam. Lakini bado mimi niseme sijaona nguvu kubwa na juhudi kubwa ambazo mmeziweka kama Serikali kuhakikisha bandari hii inaleta tija katika Taifa letu. Leo hii kila Mbunge anayechangia hapa anaomba maji, anaomba barabara, anaomba umeme na mambo mengine lakini tunachokitega uchumi kimekaa tu. Sasa niombe sana Mheshimiwa Waziri kelele hizi achana nazo. Mimi ninaamimi Serikali kwa kipindi ambacho mmekaa na *TICTS* mmejifunza mambo mengi, mmeona mapungufu yaliyokuwepo, wapi kama Serikali walikosea sasa ni wakati wa kutafuta mwekezeji ili tuingie ubia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninaamini ndugu zangu kuna wengine wameshauri wanasema Serikali iwekeze, hivi tutawekeza kwenye vitu vingapi? Na mwisho wa siku tutakachoenda kukifanya lazima tuende kukopa. Leo hii tumekopa kwa ajili ya Mradi wa Mwalimu Nyerere, tumekopa kwa ajili ya *SGR* na miradi mingine. Tukiendelea kukopa mwisho wa siku yatatokea mambo mengine ambayo tunayasikia kule Kenya. Sasa niombe sana Mheshimiwa Waziri simama imara pamoja na timu yako, tunaamini yule kijana, Mkurugenzi wa Bandari yuko vizuri sana na tumeanza kuona maboresho ambayo ameyafanya. Sasa msije mkasema mambo hayafanyiki, hayafanyiki kwa sababu bado hatujaweza kuwekeza vya kutosha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana wekeza hapo nguvu tafuta mtu ambaye anafaa

tuwekeze ili bandari yetu hii iweze kuinua uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii tumejenga *SGR* na wanafanya vizuri sana, nimpongeze sana Mkurugenzi wa *TRC,* anafanya kazi nzuri, amesimia miradi inakwenda vizuri. Lakini *SGR* hii mnategemea ni ya kubeba abiria? Hii si ya kubeba abiria ili tuweze kupata faida na *SGR* lazima tuwe na mzigo utakaotoka nje na kuingia. Kwa hiyo niombe sana Serikali iendelee kuweka nguvu ili tuone faida ya kujenga *SGR*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana, hili usimame imara, vita ya kiuchumi inahitaji kujikunja, inahitaji kuwa imara. Ukizubaa kidogo tu kelele hizi zinazopigwa usifikiri watu wanapiga kelele kwa sababu wanakutakia mafanikio. Jambo ambalo tunashauri sisi kama Wabunge tuombe sana hii timu ambayo inatafuta mtu wa kuwekeza ijipange vizuri, tutafute wanasheria ambao ni wazuri. Huyu mwekezaji tutakaye mleta atakaposhindwa pawepo na vifungu ambavyo vitambana akishindwa aondoke, lakini lazima tuweke nguvu sana kwenye bandari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niendelee sana, nirudie sana kumpongeza sana Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa, na mmesikia Waheshimiwa Wabunge bado hajaona faida, na ninyi Wabunge ni mashahidi, bado hatujaona faida kwenye banda hili. Sasa Mheshimiwa Rais kama ameliona hilo leo hii wanaleta wazo la kuwekeza, kwa nini tusi…

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bilakwate kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Festo Sanga.

**TAARIFA**

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba amezungumzia utendaji wa Bandari ya Dar es Salaam kwamba ni mzuri na ni kweli ni mzuri na kwenye ripoti iliyotoka leo ya *World Bank* inaonesha kabisa Bandari ya Dar es Salaam ndiyo inaongoza sasa kwa Afrika Mashariki kufanya kazi

vizuri ikiwa ni bandari ya 312 na wenzetu wa Mombasa wako 326, tumeshawapiku. Kwa hiyo, ni kazi nzuri ambayo anafanya Mkurungenzi wa Bandari, Ndugu Mbossa tunampongeza sana sana kwa kile anachokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bilakwate unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo naipokea na mimi naendelea kumpongeza lakini ili tumpongeze zaidi lazima tulete uwekezaji ambao una tija na tuone matunda ya bandari yetu.

Mheshimiwa Spika, niendelee kusema ndugu zangu, kazi hii inayofanyika katika Taifa hili mnaona uwekezeji mkubwa tulionao, ukienda kwenye umeme, ukiangalia miradi ya barabara iliyotajwa hapa, ukiangalia miradi ya maji ni miradi mikubwa. Mheshimiwa Rais amejipanga kuhakikisha Watanzania wanapata huduma. Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge na hili nataka niongee kwa upole sana; kazi hii ina vita katika ulimwengu wa roho na katika ulimwengu wa mwili. Inawezekana msinielewe; lakini vita hii ili tuweze kushinda na Mheshimiwa Rais aendelee kufanya kazi vizuri niombe sana mumuombee, muombeeni, Mheshimiwa Rais ana maono makubwa. Mimi juzi nilivyoenda pale Ikuu, Hayati John Pombe Magufuli wakati anaiacha ile Ikulu haikuwa vile lakini ninyi mmeona. Ukienda kwenye Mradi wa Mwalimu Nyerere unakwenda vizuri, ukienda *SGR* miradi ambayo iliachwa na Hayati leo hii inakaribia kumalizika na ameongeza miradi mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe sana tuendelee kumuombea, tuendelee kumtia moyo lakini pamoja na wasaidizi wake ili Tanzania yenye neema iweze kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Charles Kajege, atafuatiwa na Mheshimiwa Tecla Ungele, Mheshimiwa Stella Simon Fiyao ajiandae.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Vile vile kama ilivyokuwa kwa watangulizi wangu, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. Nataka niwahakikishie Watanzania kwamba kazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ndio ameianza, Watanzania tutegemee makubwa huko mbeleni tutakapokwenda. Pia, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wa Wizara hii kwa utendaji wao wa kazi nzuri ambazo wanafanya mpaka muda huu. Wameweza sasa hivi kuifanya Tanzania ipitike kwa urahisi angani, ardhini na majini, nawapongeza sana. Lakini vile vile nampongeza *Engineer* Mativila Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* na Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Mara *Engineer* Maribhe kwa kazi nzuri sana ambayo wamefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza tena Wizara hii kwa kuweza kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Nyamuswa – Bunda - Bulamba – Kisole kwa kiwango cha lami. Kwa sasa tunasafiri na kusafirisha mizigo yetu kwa raha mustarehe, nawashukuru sana. Vilevile naishukuru Wizara kwa kupanga kukamilisha vipande vya barabara kati ya Kibara na Kasaunga na pia Kisole na Kisole Kivukoni kwa kiwango cha lami. Ukamilishaji wa vipande hivi utasaidia kuunganisha barabara nzima kutokea Kisorya mpaka Nyamuswa kwa kiwango cha lami, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nitumie fursa hii kuiomba Wizara sasa kuipandisha hadhi Barabara ya kisambala …

**MHE. BONIPHANCE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** … Mugala na Musoma Vijijini. Barabara hii ina *traffic* kubwa sana ya watu pamoja na mizigo, na vile vile barabara hii ni *shortcut* ya watu waendao Musoma na vile

vile watokao Musoma kwenda sehemu za Ukerewe naomba sana Wizara ifike…

**SPIKA:** Mheshimiwa Kajege kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere.

**TAARIFA**

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** … kupandisha barabara hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kajege kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Getere wewe ukisimama kwenye taarifa wakati wenzio wanachangia na wewe ukiwa unachangia usikasirike wanaposimama kukupa taarifa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. BONIPHANCE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba wakati anazungumza barabara ya ile ya kuunganisha Kisorya amesahau kusema barabara ya kutoka Balili kwenda Mugeta nayo inapaswa kuunganisha.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kajege unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, huyo ni *Comrade,* naipokea taarifa yake. Kuna changamoto ambazo bado Wizara inatakiwa kuzitatua ili kuweza kufanikisha malengo ya Serikali yetu. Kwa mfano, kuna Shirika la *Air* Tanzania *Limited*, shirika hili limekodisha ndege kutoka Shirika la *TGFA,* lakini nikiangalia kwa sababu nimepata bahati kwamba nipo katika Kamati ya *PIC,* na Viongozi Wakuu wa *ATCL* wamekuwa wanakuja katika Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini katika kuangalia tumekuta kwamba tatizo kubwa katika *ATCL* ni mkataba kati yake na *TGFA*, mkataba huu kwa kweli si rafiki. Ninaiomba sana Serikali iuangalie tena mkataba huu ili uweze kufanywa kuwa rafiki. Lakini tatizo

lingine katika *ATCL* ni madeni iliyorithishwa, madeni hayo hayalipiki. Ningeomba Serikali iangalie namna nyingine ya kuweza kuchukua madeni haya. Vilevile kuna mwingiliano mkubwa wa Serikali kuipatia *ATCL* namna ya kufanya kazi, yaani waliache sasa Shirika la *ATCL* lifanye kazi kibiashara, lihudumie njia zenye faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano siku moja nilikuwa Mwanza, ndege ya *ATCL* ilikuwa inatoka Chato. Ndani ya ile ndege nilipoingia niliikuta ina abiria watatu lakini utakuta abiria wengi wapo hapa Dodoma wanasubiri ndege za *ATCL* kuweza kuwasafirisha. Ningeomba sana Serikali iliache Shirika hili liweze kufanya kazi yake ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni utitiri wa vituo bubu vya ukaguzi wa malori na mizigo katika barabara zetu. Ukitoka Dar es Salaam mpaka kufika Tunduma kuna vituo bubu zaidi ya 100. Haya malori yenye mizigo yakitoka Bandarini yanasimamishwa kila sehemu, yanakaguliwa kila sehemu na wakati mwingine yanchukua muda mrefu. Mfano mmoja siku moja nilikutana na dereva mmoja ambaye alikuwa anatoka Dar es Salaam kwenda Tunduma saa mbili nikamkuta akiwa amesimamishwa pale Kibaha lakini wakati narudi saa 12 jioni kutoka Morogoro nilimkuta bado amesimama pale. Wahusika walikuwa wanadai kwamba kuna cheti ambacho kilikuwa kimesainiwa lakini aliyekuwa amekisaini yuko kwenye mkutano. Kwa hiyo hakumruhusu huyo dereva aendelee na safari mpaka tena wapate aliyesaini kile cheti *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi vituo ni mojawapo ya vikwazo vikubwa sana vya biashara kati ya Tanzania na nchi zingine, lakini vile vile ni chanzo vile vile cha kuwafanya watumiaji wengine wa bandari zetu washindwe kutumia bandari yetu. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie sana hivi vituo bubu, ikiwezekana viondoke vyote vinafanya nini? Kama mizigo ikishakaguliwa bandarini kwa nini iendelee tu kukaguliwa tena njiani? Itakaguliwa kule mwishoni. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, katika jimbo langu kuna Kivuko cha Mugala - Musoma Vijijini ni kibovu, hiki kivuko kimekuwa ni kibovu kwa muda mrefu. Wananchi wanaotaka kusafiri kwenda Musoma Vijijini na wanaotoka Musoma Vijijini kuja Jimboni kwangu Mwibara wanapata tabu sana. Naomba sana Serikali sasa ikamilishe ukarabati wa hicho kivuko.

Mheshimiwa Spika, kingine ni tunahitaji kivuko kwenda katika Kisiwa cha Nafuba. Kisiwa hiki kina watu wengi sana na ni kikubwa sana, watu wengi mahitaji yao wanachukua katika nchi kavu huku. Kwa hiyo, ningeomba sana Serikali sasa iweze kutafuta kivuko kwa ajili ya kusafirisha wananchi kwenda Nafuba na kuja sehemu zingine za Jimbo la Mwibara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo jingine liliopo ni vibali vya kusafirisha mitambo ya ujenzi, kwa mfano inapotokea mkandarasi anataka kusafirisha mtambo mmoja kwenda katika mkoa mwingine kibali lazima akipate kutoka Dodoma. Hiyo inachukua muda mrefu sana kuweza kupata hivi vibali, inapoteza muda wa biashara na inakuwa kabisa ni usumbufu mkubwa, naomba kuwa na *decentralization* ya kutoa hivi vibali vya kusafirisha mitambo ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni malipo ya waliopisha Mradi wa Barabara ya Bulamba – Kibara – Kisorya. Barabara hii imeshakamilika muda mrefu lakini wahusika bado hawajalipwa. Jana wakati natoa taarifa kwa mzungumzaji mmoja niliomba Serikali iingilie kati kuweza kuwalipa wahusika fidia zao ili na wao waweze kuendesha maisha yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kusema haya machache naomba niunge mkono hoja hii na nawapongeza sana Wizara na Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tecla Ungele atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck nchemba ajiandae ajiandae.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Mungu kwa nafasi hii na pumzi ya uhai. Natoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi anayofanya ya ujenzi na huduma zingine katika jamii yetu na hasa Mkoa wa Lindi. Pongezi nyingi pia zimuendee Mheshimiwa Wizara, Mheshimiwa Naibu Mawaziri na watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa kazi kubwa wanazofanya nzuri kona zote za nchi hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na sisi Wanalindi tunapongeza na tunamshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi inayofanyika ya ujenzi wa barabara kutoka Nanganga kwenda Ruangwa na hatimaye itaenda mpaka Nachingwea; kwa kweli tunashukuru sana. Tunaona sasa hivi nuru ipo ya Mkoa wa Lindi kuunganisha kwenda Mkoa wa Mtwara kwa lami, tunashukuru sana, ilikuwa adha ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na tunaona ukurasa wa 11 katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri tunaona kuna huu utaratibu wa *EPC + Financing,* tumeona utaratibu wa Barabara ya Masasi – Nachingwea kwenda Liwale unaenda kufanyika, zile kilometa 175 tunaenda kuziona kwa kutumia lami. Ahsante sana tunashukuru sana Wananachingwea, Wanaruangwa, Wanaliwale, Wanamasasi na Mkoa wa Lindi kwa ujumla. Barabara hii ilikuwa kweye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 ukurasa wa 75. Sasa Wanalindi wanashukuru inaenda kutekelezwa, ushauri wangu katika ujenzi wa barabara hii, wakandarasi watakapofika kwa utayari wa kujenga barabara ile, ninaomba, kwa kuwa Nachingwea ni katikati, ni *center,* basi watakapokuja na mitambo yao waielekeze mingine ielekee barabara ya kwenda Masasi. Ifanye kazi kuelekea Masasi na mitambo mingine ielekee Liwale, ifanye kazi kuelekea Liwale ili kazi hii ifanyike kwa wakati mmoja. Watafurahi sana watu wale, wananchi wa Nachingwea na kwingineko kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo pia kwa habari ya viwanja vya ndege. Tunaona Uwanja wa Ndege Nachingwea na Uwanja wa Ndege wa Lindi, imeelekezwa sana, tunaendelea kuomba sana, tunaomba viwanja vile viwekwe lami ili viwanja vile vitumike

wakati wote wa masika na wakati wa kiangazi. Kwa sababu sasa hivi Lindi kunakuja *LNG,* lakini pia Nachingwea viwanja vile vinatumika pia kusafirisha hata viongozi wa kitaifa. Tukiacha hata uchumi unaoenda kuongezeka kwenye maeneo yetu, tunaomba Waziri muangalie sana Viwanja wa Nachingwea na Lindi kwa upande wa lami. Lakini pia Mbunge wa Nachingwea alishasema wale waliopisha maeneo yao kwa ajili ya upanuzi wa viwanja vile basi walipwe fidia yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbushia Barabara ya Kibiti – Lindi ina lami tayari lakini kuna maeneo Mheshimiwa Waziri korofi. Kwa mfano kuna mahali panaitwa Muhoro, wameweka pale viraka viraka ambavyo ni shida, ajali zinatokea mara kwa mara, lakini kuna maeneo kutoka Somanga kuja Nangurukuru napo kuna changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaona kuna eneo linaitwa Kiranjeranje, lakini pia kuna eneo kuanzia pale Kirangara kwenda karibu na Mchinga kwenye ile njia panda ya kwenda Moka, nako pale barabara imeonyesha kuzama kuzama na kuinuka, kuzama na kuinuka. Kama *driver* akiwa ni mgeni maeneo yale au ameenda kwa *speed* pale kuna kutokea ajali mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusingependa wananchi wapate ajali, tusingependa watu wawe navilema vya kudumu na tusingependa vifo vitokee. Tunaomba marekebisho hayo yafanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutuangalia Wananachingwea, kutuangalia Wanalindi, sasa hivi tunaenda kufunguka kuwa na mawasiliano na mikoa mingine kupitia lami. Hicho ni kilio cha muda mrefu, kulikuwa na vumbi, kulikuwa na hofu, kulikuwa na mahangaiko. Ukishafika Masasi ukiwa kwenye basi utasikia wanasema, enhee, sasa tunaenda Tanganyika, tunaenda kutanganyika sasa. Kwani hakuna viongozi? Haya nayasema kwa sababu anayesifia mvua imemnyeshea. Nimeshasafiri kwenye mabasi hayo mara kwa mara, nafahamu hali ilivyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli sasa hivi sisi Wanalindi tunasema tuna imani na barabara hizi kwamba zinaenda kujengwa. Tuna imani kabisa kwa sababu hata vitabu vinasema kwenye Waebrania 11:1: "Imani ni kuwa na uhakika wa mambo yatarajiwayo, bayana ya mambo yasiyoonekana."

Mheshimiwa Spika, sisi Wanalindi tuna imani sasa hivi kama ile barabara ya lami kutoka Masasi - Nachingwea – Liwale tumeipokea hivi tayari ni kama vile tunapita. Tunaamini hilo Mheshimiwa Waziri ataenda kutekeleza, barabara itajengwa na Wanalindi watafarijika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge napata ujumbe wenu hapa kila mmoja anaandika kwamba jina lake lilikuwepo hajaitwa. Maana mmeshaanza kusikia kwamba Serikali imeshaanza kutajwa hapa. Sasa majina yanayokuja hapa maombi ni mengi kuliko nafasi zilizopo na nafikiri uamuzi wa nani aingie, nani asiingie kikanuni tayari tunafahamu.

Kwa hiyo, baadhi yenu kwa sababu ni wa upande wa Chama cha Mapinduzi wanaweza kumwomba Katibu pale ili wale ambao mmechangia mara chache mpelekwe kwenye ile Bajeti Kuu ambayo mtaweza kuchangia pia kuhusu barabara za maeneo yenu, lakini kwa siku ya leo nitawapa tu hawa wawili kwa sababu ndiyo nimeona huku wamechangia mara chache. Mheshimiwa Hamisi Taletale amechangia mara moja na Mheshimiwa Ally Makoa amechangia mara mbili. Kwa hiyo, watapewa fursa jioni hii. Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamisi Taletale, Mheshimiwa Ally Makoa ajiandae.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kuishukuru Wizara kwa sababu nimepitia na nimeona asilimia kubwa naona Mkoa wa Songwe kwa sehemu tumeguswa kwenye bajeti hii. Kwa hiyo niwapongeze kwa kweli na sisi Wanasongwe tunaona bajeti hii imetugusa kwa sehemu, kwa sababu ukiona kutoka Barabara ya Mbarizi mpaka Mkwajuni tumetengewa kilometa 86, siyo kidogo; japo bado lakini naamini wataendelea kutufikiria zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye Barabara ya Mlowo mpaka Kamsamba kilometa 50 wametutengea. Ukiangalia Barabara ya Mpemba mpaka Ileje, kilometa 50 na maeneo mengine wametugusa. Niombe tu kwamba bajeti hii tunaomba iwe inatekelezeka na itekelezeke kweli kwa sababu Wanasongwe tumetegemea hasa kwa sababu asilimia kubwa barabara hizi ni barabara za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo bado tuna changamoto kwenye maeneo mengine kwenye barabara hasa ukizingatia Barabara ya kutoka Mlowo inayopita Isansa – Magamba mpaka Mkwajuni. Tunaomba Wizara waliangalie hili. Barabara hii tumekuwa tuna changamoto kubwa sana hasa kwa wananchi wa Wilaya ya Songwe. Tumeendelea kulizungumza mara nyingi, wananchi wa Wilaya ya Songwe hapo wanapohitaji huduma za mkoa inawalazimu kwenda kupitia Mkoa wa Mbeya. Wakitoka Mkoa wa Mbeya ndiyo wanapata usafiri mwingine kuelekea Mkoani Songwe. Kwa hiyo tuombe Serikali waliangalie jambo hili kuweza kututengenezea barabara ya kutoka Mlowo itakayopita Isansa – Magamba mpaka Mkwajuni ili kurahisisha huduma kwa wananchi wa Wilaya ya Songwe.

Mheshimiwa Spika, pia kuna barabara nyingine ambayo pia imekuwa ni changamoto ni Barabara ya kutoka Chapwa inayopita Chindi mpaka Chitete. Tunaomba barabara hii Wizara iiangalie. Tunajua jinsi wananchi wa Momba ambavyo wanajishughulisha na shughuli za kilimo, ufugaji na mambo mengine. Tunaomba barabara hii waikumbuke kwenye bajeti zao ili tuweze kuwakomboa na kuwarahisishia huduma wananchi wa Wilaya ya Momba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, naomba nizungumzie, ni kweli tunatenga bajeti sana kwenye Wizara hii, lakini tunaona changamoto kubwa miradi mingi inachelewa kutekelezeka na kuchelewa kutekelezeka kwa miradi kunapelekea miradi mingi kuongezeka gharama. Gharama za miradi zinaongezeka kutokana na miradi mingi kuchelewa kutekelezeka. Tunaomba Wizara iliangalie hili ili mwisho wa siku tusiwe tunatumia fedha nyingi kwa ajili ya mradi ambao pengine unaweza kutekelezeka kwa fedha kidogo na fedha zingine zinaweza kusaidia kwenda kwenye maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine la wakandarasi kuchelewa kulipwa malipo yao. Tumeona sisi sote kwenye taarifa hata zilizopita wakandarasi wanavyocheleweshwa kulipwa malipo yao mara nyingi imetokea faini kwa Serikali, tunalipa fedha nyingi kwa sababu ya kuchelewesha malipo ya wakandarasi. Tunaomba Wizara iliangalie, tumeona maeneo mengi wakandarasi wanachelewa kukabidhi miradi, lakini hatuoni wao wakilipa zile asilimia ambazo wanatakiwa kukatwa pale wanapokuwa wamechelewesha mradi. Kwa hiyo tunaomba Wizara pia iliangalie hili ili tuende kwa usawa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, naomba nizungumzie suala la bandari kavu ndani Mji wa Tunduma. Sisi sote tunajua 70% ya mizigo yote inayoshuka katika Bandari ya Dar es Salaam inapita ndani ya Mji wa Tunduma na tumeendelea kusema, tumezungumza sana, tunaomba Serikali waangalie umuhimu wa kujenga bandari kavu ndani ya Mji wa Tunduma ili kurahisisha huduma.

Mheshimiwa Spika, wote tunajua ya kwamba Tunduma ni lango kuu la *SADC*. Mkoa wa Songwe ni lango kuu la *SADC,* Wizara iangalie umuhimu wa kujenga bandari kavu. Sisi sote tunajua nchi yetu na maeneo mengine tuko katika ushindani wa kibiashara. Wizara izingatie na iangalie umuhimu wa kujenga bandari kavu ndani ya Mji wa Tunduma ili kurahisisha huduma na wakifanya hivi na wote wanajua kabisa Halmashauri ya Mji wa Tunduma tayari imejitahidi kwa sehemu yake kuhakikisha inapambana kupata zaidi ya ekari 2,000 kwa ajili ya kujenga

bandari kavu ndani ya Mji wa Tunduma. Tunaomba Serikali waliangalie hili kwa umuhimu wake ili kuhakikisha Halmashauri ya Mji wa Tunduma inajengwa bandari kavu kama eneo la lango kuu la *SADC* na hiyo itakuwa imerahisisha huduma sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie jambo lingine ambalo ni suala la Uwanja wa Kagera, Uwanja wa Ndege. Wote tunajua changamoto ambazo zimeendelea kutokea Kagera. Tumeona maafa, tumeona wananchi wamepoteza maisha, tumeona na changamoto hizi zinasababishwa na hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali ione umuhimu wa kujenga uwanja mwingine mpya ndani ya Mkoa wa Kagera, kwa sababu sisi sote tunajua kuna uhitaji mkubwa wa usafiri wa anga kwenye Mkoa wa Kagera. Hebu Wizara waliangalie hili na waone umuhimu wa kujenga uwanja mpya ili kuepusha maafa zaidi yanayoweza kutokea kwenye Mkoa wa Kagera. Wananchi wetu tunawahitaji na huduma tunahitaji zitolewe, tena huduma zilizo sahihi zaidi. Wizara ione umuhimu wa kujenga uwanja mpya ndani ya Mkoa wa Kagera ili tuweze kurahisisha huduma kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nizungumzie suala la *ATCL.* Wamezungumza wengi sana, naomba niishauri Wizara, naomba niishauri Serikali, ni kweli watu wamezungumza sana *ATCL,* lakini Serikali ione namna gani ya kulisaidia Shirika la *ATCL* ili lisiweze kuingia hasara kama tunavyoiona sasa. Kwa asilimia kubwa naona hata Serikali wanasababisha shirika hili kuendelea kudidimia. Nasema hivyo kwa sababu Serikali wameikodishia ndege *ATCL,* ndege zinakamatwa lakini *ATCL* bado inaendelea kuwalipa Serikali. Serikali ikae chini ijitafakari na wao watakuwa ni sehemu ya kulididimiza hili shirika. Serikali iangalie namna ya kuisaidia *ATCL* ili iweze kuinuka kutoka mahali ilipo kwenda eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamisi Taletale atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Makoa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ajiandae.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza ningependa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa mema yake anayofanyia Nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nipende kumpongeza Mheshimiwa Waziri kaka yangu pamoja na jopo lake. Huyu Waziri ana kitu ndani yake, atafika mbali. Naona kabisa wakati tunapambana na Barabara yetu ya Bigwa – Kisaki, nilimsumbua akaniita nyumbani kwake, lakini pia akaniita ofisini na jopo la wataalam 20. Nikashangaa mimi mtoto wa Kiluguru hawa wataalam 20 nitaongea nao nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale wataalam wakaniambia tunakuhakikishia hii barabara tutaipata, njia ni kupata fedha, bado naendelea kusema Mheshimiwa Waziri ana kitu ndani yake, atafika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alisema nitaongea na mama yako na leo nathubutu kusema katika ule Mkoa wa Morogoro katika Wabunge wanaopendwa na Mama Samia, mimi ni *number one. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kupata Barabara ya Bigwa – Kisaki, kilometa 73 ambayo haijawahi kutokea, mimi *number one*. Wamepita Wabunge kibao huko nyuma na wananchi wangu wameniambia usipotuletea Barabara ya Bigwa – Kisaki hurudi hapa. Wameona matangazo ya Mheshimiwa Waziri pale kwamba Juni tunakwenda kusaini ile barabara na mimi nauona mlango wangu wa kubaki Kusini Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kuipongeza hii Wizara na niendelee tena kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutupa Barabara yetu ya Ubena – Zomozi ya kilometa 11. Hii Barabara ya Bigwa – Kisaki

inakwenda kufungua mipaka na tunakwenda kukutana na mtani wangu kule Mchengerwa. Nimwombe Mheshimiwa Waziri tumeona matangazo ya Juni, 2023. Naomba *specific date* kwamba naomba tarehe na mimi nikamuwekee mziki mnene pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie hiyo tarehe ambayo tunakwenda kusaini ule mkataba, nataka Taifa lijue Mama Samia ameweka alama, ameweka mguu mzito pale Kusini Mashariki na sisi tunakwenda kuonekana, tunakwenda kutoka kwenye matatizo. Ile Barabara, leo hii Dar es Salaam wanakula matunda yanatoka Morogoro Vijijini, Iringa wanakula matunda yanatoka Morogoro Vijijini. Hata hapa Dodoma wanakula matunda yanatoka Morogoro Vijijini. Ukizungumzia Bigwa – Kisaki leo hii unazungumzia wauza *juice* wengi wa pale Dar es Salaam. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, hii Juni, 2023 tunaomba tujue *specific date* ili na nimwandalie muziki mnene asubuhi pale na kuandaa watu wampokee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie, hii Wizara ina watu ambao naendelea kuwaambia watafika mbali. Kaka yangu Kadogosa ana kitu ndani yake, atafika mbali. Mkurugenzi wa Shirika la Ndege, ndugu yangu ana kitu ndani yake, atafika mbali; lakini mtu mzito kabisa kaka yangu, bosi wa *TBA*, huyu ana kitu hasa ndani yake, atafika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, sina mbambamba nyingi. Namkaribisha Mheshimiwa Waziri Kusini Mashariki, tuzindue barabara yetu, tusaini mkataba wetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ally Makoa atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete ajiandae.

Waheshimiwa Wabunge, mijadala ambayo ni ya muhimu sana kuhusu bajeti hii tunayoendelea na kuijadili hapa, najua mnajadili mambo ya muhimu sana, lakini punguzeni sauti ili wasikike wanaochangia. Mheshimiwa Ally Makoa.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi. Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna alilvyoonesha mafanikio makubwa sana kwenye Wizara mbalimbali hususan hii Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa miradi mikubwa ya reli, barabara, bandari, ununuzi wa ndege na miradi mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitoe shukrani zangu kwa Wizara inayoongozwa na Mheshimiwa Mbarawa pamoja na Naibu Mawaziri wawili, Katibu Mkuu na Watendaji wote niwapongeze kwa juhudi kubwa za kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu haya ya kuitengeneza Tanzania katika ubora wa viwango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mambo machache, kwanza nishukuru Wizara kupitia Mheshimiwa Mbarawa kwa kukubali kuingiza ile Barabara ya kutoka Dalai – Mondo kwenda Bicha ambayo ndiyo iliyokuwa imetajwa kwenye Ilani na baadaye kidogo kukawa na sintofahamu, lakini baada ya kutusikiliza ameamua kuirudisha, namshukuru sana, hii kilometa 35, sasa ni habari njema kwa Wakazi wa Kondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishukuru pia Serikali kwa kukubali baada ya miaka miwili sasa imekubali kutupelekea fedha kwa ajili ya kipande kidogo kile cha kilometa 0.8 kutoka *NMB* mpaka *National Milling*. Nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba kipande hicho wamekiingiza, nawashukuru sana Wizara ya Ujenzi kwa kutupa faraja na matumaini. Ikumbukwe kwamba hii ni bajeti ya tatu, bajeti zote mbili hatukupata bahati ya kutengewa fedha na ndiyo kipindi hiki tumetengewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa nina *concern* ndogo kwamba barabara hii ipo kati kati ya mji, lakini inapoanzia pale Magereza mita 100 kuna mto mkubwa ambao masika yote huwa hapapitiki. Nawakumbusha Wizara pale kunatakiwa lijengwe daraja. Kwa hiyo wafahamu hilo kwamba barabara yao hii inayoingia mjini katikati kuna daraja ambalo linatakiwa lijengwe la *TANROADS*.

Daraja lililopo ni dogo sana ambalo linamilikiwa na *TARURA* na limekuwa likileta athari kubwa kwa wananchi na limekuwa likisababisha ajali kutokana na udogo na daraja lenyewe ni la muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, wiki mbili zilizopita niliuliza swali juu ya barabara hii na majibu ya Serikali yalikuja kwamba tutatengewa kilometa tatu za lami mjini ikiwepo kipande hiki cha kilometa 0.8, lakini kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijaona kama hizo kilometa tatu zimeinishwa pale. Kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Waziri kama kulikuwa na kausahaulifu kidogo nikumbushe tu, majibu ya Serikali wiki mbili zilizopita tuliambiwa tutapewa kilometa tatu ambayo kilometa hizi 2.2 ambazo zitakuwa zinatokea *TANESCO* kuelekea Daraja la Munguri B. Kwa hiyo niombe waingize hiyo kwenye bajeti ili iwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, leo hoja kubwa iliyopo katika Jimbo la Kondoa Mjini ni lile Daraja la Munguri B. Tunaishukuru Serikali ilitutengea shilingi milioni 600 katika bajeti hii tuliyonayo na katika bajeti hii tumeona kuna shilingi milioni 150. Tunaishukuru sana Serikali, lakini Mheshimiwa Mbarawa akumbuke, aliposimama Mheshimiwa Rais pale Bicha, hoja aliyomuuliza ni juu ya daraja hili na akalitolea maelezo. Kwa kweli ujenzi wa daraja hili ni muhimu sana kutokana na uchumi wetu ambao watu wengi wanalima eneo la pili la Mto Bubu, lakini pia tumefungua utalii kwenye Pori letu la Swagaswaga.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaomba daraja hili walitilie mkazo *at least* ukifika mwezi wa sita itangazwe *tender* kama zilivyotangazwa za madaraja mengine ya Mkoa wa Dodoma. Kwa hiyo hili naomba Waziri alichukulie maanani kwa sababu hakuna hoja kubwa zaidi ambayo Mheshimiwa Rais anaweza akauliza sasa hivi katika Jimbo la Kondoa Mjini zaidi ya daraja hili.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, *TANROADS* walipita Barabara ya kutoka Dodoma kwenda Babati ilipita ikamega eneo la Shule ya Msingi Nkuku na kukawa na mazungumzo ya kulipa fidia ili ile shule tuiondoe pale tuipeleke sehemu nyingine. Niombe Wizara kwenye bajeti hii watutengee fedha ili tuiondoe ile Shule

ya Nkuku tujenge shule nyingine ya msingi kwa ajili ya kunusuru madhara ambayo yanaweza yakajitokeza kwa sababu ile shule sasa hivi iko barabarani sana. Kwa kweli Wizara ya TAMISEMI wametuletea shilingi milioni 370 za ujenzi wa shule ya msingi mpya. Kwa hiyo nadhani ni kiwango hicho hicho ambacho *TANROADS* wanapaswa watutengee kwa ajili ya kunusuru maisha ya watoto ambapo shule ile iko barabarani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha uendelezaji wa miradi ya kimkakati na pia utayari wetu wa ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miezi kumi ya bajeti inayoishia Juni, 2023 Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imetekeleza miradi mingi ya miundombinu ya barabara, reli, bandari na uimarishaji wa safari za anga ikiwemo ujenzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege. Naipongeza Serikali kwa hatua nzuri za utekelezaji wa mradi wa kihistoria wa ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* pamoja na uboreshaji wa bandari utaimarisha kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi yetu. *SGR* na bandari ni nguzo imara ya kiushindani katika biashara ya usafirishaji wa ndani na nchi za Maziwa Makuu na hata za Kusini mwa Afrika na Kati. Bandari za Tanzania ni lango la usafirishaji kwa Zambia, Malawi, DR Congo, Uganda, Burundi, Rwanda, Sudan ya Kusini na hata Zimbabwe na Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi kubwa kuhakikisha ujenzi wa *SGR* unaendelea kwa kasi ile ile na pia napongeza jitihada za kuendelea kutafuta vyanzo vya fedha vya masharti nafuu kugharamia ujenzi huo. Pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa, Serikali imefanya maboresho makubwa ya miundombinu na huduma katika bandari zetu hususana bandari ya Dar es Salaam ili kukabiliana na ushindani mkubwa wa bandari zingine za ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika. Bandari ya Dar es Salaam inakumbana na ushindani mkubwa toka bandari za Mombasa (Kenya), Beira (Msumbiji), Nacala (Msumbiji), Durban (Afrika Kusini), Lobito (Angola) na Walvis Bay (Namibia). Maboresho ya bandari zetu iendane na kuondoa changamoto zingine ambazo zinasababisha gharama kubwa za usafirishaji kwa bandari zetu na kusababisha kupoteza biashara ya usafirishaji kwa bandari shindani. Ufanisi wa bandari unategemea pia maboresho ya barabara, Reli ya Kati *(TRL),* Reli ya *TAZARA*, utendaji wenye tija wa wadau wote wa bandari na hata watumishi ili kupunguza gharama za usafirishaji kwa wateja wa bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa karibu asilimia 70 ya mzigo wote wa nchi za nje unasafirishwa kwa kupitia *Dar es Salaam Corridor* ambapo DR Congo ni asilimia 38, Zambia asilimia 26, na Malawi asilimia 6. Pamoja na fursa za kijografia ya bandari zetu, mzigo unaopita sasa kwenye bandari ya Dar es Salaam, ni chini

ya asilimia 50 ya biashara yote ambayo kwa sasa sehemu kubwa inashikiliwa na bandari shindani.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa za kiushindani zinatokana na ufanisi usiokidhi ushindani na gharama kubwa za bandari na watoa huduma wa Bandari ya Dar es Salaam. Pia kuna changamoto za kiutendaji kwa mashirika ya reli ya *TAZARA* na hata reli ya kati *(TRL)* inayopelekea gharama kubwa ambazo siyo za kiutendaji, kwa ajili ya kunusuru biashara hii inayopotea kwa bandari shindani, Serikali ichukue hatua za haraka kuboresha huduma za *TAZARA* ikiwa ni pamoja ya maboresho ya miundombinu ya reli, ununuzi wa vichwa vya treni, mabehewa na vitendea kazi vingine.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali kwa haraka ishughulikie maboresho ya Mkataba wa *TAZARA* na kisha kufuta fedha ya masharti nafuu angalau kiasi cha shilingi bilioni 200. Katika kipindi hiki cha ushindani mkubwa na hata mfumuko wa bei wa mafuta ya petroli, mbolea na bidhaa mbalimbali, usafirishaji wa reli ni mojawapo ya suluhisho kubwa kupunguza mzigo wa bei kubwa kwa wateja wa bandari zetu na hata wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maboresha ya reli ya TAZARA, napendekeza kuendelea na ujenzi wa Bandari Kavu Mbeya ambayo ina fursa kubwa katika kipindi hiki katika kuwezesha kupunguza gharama za kusafirisha kwa wateja wa bandari na hata kupunguza bei za mafuta ya petroli, pembejeo na mazao ya kilimo. Bandari Kavu ya Mbeya ni njia panda kwa wateja wa nchi za Malawi, Zambia, DRC Lubumbashi na hata kwa Zimbabwe na Msumbiji. Serikali ichukue hatua za haraka kuinusuru reli ya *TAZARA* hata ikibidi kurekebisha mikataba ya umiliki na uongozi ili mradi iendeshwe kwa tija. Kuna kuchukua hatua za makusudi kwa kutumia zaidi *TAZARA* kusafirisha mizigo ambayo imeelemea hata uwezo wa barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, usafirishaji wa mizigo kwa kutumia *TAZARA* ilenge kupunguza gharama za mafuta ya petroli, pembejeo kwa wakulima na wakati huo kupunguza gharama za

kusafirisha mazao ya wakulima. Pamoja na kuboresha *TAZARA*, napendekeza kukamilisha taratibu za ujenzi wa Bandari Kavu ya Mbeya ambapo Mamlaka ya Bandari kwa kipindi kirefu wamewahakikishia wananchi kulipa fidia ya eneo lao wanalolichukua.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Bandari ya Dar es Salaam kuingia makubaliano na *TAZARA* na *TRL* ili iweze kumiliki mabehewa yake kwa lengo la kuongeza ufanisi na kupunguza gharama ambazo sio za kiushindani. Pamoja na hatua hiyo, kuna fursa kubwa ya kutafuta mwekezaji mwenye uzoefu mkubwa ikiwemo mtandao wa bandari kwa lengo la kuboresha utendaji hasa kwenye upande wa makontena. Serikali ifanye jitihada ya kupata mwekezaji ikiwemo kwa mfumo wa *PPP* kwa lengo la kuongeza biashara ikiwemo kurudisha biashara iliyopotea kwa bandari shindani.

Mheshimiwa Spika, kwa siku za hivi karibuni kuna mahitaji makubwa ya kusafirisha makaa ya mawe kwenda soko la nje na pia uingizwaji wa *Sulphur* kutoka nje lakini imepelekea kuthibitisha upungufu mkubwa wa gari kubwa hasa aina ya *tiper*. Upungufu huu unapelekea kuzorota kwa ufanisi wa huduma ya bandari.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iendelee na mkakati wa kutafuta mwekezaji wa Bandari ya Mbegani – Bagamoyo ambayo ina lango lenye kina cha asili cha mita 18 na haina kikomo cha upana wa meli ambazo zinaweza kuingia na kutoka bandarini hapo. Kutokuwepo kwa ukomo katika lango, bandari hiyo inaweza kuhudumia meli ambazo zinahudumiwa kwenye bandari kubwa duniani zenye urefu wa mita 400 na uwezo wa kubeba makasha hadi *TEUs 22,000.* Aidha, uwezo huu ni mkubwa katika eneo la Afrika Mashariki na Kati kwani kwa sasa hakuna bandari yenye uwezo kama huo. Hivyo, uendelezaji wa Bandari ya Mbegani, Bagamoyo utasaidia kupunguza msongamano wa shehena katika Bandari ya Dar es Salaam na kupelekea bandari zote kuwa shindani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto za mfumuko wa bei za mafuta na pembejeo, kuna fursa kubwa na hasa

mahitaji makubwa ya mazao ya kilimo kwa soko la ndani na nje. Uzalishaji kwa tija unategemea kwa kiasi kikubwa ubora wa miundombinu ya barabara, reli na hata anga. Serikali iweke msukumo zaidi kwenye kuboresha miundombinu ya barabara ili kurahisisha usafirishaji wa pembejeo na mazao ya kilimo. Kutokana na fursa za uzalishaji mkubwa kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, napendekeza mwendelezo wa uboreshaji wa barabara za *TANZAM* kipande cha Igawa - Tunduma; barabara ya *bypass* ya Uyole - Songwe; barabara ya *bypass* ya Iwambi - Mbalizi; barabara ya Mbalizi – Shigamba – Isongole kutokana na uzalishaji wa mazao ya kilimo; barabara ya Mbalizi – Galula – Makongorosi kutokana na uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo na madini; na pia barabara ya Isyonje – Kikondo – Makete ambayo ni muhimu sana katika kusafirisha mazao ya kilimo ikiwemo maua, parachichi na viazi kwa soko la nje.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa barabara hizi pamoja na uwanja wa ndege wa Songwe ni muhimu sana kwa usafirishaji wa mazao yetu kwa soko la ndani na nje, na kwa kiasi kikubwa utaongeza mapato ya fedha za kigeni. Maboresho ya uwanja wa ndege wa Songwe uende sambamba na ujenzi wa maghala mahususi wa maua, mbogamboga, parachichi, nyama, viwanda vya kuengeza thamani za mazao na madini, na *EPZ/Industrial Park*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ajali za mara kwa mara za Mlima Iwambi, Mbalizi na msongamano wa magari yakiwemo malori ya mizigo na mafuta ya petroli, tunashukuru kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchukua hatua za haraka kuanza ujenzi wa barabara ya njia nne kwa barabara ya *TANZAM* kipande cha Uyole mpaka Uwanja wa Ndege wa Songwe. Katika vipindi mbalimbali, viongozi wa Kitaifa waliagiza upanuzi wa kipande hiki cha *TANZAM* pamoja na ujenzi wa *bypass* ya Uyole – Songwe kilometa 40 na *bypass* ya Mbalizi – Iwambi kilometa 6.5. Ujenzi wa barabara hizi utanusuru wananchi kuendelea kupoteza maisha kwa ajali za mara kwa mara katika eneo hilo. Hatari zaidi ni kwa magari makubwa yanayosafirisha mafuta kupita barabara yenye msongamano mkubwa katikati ya Jiji la Mbeya.

Msongamano wa magari makubwa katika barabara ya *TANZAM* ni sehemu ya changamoto zinazopelekea bandari zetu kupoteza biashara kwa bandari shindani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, niungane na Watanzania wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika nyanja mbalimbali sisi Watanzania wote na Taifa letu kwa ujumla, sisi kama Taifa hatuna cha kumlipa muumba wetu zaidi ya maombi na sala kila wakati.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuungana na wananchi wa Jimbo langu la Mbulu Mjini kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali nzima ya Awamu ya Sita kwa jinsi tunavyotekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025 kwa kila sekta, tuendelee kuiombea Serikali yetu amani, upendo, mafanikio na mshikamano kwa Mwenyezi Mungu wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wangu wa dhati nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa Waziri wetu wa Ujenzi, Naibu Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Balozi Asha – Katibu Mkuu Ujenzi, Mheshimiwa Joseph Migire, Katibu Mkuu - Uchukuzi, Naibu Makatibu Wakuu wote, Wakurugenzi wote wa Wizara, Ndugu Rogatus Mativila - Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* na timu yake ya watendaji wote makao makuu na Meneja wa Mkoa wa Manyara kwa jinsi wanavyotekeleza majukumu yao na kutusikiliza changamoto zilizoko kwenye majimbo yetu na kuzitatua kwa kadri ilivyowezekana.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii muhimu sana kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambayo imewasilishwa katika Bunge letu na taarifa ya Kamati yetu ya kudumu ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu kupitia Wizara ya Fedha ijitahidi kutoa fedha za malipo ya wakandarasa wanaojenga miradi ya barabara na miundombinu mbalimbali ya ujenzi kwa wakati ili kuepuka gharama za malipo zinazoongezeka nje ya mikataba na wananchi kupokea huduma iliyotarajiwa kwa mujibu wa mikataba.

Pia Serikali iangalie utaratibu wa kuongeza bajeti ya dharura kwa Wakala wa Barabara *TANROADS* kwa ajili ya madhara yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi hali inayofanya barabara nyingi kujifunga na kuleta adha kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itusaidie mpango kabambe wa kujenga kilometa tano za zege katika barabara ya Mbuyu wa Mjerumani – Magara - Mbulu sehemu ya Mlima Magara kwa kuwa mpango wa zege katika eneo la Mlima Magara imekuwa ahadi ya viongozi wetu wakuu kutoka Serikali ya Awamu ya Nne, Tano na Sita. Hivyo basi eneo hilo ni hatarishi sana na matengenezo yake yamekuwa na gharama kubwa yasiyo na tija.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana Serikali yetu kwa mpango wa ujenzi barabara ya Karatu, Mbulu, Haydom, Maswa, Sibiti. Tunaiomba Serikali mkataba wake usainiwe haraka kwa kuwa ni kiu ya wananchi wa majimbo yote sita katika mikoa ya Arusha, Manyara, Singida, Simiyu mpaka Shinyanga. Mradi huu utagusa sana hisia ya wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa utendaji kazi mzuri, pia watendaji akiwamo Katibu Mkuu Balozi Aisha.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa naomba kuwasilisha kilio cha wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini kuhusu barabara ya kutoka Singida - Ilongero - Haydom. Barabara hii ni ahadi ya viongozi wote wa Kitaifa ambao hufika

Ilongero kuanzia Hayati Mwalimu Julius Nyerere hadi Rais aliyepo madarakani alipokuwa Makamu wa Rais alifika Ilongero akaahidi kuhakikisha barabara hii inawekwa lami.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha hata katika bajeti hii ya leo barabara hii haipo katika mpango. Ni miaka 60 ya Uhuru leo Wana-Singida Kaskazini wanalia, wanateseka, wanataabika, wanakarahika na mateso ya hii barabara.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri aipe kipaumbele barabara hii muhimu kwa uchumi wa Wana-Singida, ni roho ya uchumi wa Wana-Singida Kaskazini. Ni barabara ya msaada mno lakini imekuwa longolongo miaka nenda-rudi, na mimi Mbunge nimechoka matusi ya wananchi. Naomba lami katika hii barabara katika bajeti hii ya mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, naomba tupate walau kilometa kumi za lami katika barabara hii hadi makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Singida katika Mji Mdogo wa Ilongero. Watumishi hivi sasa hawakai kwa kukimbia mateso ya barabara hii hususan wakati wa masika na rasta zinazokera na kuharibu magari ya watu.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja ya bajeti ya Wizara hii ya Ujenzi hadi nione fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii muhimu sana kwa maisha ya Wana-Singida Kaskazini. Nataka nione kilometa kumi hadi katika Mji wa Ilongero.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Profesa Makame Mbarawa na Naibu Mawaziri wake wawili; Mheshimiwa Atupele Mwakibete na Mheshimiwa Godfrey Kasekenya kwa kazi kubwa wanazofanya kwenye kutengeneza mitandao ya barabara na ujenzi wa miundombinu mbalimbali nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utahusu umuhimu wa kujenga kwa lami barabara ya zamani ya Moshi - Arusha *(Old*

*Moshi Road)* na changamoto za barabara katika jimbo langu la Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa kwanza ni kuhusu umuhimu wa barabara ya zamani ya Moshi - Arusha *(Old Moshi - Arusha Road)*. Hii ni barabara iliyokuwa imejengwa kwa lami toka wakati wa mkoloni. Kwa upande wa Arusha, kipande cha Mkoa wa Arusha kimeshajengwa na kinaendelea kukarabatiwa kwa kiwango cha lami (Kijenge hadi *USA River)*. Kwa upande wa Mkoa wa Kilimanjaro, hakuna ambacho kimefanyika; kwa upande wa Moshi, barabara hii inaanzia *keep left* inakoanzia barabara ya Arusha kuelekea barabara ya *International School* kuelekea Daraja la Muitaliano, Magereza, Kwa Akwilini, Weruweru Sekondari kutokea *Lambo Estate.*

Mheshimiwa Spika, barabara hii ikitengenezwa, itakuwa ni ya mchepuko *(bypass)* kuingia na kutoka Mjini Moshi kama ilivyo ile ya *USA River.* Vilevile itakuwa ni ya msaada mkubwa kama kutatokea kikwazo cha aina yoyote ile cha magari kupita kwenye ile barabara kuu ya Arusha - Moshi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili utahusu changamoto za barabara zinazojengwa na *TANROADS* Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Moshi Vijijini, barabara ya Kibosho Shine - Mto Sere inahudumiwa na *TANROADS*. Wameshaweka mitaro katika baadhi ya maeneo, na haijajengwa hata kidogo kwa kiwango cha lami. Barabara hii ni muhimu kwani ni sehemu ya kusafirisha watalii kwenda Mlima Kilimanjaro kupitia njia ya Umbwe. Tunaishukuru Serikali kwani kwenye bajeti ya mwaka 2023/2024 kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali wamepanga kukarabati kilometa 2.1 za barabara hii kwa shilingi milioni 119.79.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa kuendeleza ujenzi wa barabara ya Kiboriloni - Kikarara - Tsuduni - Kidia kwa kiwango cha lami. Barabara hii inajengwa na *TANROADS* na bado haijakamilika. Mwaka 2023/2024 barabara hii imetengewa shilingi milioni 160.00 kutoka kwenye Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kibosho Shine - Kwa Raphael - *International School* ilikuwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi toka mwaka 2005 na inajengwa na *TANROADS* lakini hadi leo haijakamilika. Bado kipande cha kama kilometa nane. Tunaishukuru Serikali kwani kwenye bajeti ya mwaka 2023/2024 Serikali imepanga kujega kwa kiwango cha lami kipande cha kilometa 0.9 kwa kutumia shillingi milioni 266.2 kwa kutumia Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Rau - Uru - Shimbwe yenye urefu wa zaidi ya kilometa 13 ilikuwa kwenye ahadi ya kujengwa kwa kiwango cha lami. Tunaishukuru Serikali kwani ujenzi umeanza na mwaka huu wa fedha wa 2023/2024 Mfuko Mkuu wa Serikali utajenga kwa kiwango cha lami urefu wa kilometa 1.1 kwa kiasi cha shilingi milioni 325.05, na *Road Fund* watakarabati kilometa 2.9 kwa kutumia shilingi milioni 105.00.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Uru - *Kishumundu Parish* - Materuni iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa mpango wa kuijenga kwa kiwango cha lami. Tunaishukuru Serikali kwa kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Lakini mwaka huu wa 2023/2024 zimetengwa shilingi milioni 79.86 kukarabati kilometa 1.4, na mfuko wa barabara wametenga shilingi milioni 150.00 kuweka lami.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mabogini inakojengwa Hospitali ya Wilaya kuna changamoto kubwa ya ubovu wa miundombinu ya barabara. Hii inajumuisha barabara ya *TPC* - Mabogini - Kahe yenye urefu wa kilometa 11.4. Barabara hii imekuwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi toka mwaka 2010 ambapo waliahidi kuitengeneza kwa kiwango cha lami, lakini hadi leo ujenzi haujatekelezwa. Kwa kuwa iko chini ya *TARURA* na kwa kuzingatia bajeti finyu ya *TARURA* hadi leo ahadi hiyo haijatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na hali hiyo, nikiwa kama mwakilishi wa wananchi hawa nilipeleka ombi kwa Baraza la Maendeleo la Mkoa wa Kilimanjaro *(RCC)* kuipandisha hadhi na kuiombea ihudumiwe na Wakala wa Barabara *(TANROADS)*. Ombi hili liliridhiwa na *RCC* na bodi toka mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya hapo juu, naishauri Serikali ifanye yafuatayo; kwanza, naishauri Serikali iweke kwenye mipango kujenga barabara ya mchepuo *(bypass)* kwenye ilikokuwa barabara ya zamani ya Moshi - Arusha. Upande wa Moshi barabara hii inaanzia *keep left* ya Arusha kuelekea barabara ya *International School* kuelekea Daraja la Muitaliano, Magereza, Kijiji cha Eka, Kwa Akwilini, Weruweru Sekondari kutokea *Lambo Estate*.

Mheshimiwa Spika, pili, ninaiomba Serikali itenge fedha za kutosha na ianze kujenga kwa kiwango cha lami kipande cha barabara ya *Kibosho Shine* - Mto Sere kinachojengwa na *TANROADS*. Vilevile ninaishauri Serikali ifikirie kujenga kwa kiwango cha lami kipande cha Sere hadi *gate* la Umbwe la kupanda Mlima Kilimanjaro. Barabara hii ni mbovu mno pamoja na kwamba hutumika kusafirisha watalii wanaopanda Mlima Kilimanjaro kupitia njia ya Umbwe na kuingizia Serikali kipato kupitia sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, tatu, ninaiomba Serikali itenge kiasi cha fedha za kutosha na kukamilisha ujenzi wa barabara ya Kiboriloni - Kikarara - Tsuduni - Kidia kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, nne, ninaiomba Serikali ikamilishe ujenzi wa barabara ya *Kibosho Shine* - Kwa Raphael - *International School* kwa kiwango cha lami kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi toka mwaka 2005. Ujenzi wa barabara hii umechukua zaidi ya miaka 13.

Mheshimiwa Spika, tano, ninaishauri Serikali itenge fedha za kutosha na kukamilisha ujenzi wa barabara ya Rau - Uru - Shimbwe kwa kiwango cha lami yenye urefu wa zaidi ya kilometa 13 kama wananchi walivyoahidiwa wakati wa kampeni.

Sita, ninaishauri Serikali itenge fedha na kukamilisha ujenzi wa barabara ya Uru - Kishumundu - Materuni.

Mheshimiwa Spika, saba, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi iingize barabara ya *TPC* - Mabogini - Kahe yenye urefu wa

kilometa 11.4 kwenye mtandao wa *TANROADS* kwani *RCC* na bodi walikubaliana na ombi hili toka mwaka wa 2021. Ninaiomba Serikali itenge fedha za kutosha na ujenzi wa barabara hii uanze mara moja kwani Hospitali ya Wilaya inajengwa eneo hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya ushauri nilioutoa hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza Waziri na timu yake kwa bajeti ambayo imefafanuliwa vema sana. Nina mawazo ambayo naomba kuyawasilisha kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nianze na *EPC+F;* napongeza hatua hii ambayo kwa mujibu wa hotuba ya Waziri mikataba itasainiwa kabla ya mwezi Juni. Jambo hili linaonekana kama ndoto na wananchi wamekuwa bado gizani, nadhani wataamini pale watakapoona kweli mkataba unasainiwa. Hizi ndio *feelings* za wananchi wanaosubiri kuanza kwa ujenzi wa barabara ya Mafinga - Mgololo.

Mheshimiwa Spika, tunachokifanya ni maendeleo lakini pia ni kujenga na kuimarisha siasa na uelewa wa wananchi. Wananchi wakiwa na mashaka ni muhimu Serikali kuwaondolea mashaka, tunaita *political management* kwamba hiki kilichoandikwa ndicho kitakachotendeka. Nasema hivi kwa sababu kwa uelewa wa wananchi kutokana na Bajeti ya Ujenzi hii tunayoendelea nayo kwa maana ya mwaka 2022/2023, matarajio yao ni kwamba ujenzi ulikuwa unaanza mwaka huu, kwa hiyo wanaposikia kwamba mkataba wa *EPC+F* utasainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Juni, wanatuambia mbona kila mwaka mnaitaja tu hii barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo na kwa kuwa siasa ni *perception*, nashauri shughuli ya kusaini mikataba na wakandarasi iwe shughuli nzito ili kuimarisha imani ya wananchi kwa Serikali yao. Barabara hii imesubiriwa miaka mingi, ni ukombozi kwa uchumi wa Mufindi, Iringa na Taifa kwa ujumla

hasa kutokana na umuhimu wa mazao ya misitu na zao la parachichi.

Mheshimiwa Spika, nashauri shughuli iwe shirikishi kwa maana ya Chama, Serikali na Halmashauri (Madiwani) washiriki katika *signing ceremonies.*

Mheshimiwa Spika suala la pili ni ufafanuzi, wananchi wanafuatilia sana hizi hotuba katika mitandao, wanauliza kuwa hii barabara Kasma 4037 imeandikwa kilometa 78 na imetengewa shilingi 50.00? (ukurasa wa 248), na kwamba chanzo cha fedha ni *GoT* kwa maana Serikali ya Tanzania, na mbona kwenye hotuba Waziri ametaja hiyo *EPC+F,* je, kipi ni kipi, nami nauliza kwa lugha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika ushauri wangu, kwa kuwa jambo hili ni geni na ili kuwapa wananchi *comfort* na uelewa Mheshimiwa Waziri anapojumuisha atolee ufafanuzi ni nini hii *EPC+F.* Ni muhimu sana wananchi kuelewa na sehemu sahihi ya kueleweshwa ni wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *ATCL;* napongeza jitihada za Serikali kununua ndege na hasa ya mizigo. Hata hivyo nina ushauri kuhusu *ATCL* hasa katika suala la *delays* na kukosekana kwa *connections.* Ilivyo kama unatoka Dodoma kwenda Mbeya lazima ukate tiketi mbili, yaani Dodoma-Dar, kisha Dar-Mbeya. Nimeshauri suala hili mara kadhaa, sasa sijui ni masuala ya kitaalam au ni kitu gani. Kwa nini tusiwe na *connecting routes*?

Mheshimiwa Spika, nimeshauri pia mara kadhaa kwamba pawepo na *routes* za kuanzia Dodoma kwenda pande kuu za nchi hata kama itakuwa kupitia Dar. Kwa mfano kwa nini tusiwe na *routes Dodoma to KIA, Dodoma to Mbeya, Dodoma to Mtwara via Dar. Dodoma to Mwanza* na *Dodoma to Kigoma via Tabora.* Ikiwa juzi tumezindua Ikulu yetu maana yake ni kwamba sasa Dodoma ni *real capital city* ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia ili kuendana na kasi ya kupokea watalii kama matokeo ya *Royal Tour,* tufikirie kuwa na

ndege ambazo zitakuwa zinabeba abiria kwenda kwenye mbuga za wanyama. Tukiwa na ndege za kubeba abiria kati ya nane hadi 14, zitabeba watalii kutoka *KIA to Manyara,* Serengeti, Mikumi, Ruaha na kadhalika. Tukiwa na ndege za aina hiyo zitasaidia kupunguza gharama za kufikisha watalii mbugani lakini pia watafika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, taa za barabara katika Mji wa Mafinga; naomba kukumbusha uwekaji wa taa za barabarani kando ya barabara ya *TANZAM* eneo la Mafinga Mjini hasa Kinyanambo hadi Hospitali ya Mafinga. Suala hili linakumbushwa sana na wananchi kwa kuwa hata wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais lilizungumzwa na Mheshimiwa Waziri mbele ya wananchi na mbele ya Mheshimiwa Rais alieleza umma wa Wana-Mafinga kwamba kutawekwa taa za barabarani umbali wa kilometa mbili, naona mwaka wa fedha uko mwishoni na taa hizi bado hatujaanza kujenga. Ni ombi langu kwa niaba ya wananachi wa Mafinga kutekeleza ahadi hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara Iringa-Msembe; barabara hii ambayo ni kiungo muhimu katika biashara ya utalii, katika bajeti hii ya mwaka 2022/2023 kwa uelewa wa wananchi na sisi Wana-Iringa ni kwamba inaanza kujengwa mwaka huu, hata hivyo nimeona kwamba huenda ikatangazwa mwezi Juni, kwa wananchi wanashindwa kuelewa na hata mimi nilitarajia kwamba tutakuwa tumeanza kujenga au walau mkataba kuwa umeshasainiwa. Kwa hiyo, rai yangu ufafanuzi ufanyike, kwa sababu uelewa ni kwamba hata hii kutangaza mwaka huu pengine ujenzi hautaanza mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuboresha utendaji wa bandari kupitia mwekezaji; kwanza nawapongeza sana bandari kwa ubunifu, lakini zaidi kwa ushirikishwaji. Sisi Wabunge tumepata semina kuhusu nini kinakusudiwa kufanyika na kitakuwa na manufaa gani kwa nchi yetu. Yapo mashaka na maoni tofauti, tuyapokee lakini kama Taifa lazima tuamue kwenda mbele, haiwezekani tuendelee kuchekwa na nchi majirani kwamba tumekalia uchumi. Tuamue sasa, twende mbele.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa bahati nzuri nimetembea duniani nikiwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Nje, mfano mdogo nchi ndogo kwa eneo kama Singapore, bandari yao inafanya kazi kwa ufanisi mkubwa na ni chanzo cha mapato kwa nchi yao. Katika kufanya maamuzi tukishajiridhisha ni kwa manufaa ya Taifa letu, basi mengineyo tuweke pamba masikio, tufanye maamuzi sasa, tusirudi nyuma.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. MEDARD M. KALEMANI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani nyingi sana kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyotafuta fedha, kutoa fedha na kuleta maendeleo kwa Watanzania, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, tunaona jinsi pesa nyingi za ujenzi wa miradi ya miundombinu ikiwamo barabara, bandari na madaraja zinavyoendelea kumiminika katika maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, miradi ya barabara zilizokamilika na zinazoendelea kujengwa, zilizoorodheshwa katika taarifa ya Wizara ni kielelezo cha kazi kubwa inayoendelea kufanyika kutokana na juhudi za Mheshimiwa Rais. Nashukuru katika Jimbo la Chato pia pesa nyingi zaidi ya shillingi bilioni 5.7 katika kipindi cha miaka miwili iliyopita zimetolewa. Hii ni hatua ya kupongezwa sana. Naishukuru Serikali kwa niaba ya Wana-Chato kwa kutoa shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya kuanza kujenga barabara kutoka Bandari ya Nyamilembe kuelekea Katoke umbali wa km 50.01, bararara ya *SIDO - Ginnery* ya Chato na *Ginnery* hadi Sekondari ya Janet Magufuli. Ombi langu ni kuiomba Wizara kupitia *TANROADS* kukamilisha haraka taratibu za manunuzi ili ujenzi wa barabara hizi uanze haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi katika eneo hilo hasa katika sehemu ya upanuzi wa eneo la Gati la Nyamilembe wapo wananchi wanadai fidia, naiomba Serikali yetu ikamilishe fidia hiyo ili kundoa kero hiyo kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Chato wamenituma nitoe shukrani kwa Serikali hasa kwa Mheshimiwa Rais kwa kukamilisha ujenzi wa Gati la Bandari ya Nyamilembe, tunaomba bandari hii izinduliwe ikiwezekana na viongozi wa kitaifa ili wananchi wafikishe shukrani na furaha hizo moja kwa moja kwa Serikali yao. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu nzima ya Wizara na taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe kwa kinipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Makadirio na Mapato ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, hii ni miongoni mwa Wizara muhimu sana katika nchi yetu na kwa uchumi wa nchi yetu.

Pili, napenda kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoongoza nchi yetu kwa umakini mkubwa sana na kuiweka nchi yetu katika hali ya usalama, amani na utulivu.

Tatu, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa namna walivyotayarisha hotuba hii kwa ubora wa hali ya juu na hatimaye kuiwakilisha hotuba hii katika Bunge lako tukufu kwa ufasaha mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; kwanza ni kuhusu huduma za ndege.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali yetu kwa namna inavyojitahidi kutaka kurahisisha usafiri wa ndege katika nchi yetu. Huu ni ujasiri mkubwa uliochukuliwa na Serikali yetu ya kuimarisha usafiri wa ndege nchini. Lakini bado bei za ndege za ndani *(domestic flights)* ni kubwa sana kwa wananchi wetu. Wananchi wanashindwa kumudu bei hizo na kushindwa kufaidi matunda ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali ni kuangalia uwezekano wa kupunguza bei za ndege za ndani kwa manufaa ya wananchi wa nchi hii.

Pili ni kuhusu huduma za bandari, napenda kuipongeza Serikali yetu kwa namna inavyoonesha nia ya kutaka kuboresha bandari zetu kwa nia ya kutaka kuongeza uchumi wa nchi hii kupitia bandari. Bandari katika nchi zote duniani inakuwa ni moja kati ya vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali ni kwenda na azma yake ya kutafuta wawekazaji ambao wataweza kuendesha bandari zetu hasa ile ya Dar es Salaam ambayo iko kiuchumi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, kupitia njia ya maandishi naomba kuchangia bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Sekta hii ni sekta wezeshi katika ujenzi na maendeleo ya nchi yetu ikichangia takribani asilimia 26 katika kuleta fedha za kigeni. Hii ni sekta inayoongoza katika sekta zinazounda tasnia ya huduma *(service industry)*. Unapoangalia mafanikio na mchango wa utalii katika kuingiza fedha za kigeni ni vigumu kutenganisha usafiri na usafirishaji na utalii. Pamoja na umuhimu huu hii ni sekta ambayo tofauti na rasilimali zinazokwisha kama madini, sekta hii ni ya kudumu na huleta manufaa kadri inavyoboreshwa.

Mheshimiwa Spika, ninapoandika na kuchangia sekta hii nitambue mafanikio makubwa katika Taifa letu katika mwezi huu, hatua ya kufikia makubaliano kati ya Serikali na wawekezaji katika mradi wa kutengeneza gasi kimiminika *(LNG)* na matumizi ya gesi asilia katika magari yaendayo kasi jijini Dar es Salaam *(CNG)* ni jambo lenye tija kubwa kwa sekta hii na Taifa kwa ujumla. Mafanikio haya yanahitaji nguvu na ushiriki mkubwa wa Wizara ili tufikie malengo tunayotarajia.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuishukuru Wizara kwa kuboresha uwanja wa ndege wa Bukoba hasa eneo la uongozaji

ndege. Nilipongeze Bunge letu tukufu kupitia Kamati inayosimamia Wizara hii kwa kuishauri Serikali ijenge uwanja wa ndege mpya mkoani Kagera. Eneo la mkoa wa Kagera ukizingatia na nchi zinazotuzunguka *(location advantage)* kuna umuhimu na haja ya kujenga uwanja wa ndege mkubwa maeneo ya Omukajunguti au Kashaba ili kutoa huduma ya usafiri na usafirishaji kwa maeneo haya. Wananchi wa Rwanda, Uganda na DR Congo katika shughuli zao za kiuchumi na kijamii wanategemea eneo hili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto za uwanja wa Bukoba uliopo sasa, uwanja huu ni miongoni mwa viwanja saba vyenye abiria wengi nchini bila kuhesabu abiria wanaoshuka Mwanza kwa kuogopa kutua Bukoba. Tunaiomba sana, Serikali ijenge uwanja wa ndege mkubwa Kagera.

Mheshimiwa Spika, shirika la ndege la *ATCL* linaelekea kuanza biashara ya kusafirisha mizigo kwa ndege maalum za mizigo. Naomba na kushauri katika kutekeleza mpango huu ni muhimu kuanzia sasa kuwashirikisha wadau wa kuuza na kuagiza bidhaa toka nje ya nchi kwa lengo la kubaini wingi wa mizigo inayohitaji huduma ya ndege. Tuwe na uhakika sasa kabla ya ndege ya kwanza kuwasili, wazalishaji wa nchini na nchi jirani wahamasishwe kutafuta masoko ya moja kwa moja na maalum.

Mheshimiwa Spika, Serikali imewekeza sana kwa kujenga vivuko katika Ziwa Victoria upande wa Mashariki na Kusini, niombe na kushauri sasa ombi la kujenga vivuko katika Ziwa Victoria upande wa Mkoa wa Kagera litekelezwe.

Mheshimiwa Spika, napongeza mpango na uboreshaji na ujenzi wa maegesho Kisiwa cha Ikuza. Tunaomba na kushauri vivuko kwa kutoa huduma kati ya Magarini na Kyamkwikwi na visiwa vya Ikuza, Mazinga, Bumbiile na Kelebe ipangwe na kutekelezwa. Upo mpango wa siku nyingi wa kujenga na kuweka kivuko *Kabango Bay* kilometa 42 Kaskazini mwa Mji wa Bukoba. Kivuko hiki ni muhimu katika kuunganisha nchi yetu na Uganda katika dhana hii ya biashara huru katika Bara la Afrika lakini na mahusiano mema na nchi jjrani.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuishukuru Serikali na hususani Wizara kwa mipango ya kuboresha usafiri katika Visiwa vya Wilaya ya Muleba. Uwepo wa meli ya Clarias na meli/*boat* maalum ziendazo kasi utasaidia kuboresha maisha ya Visiwa vya Goziba, Kelebe, Bumbiile, Ikuza na Mazinga na bandari ndogo za Kyamkwikwi na Magarini nchi kavu. Tunashukuru kwa nia ya kupeleka *barge* Bandari ya Goziba ili kuwezesha meli tunaposubiri gati yetu kuboreshwa. Nashukuru kwa mipango na utekelezaji wa uboreshaji wa Bandari za Bukoba na *Kemondo Bay,* tunapoendelea na uboreshaji nishauri Bandari ya Bukoba iwekewe mazingira ya kuwezesha meli zaidi kuegesha hasa *Songoro Marine*. Tunaomba meli za Songoro ziwezeshwe kutoa huduma katika bandari na visiwa vya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, nipongeze na kushukuru kwa ujenzi wa barabara kiwango cha lami kutoka Muhutwe, Kamachumu, Buganguzi, Nshamba mpaka Muleba. Ujenzi umebakiza kilometa 7.4 kukamilika, tunaomba na kushukuru kazi iendelee kwa kumalizia eneo lililobaki. Tunaomba mchepuko wa kilometa tatu kuelekea Hospitali ya Ndolage ufikiriwe kwa kuendeleza kilometa moja iliyojengwa katikati ya Mji Mdogo wa Kamachumu.

Mheshimiwa Spika, napongeza mpango wa ujenzi wa barabara ya Mutukula, Bukoba mpaka Kagoma, ombi na ushauri ni kuwa maegesho ya magari wakati wa kushusha a kupakia abiria yaboreshwe. Sasa hivi barabara tajwa ina mabasi ya abiria mengi sana, tena mengi yakipita maeneo haya usiku na alfajiri, uboreshaji uzingatie eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu niombe kufungiwa taa za barabarani katika Mji Mdogo wa Kamachumu. Pamoja na eneo hili maboresho ya barabara ya Mutukula mpaka Kagoma yahusishwe kuweka taa Mji Mdogo wa Muhutwe, Kakindo, Izigo, Kagoma na Kikuku.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sikupata nafasi ya kuchangia kwa kuongea Bungeni, naomba nitoe mchango wangu kwa maandishi kwa kifupi sana.

Kwanza naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri iliyofanyika na inayoendelea kufanyika. Nilipata neema ya kutembelea miradi inayotekelezwa wakati wa ziara ya Kamati; *SGR*, Mamlaka ya Bandari Dar es Salaam, Mwendo Kasi Dar es Salaam, Bandari Kavu Kwala, Bandari ya Kalema - Katavi, Daraja la Busisi, ujenzi na ukarabati wa meli vivuko na chelezo na kadhalika. Kwa kweli Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukurani na pongezi zangu, nasikitika kusema kwamba Serikali haitekelezi ahadi za viongozi wakuu ipasavyo. Kuna ahadi nyingi za viongozi wakuu ambazo zilitolewa mbele ya wananchi wengi ambazo bado hazijatekelezwa licha ya ukweli kwamba anachokisema mkuu wa nchi ni *decree* na inapaswa itekelezwe.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa kwenye Jimbo la Arumeru Mashariki ni barabara kwa kuwa sehemu kubwa ya jimbo ni Mlima Meru ambako wako wananchi wanaoishi kwenye miteremko ya huu mlima. *Terrain* si rafiki kwa barabara za udongo na changarawe.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kusema kwamba jimbo hili lilikuwa limesahaulika kwa muda mrefu halijawahi kupewa hata mita moja ya barabara ya lami, lakini mwaka 2020 tulipata bahati ya kupewa ahadi ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kingori inayoanzia Malula Kibaoni hadi Ngarenanyuki iungane na barabara ya *Usa River* hadi Oldonyo Sambu.

Mheshimiwa Spika, ahadi hii ikitekelezwa tutakuwa na *ring road* ya kimkakati ambayo itaweka katikati vivutio vya utalii vya Hifadhi ya Taifa Arusha na msitu wa Mlima Meru, lakini pia itafupisha safari ya kutoka Moshi hadi Namanga kwa kilometa 33 na kuinua uchumi na ubora wa maisha ya wananchi wengi wa kata nane ambako imepita.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ifanye kila linalowezekana ahadi itekelezwe hasa ukizingatia kwamba tunaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ambao tunauanza mwakani kwa Serikali za Mitaa. Wabunge tunapata mzigo yanapokuja maswali ya ahadi za Rais kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya ujenzi wa barabara ya Sangis kwenda Akheri hadi Ndoombo ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliyoitoa mwaka 2012; hii imeanza kutekelezwa lakini inafanyika kwa kusuasua sana. Nashauri Serikali iongeze nguvu hapa ikiwezekana imalizike kabla ya mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya ujenzi wa barabara urefu wa kilometa tano Mjini *Usa River* aliyotoa Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Pombe Magufuli mwaka 2025 bado nayo inangojea utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbuguni kuanzia Tengeru inaunganisha Mikoa ya Arusha na Manyara, nasikitika haijaongelewa kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru upembuzi yakinifu umeanza lakini nashauri Waziri aiongelee wakati wa kuhitimisha kwa sababu ilisahaulika kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kutoa fedha nyingi sana za kujenga barabara na madaraja katika mkoa wetu. Kwa kweli naipongeza Serikali kwa ujenzi mkubwa wa madaraja likiwemo la Tanzanite, Kurasini, *TAZARA* Mfugale na *Inter Change* ya Kijazi, kwa kweli madaraja hayo yamebadilisha sura ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Aidha, napongeza kwa ujenzi wa barabara za mwendokasi Mbagala na Gongo la Mboto; naishukuru sana na kuipongeza Serikali.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu; naomba mradi wa *DMDP* uje katika Mkoa Dar es Salaam kutusaidia katika barabara za mitaa na naomba ujenzi wa barabara uende sambamba na taa za barabarani kwa kuwa barabara zetu zimekuwa na giza sana.

Kuhusu bandari ya Dar es Salaam, kwa kweli utendaji wa bandari ni wa kusuasua kwa muda mrefu na hasa eneo la *operation*, Wakurugenzi wa Bandari wamekuwa wakipata tuhuma mbalimbali kutokana na mifumo yetu kutosomana. Sasa naiomba Serikali tuangalie upande mwingine wa shilingi kufikiria kumuweka mwekezaji wa kuendesha bandari upande wa *operation*. Mwekezaji aendeshe bandari na kuboresha miundombinu, na sisi atupe faida yetu, cha msingi ni kuangalia mkataba uwe *win win* na maslahi ya wafanyakazi wetu yazingatiwe kulingana na mkataba wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Serikali bila kusahau Wakurugenzi wa Taasisi zetu zote zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ushauri wangu naomba uzingatiwe.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mungu. Pili nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa katika sekta hii.

Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na watendaji wote wa Wizara akiwemo *Engineer* Mlavi kwa ushirikiano mkubwa anaotupa katika Wilaya yetu ya Nyasa.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mkurugenzi wa *TPA* pamoja na timu yake kwa kuanza kuimarisha bandari ya *Mbamba Bay,* huo ni ukombozi mkubwa sana kwa Taifa na hususan wananchi wa Wilaya ya Nyasa.

Mheshimiwa Spika, katika suala ya uboreshaji huduma bandari ya Dar es Salaam naunga mkono, la msingi masuala ya kimkataba yawekwe vizuri kuangalia *flexibility* ya *revision in case* kuna lazima ya kufanya hivyo na pia kuzingatia masuala ya kiusalama.

Mheshimiwa Spika, nashukuru pia kwa hatua zinazoendelea katika kujenga Daraja la Mitomoni. Daraja hilo ni ukombozi mkubwa kwa wananchi wa eneo hilo na wananchi wa Nyasa na Songea, hali kadhalika jirani zetu wa Msumbiji. Kutokuwepo kwa daraja hili ni kikwazo kikubwa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba bajeti ijayo itengwe fedha ya kufanya upembuzi barabara ya Unyoni hadi Mitomoni kwa ajili ya maandalizi ya kujenga kwa kiwango cha lami. Nakumbusha utekelezaji kwa kiwango cha lami barabara ya Ruanda - Lituhi - Ndumbi na *Mbamba Bay* - Lituhi.

Mheshimiwa Spika, mwisho kutokana na Wilaya ya Nyasa kupokea maji mengi toka milima ya Livingstone hivyo kuhitaji fedha nyingi za matengenezo ya dharura. Ni vema bajeti ya matengenezo iongezwe.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema. Nampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi iliyotukuka ya kuliongoza Taifa letu. Nakupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na wasaidizi wao na timu nzima ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, nachangia maeneo matatu nikianza na ujenzi wa barabara ya Muhutwe - Kamachumu - Buganguzi -

Kishanda - Nshamba - Muleba *(Mujungi Road);* barabara hii ina urefu wa kilometa 54. Barabara hii ilianza kujengwa kidogo kidogo tangu Serikali ya Awamu ya Nne, mpaka jana unasoma bajeti yako ya mwaka wa fedha 2023/2024, barabara hii imejengwa kwa kiwango cha lami kilometa 38 tu. Kwa taarifa kilometa 3.8 ziko kwenye maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya barabara iliyobaki ni kilometa 12 tu ili barabara hii ikamilike. Barabara hii imejengwa kwa muda mrefu. Nimeangalia kwa makini bajeti yako ambayo naichangia, barabara hii imetengewa kiasi kidogo cha pesa ambazo zitajenga labda kilometa moja tu. Naomba sana, barabara hii ni muhimu sana, nakuomba uongeze bajeti angalau kilometa saba ili bajeti ya mwaka ujao tumalizie ujenzi wa barabara hii. Namuomba sana Mheshimiwa Waziri tumalizie ujenzi wa barabara hii kabla ya uchaguzi wa mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, pili ni ujenzi wa uwanja wa ndege wa Omukajunguti; uwanja wa ndege wa Bukoba sio salama kwa kuruka na kutua ndege zetu za *ATCL* na *Precision Air*. Ndege hizi zinahitaji kutua kwenye uwanja wa ndege wenye njia ya kuruka na kutua ndege urefu kilometa mbili. Uwanja wa ndege wa Bukoba una njia ya kuruka na kutua ndege wenye urefu wa kilometa 1.5. Kwa bahati mbaya uwanja huu hauwezi kupanuliwa kutokana na jiografia ya eneo letu. Kwa sababu hiyo, nakuomba ujenzi wa uwanja wa ndege wa Omukajunguti ufanyike kipindi hiki.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ya mwaka 2023/2024. Namshukuru Mungu kwa uwezo huu wa kuwasilisha mchango wangu nikiwa na afya njema.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Rais Samia kwa juhudi zake za kuhimiza kukamilisha miradi mikubwa ikiwemo *SGR,* barabara, madaraja, viwanja vya ndege, bandari na vivuko. Aidha, nawapongeza Waziri na timu yake ya watendaji kwa bidii

yao katika kufanikisha malengo ya Wizara pamoja na changamoto zinazojitokeza.

Mheshimiwa Spika, tunatumbua bahati tuliyonayo kwa nchi yetu kuwa na bandari kadha zilizomilki yetu, lakini zinakosa kuleta matunda tarajiwa na uwezo upo wa kutumika sawasawa kwa tija.

Mheshimiwa Spika, nikubaliane na wazo la ubia kwa bandari ya Dar es Salaam ina uwezekano wa kunyanyua uchumi wetu kwa kiwango kikubwa. Bandari ya Dar es Salaam katika sehemu yake ilipo ina uwezo wa kuhudumia nchi kadhaa ikiwemo DRC, Rwanda, Zambia, Malawi na Uganda.

Mheshimiwa Spika, kwa bandari ya Dar es Salaam kinachotakiwa ni mabadiliko ya uendeshaji na usimamizi mzuri, ni muhimu kwa kuongeza tija.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kupigiwa mfano kwenye ujenzi barabara mimi mwenyewe ni shahidi nimeona. Nilibahatika kusafiri kwa barabara kwenda Kakonko - Kayla barabara haijajengwa na juzi nimetoka Nyakanazi mpaka Kakonko lami safi sana, barabara imenyoooka kama mgongo wa ngisi, kusema kweli wanastahili pongezi sana.

Mheshimiwa Spika, mpango mzuri wa barabara ya *express way* Kibaha mpaka Morogoro ni ukombozi mkubwa na kichochea muhimu sana kwa uchumi na maendeleo, inakwenda kuondoa udhia mkubwa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na ujenzi huu wa *express way* ya Kibaha - Morogoro sijui kwa nini Wizara bado haikamilishi kujenga Daraja la Morogoro kwenye eneo la Jangwani Dar es Salaam ambao ndio kiungo muhimu sana, eneo hili ni shida sana wakati wa mvua. Ni muda mrefu tunaambiwa kwamba ujenzi utaaanza, lakini ujenzi huo hauanzi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara wa Nyamuswa – Bunda - Kisorya itambulike kama Nyamuswa - Bunda - Kisorya - Nansio kama ilivyokuwa

inatambulika toka awali (sehemu ya Kisorya - Nansio ikiwa *(Lot No.3)*. Kutoitambua kwa jina hilo kunahamisha na kupotosha jina la mradi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Lugezi - Bukongo - Masonga (sehemu ya Bulamba - Murutunguru - Masonga kilometa 32) ijengwe kwa kiwango cha lami kuepusha gharama kubwa zinazotumika kwa matengenezo ya mara kwa mara kutokana na aina ya udongo uliopo maeneo yale.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, naomba tu bandari ya Manda pale Ludewa ijengwe. Aidha, barabara kuanzia Mawengi hadi Manda na Mkiu – Liganga - Madaba zijengwe kwa kiwango cha lami.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, maboresho yanayohitajika katika mfumo wetu wa udhibiti wa Sekta ya Uchukuzi; kama ilivyo katika nchi zote duniani, mfumo wetu wa udhibiti wa nchi, kiuchumi, kiusalama na kiulinzi umegawanyika gawanyika vipande vipande vilivyo chini ya utitiri wa mamlaka za udhibiti zilizo chini ya Wizara mbalimbali kuendana na eneo lake la udhibiti zenye majukumu yanayoingiliana, kutegemeana, na wakati mwingine hata kusigana/kukinzana na kutengeneza ombwe la udhibiti katika maeneo fulani fulani. Hali hii imepelekea kuwepo kwa changamoto ya namna sahihi, rahisi na fanisi ya kuzipanga mamlaka hizo ili kuziwezesha sio tu kuifanya kazi ya udhibiti iliyokasimiwa kwanza, bali pia kuyafikia malengo yaliyokusudiwa kwa ufanisi uliokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, sekta ya uchukuzi wa abiria na mizigo ni miongoni mwa sekta za uchumi wa nchi yetu zinazoathiriwa sana na changamoto hiyo. Kwa vile sekta hii ni sekta mwezeshaji wa sekta zingine za uchumi wa nchi athari zinazoikabili haziishii kudumaza mafanikio katika sekta hii pekee, bali kupelekea/kuchangia kudumaza mafanikio katika sekta zingine za uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa maeneo yanayokabiliwa na kuathirika sana na changamoto ya ufanisi katika udhibiti

ni udhibiti wa usafirishaji mizigo hatari; usafirishaji mizigo hatari unasimamiwa na mamlaka lukuki kufuatana na ama aina ya bidhaa au aina ya hatari iliyomo katika bidhaa husika. Mfano rahisi wa kuielezea hali hii ni usafirishaji wa petroli kwa njia ya barabarani unaoangukia katika mamlaka za udhibiti zisizopungua nne.

Mheshimiwa Spika, kwa vile petroli ni nishati, na usafirishaji petroli ni sehemu ya mchakato wa usambazaji petroli, *EWURA* ina jukumu la kisheria la udhiniti wa usafirishaji petroli. Aidha, kwa vile petroli ni kemikali hatari (tena sana), *GCLA* ina jukumu la kisheria la udhibiti wa usafirishaji petroli. Kwa vile petroli huagizwa kutoka nje ya nchi kupitia usafiri wa majini, *TASAC* ina jukumu la kisheria la udhibiti wa usafirishaji petroli mpaka inaposhushwa bandarini; na kwa vile petroli husambazwa nchini kwa kupitia usafiri wa barabarani na relini, *LATRA* ina jukumu la kisheria la udhibiti wa usafirishaji petroli mara inapoondolewa bandarini.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine wa kuielezea hali hii ni usafirishaji wa vifurushi na vipeto kwa njia ya barabarani unaoangukia katika mamlaka za udhibiti zisizopungua nne:-

a) Kwa mujibu wa Sheria iliyoianzisha *TCRA*, udhibiti wa usafirishaji vifurushi na vipeto ni jukumu la *TCRA*.

b) Kwa vifurushi na vipeto vilivyofungasha kemikali hatari, *GCLA* ina jukumu la kisheria la udhibiti wa usafirishaji vifurushi na vipeto hivyo.

c) Kwa vifurushi na vipeto vilivyofungasha vimelea hatari, Wizara ya Afya ina jukumu la kisheria la udhibiti wa usafirishaji vifurushi na vipeto hivyo.

d) Kwa vile vifurushi na vipeto hivyo vinasasafirishwa kwa njia ya barabarani (mara kwa mara kwa njia ya mabasi), *LATRA* ina jukumu la kisheria la udhibiti wa usafirishaji vifurushi na vipeto hivyo.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa mamlaka zaidi ya moja, sio tu unaleta mkanganiko unaozorotesha shughuli ya udhibiti, bali pia unachangia sana katika kuzalisha urasimu na gharama kwa wasafirishaji zisizo za lazima. Hivyo basi, ningependa kupendekeza maboresho yafuatayo katika mfumo wetu wa udhibiti wa usafirishaji mizigo hatari:-

Kwanza tutunge sheria moja ya udhibiti wa usafirishaji mizigo hatari itakayosimamiwa na mamlaka moja ya udhibiti itakayozijumuisha kwa pamoja sheria-ndogo, kanuni, na taratibu za udhibiti za hizo mamlaka mbalimbali za udhibiti. Tunaweza tukawaiga wenzetu Wamarekani ambao pamoja na kuwa na utitiri wa mamlaka za udhibiti kama tulizonazo sisi, jukumu la udhibiti wa usafirishaji mizigo hatari unaangukia katika idara ya usafirishaji *(department of transport),* na unasimamiwa na sheria moja; *49CFR (49th Code of Federal Regulations)*.

Pili, Kitengo cha Udhibiti wa Usafirishaji Vifurushi na Vipeto kwa njia ya barabarani kilichopo *TCRA* kwa sasa kihamishiwe *LATRA* kwani kwa muktadha wa lugha ya usafirishaji/usambazaji, vifurushi' na vipeto ni majina-rasmi tu ya mizigo midogo. Taratibu zake za udhibiti hazitofautiani sana na zile za mizigo mikubwa.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa fedha nyingi katika ujenzi wa barabara Ushetu hasa barabara ya Uyogo - Ulowa kilometa 30 ambayo ilikuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Ushetu na wakulima wa tumbaku sasa imetengenezwa na wananchi wamenituma kuja kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, ombi la wananchi wa Ushetu ni ujenzi wa lami kwa barabara yao ya kilometa 54 kutoka Uyogo Nyandekwa hadi Nyandekwa hadi Kahama itengewe fedha ili ujenzi uanze, hii ni ahadi ya viongozi wetu wakuu wa nchi pia hata katika Ilani ya CCM imewekwa pia tunaomba kutengewa fedha kwa barabara ya Mwambomba inayopita Idahina - Nyakende - Ulewe - Ubagwe - Ulowa kilometa 224 na barabara ya Bugomba A - Butibu hadi Nyamilangano kilometa 47. Barabara hizi ni kiungo muhimu sana

kwa wananchi wa Ushetu sasa zianze kutengenezwa na zitengewe fedha. Hali ya barabara hizo ni mbaya sana, kuna baadhi ya maeneo hazipitiki kabisa. Naomba Mheshimiwa Waziri barabara hizi zitengewe fedha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMMED MAULID ALI:** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi kutoa mchango wangu kwa maandishi kuhusu bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mungu kwa kunijaalia nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, pili naomba nimshukuru Rais wetu kwa kupeleka fedha nyingi kwenye Wizara hii kwa lengo la kuhakikisha miradi yote iliyotengwa inakamilika.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita zaidi kwenye eneo la mamlaka ya bandari kuhusu uwekezaji unaokwenda kufanywa na Serikali kwenye gati na 8, 9 na 10.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatoa hofu Wabunge wenzangu na wananchi wote kwamba kinachokwenda kufanyika pale ni ubia kati ya Serikali yetu na wawekezaji hawa kwa lengo la kuongeza ufanisi. Kazi tutafanya sote na mapato ni yetu sote. Sambamba na hilo ni vizuri tukaelewa kwamba *management* pamoja na *operations* za bandari yetu zitaendelea kubaki kama zilivyo hasa kwa vile Serikali imeboresha gati na 5, 6 na 7 kwa ajili ya *general cargo* na makontena.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia mchango wangu napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mbarawa na timu yake yote kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii kwenye maeneo yote yakiwemo ya barabara, reli na anga.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Spika, nina maeneo mawili ya kuchangia katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Kwanza, Serikali imalize mgogoro kati ya wananchi wa Mtaa wa Baruti na *TANROADS*.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu kumekuwepo na mgogoro kati ya wananchi wa Mtaa wa Baruti na *TANROADS* kufuatia uamuzi wa *TANROADS* kuwataka wananchi wapishe eneo la makazi yao kwa ajili ya upanuzi wa barabara husika. Madai ya muda mrefu ya *TANROADS* ni kuwa wengi wa wananchi hawa walishalipwa fidia. Hata hivyo wananchi wanapinga madai haya. Historia fupi ya mgogoro huu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miaka ya 1990 barabara hii ilikuwa na *lanes* mbili, moja ikiingia na moja ikitoka. Baadaye Serikali iliona haja ya kupanua barabara hii. Hivyo wananchi waliofuatwa na barabara walilipwa fidia na kupewa maeneo ya kujenga katika maeneo ya Mbweni na Mabwepande. Hii ndio asili ya Mtaa wa Ubungo kule Mbweni na Mtaa wa Manzese kule Mabwepande.

Mheshimiwa Spika, mgogoro uliopo kwa sasa ni pale Serikali ilipoamua kupanua tena barabara kuwa njia nne kwa kila upande. Katika hatua hii ndipo ilipowakuta wananchi. Hawa ni wananchi ambao wamekutwa na barabara inayopanuliwa na baadhi yao wameisha katika maeneo husika kwa zaidi ya miongo mitatu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 (hususani kifungu cha 3b) ipo wazi kwamba; katika hatua zozote za kuendeleza ardhi ni muhimu "kuhakikisha kuwa haki za wakazi waliokaa muda mrefu zinalindwa…."

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali imalize mgogoro huu ili wananchi waishi kwa amani na kufanya shughuli za maendeleo na wakazi wa maeneo husika wapewe haki zao kwa kuzingatia sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali itekeleze ahadi ya muda mrefu ya kujenga barabara ya Kimara – Mavurunza – Kinyerezi.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati wa mjadala wa Wizara hii mimi na Mbunge mwenzangu wa Jimbo la Segerea, Mheshimiwa Bonnah Kamoli, tulizungumza kwa sauti kubwa sana kuhusu umuhimu wa barabara ya Kimara -Mavurunza - Kinyerezi yenye urefu wa kilometa saba na ambayo ipo chini ya *TANROADS,* niliamini Waziri alituelewa, na tangu mwaka jana na mwaka huu tumezunguka ofisi zote husika, zikiwemo kwa *CEO* wa *TANROADS* na Katibu Mkuu wa Ujenzi, *Engineer* Aisha Salim. Aidha, tumezungumza na Waziri na Naibu Mawaziri mara nyingi. Wote hawa walituahidi kwamba mwaka huu barabara hii ingeingia katika bajeti na ingeanza kujengwa. Na kweli tumeona barabara katika randama. Lakini sasa ndio imetengewe shilingi bilioni moja kwa kilometa tatu?

Mheshimiwa Spika, tangu lini bilioni moja ikajenga kilometa tatu za lami? Halafu Waziri amezungumzia kufanya *feasibility study*. Hili ni jambo ambalo tuliambiwa lilishafanyika tayari, hatuwezi kueleweka kwa wananchi. Naomba Waziri atakapohitimisha hoja yake atueleze ni lini barabara hii itaanza kujengwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Nitasubiri majibu ya Mheshimiwa Waziri kabla sijaamua kuunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba atafuatiwa na Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete na Mheshimiwa Godfrey Msongwe Kasekenya ajiandae.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie mambo machache.

Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja iliyowekwa mezani kwetu na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi pamoja na timu yake, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya katika sekta hii ya Ujenzi. Sekta ya Ujenzi ni moja ya sekta ambayo ina miradi mikubwa, miradi yote

inaendelea kutekelezwa na tumeshapiga hatua kubwa sana katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu naomba nichangie mambo matatu. Jambo la kwanza ambalo ningependa kulichangia ujenzi kwenye sekta hii ya ujenzi, sekta zote ambazo zimetajwa na Mheshimiwa Waziri una bajeti takribani za aina tatu, nne hivi. Bajeti mojawapo ni bajeti hii ambayo tunapitisha, bajeti nyingine ni zile ambazo ziko kwenye mifuko mahsusi, bajeti nyingine ni zile barabara ambazo zinapata udhamini kutoka kwa wabia wetu wa maendeleo, bajeti nyingine ni hii ambayo tumeiongelea ya *EPC+F*.

Mheshimiwa Spika, niliona Waheshimiwa Wabunge baadhi katika kuchangia akiwepo Mheshimiwa Halima jana wakati anachangia alianza kupiga hesabu kana kwamba barabara zote tunazoenda kuzijenga zinajengwa kwa bajeti hii ambayo inapitishwa kwa maana ya kipengele kimoja kimoja kwa maana ya *cash budget* ambayo inapitishwa makusanyo ya kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, nikaona nipate fursa ya kufafanua huu utaratibu tunaosema wa *EPC + F* maana yake nini na kwa nini tumebadili utaratibu tukasaini barabara yote kwa urefu wake.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara hizo hazitajengwa ndani ya mwezi mmoja na kwa kufatana na urefu zingine hata hazitajengwa ndani yam waka mmoja. Utaratibu wa *EPC+F* kwa jinsi ambavyo unatumika ni kwamba Wizara ya Ujenzi ikishafanya utaratibu wa kumpata mkandarasi na mkandarasi akaja na *finance award* Wizara ya Fedha inafanya *terms* zile, ina-*negotiate* zile *terms* inafanya majadiliano ya vile vigezo vya kupata mkopo wa kifedha ambavyo vinazingatia mambo ya riba pamoja na masuala mengine ya gharama za ukopaji, baada ya hapo kinachofata ni mkandarasi anaanza kulipwa kufatana na utekelezaji wa mradi na fedha zinatoka kwa yule ambaye ni *financier* wa mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo tulibadili utaratibu huu ili tuweze kupunguza utaratibu huu wa *certificate* kujazana. Maana

yake natolea mfano, kama barabara ya Liwale – Nachingwe - Masasi labda *financier* wake ni Benki ya *CRBD* ama *City Bank*, ama itaje benki yoyote natolea mfano. Maana yake tukishakubaliana *terms* hiyo fedha itakuwa inatoka kadri anavyotekeleza mradi. Akishatekeleza hatua fulani Wizara inakagua inakubaliana kwamba hii imeshatekelezwa Wizara inatuarifu kwamba huyu hapa ameshatekeleza sisi tunawapa ruhusa benki wanalipa hiyo fedha ambayo imepitishwa kwa ajili ya mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo kwa mazingira hayo hatutarajii hiyo ya kusema kwamba zitatumika bilioni mbili, zitatumika kilometa 200, tutalipa kufuatana na kasi ya utekelezaji tu wa Mkandarasi anavyojenga hiyo ndiyo dhana ya *EPC+F*.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ziliongelewa barabara ambazo Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanafuatilia, barabara zipo ambazo tunaendelea na majadiliano tuko hatua za mwisho. Timu yangu iko *Egypt* kwenye *annual meeting* ya *African Development Bank* na barabara hizo tuna-*conclude* tunaamini kwamba zitafanyiwa marekebisho ziingie kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ili ziweze kutekelezwa. Tuna barabara ya Magu – Isandula - Bukwimba kwenda Hungumalwa, tuna barabara ya Kahama kwenda Geita ambayo tunaweka nyongeza kwenye ile fedha ambayo ilishatolewa na mgodi.

Mheshimiwa Spika, tuna barabara ya Iguguno -Nduguti kwenda Sibiti kwa jirani yangu Mheshimiwa Francis Isack naona ameamua kuwa jirani mpaka hapa. Tunayo barabara ya Singida - Ilongero - Haydom ambayo Mheshimiwa Mbunge aliongea kwa nguvu kubwa sana na tuna barabara ya Chunya - Makongorosi kwenda Itigi. Hizi ni barabara ambazo zilishafanyiwa mazungumzo kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika na sasa hivi timu iko kule *Egypt* kukamilisha namna ya utekelezaji wa miradi mingi ikiwemo na hiyo ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho yamekuwa yakitokea pia maswali kuhusu *certificate* zinazoiva. Kwa utaratibu pale ambapo kasi ya utekelezaji wa mradi inakuwa kubwa sana kama hivi ilivyo

sasa hivi, kasi ya utekelezaji wa miradi mingi ni kubwa, inatokea *certificate* zinakuja kwenye tarehe ambapo kuna *commitment* zile ambazo ni *first charge,* kwa hiyo ni kweli ikiangukia kwenye *commitment* ambayo ni *first charge* kunakuwepo na utaratibu wa kupitisha kwanza malipo yale yakiwemo ya mishahara ya watumishi wa umma, malipo ya Deni la Taifa, lakini mara zote tunaongeaga na Wizara kuangalia zile *deadline* ambazo zinajitokeza.

Mheshimiwa Spika, kuna mazingira ambapo mradi unafadhiliwa kwa mkopo ambao unaenda moja kwa moja kwenye utekelezaji wa mradi, mradi ule kama ni wa mkopo tutakuwa tunatekeleza mradi lakini mradi ule lazima utakuwa na riba kwa sababu mradi wenyewe ulikuwa unatekelezwa una mkopo kwa hiyo tunapotekeleza mradi panakuwepo pia na riba kwenye mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge barabara hizi zitajengwa na zile ambazo zilikuwa zinaendelea kujengwa zitaendelea kujengwa na hata hivi sasa Mheshimiwa Rais pamoja na Wasaidizi wake anaendelea kututuma baadhi ya maeneo ili kuweza kuhakikisha tunatafuta fedha nyingi zaidi ili kuweza kutekeleza miradi hiyo ya maendeleo. Tuna majadiliano tumeshafanya hatua ziko za kimikataba na wenzetu wa *European Investment Bank,* ambayo inahusisha viwanja vya ndege pamoja na baadhi ya barabara na yenyewe ikikamilika Waheshimiwa Wabunge mtaarifiwa miradi ambayo inapatikana katika Majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatekeleza mirdi hii ya barabara kwa sababu ni moja ya nguzo muhimu ambazo zinafungua uchumi wetu na wananchi waendelee kuiamini Serikali yao, waendelee kumwamini Mheshimiwa Rais, waendelee kuwaamini Waheshimiwa Wabunge ambao wao wenyewe wameshuhudia jinsi wanavyoisimamia Serikali na jinsi ambavyo wanasimama kidete kwa ajili ya kuomba barabara hizo ili ziweze kupitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona kengele ya pili imeni-*alert* basi naunga mkono hoja na nawapogeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasengenya Msongwe na mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, nami ninakushukuru sana kwa kunipa wasaa huu katika kuchangia hoja iliyo mbele yetu, kwanza nianze kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mungu wa Mbingu na Dunia aliyetufanya leo tujadili hoja hii muhimu ndani ya Bunge lako Tukufu. Shukrani zangu za kipekee ziende kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ameendelea kuniamini kuwa Msaidizi wake katika nafasi hii ya Naibu Waziri sekta ya Uchukuzi kwa kipindi kingine tena. Shukrani zingine ziende kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, zaidi Waziri wetu Profesa Mbarawa ambaye amekuwa Mwalimu mwema, ametufundisha na anatusimamia vema sisi Wasaidizi wake katika nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, zaidi pia Waheshimiwa Wabunge niwapongeze wote kwa namna ambavyo mmechangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara yetu ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu pamoja na wote ambao wengine wamechangia kwa njia ya maandishi lakini wengi mmeongea. Pia familia yangu mama, watoto pamoja na familia kwa ujumla na wananchi wangu wa Jimbo la Busokelo ambao wameniamini kwa kipindi hiki cha pili awamu ya pili kama Mbunge wao na Mwakilishi wa Jimbo la Busokelo.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze katika hoja za Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge naungana nanyi kwa michango yenu yote ambao wamechangia katika Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi. Nakumbuka Bunge kama hili la mwaka jana na mwaka huu ni tofauti sana, kwa kweli

tunawashukuru sana na nitaanza kujielekeza katika ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR*.

Mheshimiwa Spika, tunampongeza Mheshimiwa Rais tangu amepata nafasi ya kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu amesimamia vyema sana miradi yetu hii ya *SGR*. Wakati anaingia madarakani katika *lot* ya kwanza ilikuwa asilimia 83.55, hivi sasa ni asilimia zaidi ya 98.1. *Lot* Namba Mbili kwa maana ya kutoka Morogoro hadi Makutupora ilikuwa asilimia 57.57 sasa ni zaidi ya asilimia 93.4. Kwa kweli kazi imefanyika na kilometa zilizokuwepo zilikuwa ni 722 na sasa ni zaidi ya kilometa 1280 ambazo Mheshimiwa Rais katika awamu yake amesaini na thamani ya miradi yenye takribani zaidi ya trilioni 23.3 katika reli hii ya *SGR*. Kwa kweli tuna kila sababu ya kumshukuru na kumpongeza na vipande vinne vimesainiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa ufafanuzi kulikuwa kuna hoja za ni lini hasa *SGR* itaanza kufanyakazi. Reli hii ya kisasa kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro yenye kilometa 300, mara nyingi tumekuwa tukijibu swali hapa Bungeni, lakini nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba mabehewa yamekwishaingia baadhi lakini mengine mabehewa ya ghorofa kutoka Ujerumani yanaingia nchini ifikapo tarehe Mbili Juni na tunategemea kupata vichwa vya treni mwezi wa Julai. Kwa hiyo, mara tu baada ya vichwa vya treni kufika tunategemea huduma zitaanza kutolewa.

Mheshimiwa Spika, kipande hiki cha Dar es Salaam – Morogoro chenye kilometa 300 tunategemea kukamilika kwa kadri mkataba wetu ulivyo ni mwezi Septemba 2023. Kipande cha Morogoro - Makutupora tunategemea kukamilika Januari 2024 kwa sasa ni asilimia 93.83 ya mradi yenye kilometa 422.

Mheshimiwa Spika, kipande cha Makutupora - Tabora kinategemea kikamilike mwezi Desemba 2026 kwa sasa ina asilimia Saba yenye kilometa 368. Kipande cha Tabora- Isaka chenye kilometa 165 kwa sasa iko asilimia 2.39. kipande cha Isaka – Mwanza asilimia 31. 07 yenye kilometa 341. Kipande cha Tabora

- Kigoma ambapo hivi sasa Mkandarasi yuko *site* na yupo kujenga *camp.*

Mheshimiwa Spika, kazi hii ya *SGR* imefanywa na wazawa wa kitanzania, Ma-*Engineer* wa Kitanzania ndiyo wame-*design*. Kupitia wataalam wetu na niwapongeze sana viongozi wote nikianza na Mkurugenzi Mtendaji wa *TRC* pamoja na Mainjinia wote walioshiriki katika *design and building* ya mradi huu ni mradi mkubwa kimkakati kwa hiyo tunategemea hata wenzetu wa ile reli ya kutoka Uvinza - Musongati mpaka Gitega yenye kilometa 317 hivi sasa mazungumzo yanaendelea Benki ya African Development imeonesha nia ya kufadhili mradi huu. Kwa hiyo, itakuwa kuna *connection* sasa kati ya reli na wa kwenda Kigoma pamoja na hii ambayo inaenda mpaka Burundi ambako kuna tani zaidi ya milioni 150 za *nickel* na ambazo tunategemea zisafirishwe kupitia *SGR* yetu. Takribani kwa mwaka tunakusudia, kwamba reli hii *minimum* itaweza kubeba tani milioni 17 kwa mwaka lakini *maximum* zaidi ya tani milioni 25. Kwa hiyo, niwapongeze wote wanaoshiriki katika ujenzi huu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka nizungumzie zaidi ni suala hili la Reli ya Kusini. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia hapa Reli ya Kusini kwamba ni mkombozi na kweli nasi Wizara tumeliona hili. Reli ya Kusini kutoka Mbamba *bay* mpaka Mtwara. Tunatambua kwamba mizigo ama makaa ya mawe yanayosafirishwa na mizigo kutoka makaa ya mawe mpaka bandarini yanaharibu sana barabara zetu. Kwa maana hiyo Serikali imefanya nini?

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, hivi sasa tunatafuta fedha kwa njia ya ubia ili reli hii ianze pia kufanya kazi kama ambavyo reli ya kati tunayoijenga.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa kuna hoja za ni lini hasa wakati mwingine behewa zile zilizokuja baadhi ya Wabunge walikuwa wanasema siyo yenyewe. Sasa nataka niwahakikishie kwamba kuna *set* za treni za kisasa *EMU* maana yake *Electrical*

*Multiple Unit* kwa lugha nyingine tunasema treni zilizochongoka vichwa vyake navyo vitawasili hapa nchini ifikapo Machi, 2023.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie Watanzania wenzangu kwamba reli hii inakwenda vizuri na tuko vizuri kwamba itakamilika kwa wakati kama ambavyo nimeeleza.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni reli ya *TAZARA*. *TAZARA* ni muunganiko kati ya Tanzania na Zambia. Tarehe 14 Machi Waheshimiwa Mawaziri wetu kupitia Baraza la Mawaziri walifanya kikao. Changamoto kubwa reli hii ilikuwa ni suala la sheria iliyopo na wenzetu waliomba tuwape nafasi kwa sababu ni Serikali mpya, kwa hiyo wana-*review* sheria zote za nchi yao ikiwemo na hii ya *TAZARA*. Hatukuishia hapo tu baada ya kuona wenzetu wana-*review* hiyo sheria na sisi tayari tulishaanza maandalizi na tulisha-*review* lakini hatuwezi kufanya maamuzi lazima tuwashirikishe kama ambavyo mkataba wetu ulivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nini ambacho kipo sasa hivi? Ni kwamba reli ya *TAZARA* tumeunda timu tatu, timu ya Mawaziri wa Tanzania na Zambia, timu ya Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji Wakuu. Timu hizi kazi yao kubwa ni kuratibu zoezi hili la *transition period* kwa sababu tayari kuna wawekezaji ambao wameonesha nia kuishirikisha sekta binafsi ikiwemo wenzetu wa China kwamba wanaweza kuwekeza katika reli hii ya *TAZARA*.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka nizungumzie zaidi ni suala zima la meli za Ziwa Tanganyika. Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa yote hususan Mikoa ya Kigoma, Rukwa pamoja na Katavi na asubuhi hapa nimejibu swali kuhusiana na suala la Meli za Ziwa Tanganyika. Tumepokea ushauri wenu kwamba, badala ya kuwa na meli moja kubwa ambayo inabeba watu 600 na tani 400 tunategemea tufanye vile ambavyo mmeshauri. Ina-*make sense* kwamba tukiwa na meli mbili ambazo zinaweza zikawa zinapishana na kwa kuwa bado tuko katika kipindi cha majadiliano, ushauri wenu umepokelewa na Serikali tutaufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kuna meli zingine ambazo tunaendelea kuzikarabati, kwa mfano meli ya MV Liemba pamoja na MV Mwongozo. Mv Liemba tunasaini makataba mwezi ujao wa Sita na MV Mwongozo tayari Mkandarasi Mshauri ameshapatikana ambaye ni *TMA*, kwa hiyo nao wanaanza kazi rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa sana hapa ni suala la viwanja vya ndege nchini. Baadhi ya Wabunge wamechangia suala la kwamba ndege zetu nchini ikifika saa kumi na mbili wakati huo huo zinakwenda kulala na binadamu tunakwenda kulala. Sasa nini kifanyike? Ni kuweka taa katika viwanja vyetu vyote nchini ili ndege zifanye kazi masaa 24.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia jambo hilo katika bajeti ijayo 2022/2023 viwanja vifuatavyo vinakwenda kufungiwa taa. Kiwanja cha Arusha, Iringa, Msalato, Kigoma, Sumbawanga, Shinyanga, Lake Manyara, Tanga, Lindi. Kwa sababu kwa sasa, viwanja ambavyo vina taa ni vichache sana, kiwanja cha *JNIA,* kiwanja cha *KIA*, kiwanja cha Zanzibar, Mwanza, Tabora, Songwe, Songea na Mtwara. Kwa hiyo, maombi yenu na namna ambavyo mmechangia bajeti hii mjue kwamba, katika mipango yetu na kwa kuwa baadhi ya viwanja tayari tumeshasaini ni miongoni mwa maeneo ambayo tunakwenda kuweka taa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna changamoto ya kiwanja cha Bukoba. Kiwanja cha Bukoba tumekipangia fedha kwa ajili ya kujenga *control tower* kwa maana ya kuongozea ndege pamoja na mifumo ya kuongozea ndege inayoitwa *Instrument Landing System* na hii mifumo itafungwa maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, tuwaombe Waheshimiwa Wabunge watupitishie bajeti yetu ili haya yote ambayo ninayasema hapa yaweze kutekelezeka. Kulikuwa pia kuna jambo la miradi ya kimkakati ambayo Mheshimiwa Waziri wangu atakwenda kuizungumzia. Kwa hiyo, katika haya kulikuwa kuna jambo pia la umiliki wa ndege ambayo pia Mheshimiwa Waziri wangu ataenda kuzungumzia hususan kati ya *ATCL* pamoja na *TGFA*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikushukuru sana kwa muda huu, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa namna ya kipekee ambavyo wameweza kuchangia bajeti yetu na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasengenya Msongwe na mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba nami nianze kuunga mkono hoja hii. Nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana katika Bunge lako Tukufu ili kuhitimisha hoja ya Mheshimiwa Waziri ambayo aliiwasilisha jana. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kwa nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa kwa jinsi ambavyo anaiongoza Wizara, nasi wengine kwa kweli tunajivunia kufanya kazi chini yake na kupata uzoefu ambao mwenzetu kwa kweli amebobea katika Wizara hii. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuishukuru familia yangu ambao uwepo wao ndiyo unanifanya niwe na utulivu. Pia nawashukuru wananchi wote wa Jimbo la Ileje ambao wametulia na wanaamini nawawakilisha vyema. Nami nasema kwa kweli ninawakilisha vyema na wananipa ushirikiano mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso; Makamu Mwenyekiti, Mama yangu Mheshimiwa Anne Kilango kwa jinsi ambavyo walichambua bajeti hii ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wabunge wote wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa michango yao. Baadhi ya hoja naamini zitatolewa ufafanuzi na Mheshimiwa Waziri, lakini mimi nitatoa ufafanuzi wa baadhi ya hizo hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amejitanabahisha kama Rais ambaye amedhamiria kwa dhati kuifungua Tanzania. Anaifunguaje Tanzania hii? Kuna vipaumbele kadhaa ambavyo Mheshimiwa Rais anavifuata. Kwanza ni kuteleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi inaelekeza tufanye nini? Kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa kwa lami, kuunganisha nchi na nchi, bandari zetu, barabara za kimkakati, kupunguza misongamano katika majiji na miji na pia kupeleka barabara za lami za ulinzi katika Tanzania. Kinachofuata baada ya kukamilisha huo mkakati, itakuwa ni kuunganisha wilaya zote na makao makuu ya mikoa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kitu ambacho kinafanyika na Wizara, kwanza nikutengeneza barabara ya mzunguko wa nchi nzima kuanzia Mtwara, Songea, Nyasa, Kyela, Ileje, Tunduma, Sumbawanga, Mpanda, Uvinza na Kigoma. Ukitoka Kigoma unakwenda Manyovu, unakwenda Kasulu ama unakwenda Nyakanazi unakwenda mpaka Rusumo – Bunazi - Omurushaka – Murongo; unarudi Omugakorongo unakwenda Kyaka, Bukoba; unarudi Lusaunga, unaenda Geita - Busisi kwenye daraja letu kubwa unavuka unaenda Kigongo - Mwanza – Musoma; Musoma - Nata unaingia kwenye Mbuga, unakwenda Arusha; Arusha unazunguka Mlima Kilimanjaro kwa lami, unakuja Himo unaweza ukaamua kwenda Same, ukaenda kwa Mheshimiwa Mama Kilango sasa ama Korogwe, unaenda Tanga; Tanga – Pangani – Makurunge – Bagamoyo - Dar es Salaam – Mkuranga - Lindi, uko Mtwara tayari kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hivyo vipande, kipande ambacho hakina mkandarasi sasa hivi, lakini viko kwenye hatua katika hizo nilizozitaja ni kutoka Kyela kwenda Ileje, lakini *soon* tutatangaza, alichosema kuanzia Mpanda kwenda Mishamo, mkandarasi yupo

na tunategemea kupata fedha kutoka Mishamo kwenda Uvinza hadi Kanyani. Kasulo kwenda Bugene tayari tuna mkandarasi yuko pale, kwa kaka yangu Bilakwate *soon* Mheshimiwa anakwenda kuandika mkataba. Ukitoka Murongo kuja kwa Omugakorongo tayari tuko kwenye hatua za manunuzi. Mheshimiwa Rais ameamua kuifungua nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema nitatoa mfano mmoja ni namna gani Mheshimiwa Rais anakwenda kupunguza misongamano katika miji na hasa majiji. Nitaongelea Jiji la Mbeya ambalo waliopita kwa kweli ni mtihani kwa sasa. Mheshimiwa Rais kwanza alitoa kilometa 29. Ulikwenda ukasema barabara inaning'inia, inaishia Ifisi, kwa nini isifike *airport?* Mheshimiwa Rais anaongeza kilomita nne, ziko kwenye manunuzi. Pia ameirudisha kutoka Uyole kuja Mlima Nyoka, badala ya 29 sasa ni 37. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Mji wa Mbeya ni mfinyu, wananchi wa Mbeya waelewe kwamba ile barabara ambayo inapitika sasa itakuwa ndiyo *diversion*. Kwa hiyo, kulia zinajengwa barabara mbili na hiyo barabara ya sasa baadaye ndiyo itatumika kama barabara ya mwendokasi kwa Miji wa Mbeya. Barabara yote sehemu kubwa itawekwa taa pamoja na vivuko na kwa watembea kwa miguu. Huyu ndio Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anavyotaka kuipanga miji yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitaki kuongelea Dodoma, wanaotembea wanaona kinachofanyika. Barabara kwa Dodoma tuna mzunguko wa nchi ambao tunajengwa, tuna mzunguko wa kati, tuna mzunguko wa ndani. Huo ndiyo utakuwa Mji wa Dodoma, lakini kwa kaka yangu hapa tutajenga *Songea Bypass.* Kwa *African Development* kwa fedha ya *World Bank. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka tu niseme baadhi ya mambo ambayo yanafanyika. Hapa katikati, barabara za *EPC* ambazo zinatembea hapa katikati kuanzia Songea kwenda kwa kaka yangu Mgungusi pale Malinyi mpaka Ifakara tunakuja mpaka Mikumi, mpango sasa ni kujenga barabara ya kutoka Mikumi kuja Kilosa kwa kaka yangu Mheshimiwa Profesa Palamagamba ili mtu

akitoka Songea anakuja Dodoma anatoka Mikumi anakuja Kilosa anakuja Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutoka Kongwa – Kibaya - Orkesumet kwa kaka yangu Mheshimiwa Ole-Sendeka mpaka Arusha, lakini tunaanzia Kiberashi tunakuja Kibaya - Chemba – Kwamtoro – Singida, barabara ya Tanga ameishaifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unavyoona magogo yote haya yanatoka Mgololo, *EPC + F* inaanzia Mafinga kuchukua ambako mpaka sasa hivi ni barabara ya changarawe kuijenga kwa kiwango cha lami kwa kutumia mtindo huu wa *EPC + F. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kaka yangu Mheshimiwa Kuchauka alisimama, Mheshimiwa Ungele alisimama, kaka yangu wa Nachingwea alisimama. Barabara kutoka Masasi - Nachingwea hadi Liwale inakwenda kujengwa kwa *EPC + F*. Tuna barabara ambayo nataka niwahakikishie ndugu zangu wa Mtwara; Mnivata – Tandahimba – Newala – Masasi yenye kilomita 160, *lot* mbili; Mnivata hadi Mitesa, Mitesa hadi Masasi, saa yeyote mkataba utasainiwa. *No objection* imeshatolewa, kwa hiyo, tunakwenda kufungua pia huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna Barabara ya Igawa kwenda Tunduma, *EPC + F* na katika Mkoa wa Mbeya kutakuwa pia na *Bypass* ambayo itaanzia Uyole hadi Songwe ili magari makubwa hayo yasipite hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengi wanataka nitaje barabara zao, lakini naomba nitaje barabara moja ambayo sisi kama Wizara tunaambiwa katika barabara zote zile kubwa hasa *trunk road* ambayo imebaki ndefu ni barabara ya kutoka Mbalizi – Mkwajuni – Makongorosi – Rungwa. Ukifika Rungwa itaenda Ipole kwa kaka yangu Mheshimiwa Kakunda ama unakuja Itigi. Hii Mheshimiwa Waziri amesema tutaitafutia utaratibu maalum, japo tumeanza kuijenga upande huku na kutoka Itigi kuja huku, Makongorosi kuja huku, lakini hilo ndilo eneo ambalo tukishajenga tutakuwa tumeunganisha sasa kusini kwenda kaskazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake ni nini? Anachokifanya sasa hivi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nimezungusha hizo Barabara, lakini ukitoka Nyasa – Mbinga – Songea - Njombe, utaamua ukitoka Njombe uje Iringa, unakuja Dodoma; Dodoma unaweza ukaamua kwenda Kongwa ama ukaenda Babati huko Arusha, unatoka Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ukitoka Dar es Salaam kwenda Kigoma sehemu pekee ambayo sasa unaweza ukatembea kwa vumbi ni kati ya kaeneo kanaitwa Chagu – Kaizilava, bado kama kilomita 13 na Uvinza – Malagarasi ambapo wakandarasi wako *site. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lile eneo ulilosema, sasa hivi tunatoka Mpanda – Luhafwe, Lohafwe – Mishamo. *African Development Bank* sasa hivi tupo na mpango watukamilishie barabara hiyo kutoka Mishamo hadi Uvinza. Kwa kweli tunakwenda vizuri sana kwenye miundombinu. Wanaotaka ku-*google* waangalie, kwenye miundombinu Tanzania sasa hivi ni wangapi? Ndiyo maana Mheshimiwa Rais hakupata hiyo tuzo kwa bahati mbaya, ni kwa sababu ya hii kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nadhani makofi hayo yanaashiria kwamba Waheshimiwa Wabunge hawana swali la nyongeza, wamesikia maelezo ya barabara zote. Kwa hiyo, nadhani wamekusikia kwa kweli. Wamekusikia Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani haya makofi yatakuwa yanaashiria tumekuelewa, huna haja ya kuendelea kuzungumza. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, bandari zote sasa hivi mpango ni kuziunganisha kwa kiwango cha lami. Tuna bandari tumejenga Karema, tumeishatangaza tenda Mpanda – Karema, tuna barabara ya Lyazumbi kwenda Kabwe, ipo kwenye mpango, barabara ya kutoka Sumbawanga – Matayi hadi Kasanga imeshakamilika. Bandari hizi zote tumeshazijenga. Pia tuna barabara ambazo zinaunganisha na nchi ambazo bado. Moja ya barabara hizo ni Likurufusi – Mkenda barabara ambayo muda

wowote kuanzia sasa hivi tutaitangaza kilomita 60 kuanzia Likurufusi hadi Mukulu kilomita 60. Mkataba upo tayari kwa ajili ya kusainiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara za kutoka Songea kuja kuunganisha na Mkoa wa Njombe ziko tayari kusainiwa na nyingine wakandarasi wako *site*. Sasa hivi tunajenga barabara kwa kiwango cha zege kutoka Njombe kwa maana ya Itoni – Lusitu – Mawengi kuja Manda. Barabara ni bora kabisa katika Afrika kwa kiwango cha zege. Tumeshakamilisha kilometa 50, tunaendelea kujenga kilometa 50. Tuna barabara ambazo zinaunganisha Mkoa wa Njombe kupitia Makete kuja Isyonje kuunganisha na Mkoa wa Mbeya, wakandarasi wako *site* wanafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna barabara inatoka Kyela - Katumba Songwe – Ngana – Ikinga – Ibungu – Isongole, mkandarasi muda wowote anakabidhiwa *site* aanze kujenga kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini siyo kwa umaana, Mkoa wa Arusha tumepata maelekezo maalum. Baada ya *Royal Tour* kiwanja cha *Lake Manyara* kimeshalipiwa fidia, tunaanza kukijenga, lakini kutokea hapo hapo *Lake Manyara* ambapo ni Karatu, tunajenga *EPC* kutoka Karatu kuja Mbulu – Haydom – Idarafa – Sibiti – Lalago hadi Maswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Barabara ya Mto wa Mbu – Engaruka – Oldonyo Lengai – Sale hadi Waso ambapo unakuwa upo kabisa kwenye *Klein's Gate* ya Serengeti tumeshakamilisha kilomita 40 na maelekezo yametolewa maalum kwenye maeneo yote korofi kuna kilomita kama 39 tujenge kwa kiwango la lami.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, nadhani mpaka tutakapomaliza Bunge, maswali ya nyongeza yote yamejibiwa leo kuhusu Miundombinu.

Kabla hajaja mtoa hoja, kuna wageni wako hapa Bungeni, wageni kutoka *Toyota Tanzania Limited,* yupo Ndugu Noah Kadiva, Meneja Mkuu; yupo Ndugu Jamal Chembera, Mkuu wa Mauzo; yupo Ndugu Jackson Jaredi, *Tender Sales Executive;* yupo pia Mhandisi Elias Kafuku kutoka Wizara ya Ujenzi na Ndugu David Nganila kutoka *GPSA,* karibuni sana Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana katika Bunge hili tukufu la bajeti hii kukamilisha kazi tuliyoianza jana tarehe 22 Mei, 2023 ambapo niliwasilisha hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Bunge kwa jinsi mlivyoliongoza na kusimamia majadiliano ya hoja hii. Aidha, nachukua fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge letu Tukufu kwa kuwa wazi na kutoa maoni na michango yao ya kina wakati wa majadiliano haya. Ninawathibitishia kwamba michango yenu yote tumeichukua kwa uzito mkubwa na kwenda kuifanyia kazi ili kuendelea kuleta ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nimshukuru Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati kwa hoja nzuri zilizotolewa na Kamati yake. Nakiri

kwamba hoja hizo ni muhimu sana kwa maendeleo na ukuaji wa sekta ya ujenzi na uchukuzi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliyochangia katika bajeti yangu. Waheshimiwa Wabunge 75 wamechangia wakati wa majadiliano ya hoja hii ambapo Waheshimiwa 67 wamechangia kwa kuongea na Waheshimiwa nane wamechangia kwa maandishi. Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja kuu zilizowasilishwa katika majadiliano haya ni kama ifuatavyo:- Kwanza kabisa ni ujenzi na ukarabati wa barabara mbalimbali nchini ambayo imezungumzwa kwa kina Mheshimiwa Naibu Waziri anayesimimia Sekta ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili lilikuwa ni utekelezaji wa miradi kwa utaratibu wa *EPC + Finance* ambao leo ndiyo mpango mzima katika Bunge letu. Hii imezungumzwa kwa kina na Mheshimiwa Naibu Waziri anayesimamia sekta ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala ya fidia kwa wananchi waliyoathirika na ongezeko la upana wa eneo la hifadhi ya Barabara. Kuna suala la ongezeko la gharama ya miradi ya barabara *(variation)* kwenye miradi ya barabara, kuna suala la ushirikishwaji wa sekta binafsi katika uendeshaji na uendelezaji wa bandari zetu hasa Bandari ya Dar es Salaam. Pia kuna suala la marekebisho ya Sheria ya Reli ya *TAZARA* na Reli ya *TRC* ambalo limezunguzwa kwa kina na Mheshimiwa Naibu Waziri anayesimamia sekta ya uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, la saba usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa viwanja vya ndege ambayo imezungumzwa kwa kina na Mheshimiwa Naibu Waziri anayesimamia sekta ya uchukuzi. Kuna hoja nyingine ya ukamilishaji wa ujenzi wa Reli ya *SGR* na kuanza kutoa huduma kwa vipande vilivyokamilika; na hii imeshazungumzwa; na kuna umiliki wa Shirika letu la Ndege la *Air Tanzania;* na mwisho, kuna suala la ujenzi na ukarabati wa meli

katika Ziwa Tanganyika ambapo na yenyewe imeshazungmzwa na Mheshimiwa Naibu Waziri anayesimamia sekta ya uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, muda mchache uliopita kama nilivyosema Waheshimiwa Naibu Mawaziri wa Wizara yangu wamemaliza kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa kuzingatia maeneo ya kisekta kwa ufasaha na weledi mkubwa, ahsanteni sana Waheshimiwa Naibu Mawaziri, ninashukuru sana kwa jinsi ambavyo mmejibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge na mimi nitajaribu kujibu hoja chache zilizobakia. Aidha, naomba kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba Wizara itajibu hoja zote za Waheshimiwa Wabunge kwa maandishi na kuziwasilisha Bungeni kabla kuhitimisha kwa Mkutano wa Bunge hili la Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nianze kuhitimisha hoja yangu kwa kutoa ufafanuzi wa kiujumla kwa baadhi ya hoja zilizojitokeza kwenye maeneo makubwa yaliyojitokeza. Kwanza kwenye sekta ya uchukuzi; hoja kubwa ambayo imejitokeza kwenye mjadala wetu huu ni ushirikishwaji wa sekta binafsi katika uendeshaji na uendelezaji wa bandari nchini.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge takribani 80% waliochangia sekta ya uchukuzi wamejikita zaidi kwenye ushirikishwaji wa sekta binafsi kwenye uendeshaji na uendelezaji wa Bandari ya Dar es Salaam. Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia wamekubaliana na hoja hii na wengine wamechangia kwa hisia kali sana na wamesema tumechelewa kuleta sekta binafsi kwenye uendeshaji na uendelezaji wa Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tumewasikia, Serikali tumewasikia tunaenda kulifanyia kazi mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa wamefanya hivyo kwa sababu wanajua Bandari ya Dar es Salaam ndio lango kuu la uchumi wa nchi yetu. Asilimia 37 takribani trilioni 7.78 ya makusanyo ya mapato ya kiforodha ya *TRA* yanakusanywa kwenye Bandari ya Dar es Salaam. Hili ni jambo kubwa na hili ni

jambo muhimu na lazima tulisimamie kwa nguvu zetu zote. Aidha, mara nyingi Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amesema kwamba bandari inaweza kuchangia asilimia kubwa sana ya bajeti ya nchi yetu kama tutaisimamia vizuri na kwa uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwapitishe haraka kwa utendaji usioridhisha wa Bandari ya Dar es Salaam; *TPA* mwaka 2015/2016 ilihudumia mizigo tani 15,670,000; na mwaka 2020/2022 ilihudumia takribani mizigo tani 20,730,000 sawa na ongezeko la asilimia 30.5. Kiwango hiki kinaonekana ni kikubwa ambacho ni wastani wa ongezeko la asilimia 4.3 lakini ni kidogo kutokana na mpango mkakati wa *TPA* ambayo ilisema kwamba lazima ongezeko la bandari la mizigo liwe kati ya asilimia 10 mpaka asilimia 12.9 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kuna sababu ambazo zimechangia kutofikia lengo hili; sababu ya kwanza ni changamoto ya uendeshaji. Sababu ya pili kubwa ni changamoto ya ucheleweshaji wa mizigo pale nangani Bandari ya Dar es Salaam. Meli inakuwa-*charged demurrange charge* ya takribani dola 25,000 kwa siku ikichelewa na gharama hizi zote zinakwenda kwa mlaji yaani mimi na wewe.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya tatu ni changamoto ya uwekezaji mdogo kwenye ununuzi wa mitambo, bandari zozote ni lazima uwe na mitambo ya kisasa na mitambo mikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya nne ni usimikaji wa mifumo ya TEHAMA ambayo imesababisha ucheleweshaji mkubwa wa utoaji wa mizigo bandarini;na changamoto ya tano ni ukarabati na ujenzi wa magati mapya. Bandari ya Dar es Saalam ina magati kumi na mbili tu, lakini bandari nyingine mtaona zina magati karibuni hamsini. Pia mwisho kulikuwa hakuna ufumbuzi katika mnyororo mzima wa usafirishaji wa mizigo kuanzia kwenye meli mpaka kwa mdau ambaye unampelekea huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Dar es Salaam ina ushindani mkubwa kwenye bandari nne duniani hasa kwenye mizigo ya Zambia, Malawi, Rwanda, Uganda na *DRC*. Bandari ya kwanza ambayo inatupa *pressure* kubwa na ushindani mkubwa ni Bandari ya Mombasa. Bandari ya Mombasa inamilikiwa na Mamlaka ya Bandari ya Kenya. Bandari hii ina gati kumi na saba, Dar es Salaam tuna gati kumi na mbili. Magati kumi na tatu ni ya mizigo ya kawaida, magati sita ni kwa ajili ya kuhudumia makasha na kati hiyo bandari ya kuhudumia makasha, *Container Terminal Two* inaendeshwa na *private sector,* haiendeshwi na *Kenya Port Authority, private sector*. Inaendeshwa na *Mediterranean Shipping Company* hii ni kampuni ya Kiitaliano, hakuna suala la usalama, hakuna suala la nini, inaendesha hiyo kazi.

Mheshimiwa Spika, bandari ya pili ni gati maalum kwa ajili ya kushushia nafaka *(Grain Terminal)* ambayo inaendeshwa na *private sector, Grain Bulk Handler Limited* ya Kenya ndio inaendesha, ni *private sector*. Kwa hiyo, tusiogope *private sector* kwenye kuendesha bandari. Tusiwe waoga, ni aibu kuona mtu anasimama anasema anaogopa *private sector,* inaonekana mtu wa ajabu kwenye kuendesha bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bandari nyingine ambayo inatupa *pressure* kubwa ni bandari ya Durban. Bandari ya Durban inamilikiwa na *Transnet National Port Authority* ya *South Africa*. Bandari hii ina magati 50. Magati 31 ni ya kawaida, magati ya kuhudumia makasha ni kumi na magati kwa ajili ya mafuta, makaa ya mawe na chuma ni tisa. Magati 31 ya kawaida na magati kumi ya kuhudumia makasha inaendeshwa na *Transnet Port Terminal* siyo *Transnet National Port Authority,* hii ni kampuni tofauti. Magati tisa ya mafuta na makaa ya mawe na biashara au bidhaa za chuma na saruji yanaendeshwa na *private sector, Durban Bulk Spring Company* inaendeshwa na *Spring Leaf* na *Total Bad Freight* ni *private sector*.

Mheshimiwa Spika, kwa vile duniani kote unapokwenda ni *private sector* inaendesha bandari hasa maeneo ya kontena.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Beira, Msumbiji; hii ni bandari inayotupa ushindani mkubwa. Bandari hii inamilikiwa na Shirika la Bandari na Reli la Msumbiji na ina magati kumi na moja. Magati ya shehena za mchanganyiko na magati ya kushushia kontena. Gati hizi zote za shehena ya mchanganyiko na magati ya kushushia makontena au makasha inaendeshwa na kampuni ya *Gold Elder Mozambique* ambayo yenyewe ni *private sector.*

Mheshimiwa Spika, ukienda bandari inayotupa *pressure* tena ya Namibia Bandari ya *Walvis Bay* ya Namibia. Bandari hii inamilikiwa na Mamlaka ya Bandari Namibia na gati ya kushushia makontena au makasha inaendeshwa na kampuni ya *Terminal Investment Limited* ni *private sector* na hakuna *issue* ya *security,* watu wanaogopa; tunaogopa nini Watanzania? Ni aibu kuwa tunaogopa ogopa, ni aibu sana.

Mheshimiwa Spika, natoa mifano ya bandari mbili za mwisho; Bandari ya *Tanger Med Port* ya Morocco. Bandari hii inamilikiwa na Mamlaka ya Bandari ya *Tanger Med* ya Morocco, ina magati manne ambayo yanafanya kazi ya kushusha makontena ambayo yana uwezo wa kushusha kontena 9,900,000 kwa mwaka, wakati bandari ya Dar es Salaam inashusha makontena 760,000; hii inashusha 9,900,000 na ina *terminal* nne au ina magati manne makubwa. Gati ya kwanza inaendeshwa na *private sector* ambaye anaitwa *MPM Terminals*, gati ya pili inaendeshwa na *private sector* inaitwa *Euro Gate* ya *Europe;* gati ya tatu inaendeshwa na *private sector* na gati ya nne inaendeshwa na *private sector*. Zote zinaendeshwa na *private sector.*

Mheshimiwa Spika, naweza kutaja yaani bandari nyingi duniani zinaendeshwa na *private sector* na hatujawahi kusikia *issue* ya *security* na hizi kampuni zinafanya vizuri lazima Watanzania tubadilike.

Mheshimiwa Spika, tuna uzoefu sisi wa kuendesha *TICTS* katika endeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam. Itakumbukwa kuwa kwa mara ya kwanza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliingia mkataba na *TICTS* mnamo mwaka 2000 wa

kukodisha Kitengo cha Makasha cha Bandari ya Dar es Salaam, kuanzia gati namba nane mpaka namba kumi na moja. Mkataba ule kwanza ulikuwa na shida, lakini mwaka 2017 tulikaa sisi na timu ya wataalam, tulibadilisha mkataba ule na ndiyo iliyotusaidia tukaweza kumalizana nao mwezi Desemba mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mapungufu mengi kwenye utendeshaji wa *TICTS*. *TICTS* haikuweza kuleta ufumbuzi katika mnyororo mzima wa usafirishaji wa mizigo na matokeo yake kwanza ilitokea alishindwa kufikia viwango vya kimataifa vya ushushaji wa mizigo na matokeo yake meli zilikaa nangani kati ya siku kumi mpaka siku kumi na nne. Kulikuwa na ucheleweshwaji mkubwa wa mizigo kutoa bandarini na tukalazimika tusiendelee tena na ule mkataba wa *TICTS.*

Mheshimiwa Spika, tunahitaji wawekezaji mahiri kwenye Bandari za Dar es Salaam. Tunahitaji au Serikali inahitaji waendeshaji na wawekezji wa bandari ambao wana ujuzi wa kimataifa ambao tunawaita *Global Port Operators* wenye uwezo na sifa zifuatazo; kwanza wawe na uwezo wa kufikia viwango vya kimataifa pamoja wawe na ufanisi utakaowezesha Bandari ya Dar es Salaam kuwa washindani na bandari nyingine; hiyo ni *condition* ya kwanza.

Pili, wawe na uwezo wa kutoa ufumbuzi katika mnyororo mzima wa usafirishaji *(end to end total logistic chain solution)* kutoka toka mzigo unaingizwa kwenye meli mpaka unafika kwa mteja.

Tatu, wawe na mtandao mpana wa kupata mizigo kwenye soko la usafirishaji mali duniani. Hatutaki mtu ambaye hata kutafuta mzigo hawezi, hapana tupate kampuni kubwa ya kimataifa amabyo inajulikana duniani; na nne, wawe na uwezo wa kimataifa katika kuendeleza na kuendesha shughuli za kibandari.

Mheshimiwa Spika, kama tutapata wawekezaji kama hao matokeo yake ni kama ifuatavyo; kwanza kupunguza muda wa meli kukaa nagani kutoka siku tano za sasa mpaka kufikia saa 24

au siku moja. Hii itaongeza idadi ya meli zinazokuja bandari ya Dar es Salaam.

Pili, kupunguza muda wa ushushaji wa makasha kutoka siku nne za sasa mpaka kufikia siku moja na nusu; tatu kupunguza muda wa uendeshaji mizigo *(truck turn around*) kutoka saa mbili za sasa hadi kufikia dakika thelathini. Gari inaingia *within thirty minutes* inatoka bandarini. Huyo ndiyo mtu tunayemtaka.

Mheshimiwa Spika, nne, kuongeza shehena ya mzigo kutoka tani 20,108,000 za sasa mpaka kufikia tani 47,570,000 mwaka 2033; tano, kuongeza mapato yanayotokana na kodi ya forodha kutoka shilingi trilioni 7.756 mwaka 2022/2023 mpaka kufikia trilioni 26.709 mwaka 2030, tunamtaka mtu kama huyo. Tukifikia hapa 70% au 80% ya bajeti itakuwa inatoka bandarini; na sita, kulinda ajira zilizopo na kuongeza mnyororo wa ajira mpya mpaka kufikia 28,990 tunataka mtu kama huyo.

Saba, kushusha kwa gharama ya usafirishaji kupitia bandari ya Dar es Salaam ambapo itachangia kupunguza gharama za bidhaa zinazoingia nchini; na nane, tunataka mtu ambaye kuchagiza ukuaji wa sekta nyingine za usafiri kama vile reli, mnajua tumetumia pesa nyingi kujenga reli, tunataka mtu atakayeleta mzigo wa kutosha ili kuipa reli yetu mzigo wa kutosha, huyo ndio muwekezaji tunayemtaka.

Mheshimiwa Spika, suala la uwekezaji halina mjadala, Serikali imeamua inakwenda mbele lazima Bandari ya Dar es Salaam tuweke wawekezaji ambao wataleta maslahi mapana ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo; Bandari ya Dar es Salaam ina *limitations* zake na *limitations* za Bandari ya Dar es Salaam inakuja kwa sababu kila siku kuna meli mpya za teknolojia mpya. Kwa mfano, meli ambayo inaweza kubeba makontena 18,000 yenyewe kwenye *entrance channel* inatakiwa mita 250, Bandari ya Dar es Salaam sasa hivi *entrance channel* pale inapovuka *ferry* ni mita 170, hatuwezi ku-*extend* tena itafika wakati.

Mheshimiwa Spika, sasa tukitaka meli kubwa zenye urefu wa mita 370 lazima twende Bandari ya Bagamoyo na ndugu zangu Serikali imeshaamua mwaka huu wa fedha kwenye bajeti tumezungumza ukienda kwenye ukurasa wa 117 kifungu cha 11 tumesema tunaenda kuanza Bandari ya Bagamoyo. Bandari ya Dar es Salaam itafanya kazi, lakini kwa zile meli kubwa ambazo zitashindwa kuingia kwenye Bandari ya Dar es Salaam itakwenda Bandari ya Bagamoyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri alilizungumzia hili la reli ya Mchuchuma, hili jambo limezungumzwa mara nyingi na Mheshimiwa Kingu amelizungumza leo hapa na amelizungumza kwa uchungu mkali na hisia kali na kwa kweli *feasibility study* imeshafanyika. Lakini Waheshimiwa Wabunge ninaomba sana Sheria yetu ya *PPP* sasa hivi ni ngumu sana kuleta mwekezaji, lakini tumepata fursa nimeshasema mara ya kwanza, mara ya pili nategemea itakuja, ninaomba sana tufanye maboresho makubwa ili tuweze kufungua nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutasema, tutazungumza lakini bila ya kufanya mabadiliko kwenye Sheria yetu ya *PPP* hatutoweza kuwafanyia watanzania haki. Waheshimiwa Wabunge tuna jukumu kubwa na sheria hiyo itakuja ninaomba tuifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la umiliki wa ndege, tumekubaliana na Wabunge wote kwa kweli suala la umiliki wa ndege ni sahihi liende *Air Tanzania* na Serikali imeunda timu ya wataalam, inajumuisha wataalam hapa nchini na kutoka nje wenye uelewa wa masuala ya usafiri wa anga na uendeshaji wa mashirika ya ndege ili kupitia muundo wa sasa wa *Air Tanzania* ikiwa ni pamoja na suala la umiliki wa ndege. Timu hiyo tayari imekamilisha kazi yake na itawasilisha taarifa yake kwenye kikao cha Baraza la Mawaziri wakati wowote na uamuzi utatoka.

Naomba niwahakikishie tu kwamba tutafanya maamuzi sahihi kwa maslahi ya *Air Tanzania* na kwa maslahi ya Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye sekta ya ujenzi; kupanda kwa gharama kwneye miradi ya maendeleo *TANROADS;* kuna mambo ya msingi ambayo yanasababisha kupandisha gharama za miradi. Jambo la kwanza kabisa ni mabadiliko ya usanifu *(poor design),* miradi mingi inapandisha hela ama miradi mingi inaongezeka hela kwa sababu ya *poor design,* hili tumelijua ndani ya *TANROADS* tumejipanga sasa kwamba tuhakikishe kuwa *design* tunazozifanya zinaenda na viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo linasababisha kupanda kwa gharama za ujenzi ni mabadiliko kwenye *site*. Unaweza ukaanza *site* yako ya ujenzi, ukafika pahala ukakutana na mwamba, hiyo lazima itabadilisha gharama za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, ya tatu ni mpangilio mbovu wa kazi; kama unaenda kufanya kazi, lakini mpangilio wako siyo sahihi hiyo *definitely* itabadilisha gharama za ujenzi na hili tumelijua *TANROADS* tunajipanga vizuri.

Suala la nne ni ucheleweshwaji wa kutoa maamuzi; utoaji wa maamuzi ni muhimu kwenye kujenga, unaweza kufanya kazi mara *TANROADS* hajatoa, mara Meneja hajatoa, hiyo pia inasababisha ucheleweshwaji au uongezaji wa gharama ya kazi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni hali ya hewa, kwa mfano pale Makete. Makete ukikosea muda wa kujenga karibuni miezi sita pale ni mvua. Usipokuwa makini hii italeta shida, sasa wakandarasi na wataalam wetu wa *TANROADS* hilo walijue na la mwisho linalosababisha ni mawasiliano mabovu kati ya mtaalamu yaani mshauri elekezi na mkandarasi na *client* yaani sisi *TANROADS,* hili tunalifahamu na yote haya tunayafahamu. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge mtuamini, tunaenda kuyafanyia kazi ili kuhakikisha kwamba tunaenda ku–*control* hizi *variation* za miradi ya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni taa za barabarani; tunafahamu kwamba taa za barabarani ni muhimu sana kwenye usalama wa watumiaji wa barabara, pia zinatoa fursa wananchi

kufanya kazi zao usiku na mchana. Serikali tumeamua kwamba barabara zote zitakazojengwa na *TANROADS* sasa tutafunga taa za barabarani na zile ambazo zilishajengwa tutakwenda kufunga taa za barabarani. Hatuwezi kuendelea tunatumia hela nyingi kujenga barabara lakini tunaacha giza, hilo halikubaliki. Tumeamua na tumeshatoa maelekezo kwamba barabara zote sasa zitafungwa taa ili wananchi wetu waweze kufanya kazi usiku na mchana.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya *EPC* lakini sitaki niizungumze kwa sababu *EPC* ndio *my baby,* ndio kwa mara ya kwanza Serikalini Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi tumeanzisha *EPC+Finance*. Mwaka jana wote mlikuwa hamtuamini hapa, wengine mlisema tunasema tu lakini haitekelezeki, lakini leo mambo mmeyaona wenyewe. Baada ya miaka minne tutaandika historia ya nchi yetu. Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza sana, sitaki kulizungumza jambo hili naomba hili jambo ni kubwa sasa sisi malengo yetu ni kuangalia *Dar es Salaam Express Way* kutoka Dar es Salaam, kutoka Kibaha - Chalinze na Morogoro. Hilo ndio lengo letu kubwa. *EPC* tumemaliza sasa tunaangalia *Dar es Salaam Express Way*.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara za Waheshimiwa Wabunge hapa kwa mfano Mheshimiwa Ramadhani jana alisema kwa masikitiko makubwa mpaka alikuwa kidogo anataka kulia anasema Kinyaturu anasema kila lugha, kwa vile tumeamua kwamba tunaenda kujenga barabara hiyo kwanza tutaanza kwa kilometa 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge wa Nansio vilevile kuna changamoto kubwa kule kwake, hasa kwenye kupata *material* ya ujenzi. Kila siku kujengea changarawe inakuwa ni shida. Tumeamua kwenda kuijenga ile barabara kutoka Rugezi mpaka Nansio yenye urefu wa kilometa 12 kwa kiwango cha lami na tutaitangaza mapema mwakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Mheshimiwa Mbunge wa Sumve ambaye na yeye ana changamoto pale wilayani kwake, kwamba hakuna barabara yoyote ya lami. Tumeamua sasa nayo

tunaenda kuijenga kwa lami. Mheshimiwa Gulamali vilevile na yeye kuna barabara yake tumesema kwamba tunaenda kujenga angalao kilometa 10, Puge – Ziba mpaka Chomo, lakini tunaanza kwa kilometa 10 tunahakikisha kwamba tunaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamesema barabara zao nyingi, zote tumezichukua na tunaenda kuzifanyia kazi kuhakikisha kwamba, tunazijenga kwa kiwango cha lami kwa asilimia 100. Mwisho kabisa napenda kuchukua fursa hii tena kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupa fedha nyingi kwenye Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Tunaomba kumwambia tu kwamba, hatutamuangusha, kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Hoja imeungwa mkono; Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tujielekeze kwenye Kitabu cha II, Matumizi ya Kawaida, Fungu 98 – Sekta ya Ujenzi. Ukurasa wa 612, kwenye vishkwambi pia ni ukurasa huohuo wa 612.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa muda uliosalia tunaenda kwenye mafungu.

Katibu.

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 98 - Sekta ya Ujenzi

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…...................….……Sh. 2,144,592,800
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*………….Sh. 820,005,900
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*………….Sh. 670,674,600
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*….Sh. 269,373,600
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*……Sh. 494,392,800
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*………………………Sh. 322,624,500
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit*……………………........Sh. 274,060,500
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*...................................Sh. 212,727,500
Kifungu 2002 – *Technical Services Division*…..……Sh. 18,025,069,800
Kifungu 2005 – *Roads Division*………..………………Sh. 24,395,891,500
Kifungu 5002 – *Safety and Environment Unit*…….........Sh. 428,283,100
Kifungu 6001 – *Airport Construction Unit*……….........Sh. 337,695,400

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

### Fungu 62 - Sekta ya Uchukuzi

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……..............................Sh. 3,659,509,200
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…..............Sh. 785,802,200
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*……..............Sh. 1,883,726,200
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*.....Sh. 333,725,200
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*….....Sh. 605,280,200
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*…………………......Sh. 482,206,200
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit*…………………....Sh. 477,763,200
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*….............................Sh. 520,313,200
Kifungu 2005 – *Transport Infrastructure Division*…..Sh. 1,466,472,900

Kifungu 2006 – *Transport Services Division*……….Sh.106,879,625,200
Kifungu 5002 – *Transport Safety and Environment Division*..............................................Sh. 1,121,175,300

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 62 -Sekta ya Uchukuzi**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*………….Sh. 113,839,609,000
Kifungu 2005 – *Transport Infrastructure Division*......................................Sh. 1,419,527,122,000
Kifungu 2006 – *Transport Services Division*………..Sh. 434,963,178,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 98 - Sekta ya Ujenzi**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*…………Sh. 246,371,400
Kifungu 2002 – *Technical Services Division*.............Sh. 53,105,214,000
Kifungu 2005 – *Roads Division*……………..………..Sh. 1,266,574,916,100
Kifungu 5002 – *Safety and Environment Unit*……....Sh. 1,370,147,000
Kifungu 6001 – *Airport Construction Unit*…..............Sh. 98,546,408,500

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae. Mtoa Hoja, Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kutoa Taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Taarifa ya Kamati ya Matumizi Ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Hoja imeungwa mkono, asanteni sana. Sasa nitawahoji. Waheshimiwa Wabunge wanaafiki Hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 waseme ndiyo, wasioafiki Waseme siyo.

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Nadhani walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kutangaza rasmi kwamba, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 yamepitishwa rasmi na Bunge. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wabunge nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na watendaji wengine chini ya Wizara hii kwa kupitishiwa bajeti yao na Bunge. Na tunawatakia kila la heri katika kutekeleza ahadi ambazo mmezitoa kwenye hotuba yenu, lakini pia ahadi ambazo mmewapa Wabunge kupitia michango yao walipoeleza changamoto za maeneo yao ya uwakilishi. *(Makofi)*

Katika kuwatakia heri huko tumesikia pia, barabara nyingi zimetajwa hapa, nyingine kazi zimeishaanza, nyingine zinaenda kuanza. Tunaamini kwamba, maswali mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge huwa wanauliza yanapofikia maswali ya Wizara hii yatapungua hapa Bungeni. Kwa hivyo, tunawatakia kila la heri. Lakini pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Miundombinu, Makamu Mwenyekiti, pamoja na wajumbe wote wa Kamati hii, mnafanya kazi nzuri sana ya kuisimamia Wizara hii. Mawazo yenu ambayo huwa mnayatoa kila kipindi wanayafanyia kazi ndiyo maana bajeti inaweza kuja ikapita kwa namna hii; maana ninakumbuka mwaka jana mambo hayakuwa rahisi hapa, lakini mambo safari hii yameenda vizuri, maana yake Kamati inafanya kazi yake vizuri. Kwa hiyo, tunawashukuru sana na tunawapongeza sana kamati yetu; na Wabunge wote kwa kweli, kwenye hoja hii kila Mbunge alitaka azungumze kuhusu mambo, kwa wale wa viti maalum mikoa yao ya uwakilishi, lakini kwa ujumla wake lakini na wale wa majimbo kila Mbunge alitaka asimame; mwingine aishukuru Serikali katika mambo makubwa yaliyofanyika huko na mwingine aikumbushe Serikali yale ambayo bado.

Kwa ujumla wake, Mheshimiwa Waziri ametaja hapo barabara nyingi na wote mmepiga makofi. Naibu Waziri naye ametaja barabara nyingi wote mmepiga makofi na Naibu Waziri wa Uchukuzi ametaja mambo mazurimazuri ya viwanja vya ndege na wote mmepiga makofi kuashiria kwamba, maeneo yetu mengi yameguswa. Hata kama hayataisha yote, hii ni bajeti ya mwaka mmoja, kwa hiyo ni dhahiri tunaanza mahali halafu wataendelea kadiri muda unavyokwenda na sote ni mashahidi kwa dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha ile tuzo aliyoipata ya miundombinu Afrika, basi mambo yanaendelea kuwa mazuri zaidi na zaidi kadiri muda unavyokwenda. *(Makofi)*

Tunamshukuru pia, Waziri wa Fedha, amesema vizuri hapa. Kwa hiyo, tuna uhakika zile ahadi zilizotolewa fedha zitakuwa zinaendelea kutoka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mambo machache; la kwanza ni Tangazo la Kikao cha Kamati ya Uongozi mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge, tutakutana *Speaker's Lounge* kwa ajili ya kikao hicho muhimu na wote tuhudhurie.

Jambo la pili na la mwisho; Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka Mheshimiwa Kuchauka kuna siku alichangia hapa kuhusu Bwawa la Mwalimu Nyerere liko wapi, na nikamuuliza maswali mengi mengi sana hapa na wengine wakatoa taarifa za ziada; na nilisema kwamba ningehitaji ramani, lakini kwa namna mchango ule ulivyokwenda nikampa nafasi akamalizia kuchangia. Kwa hiyo, kwenye hilo sikuwa nimemzuwia kuchangia, alimalizia mchango wake, lakini kwa sababu, Taarifa zetu Rasmi za Bunge zinaendelea kuwa na yale maswali ambayo Mheshimiwa Kuchauka alikuwa anaulizwa na mimi hapa mbele, lakini pia na taarifa zile walizokuwa wanazitoa za ufafanuzi, alitoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, lakini pia alitoa Taarifa Mheshimiwa Dkt. Chamriho.

Sasa ile ramani nimeletewa hapa na imesainiwa tarehe 22/05/2023. Na nikiipitia hii ramani kwa niaba yenu wote ni dhahiri inaonesha eneo la Liwale, lina sehemu kubwa sana ambayo imezungushiwa kwamba ndilo eneo la mradi wa Bwawa la Nyerere. Sasa ili Taarifa zetu Rasmi za Bunge zikae vizuri, Mheshimiwa Kuchauka ule mchango wake uliokuwa unahusu eneo la mradi ni dhahiri kwamba yale aliyokuwa anayasema Mkoa wa Lindi nao unapaswa kuwa unahusika kwenye mradi ule wa Bwawa la Nyerere. *(Makofi)*

Kwa hiyo, huko nyuma umekuwa hautajwitajwi na ndiyo ilikuwa hoja yake. Na hata kwenye, kule pengine kufaidi ile miradi ule Mkoa ulikuwa hautajwi, ilikuwa inatajwa Morogoro na Pwani. Kwa hivyo, sasa kwa mchango ule aliokuwa ameutoa na kwa ufafanuzi ambao tuliuhitaji hapa ndani na sasa ramani imekuja, hakuna sababu ya Mkoa wa Lindi kutokuwa sehemu ya huu mradi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nitumie fursa hii yale maswali sasa yaliyokuwa yameulizwa kwa kuonwa ramani hii, makatibu watatazama

maswali yapi yasiwe sehemu ya mchango wa Mheshimiwa Kuchauka, ili mchango wake uwe umekamilika kwa namna inavyopaswa. Kwa hiyo, nimeona niliweke hilo vizuri kumtendea haki Mheshimiwa Kuchauka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kwa muktadha huo sasa Serikali itachukua, kwa sababu alichangia hoja hii wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hivyo, upande wa Serikali muuchukue sasa mchango wake na muone namna ya kuufanyia kazi, ili Mkoa wa Lindi uingie uwe sehemu ya mikoa ambayo ina mchango katika Bwawa la Nyerere, lakini pia yale aliyokuwa anatoa kama mapendekezo, basi ninyi mtayatazama kwa utaratibu wenu wa kawaida. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, Naahirisha Shughuli za Bunge Mpaka Kesho Saa 03:00 kamili Asubuhi.

*(Saa 1.54 Usiku Bunge Liliahirishwa Hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 24 Mei, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*